**2 FEBRUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

________

## MAJADILIANO YA BUNGE

_________

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Tano - Tarehe 2 Februari, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

Naibu Spika *(Mhe. Daniel B. Sillo)* Alisoma Dua

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/2027 - 2028/2029.

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031), Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/2027 – 2028/2029.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Namwita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 69

### Mradi wa *TACTIC* Jimbo la Bunda Mjini

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa *TACTIC* Awamu ya Tatu utaanza kutekelezwa katika Jimbo la Bunda Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *TACTIC* kwa Halmashauri ya Bunda Mjini utatekeleza miradi mitatu ambayo ni Ujenzi wa Soko Kuu, Ujenzi wa Stendi ya Mabasi na Ujenzi wa Barabara zenye urefu wa kilometa 4.5. Miji yote ya kundi la tatu, ukiwemo Mji wa Bunda, utekelezaji upo hatua ya usanifu. Baada ya hapo taratibu za kutangaza zabuni zitafuata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi unasubiriwa kwa hamu kubwa sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; mbali na kilometa ambazo amezitaja, ingawa wenyewe wanajua 25, kulikuwa kuna ahadi ya ujenzi wa kilometa 10 za lami kwenye Mitaa ya Bunda Mjini tangu Awamu ya Serikali ya Nne. Ni lini ahadi hii itatekelezwa ukizingatia Halmashauri ya Mji wa Bunda ina kilometa moja tu ya lami na ni ya zamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mbali na kwamba, kwenye Mradi wa *TACTIC* kuna ujenzi wa masoko, lakini ninajua Serikali wana mpango wa kusaidia halmashauri ambazo bado hazijaimarika kimapato, kuwasaidia ujenzi wa masoko ya kimkakati. Kwenye Kata ya Nyasura kuna Soko la Kimkakati la Manjebe ambalo litasaidia halmashauri yetu kupata mapato. Ni lini sasa wataisaidia Halmashauri

ya Mji wa Bunda ili kujenga Soko la Manjebe na Wananchi wa Bunda Mjini waweze kuinuka kiuchumi? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tangu Awamu ya Nne ya Tano na sasa Awamu ya Sita imeendelea na uendelezaji wa miundombinu, hasa hasa ujenzi wa barabara za lami, ikiwemo ndani ya Mji wa Bunda. Mpaka sasa tuna kilometa za lami zipatazo 2.27 na tunaendelea na ujenzi wa barabara hizo ikiwemo Barabara ya Ikizu kwenda Maduka Saba ambayo, Mheshimiwa Mbunge anaifahamu vizuri, kwa sasa ujenzi umefikia zaidi ya 60%. Ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge tutaendelea na ujenzi wa barabara zote ambazo zimetajwa kwa kadiri ambavyo tutakuwa tunatenga kwenye bajeti na kwa kadri ambavyo mpango wetu unatuelekeza, ikiwa ni pamoja na mpango uliowasilishwa hapa mbele ya Bunge lako leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuhusu masoko ya kimkakati na husussani Soko la Mwanjabe. Ninamwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Bunda *TC* waandae andiko la kimkakati litakalokidhi vigezo, litapokelewa kwenye Wizara yetu ya Mipango na kupelekwa Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kupatiwa fedha kwa ujenzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Mji wa Vwawa ni moja ya miji ambayo iko kwenye hii Miradi ya *TACTIC* Awamu ya Tatu. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huo katika Mji wa Vwawa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mji wa Vwawa ni miongoni mwa miji 18 ambayo

tunakwenda kutekeleza huu Mradi wa *TACTIC*. Kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, tunakwenda kuanza utekelezaji wa mradi huu mara baada ya shughuli hizi za usanifu kukamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Tarime una Miradi mitatu ya *TACTIC,* ambayo ni Stendi ya Kimange, barabara za lami ikiwepo Barabara kutoka Lebu – Kebaga mpaka Biyambu, ambayo ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Tarime pamoja na Mradi wa Dampo. Ninataka kujua ni lini sasa miradi hii itaanza na kukamilika kwa manufaa mapana ya wananchi wa Tarime Mji? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Tarime ni miongoni mwa miji inayokua kwa haraka. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyoupambania huu Mji wa Tarime; tupo katika mpango wetu wa kutekeleza huu Mradi wa *TACTIC* Awamu ya Tatu na ngazi ya usanifu wa dhana, pamoja na usanifu wa awali tuko mwishoni kuukamilisha. Tutakwenda kutangaza zabuni, kuanza ujenzi mara moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 70

### Ukarabati wa Kituo cha Afya na Nyumba za Watumishi - Masama

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya Masama pamoja na nyumba za watumishi wa Kituo hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Saashisha kutoka Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Masama kilijengwa Mwaka 1979, hali inayosababisha kuwa na miundombinu michache na chakavu. Kituo hicho kinahitaji miundombinu muhimu, ikiwa ni pamoja na jengo la huduma za wagonjwa wa nje *(OPD),* maabara, jengo la huduma za uzazi, jengo la upasuaji, jengo la kufulia, kichomea taka, vyoo vya nje na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya tathmini na kuainisha vituo vya afya kongwe 532 kote nchini, ambavyo vinahitaji kuongezewa na kukarabatiwa miundombinu yake. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 102.08 zinahitajika, kwa ajili ya uboreshaji wa vituo hivyo. Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya kongwe kote nchini, kikiwemo Kituo cha Afya Masama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nini maswali mawili ya nyongeza:  swali la kwanza; wakati tukisubiri Serikali ilete fedha, kwa ajili ya ukarabati, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuanzisha huduma ya upasuaji kwenye kituo hiki, ambayo ni huduma muhimu sana kwa watu wa Masama?

*Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Hospitali ya Wilaya ya Hai iko katikati na inapokea wagonjwa wengi sana wanaotokana na ajali kwenye maeneo mbalimbali kwenye Barabara yetu ya Arusha kwenda Moshi, lakini mpaka sasa hivi hatuna theatre, kwa ajili upasuaji. Je, Serikali ni lini italeta fedha ya kujenga theatre, kwa ajili ya*

*upasuaji katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Hai?* **[MANENO HAYA SIYO SEHEMU YA TAARIFA RASMI ZA BUNGE]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kituo chetu cha Afya cha Masama, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza maswali ya msingi. Pili, ninamwelekeza Mkurugenzi kuendelea kutenga fedha za ndani na kuanza ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo chetu cha Afya cha Masama.

*Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tayari halmashauri ilijenga jengo la upasuaji katika Hospitali ya Hai na tayari kazi za upasuaji zinafanyika pale, wataalam wangu wameni-brief. Ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, kama taarifa hazijafika kwa wakati, ninamwomba DMO aweze kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge, lakini pia, Mkurugenzi anifikishie taarifa sahihi kwa Mheshimiwa Mbunge kwa maana ya kwamba, Hospitali ya Hai imeshaanza matibabu hayo ya upasuaji hadi upasuaji wa mifupa. (Makofi)* **[MANENO HAYA SIYO SEHEMU YA TAARIFA RASMI ZA BUNGE]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Serikali iliahidi kujenga vituo vya afya vya kimkakati, ili wananchi wasiendelee kufuata huduma katika umbali mrefu sana. Katika Wilaya yetu ya Kilolo kuna Kata za Kimara, Idete, Ukwega, Kwiugumu na Image, wananchi wanapata mateso sana kufuata huduma za afya na barabara hazipitiki. Mpaka sasa hivi madaraja hayapo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je ni lini sasa hivi vituo vya kimkakati vitajengwa, ili wananchi wasiendelee kupata mateso makubwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilimetenga bajeti ya zaidi ya vituo 120 katika majimbo 120 vya kimkakati, zaidi ya shilingi bilioni 30. Tayari tumeomba fedha zingine, kwa ajili ya majimbo 94 pamoja na yale majimbo ambayo ni mapya, yote yataingia katika mpango huo na tutakwenda kujenga hivi vituo vya afya vya kimkakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona. Ninaomba maswali yawe mafupi.

Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Hunyari kimejengwa ni miaka mitatu sasa hakina jengo la upasuaji. Wananchi wenyewe wakaamua kujenga jengo na Serikali ikasema itakwenda kuwasaidia kulimalizia. Sasa ni lini jengo hili litakwenda kumaliziwa kwenye Kituo cha Afya cha Hunyari? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere. Kwanza tunawapongeza wananchi kwa hatua waliyochukua na kuanza kujenga majengo hayo katika hospitali aliyoiainisha. Ninamwelekeza Mkurugenzi aweze kutenga fedha na kuanza ujenzi wa majengo yanayopelea katika hospitali hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Charles Mhando, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza naanza kwa kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuletea pesa wiki iliyopita shilingi bilioni 1.4, kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali yetu ya Magunga. Hospitali ya Magunga imezeeka sana, imechakaa na ina umri karibu miaka 73 sasa. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari twende pamoja katika hospitali ile, kwa ajili ya kufanya tathmini, ili ikiwezekana tufikirie kujenga majengo mapya badala ya kuendelea kuweka viraka katika hospitali ile, ambayo inakuwa ni gharama kubwa zaidi kwa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pamoja na timu ya wataalam tutaongozana pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwenda kwenye hospitali hiyo kufanya tathmini na kuendelea kuboresha miundombinu ya hospitali hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Karema, Kituo cha Afya cha Kasekese na Kituo cha Afya cha Mwese kuna tatizo kubwa la ukosefu wa Jengo la Mama na Mtoto, Maabara na nyumba za watumishi. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha,ili iweze kukamilisha hivyo vituo vya afya? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika,

kama nilivyosema awali kwamba, zaidi ya vituo 532 vimeishatengewa bajeti ya shilingi bilioni 102.08. Kwa hiyo, pamoja na vituo ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviainisha vimo katika ukarabati huu mkubwa na kuweza kujenga majengo mengine ambayo yanahitaji, kama maabara, ili kuendelea kupata huduma kwa wananchi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Benjamini Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Kahama Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Hospitali ya Manispaa ya Kahama Kupandishwa Hadhi**

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Manispaa ya Kahama kuwa Hospitali ya Rufaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya maboresho katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama, ikiwa ni pamoja na kuwezesha utolewaji wa huduma za kibingwa. Huduma za kibingwa zinazotolewa ni pamoja na huduma za magonjwa ya ndani *(internal medicine),* matibabu ya mifupa, magonjwa ya uzazi, magonjwa ya macho, pamoja na huduma za uchunguzi wa mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Kahama Manispaa ina upungufu wa miundombinu muhimu ikiwemo jengo la huduma za dharura, jengo la huduma za wagonjwa mahututi na baadhi ya vifaa vya huduma za uchunguzi. Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu muhimu katika hospitali hiyo kisha kufuata

Miongozo ya Wizara ya Afya kupandisha hadhi kuwa hospitali ya hadhi ya mkoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benjamin, swali la nyongeza.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuhusu kuboresha huduma katika hospitali yetu ya Manispaa ya Kahama, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali inatenga bajeti kwa ajiili ya kuboresha huduma kwa kujenga jengo la dharura na kuweka vifaa vya uchunguzi kwa maana ya *CT- Scan*. Sasa ni lini Serikali ina mpango wa kupeleka *CT- Scan* kwenye hospitali hii ambayo inapokea wagonjwa wengi sana kutoka hospitali zingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini sasa Serikali ina mpango wa kuboresha na kukamilisha majengo ya zahanati ambayo yamefikia hatua za lenta kama vile Chalya, Nyandekwa na sehemu zingine za Wilaya yetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ngayiwa. Kwanza, ninampongeza Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI anatoa michango mizuri kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kwa idadi kubwa ya wagonjwa ambao tunawapokea katika hospitali hii ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na uhitaji wa *CT- Scan* kwa ajili ya upimaji, uchunguzi wa mifupa kwa wagonjwa wetu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa maana ya kwamba ndani ya muda mfupi Serikali imekwishafanya tathmini na uhitaji huo tumeshauona, tunaipeleka *CT-Scan* pale ili iende kutoa matibabu kuwahudumia wahitaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zahanati nilikwishaeleza hapa kwamba zaidi ya zahanati 1,841 zinakwenda kufanyiwa ukarabati na kumaliziwa maboma, Serikali inajielekeza zaidi katika miradi hii ambayo tayari imekwishaanzishwa ili tuweze kuikamilisha kabla ya kuanza miradi mingine ya zahati na vituo vya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa John John Nchimbi, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata yangu ya Mpepo katika Wilaya ya Nyasa ndiyo kata ya pili kwa ukubwa katika Wilaya yangu. Kwa bahati nzuri inapakana na nchi ya jirani ambapo mwaka jana ilisababisha maambukizi ya ugonjwa wa *M-Pox* kutoka katika nchi ya jirani, lakini kata hiyo mpaka sasa pamoja na unyeti wake haina kituo cha afya. Nini kauli ya Serikali ili kulinda maisha ya wananchi wa Nyasa kutokana na njia hiyo ambayo imeonekana inapitisha magonjwa mengi na bado hakuna sehemu ya afya ya kuwalinda wananchi wangu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa John John Nchimbi, Mbunge wa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inaendelea kupambana na haya magonjwa ya mlipuko, kupitia vile vituo vya kimkakati Mheshimiwa Mbunge ataweza kutuambia kama kituo hicho kiende kikajengwe katika kata hii, yeye mwenyewe atatupa uelekeo huo na tutaona namna gani ya kwenda kuboresha katika kituo chetu cha afya hicho na tunaweza tukajenga kituo cha kimkakati katika Jimbo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 72

**Kuzuiwa Kuendeleza Ardhi Wananchi wa Mbalawala**

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE** aliuliza:-

Je, kwa nini wananchi wa Kata ya Mbalawala wamezuiwa kuendeleza ardhi wanayomiliki kwa maelezo kuwa ni sehemu ya Bonde la Kati Singida?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini. Bonde la Mzakwe linasimamiwa na Mamlaka ya Bonde la Wami Ruvu *Water Basin* na Mamlaka ya *DUWASA* na siyo Bonde la Kati la Singida kama swali lilivyoelekezwa. Bonde hili lilipimwa kisheria na kusajiliwa Aprili, 2000 kwa ramani yenye Namba 45977.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo lina ukubwa wa hekta zaidi ya 34,000 na lipo katika Kata za Chihikwi, Kawawa, Matangizi, Makulu na Mtaa wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizopelekea kuzuiwa kufanya maendelezo katika bonde hilo ni kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kuwa kuna zaidi ya visima 20 vinavyotoa huduma ya maji yanayotumika na wananchi wa Dodoma Mjini na maeneo jirani, eneo ilo kitaalam lina kimo cha maji kilichopo juu. Serikali imechukua hatua za kusitisha upimaji na umilikishaji pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari ya kuendeleza eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paschal Inyasi, una swali la nyongeza?

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Mitaa hii mitano na siyo Kata, Mitaa hii mitano ilipimwa kama vijiji mwaka 1973. Je, ni hatua gani Serikali inachukua kuwanusuru wakazi wa Kata hii ya Mbalawala wapatao takriban 12,000 ambao wanategemea ardhi hii kwa maisha yao ya kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wakati Serikali inajiandaa kutwaa Bonde la Mzakwe iliwafidia wakazi wa vilivyokuwa vijiji vya Mzakwe na Mchemwa, baadhi kuwahamishia katika Kata ya Chahwa ambayo sasa hivi iko kwenye Jimbo la Mtumba. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia wakazi wa mitaa hii ya Kata ya Mbalawala ili wapishe Bonde la Mto Ruvu kama ilivyowafidia waliokuwa wakazi wa Vijiji vya Mzakwe na Chahwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Inyasi, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na swali la pili, kwa maana kwamba sisi TAMISEMI ndiyo wamiliki wa ardhi, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona namna gani ya kuendelea kuwafidia wale ambao hawajapata kwa sababu Serikali imeendelea kutoa fidia katika maeneo mengi sana nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, mimi na Mheshimiwa Mbunge tutakaa pamoja na Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Ardhi kuona namna gani tunaweza tukafikisha maendeleo haya kwa wananchi wetu kwa maana ya kwamba vijiji vimeshapimwa toka

mwaka 1973, tuone namna gani sahihi ya kuendeleza eneo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Hatma ya Mradi wa *TASAF***

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, nini hatma ya Mradi wa *TASAF* nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kukamilika kwa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, Serikali inaendelea na maandalizi ya Awamu ya Tatu ya Mpango ili kuimarisha hifadhi ya jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kwa Awamu ya Tatu ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kunathibitisha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuiendeleza *TASAF* kama chombo cha kimkakati cha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya 2023, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na Mipango ya Maendeleo ya Muda Mrefu, wa Kati na Mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hii mkazo utawekwa zaidi kwenye Kaya kuhitimu, kujitegemea kiuchumi, ajira pamoja na ushirikishwaji wa kaya katika mifumo ya kawaida ya huduma za Serikali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali iliahidi kutumia taarifa za *TASAF* katika utekelezaji wa awali wa bima ya afya kwa wote kwa maana ya *pilot study*. Je, ni nini kimefanyika mpaka hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya kuwaondoa watu kwenye utaratibu wa *TASAF* kwa kisingizio cha kuhitimu kwa maana ya ku-*graduate* ilihali bado wangali maskini wa kutupwa. Je, Serikali haioni sababu ya kuiondoa dhana hii ya uhitimu ili kuwaondolea adha maskini hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi 2022 imetambulika kaya zaidi ya 3,900,000 ambao wako katika kaya maskini. Katika kaya hizo, kaya 931,000 zimetambulika na tayari zimewekwa katika kanzidata. Kwa sasa kaya 276,000 zinawekwa katika mpango wa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa bima ya afya kwa wote wakati Serikali inaendelea kuchambua na kuendelea kutambua hizo kaya maskini ambazo tayari zinatakiwa ziingie katika utekelezaji wa bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye swali lake la pili kuhusu walengwa kuhitimu, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya fedha kama chachu ya kuimarisha uchumi katika kaya maskini. Hata hivyo, katika utekelezaji wa mpango wa pili *(PSSN2)* Serikali imeendelea kusisitiza na kuwapa nguvu walengwa wa kaya maskini waweze

kujitegemea kiuchumi. Hela zinavyotolewa ni kuwezesha zile kaya ziweze kusimama na kuweza kujitegemea kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Serikali imeendelea kuwawezesha na kuwaunganisha katika fursa mbalimbali walengwa ambao wako katika mpango ili waweze kujitegemea kwa kuwaunganisha na fursa kama mikopo ya halmashauri lakini kuwapa elimu ya ujasiriamali, pamoja na kuwapa rasilimali za uzalishaji kwa ajili ya kwenda kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimu Serikali imekuwa ikifanya tathmini ya kina ili kuona kama zile kaya zina uwezo sasa wa kusimama zenyewe na zimeimarika kiuchumi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Ujenzi wa Mnara wa Mawasiliano katika Jimbo la Tunduru Kusini**

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga mnara wa mawasiliano katika Vijiji vya Kazamoyo, Imani na Kilimani katika Jimbo la Tunduru Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

Mhandisi Fadhili Sandali Chilombe, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne jumla ya minara 1,041 imejengwa na inatoa huduma za mawasiliano kwa wananchi. Kati ya minara hiyo, minara 758 imejengwa kupitia Mradi wa Tanzania Kidigitali ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais, tarehe 13 Mei, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* inaendelea na jitihada za kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote yaliyosalia ambapo tarehe 5 Desemba, 2025 mikataba ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata 201 ilisainiwa na utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kupitia *UCSAF* imepanga kufikisha huduma hizo katika maeneo mengine 280, yakiwemo maeneo ya kimkakati kama vile reli ya kisasa, hifadhi za Taifa, barabara kuu na maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na taasisi zake na makampuni ya simu, inaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Miaka Mitano (2025 – 2030) wa ujenzi wa minara ya mawasiliano ya simu wenye lengo la kumaliza au kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Lukumbule ina minara minne ya mawasiliano iliyojengwa na Makampuni ya Simu ya *VIETTEL* (mnara mmoja) na *TTCL* (minara miwili) pamoja na mnara wa *Helios Towers Tanzania* ambao *Vodacom, Airtel* na *Honora* wanautumia kwa pamoja kwa kuweka vifaa vyao vya mawasiliano. Aidha, kutokana na changamoto ya mawasiliano katika Kata hiyo, Vijiji vya Kazamoyo na Imani vimejumuishwa katika mradi wa mawasiliano vijijini, awamu ya tisa unaotekelezwa na Wizara. Usanifu wa minara katika vijiji hivyo umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mapema Februari, 2026 na

kukamilika mwishoni mwa Mei, 2026, ambapo wananchi wataanza kunufaika na huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Kilimani kitapata mawasiliano kupitia mnara wa Kazamoyo mara utakapokamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Fadhili, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni pamekuwa na ongezeko kubwa sana la watumiaji wako wa simu kwenye baadhi ya maeneo ndani ya Jimbo la Tunduru Kusini, hali hiyo imesababisha baadhi ya minara kuzidiwa na ubora wa mawasiliano kutoka kwenye minara hiyo kupungua.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kwenda kufanya *review,* kwa maana ya mapitio kwenye baadhi ya minara ili kuangalia uwezekano wa ama kuongeza masafa au kujenga minara mingine karibu na maeneo hayo?

(b) Je, kama inakubaliana na mimi, kazi hiyo itaanza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mhandisi Fadhili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufanya tathmini upya ni kweli baadhi ya minara kutokana na kuongezeka kwa watumiaji inakuwa inazidiwa. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kutuma wataalam katika

maeneo ya Jimbo la Tunduru Kusini ili wafanye tathmini na kubaini changamoto hiyo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Cornel Magembe, swali la nyongeza.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Kuna vijiji takribani vitano katika Jimbo la Chato Kaskazini, ambavyo ni Vijiji vya Mkungo, Nyakato, Buzirayombo, Itale na sehemu kubwa ya Ilyamchele. Vijiji hivi havipati mawasiliano kwa sababu hakuna mtandao na hii husababisha utoaji wa elimu hasa kwenye shule za msingi na Sekondari ambako sasa wanatumia TEHAMA wanafunzi wanashindwa kupata haki yao kama wanafunzi wengine. Je, Wizara ina mpango gani wa kwenda kuweka mtandao katika maeneo hayo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la ndugu Mheshimiwa Magembe, Mbunge wa Chato Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi, tunatambua changamoto ya mawasiliano nchi nzima na ninaamini kila Mbunge aliyemo katika jengo hili ana changamoto ya mawasiliano katika Jimbo lake kwenye sehemu moja au nyingine. Ndiyo maana sisi kama Wizara tunaandaa mkakati wa miaka mitano wa kuyafikia maeneo yote yenye changamo ya mawasiliano na tunaamini katika kipindi hiki cha miaka mitano, tutafika kila eneo kule ambako hakuna minara, tutajenga minara mipya, kule ambako minara imezidiwa, tutaiongezea nguvu ili kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 changamoto ya mawasiliano katika Majimbo mbalimbali na hapa nchini iwe imepungua kwa kiasi kikubwa au tumeimaliza kabisa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa ninawaona, maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga minara katika Kata za Mtunguru, Mkwedu, Chilangala pamoja na Mikumbi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Nawanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Wizara inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Minara 280 katika bajeti hii na katika bajeti ijayo tutatekeleza tena mradi wa kujenga minara mingine 280 ambayo katika mradi huo Kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge nazo tutazipatia kipaumbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Haiderali Hussein, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mnara wa mawasiliano katika Kata ya Mughunga, Ilongero Singida Vijijini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Singida Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la swali la msingi, kwamba tumeandaa mkakati mahsusi wa miaka mitano wa kujenga minara mbalimbali nchini katika maeneo yote yenye changamoto ya mawasiliano. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mkakati huo na eneo lake hilo lenye changamoto pia tutalifikia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi ya swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Kata za Kitwai na Naberera Wilayani Simanjiro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mkakati wetu wa miaka mitano wa kuhakikisha kwamba nchi hii yote inapata mawasiliano, tutajenga minara, kama nilivyosema, katika maeneo mbalimbali ili kuyafikia maeneo yote yenye changamoto. Yale ambayo yana minara, lakini hayana mawasiliano ya kutosha au yana changamoto tutaiongezea nguvu. Kwenye eneo lake hili la Simanjiro ambalo hakuna minara ndani ya hiki kipindi cha miaka mitano tuna uhakika tutakuwa tumefika na tumejenga minara kwa ajili ya kuondoa changamoto hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo, hasa katika Jimbo la Nanyumbu, minara ipo lakini wananchi wanahitaji huduma zaidi ya ule mnara wa mawasiliano. Je, Serikali haiko tayari kuwashauri wawekezaji wengine wakatumia ule mnara mmoja ili kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano wa maeneo yote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kampuni za simu zinachangia baadhi ya minara katika baadhi ya maeneo; mnara mmoja kampuni mbili ama matatu zinaweka vifaa vyao vya mawasiliano. Kwa hiyo nichukue nafasi hii pia kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kulifanyia kazi suala hili ili hiyo minara kama ina changamoto au imezidiwa, basi waangalie uwezekano wa kuwasiliana na kampuni ili waongezewe nguvu. Kama kuna uwezekano mwingine pia basi kampuni ziruhusiwe kuwekeza zaidi kwenye mnara huo ili kampuni mbili ama tatu yaweze kutoa huduma kwa kutumia mnara mmoja. Zoezi hilo litafanyika kwenye baadhi ya maeneo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tarime Vijijini lipo mpakani mwa Kenya. Kwa hiyo Kata za Susuni, Mwema, Sirari, Nyanungu, Gwitiryo tunapata mawasiliano kutoka Kenya; lakini vilevile maeneo kama Mrito kwenye mgodi pale wa dhahabu, Gorong'a karibu na Hifadhi ya Serengeti hakuna mawasiliano kabisa. Nimeuliza swali hili miaka mitano imepita sasa ninaomba Serikali iniambie. Je, ni kwa nini wananchi wa maeneo hayo wanapata shida ya mawasiliano mpaka leo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kupata nafasi na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Niombe kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Waitara. Tunatambua changamoto iliyopo uhafifu wa mawasiliano hasa katika maeneo ya mipakani ikiwemo Sirari, Tarime pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine, kama Serikali tunaendelea kufanyia kazi kuhakikisha tunaongeza nguvu katika minara iliyopo katika maeneo ya mipakani; na sasa katika awamu yetu ya kumi na moja eneo hilo litakuwa la kipaumbele ikiwemo maeneo yanayopita *SGR,* lakini pia maeneo ya barabara kuu pamoja na maeneo ya mipakani kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikitukabili unajikuta mkifanya *adjustment* katika maeneo ya minara katika maeneo ya mipakani baada ya muda nchi za wenzetu pia wamekuwa wakifanya *adjustments.* Kwa hiyo unajikuta unarekebisha hali leo baada ya muda unajikuta pia changamoto inaendelea kurudi pale pale na inakuwa inapelekea masuala ya *roaming* na kusoma minara mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kufanya ukaguzi na usimamizi zaidi mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba kutakuwa na *adjustment* ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata mitandao kutoka mawasiliano ya Tanzania pekee. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, sasa aulize swali lake.

Na. 75

**Reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam hadi Kusini**

**MHE. NAPE M. NNAUYE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanza upembuzi wa ujenzi wa reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam hadi Kusini kufuatia maandalizi ya Mradi wa *LNG*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TRC* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya *standard gauge* ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma yenye jumla ya kilometa 1,000. Aidha, kwa sasa Serikali inaendelea na utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, ikiwemo kutumia utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Kwa upande wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara, Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Mpango Kabambe wa *East African Railway Master Plan* imetambua umuhimu wa kipande hiki cha reli kitakachounganisha Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Mtwara kutokana na umuhimu wake kiuchumi, kijamii na utengamano wa Kikanda. Hata hivyo, kwa sasa reli hiyo bado haijawekwa katika mipango ya Serikali kwa kutumia fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kufafanua kuwa, kwa sasa Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya *SGR* na miradi mbalimbali ya kimkakati nchini; na miradi hiyo iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo inatekelezwa kwa awamu kutokana na uhitaji wa fedha nyingi kwa wakati mmoja. Hivyo, nitoe rai kwa wawekezaji kutoka sekta binafsi na kampuni za fedha kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa miradi ya reli ikiwemo reli ya kusini kwa kuanza na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu haya ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kama Serikali ilivyokiri, kwamba mradi huu ni wa muhimu, lakini ni wa muhimu kwa nchi yetu

kuliko ilivyo wa muhimu kwa nchi nyingine za Afrika Mashariki, ikiwemo kuongeza thamani na utekelezaji wa haraka wa Mradi wa *LNG* wa Lindi ambao ni mradi mkubwa kuliko yote katika historia ya nchi yetu. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuuchukuwa mradi huu kutoka kwenye miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuufanya mradi wa Serikali yetu ili tuutekeleze utupe *advantage* kwa nchi za Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ipo tayari kushirikiana na wabia wanaotekeleza Mradi wa *LNG* wa Gesi wa Lindi katika kutafuta rasilimali za ujenzi wa reli hii kwa sababu nao ni wanufaika wakubwa wa kusafirisha mizigo na wananchi watakaokwenda kutekeleza mradi huu wa gesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Nape Nnauye kwa swali lake la msingi na maswali ya nyongeza ambayo ameyaongezea. Ninakubaliana naye kwamba mradi huu ni muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Serikali ilipoamua kuuingiza kwenye *Master Plan* ya *East Africa* msingi wake ni nini? Ni kutaka uingizwe katika vipaumbele vya Kanda ya Afrika Mashariki; lakini mbili ni kutaka tushirikiane katika utafutaji wa pamoja wa rasilimali fedha kwa miradi yote iliyopo katika kanda hii; na tatu ni kutaka mradi huu usomane na miradi mingine inayotekelezwa katika jumuiya hii; kwa hiyo ndiyo hoja ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na kwamba ni muhimu na kwamba tuiingize kwenye kipaumbele chetu, hilo tumelipokea na tunakubali kwamba ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili ambapo kimsingi ni dhana ya *PPP;* kwamba je, Serikali haioni sasa ni muhimu kushirikiana na wawezekaji wanaofanya Mradi wa *LNG*. Pengine labda uniruhusu niseme kwa ufupi sana kuhusu *concept* ya *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali zote duniani zinatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa mataifa yao; na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameendelea kuweka mazingira mazuri na rahisi ili wawekezaji, ama sekta binafsi iweze kunawiri na kustawi katika nchi yetu ili ishiriki katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwenye upande wa reli ukitazama miradi ambayo inatekelezwa, ukiangalia kuanzia kipindi cha uhuru mpaka miaka 2020 tulikuwa na reli ya mita *gauge* ambayo ni kama 2700 pamoja na *TAZARA* ambayo ni kilomita kama 975, ukijumlisha kwa pamoja ni kilomita 3,600. Mipango ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake ni nini? Ni kujenga reli ya *SGR* peke yake yenye urefu takriban 4,700. Tayari hivi ninavyozungumza miradi yenye urefu wa kilometa 2,100 imekwishaanza kutekelezwa; na ipo kwenye mpango wa kujenga reli ya kusini kilomita 1,000 kaskazini, kilometa 1,000 pamoja na reli ya mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua miradi hii peke yake fedha inayohitajika kwa ujenzi ni matrilioni. Hapo ndipo unakubali kwamba ni lazima uzishirikishe sekta binafsi katika kujenga miundombinu hiyo. Ukishamaliza kuijenga bado utahitaji vitendea kazi, vichwa na mabehewa. Ndiyo maana kwa kutambua hilo sekta ya uchukuzi kama Serikali ilibadilisha Sheria Namba 10 ya Mwaka 2017 ili kuruhusu sekta binafsi kuingia katika ujenzi wa miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, nimhakikishie Mheshimiwa Nape Nnauye pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inatambua umuhimu huo na kwa kweli inakaribisha wadau wote, wale wa *LNG* pamoja na wadau wengine waje tushirikiane kujenga uchumi. Hii ni kwa sababu tulipoanza kujaribisha tumeona faida yake. Kule *TAZARA* kama tunavyofahamu tuliporuhusu *open access,* yaani watu walete mabehewa na vichwa vyao, takriban nusu ya mzigo imeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Bandarini vilevile tuliporuhusu sekta binafsi washiriki katika ujenzi wa nchi yetu tumeona meli

zimeongezeka kutoka 4,200 zipo 4,800, mzigo umeongezeka kutoka tani milioni 17 zilizokuwepo mwaka 2020 leo zipo tani milioni 32. Kwa hiyo sekta binafsi ni muhimu sana na Serikali inawakaribisha katika kushiriki kwenye nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inaendelea na ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay, lakini pia kuna usafirishaji mkubwa wa makaa ya mawe kutoka Nyasa na Mbinga kwenda Mtwara; lakini pia tunategemea Mradi mkubwa wa Liganga na Mchuchuma. Katika majibu ya msingi ya Naibu Waziri amesema kwamba upembuzi yakinifu wa kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa *SGR* kutoka Mtwara kwenda Mbamba Bay umeanza kutekelezwa. Je, itachukua muda gani kukamilisha upembuzi yakinifu na mradi huo ukaanza kutekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu swali hili linagusa takriban Wabunge wote wa Kusini; na pengine wangesimama kutaka kuuliza reli ya kusini itaanza kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe maelezo kwa ufupi sana. Serikali inatambua umuhimu wa reli ya kusini, kwanza kama kiunganishi cha Bandari ya Mbamba Bay na Bandari ya Mtwara, kwa sababu hizi mbili zikiungana unarahisisha usafirishaji; na nini kimekifanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za awali Serikali imekwishaanza kujenga Bandari ya Kisiwa Mgao pale Mtwara bandari ya pili ambayo itakuwa maalum kwa ajili ya kusafirisha *dirty cargo;* yaani *cement*, makaa ya mawe na kadhalika; zaidi ya bilioni 435 zimeelekezwa pale. Pia ujenzi wa bandari ya Mbamba Bay ambao utagharimu zaidi ya bilioni 70, ni hatua muhimu kuelekea kwenye

jambo hilo. Tatu, fidia imelipwa kule Ludewa kwa wananchi waliopo kwenye maeneo ya Liganga na Mchuchuma, hiyo ni hatua pia. Nne sasa, tumekwishafanya usanifu. Kama nilivyosema, tunatafuta wawekezaji binafsi ambao tutashirikiana nao ili tuanze kujenga. Ninatoa rai tena kwa watu wote wa ndani na nje ya nchi ambao wapo tayari kushirikiana na Serikali, twendeni tukajenge reli hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Salehe Motto, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; lakini ninashukuru kwa majibu mazuri maana swali langu tayari limeshajibiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ninakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, Mbunge wa Mtambile, sasa aulize swali lake.

**MHE. SAID I. MZIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali langu namba 46, ninaomba majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Ni namba 76 Mheshimiwa, ninaomba urudie, ni namba 76.

**MHE. SAID I. MZIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni namba 76.

Na. 76

**Ukarabati wa Vituo vya Polisi Jimbo la Mtambile**

**MHE. SAID I. MZIMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga Bajeti kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya Polisi Mtambile na Kengeja kwa kuwa vimechakaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishafanya tathmini ili kubaini gharama halisi za ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi cha Kengeja baada ya kituo kinachotumika sasa kuwa kichakavu na kwamba hakiwezi kufanyiwa ukarabati. Kiasi cha fedha shilingi milioni 165 zinahitajika. Tathmini kwa ajili ya kubaini gharama halisi ya ukarabati wa Kituo cha Polisi Mtambile zimefanyika na kiasi cha fedha cha shilingi milioni 90 zinahitajika. Fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Polisi vya Kengeja na Mtambile zinatarajiwa kutengwa toka kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, swali la nyongeza.

**MHE. IBRAHIM S. MZIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa vituo hivi vinahudumiwa na ndugu zetu wa polisi ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kulinda nchi yetu. Je, Mheshimiwa Waziri, yupo tayari kuambatana nami kwenda Jimbo la Mtambile kujionea hali halisi ya makazi ya polisi wetu hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Ibrahim; na ombi lake la kwenda Mtambile nimelipokea na nipo tayari kuambatana naye kwenda Mtambile.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ninawaona, maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Asha Omar Rashid, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA OMAR RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninashukuru kwa kunipatia fursa hii nami kuuliza swali langu la nyongeza. Pale Mkoani kwangu Kaskazini Pemba pana Kituo cha Polisi cha muda mrefu. Kituo kile kilizinduliwa tarehe 25 Juni, 1979. Kwa kuongezeka wananchi katika Mkoa ule wa Kaskazini Pemba. Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya polisi katika Wilaya ya Micheweni na Wilaya ya Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na jengo la *RPC* wa Mkoa wa Kaskazini Pemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge swali la nyongeza huwa ni moja kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Asha Omar, Mbunge wa Viti Maalum, Kaskazini Pemba, kwa swali lake zuri; na nimpongeze sana kwa kuwa karibu sana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama hasa Jeshi la Polisi na kubaini pia changamoto zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleza katika majibu yangu ya msingi wakati nikijibu wiki iliyopita, kwamba kwa upande wa ujenzi wa vituo vya polisi vya mkoa tulikuwa tunakiri kwamba tuna mikoa mitano ambayo ilikuwa haina vituo vya polisi; lakini kwa upande wake alikuwa anaongelea zaidi kuhakikisha kwamba anafanya ukarabati wa jengo la *RPC* katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambalo hilo nalo lipo kwenye mpango wa ukarabati kama ambavyo tunaendelea nao. Kwa sasa tuna miradi 56 ya ukarabati nchi nzima katika ngazi na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo ninaamini kwamba tukienda kwenye hatua ya pili ya mpango wa kukarabati jengo hilo nalo litaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa yale majengo mawili ya wilaya kwa maana Wilaya ya Wete na Wilaya ya Michiweni Kaskazini Pemba nayo yapo kwenye majengo 75 ambayo kwa sasa

ama yapo kwenye hatua ya ukarabati ama ujenzi upya kwa wilaya zetu 75 za nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali kupitia Jeshi la Polisi tupo kwenye hatua ya kukamilisha mpango mkakati wa miaka mitano ijayo. Wakati tukiendelea na hatua hiyo, tunaendelea vilevile kutathmini hali ya majengo ya vituo vya polisi, makazi ya askari na maeneo mengine yakiwemo hospitali na majengo ya mazoezi ya vikosi vyetu vya *Field Force* na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue, wapo Wabunge wengi ambao wamehitaji ama kujengewa ama kufanyiwa ukarabati vituo vya polisi. Kwa ruhusa yako ninaomba niwatambue Mheshimiwa Florence George Samizi, Mheshimiwa wa Kigoma, Mheshimiwa Joseph Copriano Isack au Kadogo wa Monduli wamehitaji hilo, ninatambua pia hitaji lake, Mheshimiwa Anne Kilango Malacela naye na nimemwahidi nitakwenda pia kwenye eneo lake, pamoja na Mheshimiwa Ester Bulaya naye pia alihitaji pale Bunda Mjini, naye nimemwahidi pia nitakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nina swali dogo la nyongeza. Kama ikimpendeza Mheshimiwa Naibu Waziri atalijibu au atalichukuwa. Wilaya yetu ya Malinyi tumekuwa tuna shida ya gereza la mahabusu kwa muda mrefu sana. Eneo limepatikana lakini kumekuwa kuna ucheleweshwaji wa kukamilisha ambayo inawafanya wahusika kusafiri umbali mrefu sana kwenda Wilaya ya Ulanga. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha suala hili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimfahamu ili niweze kujibu vizuri; amekusudia mahabusu ya polisi au ya gereza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu ya gereza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaongelea kuhusu suala la Jeshi la Polisi lakini kwa sababu Magereza na yenyewe ni sehemu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini ninaomba tu nimjibu Mheshimiwa Kapoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yapo baadhi ya magereza yamekuwa na changamoto ya uchakavu wa majengo. Hata hivyo, moja ya eneo ambalo amelitaja la jimbo lake kwamba wilaya nzima ya Malinyi hakuna gereza na kupeleka eneo la pili; tunakuja na mpango na tutaueleza kwenye bajeti ya mwaka huu kwamba ni mpango gani kwa upande wa Jeshi la Magereza, tutaenda kuboresha magereza katika maeneo ambayo yana uhaba likiwepo eneo lake la Malinyi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwinyi Jamal, swali la nyongeza.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa ruksa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja katika Jimbo la Bumbwini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekeza nguvu kubwa sana katika uchumi wa nchi na maeneo mengine; je, haioni sasa kuna haja ya kujengwa kituo kikubwa cha polisi katika jimbo hilo kutokana na uchumi wa nchi ulivyokuwa?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwinyi Jamal swali lake la nyongeza kuhusiana na jimbo lake la Bumbwini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba Bumbwini kwa sasa ni eneo la kimkakati hasa kwa uchumi wa Zanzibar, kwani Bumbwini inaenda kuelekea kujengwa uwekezaji wa bandari kubwa mpya; Bandari ambayo itakuwa na maeneo karibu matano. Katika bandari ile kwa bahati nzuri wakati nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa mkoa ule, niliwahi kupata fursa ya ushiriki kidogo wa maandalizi ya bandari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango ulioandaliwa wa eneo lile la Bumbwini kumeandaliwa kujengwa miundombinu yenyewe ya bandari, miundombinu ya barabara za kisasa lakini pia kujengwa mji mdogo. Katika mpango uliowekwa wa mji mdogo ndani yake kuna ujenzi wa kituo kikubwa cha polisi ambacho kitaweza kusaidia kuimarisha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mattar Ali Salum, swali la nyongeza.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali imewekeza vituo vingi vidogo vidogo na sasa vituo hivyo vyote havifanyi kazi ikiwemo kituo changu cha Jimbo la Shaurimoyo na vituo vingine. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvifufua vituo hivyo vikaanza kufanya kazi ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mattar swali lake la nyongeza

ambalo linahusu vituo vidogo vya polisi kwa maana ya daraja C1 au *police post*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri hasa kwa Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, kulijengwa vituo vingi vya *police post* katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, ninaomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza siyo vituo vyote vidogo vidogo kuwa havitumiki, vipo baadhi yake vinatumika. Mfano wa vituo vidogo vidogo vinavyotumika ni Kituo cha Mkunazini, Kituo cha Vuga na vinginevyo. Kwa vile ambavyo kwa sasa havitumiki tumefanya tathmini kupitia Jeshi la Polisi kuona namna gani nzuri ya utumiaji wa vituo vidogo vile vya polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tukiri vingi ya vituo hivyo vipo maeneo karibu karibu. Kwa hiyo Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeona haja ya kuwatumia Askari wa Ulinzi Shirikishi kwa kushirikiana na Polisi wa Shehia ili wafanye doria badala ya kuweka askari wengi kwenye kituo kimoja na kutoa huduma bila ya ufanisi kama ambavyo ingetarajiwa. Kwa hiyo, bado vituo hivyo tuna mpango wa kuvitumia, lakini kwa utaratibu mwingine kinyume na ule wa awali hadi hapo tutakapokuwa na askari wa kutosha wa kuweza kuwaweka vituoni na wengine kufanya doria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Timoth Geofrey, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tarehe 29 Oktoba, 2025 Jimboni Kawe vilichomwa Vituo vya Polisi vitatu. Kwetu sisi Wanakawe jambo hili tunalichukulia kama jambo la dharura. Je, ni lini Serikali itajenga vituo hivi ili kurejesha hali ya huduma ya kipolisi katika maeneo husika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani

ya Nchi, ninaomba nimjibu swali lake Mheshimiwa Timoth kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tarehe 29 Oktoba, 2025 kulitokea uharibifu wa mali mbalimbali za Serikali ikiwepo baadhi ya Vituo vya Polisi katika baadhi ya maeneo. Ninaomba nimwambie Mheshimiwa Timothy kwamba Serikali inaendelea kukamilisha kazi ya tathmini na kuja na mpango wa dharura wa kuona namna gani ya kuweza kurejesha huduma kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Itwangi sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

Na. 77

**Mradi wa Maji wa Vijiji 18 Tinde**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI K.n.y. MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Vijiji 18 vya Tinde *package*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Itwangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya India ili kupata kibali cha kuendelea kutumia fedha kiasi cha dola za Marekani milioni 6.9 zilizobaki kwenye mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 268.35 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Usambazaji katika Miji ya Tinde na Shelui sambamba na vijiji 18 vya Wilaya ya Shinyanga pamoja na Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hatua iliyofikiwa na Serikali imeshawasilisha ombi maalum kwa Serikali ya India mwezi Januari, 2026 baada ya kusitishwa kwa matumizi ya mkopo huo. Ni mategemeo ya Serikali kuwa taratibu za kuruhusu matumizi ya fedha hizo yatakamilika na Wakandarasi kupatikana kabla ya kwisha kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mpango wa muda mfupi, Wizara itaunda timu ya wataalam ambayo itafanya tathmini katika jimbo la Itwangi ili kubaini na kuwezesha vijiji vyote vilivyo karibu na mitandao ama matoleo ya maji vinasogezewa huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari sasa kuleta timu ya wataalam mara baada ya Mkutano huu wa Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ipo tayari kutumia sasa Mradi wa Bukene pamoja na Mradi wa Isemela ambao bado unatekelezwa kuweza kufikisha huduma ya maji katika Vijiji vya Zobogo, Tinde, Nuru pamoja na Igulamya? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Serikali iko tayari na kama nilivyojibu katika swali la msingi, Wizara inatarajia kuunda timu ambayo itaenda kule Itwangi na kwenda kufanya tathmini na kujiridhisha na hali halisi ya huduma ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi 3,714 ambayo Serikali iligharimu takribani shilingi trilioni 1.8, ndani ya Itwangi kulikuwa na miradi tisa iliyokamilika yenye gharama ya shilingi bilioni 12.7. Ndani ya Jimbo hili tunayo miradi inayoendelea miwili ambayo ina gharama ya shilingi bilioni 8.9 ikiwemo na kuhakikisha kwamba vijiji vilivyobaki katika eneo hilo ni vijiji 14 tu ambavyo vimebaki bila kuwa na huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, eneo la Tinde, pamoja na Didia, pamoja na Samuye yote yataingizwa katika utaratibu wa kupata huduma ya maji safi na salama. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, swali la nyongeza.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali iliahidi kuboresha miundombinu ya maji kwa kuwajengea tenki la lita 1,000,000 Kijiji cha Likonde, Kata ya Mayanga na ahadi hiyo iitolewa tarehe 27 Septemba, 2022 ambalo litaenda kuwasaidia wakazi zaidi ya 24,000. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini? Ninaomba nisisitize neno "lini?"

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kidogo, ninaomba kujua ni jimbo gani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ni jimbo gani tena?

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Jimbo la Mtwara Vijijini.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi nchini kote na nchi yetu ina vijiji takribani 12,318. Katika utekelezaji wa miradi ni vijiji 1,575 tu ambavyo vimebaki kutofikishiwa huduma rasmi ya maji. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, eneo hilo tunalichukua likiwemo ndani ya miradi 878 ambayo haijakamilika yenye gharama ya shilingi trilioni 1.3. Tunaamini kwamba miradi hii itakapokamilika yote kwa ujumla na eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliongelea basi litakuwa limekamilika katika utekelezaji huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kuwa, kuna miradi miwili Makete ambayo walisaini takribani miaka minne imepita na miradi hii haijaendelea. Mradi wa Usalimwani, Mfumbi, Kidope na Madihani imesimama hadi saizi. Kwa kuzingatia utendaji wako wewe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Waziri wake wanafanya kazi vizuri sana; Ni ipi lugha ya matumaini kwa wananchi wa Makete ili waweze kupata maji kwenye miradi hii miwili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Kaka yangu Mheshimiwa Festo Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tunakiri kwamba kumekuwepo na changamoto katika utekelezaji wa miradi hii miwili, lakini Serikali sasa imeshaweka mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba tunaenda kumrejesha mkandarasi ambaye alikuwa ameshaondoka, alikuwa ameshasitisha utekelezaji wa mradi na sasa madai yake tayari Serikali imeyafanyia kazi na atarudi *site* na ataendelea kufanya kazi ili mradi ukamilike kwa wakati. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, swali la nyongeza.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea maji katika Mji wa Katoro akiyatoa eneo moja linaitwa Chankorongo. Tangu dunia iumbwe maji hayajawai kufika Katoro, lakini sasa yamefika Katoro kwa gharama ya shilingi bilioni nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kufahamu maji yameshaletwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, je, ni lini sasa Serikali itakuja kusambaza maji hayo ili wananchi waweze kunufaika na maji kuliko kubaki tu na historia ya kwamba maji yamefika Katoro na hayajasambazwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe pia Mheshimiwa Waziri…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali la nyongeza ni moja.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ntemi Kija, Mbunge wa Katoro, hakika ameanza kazi yake vizuri na anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza tunachohitaji katika utekelezaji wa miradi hii ni kupata ama kubainisha chanzo cha maji na baada ya hapo kujenga miundombinu *(transmition line main)* na baada ya hapo sasa tunakuja kwenye usambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimtoe hofu kwa sababu kazi ya kupata chanzo imekamilika, kazi ya kujenga miundombinu ya kufikisha maji katika eneo la Katoro imekamilika. Sasa kazi iliyobaki ni ndogo sana kwa Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, usambazaji wa maji katika Mji wa Katoro unaenda kufanyika kwa haraka sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, Mbunge wa Monduli sasa aulize swali lake.

Na. 78

**Kukamilisha Mradi wa Maji Vijiji 13-Monduli**

**MHE. ISACK J. COPRIANO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha Mradi wa Maji wa Vijiji 13 vya Jimbo la Monduli?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, Mbunge wa Jimbo la Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na awamu ya kwanza ya upanuzi wa Skimu ya Maji ya Jiji la Arusha kutoka eneo la Ngaramtoni kwenda Vijiji 13 vya Nanja, Mti Mmoja, Arkaria, Arkatan, Lepurko, Eng'aroj, Losimingori, Lashaine, Meserani Juu, Meserani Bwawani, Engorika, Engiloriti na Naalarami vya Wilaya ya Monduli mkoani Arusha. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 61.5, ujenzi wa tanki moja lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 500,000, ujenzi wa mbauti mbili za kunyweshea mifugo sambamba na ujenzi wa vituo 16 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 15% ambapo kwa mujibu wa mkataba unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2026 na unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wananchi 34,000. Aidha, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha utekelezaji wa mradi huo unakamilika ili uweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi na itahakikisha fedha zinapelekwa kadri zinavyopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, swali la nyongeza.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali dogo la nyongeza. Unajua fika Wilaya ya Monduli kwa sasa ni kame na ukizingatia mabwawa yote yamekwisha maji na wananchi wa Monduli wanapata maji Arusha. Je, Waziri haoni sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuiangalia Monduli kwa jicho la huruma ili wananchi wale wapate huduma ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Isack Joseph.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Kaka yangu, nilifanya ziara katika Jimbo la Monduli mwaka jana na mwaka juzi akiwa Diwani na tuliweza kutembelea miradi mingi ikiwemo na bwawa lililokuwa linajengwa na tukachukua hatua kwa wakandarasi ambao walikuwa wanaleta uzembe katika utekelezaji wa miradi ndani ya Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji pia wa huduma ya maji katika Wilaya ya Monduli na Jimbo la Monduli ni 77% mpaka sasa ambapo miradi zaidi ya mitano imekamilika yenye gharama ya shilingi bilioni 3.4 na kuna miradi mingine inayoendelea takribani miradi 10 yenye gharama ya shilingi bilioni 41 ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alituelekeza Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba tunazipeleka Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi ambao unaendelea sasa ambao umefikia 15% wenye gharama ya shilingi bilioni 20.3. Kwa hiyo, tunaamini kabisa katika uwekezaji huu ndani ya Jimbo la Monduli miradi hii itakapokamilika, ongezeko la upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Monduli hautakuwa na changamoto yoyote. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sara Msafiri, swali la nyongeza.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongea. Jimbo la Mvomero lina miradi sita ya maji inayoendelea ambayo imekuwa ikisuasua kutokana na changamoto za kifedha ikiwepo Mradi wa Maji wa Tandale - Homboza na Mradi wa Dakawa. Je, lini Serikali itapeleka fedha ili hii miradi sita ikamilike kwa wakati na wananchi waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la dada yangu Mheshimiwa Sara Msafiri, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara kwenye Jimbo la Mvomero na Mradi huu wa Dakawa pamoja na Tandale ni kweli kabisa kwamba ni mkombozi kwa wananchi wa Mvomero utakapokamilika, lakini kati ya miradi ambayo 878 inayoendelea yenye gharama ya shilingi trilioni 1.3 na hii miradi iko humu. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha miradi viporo vyote inaisha ili wananchi waweze kuona matokeo na maji yatoke kwa ajili ya matumizi ya maji safi na salama. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joshua Nassari, swali la nyongeza.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Nitumie nafasi hii kuipongeza kwanza Wizara ya Maji kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kwenye majimbo yetu huko, lakini nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Uwilo pale Arumeru pamoja na Mradi mkubwa wa Maji wa Embaseni - Kikatiti pale Arumeru, ni lini Serikali itapeleka fedha ili wakandarasi waweze kurudi

*site* na miradi hii iweze kuendelea kwa sababu tayari ilikwishaanza lakini imesimama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassari, Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Nassari kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, lakini kubwa zaidi ushirikiano wake na Wizara ya Maji katika kubainisha changamoto zinazotokea katika jimbo lake. Tunamhakikishia kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itapeleka fedha ili kuhakikisha miradi hii inakamilika na iweze kutoa matokeo na wananchi waweze kuona maji kwenye bomba hatimaye sasa nchi yetu isiwe na tatizo la *water stress*. Kwa hiyo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo tunalichukua kwa makini sana. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji ulioko katika Kata ya Rwazera ni mradi ambao ni tegemezi kwa Kata ya Kamwanga, Bugalama, Isulwabutundwe, lakini ujenzi wa mradi huu unasuasua sana, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda nami kuuona huo mradi ili wasukume pesa ukamilike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasheku Musukuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Kasheku Musukuma ameendelea kuwasiliana na Wizara ya Maji na ameendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba tunachukua hatua katika mradi huu. Sasa kwa ombi lake hili mahsusi

kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Musukuma kwenda katika jimbo lake na kuangalia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina swali la nyongeza. Mradi wa Maji wa Miji 28 Rorya, Tarime umesimama kwa muda mrefu na Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami mradi ule umekwenda kwa kusuasua sana kwa muda mrefu kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mradi huu wa kutoka Tarime – Rorya ambao awali tulitegemea mradi huu pia ukatoe huduma maeneo ya Serengeti, Mugumu kule ni kweli umesuasusa. Hata hivyo, Wizara tumechukua hatua ya kukaa na Wakandarasi wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha. Mradi huu Mkandarasi aendelee kuutekeleza ili lengo ni kwamba atakapokuwa ana-*raise certificate,* basi Serikali itaweza kumlipa kulingana na kazi atakayokuwa ameifanya. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa John John Nchimbi Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Ujenzi wa Kiwanda cha Kukoboa Kahawa – Nyasa**

**MHE. JOHN J. NCHIMBI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha kukoboa Kahawa Nyasa kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dennis Londo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba nijibu swali namba 79 la Mheshimiwa John John Nchimbi, Mbunge wa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Nyasa inazalisha kahawa aina ya *Arabica* kwa wastani wa tani 2193 kwa mwaka. Kutokana na uzalishaji huu, Mheshimiwa Rais aliona umuhimu wa kuwa na kiwanda katika eneo hili. Hivyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Nyasa imetenga eneo lililopo Kitongoji cha Ndanda, Kijiji cha Kingirikiti Kata ya Kingirikiti kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kukoboa kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili lina ukubwa wa hekta nne na lina miundombinu wezeshi kama vile barabara, maji na umeme. Aidha, eneo hili linamilikiwa na Serikali na lipo tayari kwa ajili ya uwekezaji kwa kujenga kiwanda cha kukoboa kahawa. Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kukoboa kahawa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John John Nchimbi, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza baada ya kupata majibu haya mazuri. Swali la kwanza; Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais anapokuwa ametoa ahadi na pia ahadi hiyo inapokuwa imewekwa katika Ilani ya chama ni ahadi ambayo inatakiwa itekelezwe na Serikali na siyo kuwasubiri *Private Sectors* ambao wanaweza wakaja muda wanaopenda wao na ikapita hata miaka mitano inayotarajiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je Serikali haioni umuhimu wa kukusanya wataalam wake waende kuwasaidia wananchi wa wilaya yangu kuwezeshwa kusaidiwa kupata mikopo ambayo ni ya riba nafuu kutoka maeneo ya Serikali kama *Agricultural Bank*, *TIB* na Benki ya Ushirika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa John John Nchimbi kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Ni kweli ninaungana naye Mheshimiwa Rais anapotoa ahadi jukumu letu sisi kama Serikali ni utekelezaji wa ahadi hiyo. Kimsingi Serikali imeshaanza utekelezaji wa ahadi hiyo na ndiyo maana Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa imeshatoa miche 2,000,000 kwa wakulima wa kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo wameshanunua eneo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda, uzalishaji wa kahawa Nyasa umeongezeka na ndiyo maana kuna umuhimu wa ujenzi wa kiwanda. Ukisoma Dira ya 2050 inazungumzia ushirikishwaji kwa maana tunazungumzia Uchumi Jumuishi na Sekta Binafsi ina mchango wa 70%. Ndiyo maana Serikali kupitia taasisi za fedha, kupitia wadau kama Vyama vya Ushirika tunaendelea kuhamasisha kuwekeza katika viwanda vya kati ili kushiriki kikamilifu katika dhana ya Uchumi Jumuishi kama nguzo ya Dira ya 2050 inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la uwezeshaji wa Serikali ninaungana na Mheshimiwa Mbunge. Ndiyo maana sisi kama

Serikali tumeshatoa mwongozo kwa halmashauri kuona kwamba mazao ambayo yanatokana na maeneo husika tunaenda kuyajengea uwezo Vyama vya Ushirika. Pia kuomba fedha maalum kupitia bajeti ya Serikali kuona uwezeshaji wa ujenzi wa viwanda hivyo ili kuongeza mnyororo wa thamani, kuongeza thamani ya mazao, kupunguza gharama ya uzalishaji na kuchochea uzalishaji katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ibrahim Shayo, swali la nyongeza.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, Moshi ni Mji ambao ulikuwa na viwanda vingi sana, lakini viwanda vile sasa hivi vimekufa na vimechukuliwa na wawekezaji na wale wawekezaji hawawekezi wamevichukua tu kama magofu. Ni lini Serikali itaweza kuwanyang'anya viwanda vile na kuvifanyia kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilivitoa viwanda hivi kwa wawekezaji kwa nia ya uzalishaji. Mkataba wa makabidhiano wa viwanda hivi kwa hao wawekezaji unawataka wauheshimu kwa maana ya kuendelea na shughuli za uzalishaji. Ndiyo maana kwa Moshi kuna Kiwanda cha Kilimanjaro *Machine Tools* ambacho mimi mwenyewe nilikuwa pale wiki mbili zilizopita kazi za uzalishaji inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo mengine ambayo wawekezaji wamepewa viwanda hivi na havizalishi, rai yetu ni moja tu kuwaambia kwamba, aidha warudi kwenye uzalishaji ama Serikali itachukua hatua ya kuwapatia viwanda hivyo wawekezaji ambao wana nia ya dhati ya kushiriki katika ujenzi wa Dira ya 2050 kwenye Uchumi wa Viwanda na Uzalishaji kwa ajili ya shughuli ya kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Ujenzi wa Barabara ya Tanganyika hadi Uvinza**

**MHE. JANETH P. PINDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Barabara ya kutoka Wilaya ya Tanganyika hadi Uvinza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu ambapo ujenzi kwa sehemu ya kwanza ya Mpanda – Vikonge kilomita 37.65 umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya pili ya Vikonge – Luhafwe kilomita 25 unaendelea na umefikia 70% na ujenzi wa sehemu ya tatu ya Luhafwe – Mishamo kilomita 37.35 unaendelea na umefikia 30.6%. Kwa sehemu iliyobaki ya Mishamo – Uvinza urefu kilomita 95.6, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH P. PINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa katika barabara hii ina vipande na Wakandarasi wa kutoka Vikonge – Luhafwe, lakini kutoka Luhafwe – Mishamo,

wakandarasi hawapo *site*. Je, ni lini Serikali itatoa pesa kwa ajili ya ukamilishaji wa kipande hiki cha barabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Barabara hii kutoka Katavi – Uvinza na Serikali imeweka utaratibu au mpango wa kuunganisha barabara. Je, ni lini Serikali itakamilisha barabara hii ili kuondokana na adha ya usafiri kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi pamoja na Kigoma? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipande hiki cha Luhafwe – Mishamo ambacho kinajengwa na *CHICO* kulikuwa na changamoto kidogo, lakini tumeshaitatua na Mkandarasi anarudi *site* kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la barabara ya kuunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma pamoja na Mkoa wa Rukwa. Kutoka Kibaoni – Stalike, Mkandarasi alikuwa anasuasua tayari ameshalipwa malipo yake na yuko *site* anaendelea ili kuunga Kibaoni – Mlele – Stalike. Nimpe Mheshimiwa Mbunge habari njema kabisa kwamba, tunaenda kuunga Katavi na Kigoma kuanzia Mishamo – Uvinza, kandarasi itatangazwa muda siyo mrefu kukamilisha hizo kilomita zote 95. Muda siyo mrefu tunakwenda kutangaza hiyo tenda kila kitu kipo tayari. Kwa hiyo tutakuwa tumeunganisha kutoka Kibaoni – Uvinza – Mishamo – Mpanda hiyo ndiyo kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuiunganisha mikoa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona muda wetu ukiwa umeshakwisha maswali bado mengi. Mheshimiwa Haidary Sumry, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Barabara ya Stalike – Mpanda mpaka Mpanda Ndogo imejengwa mwaka 2012, lakini bado wananchi wa maeneo

hayo hawajalipwa fidia. Ninauliza ni lini wananchi hawa ukizingatia muda huo kuanzia 2012 watalipwa fidia yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama afuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema toka mwaka 2012, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge tuweze kuonana naye ili kujua changamoto ni nini, kwa sababu 2012 ni muda mrefu. Nimuombe tu Mbunge baada ya hapa tuweze kuona ni wananchi wapi ambao hawajalipwa na wanastahili hayo malipo yake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swali lake.

Na. 81

**Ujenzi wa Barabara ya Ipole – Rungwa na Sikonge**

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Ipole – Rungwa na Sikonge – Kipili kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Amos William Maganga, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Ipole –

Rungwa inayounganisha Mikoa ya Tabora na Mbeya umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Sikonge – Kipili Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Baada ya Usanifu kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja tu la nyongeza. Kwa vile Barabara ya kutoka Ipole – Rungwa imekuwa kwenye ahadi ya Serikali kwa kipindi kirefu sasa na barabara hii imekuwa ni sehemu ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Je, Serikali haioni umuhimu kwamba sasa fedha zipatikane na barabara hiyo ianze kutengenezwa na impendeze Mwenyezi Mungu hii barabara ikamilike hata kabla ya mwaka 2030?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Mbunge kwamba hii barabara imeshafanyiwa usanifu na kwa sisi kama Serikali imekuwa ni moja ya barabara kubwa na Barabara Kuu *(Trunk Road)* ndefu ambayo haijajengwa kwa kiwango cha lami. Tunavyoongea sasa hivi, Serikali inatafuta chanzo sahihi kwa maana ya kuijenga hiyo barabara kuanzia Ipole – Rungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakubaliana nami, lakini kutoka Rungwa – Singida ambako tumeshaanza na kutoka Rungwa – Makongorosi ili kuiunga Tabora, Singida na Mkoa wa Mbeya kwa kiwango cha lami. Mpango upo mkubwa wa kutafuta chanzo cha uhakika ili kuikamilisha barabara hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 82

**Ujenzi wa Barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Korogwe**

**MHE. CHARLES M. NJAMA** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa kilomita 10 itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya *Old* Korogwe ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Mabokweni yenye urefu wa kilometa 127.69. Mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Old Korogwe – Kwamndolwa yenye urefu wa kilomita 10 upo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Mara baada ya kumpata Mkandarasi ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mhando, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Je, kilomita 2.45 za kutoka Korogwe *Girls* – Stesheni zitafanyiwa upanuzi ili kuendana na ujenzi wa barabara mpya kutoka *Old* Korogwe – Kwamndolwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoanza hii barabara ni kuanzia *Old* Korogwe – Kwamndolwa. Nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Tanga kwamba kwa kuwa hii barabara inaenda Korogwe *Girls* waende wakaiangalie na kuona kama imefanyiwa usanifu ama kama haijafanyiwa usanifu iweze kufanyiwa usanifu ili tuweze kuunga hizo kilometa 2.5 kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Itigi, sasa aulize swali lake.

Na. 83

**Kupandisha Bei Zao la Dengu**

**MHE. YOHANA S. MSITA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kupandisha bei ya zao la dengu baada ya bei kuporomoka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza Mkakati wa kusambaza mbegu bora za dengu nchini ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kusambaza kilo 400 za mbegu mama za dengu kwa wakulima wa Halmashauri ya Itigi zenye uwezo wa kuzalisha tani nne za mbegu bora. Lengo ni kuhakikisha wakulima wanaongeza tija na uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa na kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vilevile inaendelea na taratibu za kufungua soko la dengu Nchini Malaysia. Upatikanaji wa soko hilo utaruhusu zao la dengu kuingia rasmi katika soko la Malaysia. Hatua hiyo itaongeza wigo wa masoko na hivyo kuimarisha bei kwa mkulima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, swali la nyongeza.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itapeleka wataalam kwenye Jimbo la Itigi kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu wa dengu ili waweze kuongeza tija zaidi kwenye zao la dengu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kwa ajili ya kwenda kuongea na wale wakulima kwa sababu wana mambo mengi sana?  Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nimpongeze Mheshimiwa Yohana Msita, Mbunge wa Itigi, ameanza vizuri kazi yake ya Ubunge, ni Mbunge mpya lakini unauona umakini wake. Nimthibitishie tu kwamba, moja, Serikali tutaendelea kupeleka wataalamu, lakini wale waliopo sasa hivi maafisa ugani, tutaongeza msukumo ili kuhakikisha wanafanya hiyo kazi kama ambavyo imekusudiwa kwa sababu lengo letu ni kuongeza tija ya zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mimi niko tayari kuongozana naye katika Jimbo la Itigi, uzuri hapa siyo mbali tunaweza tukaenda na kurudi. Kwa hiyo, niko tayari muda wowote ambao yeye Mheshimiwa Mbunge atakuwa na hiyo ratiba

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.  Tunaendelea na Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui, sasa aulize swali lake.

Na. 84

**Madai ya Wakulima wa Tumbaku Uyui**

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR** aliuliza:-

Je, Serikali inawasaidiaje wakulima wa tumbaku kupitia *AMCOS* kulipwa fedha jumla ya dola milioni 1.2 wanazodai kwenye kampuni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika msimu wa 2024/2025 wakulima wa tumbaku waliuza kilo milioni 185.7 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 475.45. Kati ya kiasi hicho, dola za Marekani milioni 470.95 sawa na 99.05% zimeshalipwa. Aidha, kiasi kinachodaiwa ni dola za Marekani Milioni 4.51 sawa na 0.95%. Kati ya kiasi kinachodaiwa, dola za Marekani 298,007.23 ni kutoka Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufuatilia madai ya wakulima wote wa zao la tumbaku ikiwemo wakulima kutoka Wilaya ya Uyui ili kuhakikisha madai yote ya wakulima wa zao la tumbaku hiyo yanalipwa kabla ya mwezi Machi, 2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shaffin, swali la nyongeza.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri sana kwa majibu mazuri ambayo kwa kweli yanatia moyo. Ninaomba niulize swali la kwanza; Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo ambalo linaweza kutokea ya bei ya tumbaku kushuka na kwa kuzingatia kwamba wakulima tayari walishalima tumbaku yao, walishafulia mabedi na tayari walishaweka mbolea: mbolea ambazo ni *NPK, CAN* na *UREA* ambazo mpaka sasa hazijapewa ruzuku?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali itaweka lini mpango mzuri wa utaratibu rasmi wa ushirikishi na kuruhusu kampuni za tumbaku kwenda kujinadi kwa wakulima ili mkulima awe na haki ya kuchagua kampuni ambayo ana maslahi nayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui, ni moja ya Wabunge makini sana, ambaye anafanya kazi nzuri katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu kwamba, moja, sisi kama Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakabiliana na anguko la bei katika mazao yote nchini ikiwemo tumbaku. Moja ya jambo kubwa ambalo tunalifanya ili kutoa ruzuku ya pembejeo, maana yake ni kumpunguzia mkulima gharama ili azalishe kwa gharama ya chini na akishazalisha aweze kuuza katika bei inayohusika, hata panapotokea anguko la bei maana yake walau mkulima anaweza akapata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunaendelea kujenga viwanda vya kuchakata haya mazao vikiwemo viwanda vya kuchakata tumbaku. Yote ile ni kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama. Tuna viwanda ambavyo, *AMCOS* zinakaribia kujenga vile viwanda vya vifungashio. Lengo lote lile ni kutaka kumpunguzia mkulima bei ya zao lake. Kwa hiyo, kitu ambacho nikuthibitishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba moja ya mkakati wa Serikali ni kuhakikisha mazao yote yanaingia katika mpango wa ruzuku, lakini kwa awamu na kwa kuzingatia mahitaji ya kila wakati, ikiwemo hili eneo ambalo ameliainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa kampuni kwenda kujinadi, kwa sababu tumekuwa na kila mwaka tuna mkutano wa wadau wa tumbaku na jambo hili lilishakuwa linafanyika hapo nyuma kabla ya kubadilishwa mfumo wake, basi sisi kama Serikali tumelipokea na katika kikao kinachokuja kwa wadau tutalifikisha pale.

Wadau watalijadili na yale watakayokubaliana, sisi Serikali tutakuwa tayari kuyatekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Thomas Mvano Alan, Mbunge wa Kakonko, sasa aulize swali lake.

Na. 85

**Hitaji la Soko la Uhakika la Muhogo**

**MHE. ALAN T. MVANO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wakulima wa zao la muhogo Kakonko wanapata soko la uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza zao la muhogo nchini kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji, kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya bidhaa za muhogo na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuchakata muhogo ili kuongeza thamani ya zao hilo. Moja ya eneo la kimkakati katika kuendeleza muhogo ni Halmashauri za Wilaya ya Kakonko na Kibondo, Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026, imetenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya masoko, kukaushia, kuchakata na kuhifadhi muhogo katika Halmashauri ya Kakonko. Tayari Wizara imefanya tathmini ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo pamoja na kuandaa usanifu, michoro na gharama za awali kwa ajili ya kuanza kumtafuta mkandarasi wa ujenzi. Wizara inaamini taratibu zote zitakamilika mapema ili kuhakikisha wakulima wanaanza kuongeza thamani ya zao la muhogo, kupunguza upotevu baada ya mavuno na kuimarisha upatikanaji wa masoko kwa wakulima. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alan, swali la nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nipongeze na nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa, Mkoa wa Kigoma umekuwa ukizalisha zaidi ya tani milioni moja za muhogo kwa mwaka. Wilaya ya Kakonko imekuwa ikizalisha zaidi ya tani 184,000 na Wilaya ya Kibondo mathalani zaidi ya tani 174,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza la nyongeza; je, Wizara ya Kilimo ina mpango gani wa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kupanua wigo wa masoko ya zao hili la muhogo ndani ya Wilaya ya Kakonko na Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa bei ya zao la muhogo ilianguka sana, kutoka kuuzwa shilingi 800 hadi 1,000 kwa kila kilo moja kwenda kuuzwa shilingi 150 hadi shilingi 200. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru wananchi ambao ni wakulima wa zao la muhogo ambao hadi sasa wameshindwa kuvuna zao hilo, kwa sababu hata wakivuna hawawezi kuuza kwa bei iliyoko sokoni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia bwana Alan Mvano ameanza vizuri kuwafuatilia wananchi wake wa Jimbo la Kakonko na ninaomba nimjibu kwamba, moja sisi kama Serikali, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara tumekuwa tukifanya kazi kwa ukaribu sana. Ndiyo maana utaona katika moja ya hatua ya awali sisi ambayo tunaifanya sasa hivi ni jukumu la kujenga soko katika Halmashauri ya Kakonko. Wizara ya Viwanda na Biashara itakuja ku-*complement* jambo hili kwa kujenga viwanda ambavyo vitasaidia wakulima katika eneo hilo. Kwa hiyo, huo ni mpango ambao upo na ni endelevu kwa muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa Serikali baada ya bei kushuka; mpango wa Serikali ndiyo huo ambao tumeainisha kwamba kwa nini tunajenga soko. Lengo ni kuhakikisha kwanza moja, tunaongeza thamani, ndiyo maana utaona tumeainisha hapa kwamba tunataka wananchi waongeze tija kwa kuchakata yale mazao yao yaweze kudumu kwa muda mrefu ambapo tunaamini kwamba ukishakausha muhogo badala ya kuuza katika bei ya chini unaweza ukakaa kwa muda mrefu na ukapata bei ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Serikali, jambo hili tunalifahamu na tunalifanyia kazi kwa ukaribu kabisa. Kwa hiyo, tu nimthibitishie tu Mbunge kwamba moja ya kazi kubwa ambayo tutaendelea kuifanya katika eneo hili ni kuboresha haya mazingira ili bei ya muhogo isiweze kushuka kama ambavyo ameainisha hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Mussa Godfrey Mbuga, Mbunge wa Kisesa, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Mbinu za Kukabiliana na Tembo – Kisesa**

**MHE. MUSSA G. MBUGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mbinu gani mpya za kukabiliana na tembo vijiji vya Ng'hanga, Mwambongo, Matale, Longalonhinga, Sakata, Nyanza na Banhya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuboresha na kuibua mbinu mpya, Serikali imeendelea kutumia teknolojia mbalimbali ikiwemo uzio wa umeme kwa ajili ya kuimarisha udhibiti wa tembo wanaoingia kwenye makazi na mashamba ya wananchi. Aidha, Serikali kupitia wadau wa uhifadhi ina mpango wa kuweka uzio wa umeme kuzunguka mpaka wa Hifadhi ya Pori la Akiba Maswa kwa upande wa magharibi unaopakana na makazi ya wananchi utakaozuia tembo kutoka nje ya hifadhi na kuleta madhara kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, Serikali imeandaa Mkakati mpya wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori wa miaka 10 kuanzia 2025/2026 hadi 2035/2036. Mkakati huu utatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara za kisekta ikiwemo: TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuhakikisha kuwa jitihada za kupunguza changamoto hii zinafanyika kwa pamoja na kwa ufanisi zaidi. Aidha, ushirikiano mpana wa Wizara mbalimbali unaifanya nchi kuwa na mfumo thabiti ulioratibiwa na unaozingatia maslahi ya watu na uchumi wa Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, swali la nyongeza.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuzingatia kwamba Jimbo la Kisesa hasa Kata za Mwasengela na vijiji vyake, Sakasaka na vijiji vyake, Mwakisandu na vijiji vyake na Mbugayabanghya ni lango la tembo kuingia katika makazi ya watu. Kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa inaahidi kuwapelekea gari kwa ajili ya kufanya doria Wananchi wa jimbo la Kisesa hususani kata nilizotaja, lakini haijawahi kutekelezwa kwa muda mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka gari kwa ajili ya lindo, kwa ajili ya Jimbo la Kisesa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana nami Jimboni Kisesa ili ajionee madhara yanayosababishwa na tembo pamoja na uharibifu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Musa, ninaomba kwanza nimpongeze sana kwa namna anavyofuatilia changamoto za wananchi wake. Niwaambie Wana-Kisesa wamechagua mtu sahihi, kwa wakati sahihi na kwa nafasi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna changamoto ya gari, lakini ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mapema tu ndani ya mwaka huu wa fedha, Serikali itapeleka gari kwa ajili ya kutoa huduma katika jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni suala la wajibu kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika eneo lake na kukagua na kuangalia changamoto zilizopo ili tuzipatie utatatuzi wananchi wetu waendelee kuwa na furaha ya uwepo wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 87

**Ushiriki wa Wanawake Wajasiriamali kwenye Dira ya Maendeleo 2050**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanashiriki moja kwa moja kwenye utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali katika kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 hususani Nguzo ya Kwanza ya Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani na Nguzo ya Pili ya Uwezo wa Watu wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hiyo ni pamoja na: kupunguza mkwamo na kupanua upatikanaji wa mitaji na masoko kwa wanawake ili kuongeza uzalishaji; kubainisha na kutekeleza jitihada zenye lengo la kuwawezesha wanaume na wanawake kutambua na kutumia fursa za kiuchumi; utekelezaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi; na kuwezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, teknolojia na viwanda ili biashara zao zikue na kuchangia uchumi wa Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mzuri ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; ni kwa namna gani elimu na mafunzo yanayotolewa kwa wanawake wajasiriamali yanakidhi mahitaji ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali inahakikishaje majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi yanakuwa siyo miradi ya muda mfupi, lakini yanakuwa endelevu ili kukidhi na kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Janeth amekuwa mstari wa mbele sana kuhakikisha vikundi na majukwaa mbalimbali yanaweza kufanya kazi kwa usahihi. Kwa Mkoa wake wa Dar es Salaam amekuwa akifanya mara nyingi na amenishirikisha hata hapo nyuma kwa kweli anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna gani elimu na mafunzo yanatolewa na Serikali kuendana na uhitaji wa Dira 2050, hakika sisi kama Wizara tunapaswa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais ametupa nguzo ya kuona kwamba tunahakikisha kwenye Dira ya Taifa, ile nguzo ya kwanza, uwezeshaji wa wanawake na wanaume kiuchumi tunaisimamia vizuri. Katika hili tunafanya mafunzo mbalimbali na tunashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuona kwamba mafunzo haya yanakamilika. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inaingia kwa sababu Waheshimiwa ma-*DC* na ma-*RC* ndiyo walezi wa haya majukwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kule elimu inapatikana kupitia Maafisa Maendeleo ya jamii wetu katika halmashauri. Vilevile, tayari tuna jukwaa ambalo la kidijiti. Mheshimiwa Waziri Dorothy Gwajima anaendesha mikutano mitandaoni na wiki iliyopita tayari

tumeweza kuzindua Sekretarieti ya Taifa ya majukwaa haya. Lengo ni kuona kwamba tunashirikiana sasa na hawa Sekretarieti kuona elimu sahihi inaendelea kuwafikia wengi na kuhakikisha mahitaji ya dira yanaweza kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukuliaje majukwaa haya katika uendelevu wake. Sisi kama Wizara tumejipanga kikamilifu kuandaa mwongozo ambao unaelezea namna ya uundwaji wa haya majukwaa, lakini vilevile uendeshaji wake. Majukwaa haya yanajengwa na vikundi na vikundi hivi viko pale halmashauri. Maafisa maendeleo ndiyo wetu wa jamii wanavisimamia kuhakikisha vinaweza kuendana na mwongozo uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uendelevu unakuwepo wa uhakika kwa sababu taratibu na namna ambavyo tumeweka katika mwongozo inavibeba hivi vikundi na inakuwa na manufaa zaidi kwa sababu, kwenye kikundi wanakutana wanawake wenye elimu mbalimbali: mwingine ni mzuri katika kuongea; mwingine ni mzuri katika kutafuta masoko; na mwingine ni mzuri katika kuona uboreshaji wa bidhaa aliyonayo. Kwa hiyo, pale kwenye vikundi kwa umoja wao, wanakwenda kuona kwamba sasa wanasogezana mbele na uendelevu unakuwa wa uhakika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante kwa majibu mazuri kwa maswali la Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 88

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Nyabiyonza na Nyakakika – Karagwe**

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* Tarafa za Nyabiyonza na Nyakakika kwani kuna umbali mrefu toka Chuo cha *VETA* Kayanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu Hafidh, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Wilaya ya Karagwe, Serikali imejenga Chuo cha *VETA* cha Wilaya kilichopo Kayanga ambacho kina mabweni na kinaendelea kutoa mafunzo. Kwa sasa wanachi wa Tarafa za Nyabiyonza na Nyakakika wanaweza kuendelea kutumia chuo hicho kwa kuwa kinatoa huduma ya malazi katika mabweni yaliyojengwa kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka umbali mrefu.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshuruku Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa Wanakaragwe, ninaamini ombi langu kutokana na umbali wa tarafa hizi mbili kwenda kwenye Kituo cha *VETA* Kayanga Mjini, Wizara itaendelea kulifanyia kazi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Chuo cha *VETA* pale Kayanga Mjini kipo katikati ya mji na hakina uzio. Je, ni lini Serikali itatujengea uzio?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Chuo kina uwezo wa ku-*accommodate* wasichana 52, lakini hivi sasa chuo kina wasichana

125. Je, Serikali itatujengea lini bweni lenye uwezo wa kuwa-*accommodate* wasichana wote? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Bashungwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza kwa kufuatilia mambo yanayohusiana na jimbo lake, lakini Serikali inatambua kwamba, uhitaji wa uzio kwa Vyuo vya *VETA* ni kwa vyote vile ambavyo vimejengwa vya wilaya. Serikali inafanyia kazi kwa awamu suala hili ambapo Chuo cha *VETA* cha Kayanga ni miongoni mwa vyuo ambavyo vipo katika mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; ninakubaliana na yeye kwamba, bweni lile ambalo lipo sasa hivi la wasichana halitoshi, lakini hatua za dharura zimechukuliwa. Kuna jengo moja la Chuo cha Kayanga limefanyiwa ukarabati, kwa ajili ya kuwaweka wasichana wetu na ujenzi umeshakamilika. Fedha ya kupeleka *furniture* imetengwa kwa hiyo, muda wowote *furniture* zitapelekwa na watoto wataanza kutumia bweni hilo ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua wasichana 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeweka mpango wa muda mrefu wa kujenga jengo la wasichana ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua wasichana 200. Kwa hiyo, naamini wasichana wa Wilaya ya Karagwe watakuwa wapo salama na watapata mafunzo ipasavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu kwa

upande wa Serikali. Ninaomba nilete matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo.

Kwanza ni wageni 36 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Taasisi ya Ahmadiyya Muslima Jamaat Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; tunao wageni nane wa Bunge kutoka Bunge la Zambia; tunaye Mheshimiwa Malungo Chisangano ambaye ni Mheshimiwa Naibu Spika wa kwanza wa Bunge la Zambia; Ndugu Charles Haambote, *Director, Social Commetees and Secretary to the Delegation;* tunaye Ndugu Lombe Musonda, *Protocal Officer* na Ndugu Muka Kazela *ADC*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni hao wameambatana na mwenyeji, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika ambaye ni Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, ahsante sana.

Wageni sita wa Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar ambao ni Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Ndugu Elijah Mwandumbya - Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia uchumi; Dkt. Amina Msengwa - Mtakwimu Mkuu wa Serikali; Ndugu Moses Ndulle - Mkurugenzi wa Idara ya Mipango; Ndugu Vicky Jengo - Kamishna Msaidizi wa Bajeti; Ndugu Mbayane Saruni - Kamishna Msaidizi Idara ya Sera; na Ndugu Saada Alluya - Meneja Ushauri wa Sera za Kodi, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni 13 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; yupo Dkt. Tausi Kida ambaye ni Katibu Mkuu; Dkt. Fred Msemwa - Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango; yupo Ndugu Gilead Terri - Mkurugenzi Mtendaji wa *TISEZA* na Dkt. Mursali Milanzi - Naibu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango ya Kitaifa.

Pia yupo Dkt. Linda Ezekiel - Naibu Katibu Mtendaji Ufuatiliaji na Tathmini; Dkt. John Mduma - Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *WCF;* na Dkt. Riziki Nyello - Mhadhiri Chuo cha Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Yisambi Mwaishemele ambaye ni *Program Director - Insights and Partnership – Gatsby Africa* kutoka Afrika; Ndugu Angela Shayo - Mkurugenzi Mipango ya Kitaifa na Ndugu Felista Fatugubonye - Mkurugenzi wa Mipango ya Bajeti. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Mkumbo ni kama ifuatavyo; wapo wadau wa maendeleo, wapo wajumbe wa timu ya uandishi wa mipango, Wakuu wa Idara na Vitengo Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Watendaji Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni wa Mheshimiwa Yohana Stephen Msita ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Jijini Dodoma, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, watumishi wachezaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai wakiongozwa na Viongozi wa Chama cha Netiboli Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa John Nchimbi ambao ni Ndugu Brighton John, mshereheshaji kutoka Jijini Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni Madaktari, Wenyeviti wa Mtaa na Wafanyabiashara kutoka Tarime, Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa Fargason Aron Nkingwa ambao ni wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliolitembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; wageni wanne kutoka *Sanyorina Africa Limited* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanachama 22 wa Umoja wa Wauza Nafaka kutoka Manispaa ya Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 20 wa Shahada ya Kwanza ya Maendeleo ya Miji na Usimamizi wa Mazingira wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Saashisa Mafuwe.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninasimama kwa Kanuni ya 56 kuomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa nina swali la msingi, niliuliza maswali ya nyongeza mawili. Kwenye swali langu niliuliza kwamba Serikali ni lini itajenga *theatre* ya upasuaji katika Hospitali ya Wilaya ya Hai?

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu niliyopewa na Mheshimiwa Naibu Waziri yalionesha kwamba Hospitali ya Wilaya ya Hai inayo *theatre* ya upasuaji na kwamba, Mheshimiwa Mbunge hana taarifa na kumtaka Mkurugenzi na *DMO* wanipe taarifa, ilihali mimi nina taarifa sahihi na bahati nzuri, ninatembea sana kwenye hospitali hiyo na ninaifahamu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali hiyo ilikuwa kituo cha afya ikapandishwa hadhi ikawa hospitali ya wilaya kwa hiyo, haijawahi kujengwa jengo la upasuaji. Sasa hivi nimeongea na *DMO,* nimeongea pia na *RMO,* imejengwa nje ya Wilaya ya Hai. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri akafikiri ipo Hai. Mpaka sasa hivi hatuna jengo la upasuaji Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako ili niweze kupata majibu sahihi ya Serikali na kuzingatia kwamba Wilaya ya Hai tunahitaji jengo la upasuaji na siyo kwamba mimi sina taarifa, taarifa ninazo vizuri sana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, amenukuu Kanuni ya 56, kwa maana ya Mwongozo. Kanuni ya Mwongozo ni Kanuni ya 79 kwamba, leo alikuwa na swali la msingi, Swali Namba 70, limejibiwa vizuri ila ana changamoto kwenye swali la nyongeza. Sasa Kiti kitarejea majibu ya nyongeza na baadaye kitatoa mwongozo aliouomba. Ahsante sana.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninasimama chini ya Kanuni ya 79 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita kwenye mjadala wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wapo Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, walitoa maoni yao juu ya mtizamo wao kuhusu rushwa na ufisadi vinavyoweza kuwa kikwazo katika kufanikisha maono ya Mheshimiwa Rais katika hotuba yake. Walipendekeza pia, umuhimu wa uhuru wa vyombo vya dola pamoja na kuongeza uwajibikaji wa vyombo hivyo, ili maono hayo yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kauli hizo tumesoma kwenye vyombo vya habari, likiwemo Gazeti la Mwananchi la tarehe 31 Januari na vyombo vingine mbalimbali ya habari vikiripoti kwamba, Waheshimiwa Wabunge hao wameitwa TAKUKURU. Gazeti la Mwananchi limemnukuu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwamba, lugha aliyoitumia ni atawafuata, kwa ajili ya kupata taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii licha ya kuonekana kwamba, ina nia njema, lakini ina hatari ya kuweka rejea, kwa maana ya *precedent* kwamba vyombo vya dola na mamlaka nyingine, kinyume na Ibara ya 100(1), ikisomwa sambamba na Kifungu cha Tatu cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ambavyo hivi vyote kwa pamoja vinawapa Wabunge uhuru wa kujadili, vinazuia mamlaka nyingine zozote zile kuhoji yanayotendeka ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba Mwongozo, utuongoze kwa sababu ya kuhakikisha kwamba hatua hii haiwezi kutumika huko baadaye kuwatisha au kuwanyima uhuru Wabunge kutoa Mawazo yao. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Ado Shaibu Ado kwa Kanuni ya 79 akiomba Mwongozo wa Kiti.

Sasa Mwongozo wa Kiti; kwanza, Kanuni ya 79 naomba niisome; "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa ama haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Mheshimiwa Spika yatatolewa hapohapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Kwa kuwa jambo hili halijatokea mapema leo na kama inaruhusiwa au hairuhusiwi, sasa halijatokea leo mapema Bungeni. Kwa hiyo, Mwongozo wa Kiti ndiyo huo, hilo jambo Kiti hakina taarifa

nalo kwa sasa, basi tukipewa taarifa itafuatiliwa, lakini kwa kimsingi wa kanuni hii jambo hilo halijatokea leo mapema. Huo ndio Mwongozo wa Kiti. Nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba inayofuata, nitampisha Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN,** ***ndc*** **– KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027–2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027–2030/2031 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027; na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali Katika Muda wa Kati ya 2026/2027 hadi 2028/2029.**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, ili aweze kuwasilisha taarifa yake. Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kifungu cha 6(2)(b) cha Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango (Sura 127) na Kanuni ya 113(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako likae kama Kamati ya Mipango, ili kupokea, kujadili na kushauri kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027– 2050/2051, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027– 2030/2031 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kutoa shukrani na pongezi. Kwanza, ninamshukuru Mungu kwa kutujalia neema ya uhai, afya njema, amani na utulivu na kutupa fursa ya kukutana katika Bunge hili la Kumi na Tatu, Mkutano huu wa Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo, kupata tena heshima na imani ya Watanzania ya kuweza kuliongoza Taifa letu kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyopata kushika nafasi hiyo ya pili kwa ukubwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mkoani Singida, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua tena kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninamwahidi bidii na weledi katika kazi na utiifu kwake binafsi, kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Chama Cha Mapinduzi na kwa Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa heshima na imani kubwa waliyopata ya kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, ninampongeza sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kwanza jina lake kupendekezwa na Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, lakini pili kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, aidha ninampongeza pia Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge waliochaguliwa kutuongoza katika Bunge hili la Kumi na Tatu. Tuna imani kubwa kuwa mtaliongoza Bunge hili la Kumi na Tatu kwa busara, haki, na weledi mkubwa ili kuliwezesha kuendelea kuwa Muhimili imara wa demokrasia, uwajibikaji na utawala wa sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi na kupewa dhamana kubwa ya kuwawakilisha Watanzania katika Bunge lao na kutupatia fursa ya kutunga sheria, kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, ninayo heshima kubwa na ya kipekee sana kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ubungo, Jijini Dar es Salaam kwa kunipa heshima ya kuwawakilisha tena hapa Bungeni. Aidha ninakishukuru sana Chama Cha Mapinduzi kwa kunipa heshima ya kugombea tena katika Jimbo la Ubungo. Ninawaahidi wananchi wa Ubungo na Chama Cha Mapinduzi utumishi wenye bidii, weledi, heshima na utiifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na mbili, nnaomba nihitimishe shukrani na pongezi kwa kuwashukuru Walimu wote walionifundisha na kunilea kuanzia Elimu ya Msingi hadi Chuo Kikuu. Kwa leo wamewakilishwa na Mwalimu Said Swalehe Magema yupo hapa. Mwalimu Magema ni Mwalimu Mstaafu aliyenifundisha Shule ya Msingi Mgela iliyopo Kata ya Mtoa, Wilaya ya Iramba. Mwalimu huyu alinifundisha darasa la kwanza na baadaye Somo la Kiingereza darasa la tatu mwaka 1983, miaka 43 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mwalimu Magema ndiye aliyenileta habari za mimi kuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari mwezi Disemba, 1987, nikiwa nyumbani sina habari yoyote ya kuchaguliwa kuingia sekondari. Mwalimu Magema kwa niaba ya wenzako wote walionifundisha na kunilea na kuwafundisha na kuwalea Wabunge hawa, ahsante sana Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Kwa muda wa takribani miaka miwili, kati ya Aprili 2023 na Julai 2025, Tanzania iliingia katika mchakato wa kuandika Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo, hatua hii ilifuatia kukamilika kwa kipindi cha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo mwaka 2025 na maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuandaa dira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kuandika dira ya Taifa ulikamilika mwaka Julai, 2025 na dira mpya ilizinduliwa rasmi na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Julai, 2025 baada ya kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Dira hii itatekelezwa katika kipindi cha miaka 25 mwaka 2026/2027 hadi 2050/2051 na inajulikana rasmi kama Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu au mwelekeo wa Dira 2050 ni kuwa na Taifa jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Malengo mahsusi manne ya dira ni nchi kuwa na uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani. Maisha bora na ustawi kwa wote, Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi na jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2050, Serikali imeandaa nyenzo tatu muhimu ambazo ninaziwasilisha hapa leo Bungeni. Nyenzo hizi ni:-

(i) Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu *(Long-Term Perspective Plan – LTPP)* itakayotekelezwa kuanzia Mwaka 2026/2027 hadi 2050/2051, ambao ni nyenzo ya kimkakati itakayoongoza mipango yetu kwa kipindi cha miaka 25.

(ii) Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano *(Fourth Five Year Development Plan – FYDP4)* utakayotekelezwa kuanzia Mwaka 2026/2027 - 2030/2031, ambao unatafsiri kwa mapana Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Taifa wa Muda Mrefu katika kipindi cha muda wa miaka mitano ya kwanza.

(iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka *(Annual Development Plan – ADP)* ya Mwaka 2026/2027 ambao unatafsiri maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa na ambao ndiyo utakuwa nyenzo ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwasilishe nyenzo ya kwanza ambayo ni Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (*Long-Term Perspective Plan)* 2026/2027 hadi 2050/2051.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina historia ndefu ya kuandaa mipango ya maendeleo. Mpango elekezi wa maendeleo wa muda mrefu wa kwanza uliandaliwa mwaka 1964, ukiwa ni wa kipindi cha miaka 16 kuanzia 1964 mpaka 1980. Mpango huu ulipangwa kutekelezwa kupitia mipango ya muda wa kati mitatu: 1964 mpaka 1969; 1969 mpaka 1974; na 1975 mpaka 1980. Hata hivyo, mipango hii haikutekelezwa kikamilifu kutokana na changamoto za kiuchumi zilizoikumba dunia na nchi yetu, ikiwemo ukame na hali mbaya ya hewa, kuharibika kwa soko la mafuta duniani na vita kati ya Tanzania na Kagera ya mwaka 1978/1979. Kutokana na changamoto hizi, utekelezwaji wa mpango elekezi ulisitishwa rasmi mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1981 Serikali iliandaa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Pili wa Miaka 20 (1981

mpaka 2000). Mpango huu ulipangwa kutekelezwa kupitia mipango ya muda wa kati minne. Hata hivyo, mpango huu nao haukutekelezwa kikamilifu kutokana na majanga ya kiuchumi yaliyoendelea kuikumba dunia na nchi yetu katika miaka ya 1970 na miaka ya 1980, hali iliyolazimisha nchi yetu kujielekeza kutekeleza mipango ya muda mfupi na ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, mipango ya muda mfupi na ya dharura iliyotekelezwa ni pamoja na Programu ya Kitaifa ya Kujihami Kiuchumi *(National Economic Survival Programme)* iliyotekelezwa mwaka 1981 – 1982; Programu za Kurekebisha Uchumi *(Structural Adjustment Programmes)* zilizotekelezwa mwaka 1983 mpaka 1985; na Programu za Kufufua Uchumi *(Economic Recovery Programmes)* ambazo zilizotekelezwa kati ya mwaka 1986 hadi 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya hapo juu, Tanzania haikuwahi kutekeleza kikamilifu Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu hadi mwaka 2000 ilipozindua Dira ya Kwanza ya Taifa ya Maendeleo (Dira 2025). Hata hivyo, Dira hii haikuanza kutekelezwa mapema kutokana na kutokuandaliwa kwa mpango elekezi wa muda mrefu wa maendeleo ambao ulipaswa kutafsiri maono na matarajio yaliyomo katika dira hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ilitokana na masharti ya taasisi za kifedha duniani za *IMF* na *World Bank* ya kuitaka Tanzania kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa kupunguza umaskini yaani (MKUKUTA), ikiwa ni sehemu ya kukidhi masharti ya kukidhi vigezo yaliyowekwa kwa nchi maskini kusamehewa madeni chini ya Mpango Maalum wa Nchi Maskini zenye Madeni Makubwa yaani *(Heavily Indebted Poor Counties - HIPC)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025 na kubaini kuwa dira hiyo ilikuwa haijaanza kutekelezwa kikamilifu kama ilivyotarajiwa kutokana na kukosekana kwa mpango elekezi wa kuongoza utekelezaji wake. Kufuatia tathmini hiyo, Serikali iliandaa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Kwanza *(First Long-Term Perspective Plan)* wa miaka 15 (kuanzia

2011/2012 hadi 2025/2026), ulioandaliwa kwa ajili ya kuongoza utekelezaji dira kwa miaka 15 iliyokuwa imebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, hii ni mara kwanza kwa nchi yetu kuandaa dira na mpango elekezi kwa wakati mmoja. Hii inamaanisha kuwa, hatuna sababu ya kuchelewa kuanza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Kwa sababu nyenzo zote tunazo. Mpango wa muda mrefu tunao, Mpango wa muda wa kati tunao na tutakuwa na mpango wa mwaka mmoja. Kwa hiyo, tunataka kuchukua nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi na maelekezo yake. Ndiye Rais wa kwanza kuandaa dira na mpango elekezi wa muda mrefu na mpango wa miaka mitano kwa pamoja, nyenzo hizi tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* mpango elekezi wa miaka 15 ambao nimeueleza ulitekelezwa kupitia mipango ya muda wa kati wa miaka mitano, mitatu, ambayo tunaiita *FYDP*. *FYDP* ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2011/2012 mpaka 2015/2016*,* ukiwa na dhima ya Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi *(Unleashing Tanzania's Latent Growth Potential)*. *FYDP* ya pili ilikuwa ni mwaka *2016/17* hadi 2020/2021 ikiwa na dhima ya Kukuza Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu *(Nurturing Industrialisation for Economic Transformation and Human Development)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti*, FYDP* ya tatu tulitekeleza ambayo ndiyo tunamaliza nayo ni 2021/2022 hadi 2025/2026 iliyokuwa na dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu *(Realising Competitiveness and Industrialisation for Human Development)*. Huu ndiyo mpango ambao tunamaliza nao na utekelezaji wake unaisha rasmi tarehe 30 Juni, 2026 ili kutoa nafasi kwa mpango mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini iliyofanywa je, utekelezaji wa mpango elekezi wa muda mrefu wa miaka 15 ambao nimeueleza ulionesha mafanikio mbalimbali, niyataje machache tu, mawili. Mafanikio haya ni pamoja na kukua kwa pato la Taifa kwa wastani wa

asilimia 6.2 kwa miaka 20 mfufulizo kati ya mwaka 2002 na 2024 ikionesha kwamba uchumi wetu ulikuwa na ustahimilivu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fanikio la pili ni kuongezeka kwa wastani wa pato la mtu mmoja mmoja kutoka Dola za Marekani 453 mwaka 2000 hadi kufikia Dola 1,271 mwaka 2024. Kwa hiyo, tumepiga hatua kubwa katika miaka hiyo 20. Pato la Taifa la mtu mmoja mmoja kwa nchi yetu Dola 453, leo tunazungumzia 1,271 na kwa kweli *projection* za *IMF* zinaonesha kwamba uchumi wetu kwa mwaka huu utakuwa umekua kufikia Dola za Kimarekani bilioni 95. Hii itatupeleka kwenye *per capital* ya Dola za Kimarekani 1,415.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi kubwa imefanyika lakini ukitaka kusisitiza hilo ni kwamba mwaka 2000 Tanzania kuitafuta ilikuwa uende kuitafuta miongoni mwa nchi maskini zaidi duniani 10, leo hii Tanzania unaitafuta kwenye miongoni mwa nchi zenye uchumi mkubwa 10 katika Afrika hii. Kwa hiyo, kutoka chini kule 10 kwenda huku juu 10 kazi kubwa imefanyika katika miaka hiyo 20 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hali ya ubora wa maisha iliimarika zaidi katika kipindi cha utekelezaji wa *LTPP* 2025 na inathibitishwa na kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kwa Mtanzania. Mwaka 2000 Mtanzania alikuwa anaishi kwa wastani wa umri wa miaka 51, mwaka 2022 tuliongezeka na kuanza kuishi kwa wastani wa umri wa miaka 66. Tafiti zinaonesha kwamba ilipofika mwaka jana, wastani wa kuishi kwa mtanzania ni miaka 68.3. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba hali ya ubora wa maisha inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025 na *LTPP* yake ilibainisha changamoto kadhaa zilizosababisha kutokufikiwa kikamilifu kwa malengo yaliyowekwa. Changamoto hizi ni pamoja na tija ndogo ya uzalishaji katika kilimo; kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani; kasi ndogo ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; upungufu na udhaifu wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira 2050 inalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuweka msingi wa kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Dira iliyopita, pamoja na kuibua fursa mpya zitakazoisukuma mbele zaidi nchi yetu katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kuelekea mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwelekeo wa Jumla wa Mpango Elekezi 2050; Mpango Elekezi umeainisha malengo mahsusi na afua kwa kuzingatia shabaha na vipaumbele vilivyobainishwa katika Dira 2050. Kwa kuzingatia kasi kubwa ya ongezeko la watu nchini na athari zake katika upatikanaji wa ardhi, huduma za jamii na miundombinu na kwa kuzingatia haja ya kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kukuza uwekezaji nchini, Mpango Elekezi umeweka mkazo maalum katika mambo sita yafuatayo: -

(i) Upangaji miji endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira;

(ii) Ushirikishwaji mpana katika kupanga mipango ya maendeleo;

(iii) Kupanua na kuongeza ubora wa huduma za jamii;

(iv) Kuongeza tija katika kilimo, uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma kwa kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia (ikiwemo matumizi ya dijitali), ubunifu na uongezaji thamani mazao mbalimbali;

(v) Kuweka mazingira rafiki na yanayotabirika ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi;

(vi) Kufanya mageuzi katika mfumo wa utawala na mabadiliko ya utamaduni na mitazamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Falsafa ya Maendeleo ambayo tunakwenda nayo. Msingi wa Mpango Elekezi na Dira ya Taifa ya

Maendeleo inalenga kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi kwa wote, lenye haki na linalojitegemea. Katika kujenga Taifa lenye ustawi kwa wote, Dira inalenga kukuza pato la Taifa na pato la mtu mmoja mmoja kwa kuzingatia usawa wa fursa kwa wote. Katika kujenga Taifa linalojitegemea, Dira inaelekeza kutumia rasilimali za Taifa kimkakati na kuwa wabunifu katika kuvunja mnyororo wa utegemezi huku tukizingatia na kutumia fursa za utengamano wa kikanda na jumuiya ya kimataifa, bila kujitenga na dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga Taifa jumuishi, Dira 2050 na Mpango Elekezi inaelekeza kuhakikisha kwamba fursa sawa kwa wote na kwa makundi yote bila kujali hali zao. Aidha, katika kujenga Taifa lenye haki, Dira 2050 inaelekeza kuzingatia utawala wa sheria, usawa mbele ya sheria na uwajibikaji katika muktadha wa demokrasia. Kwa msingi huo, falsafa ya Mpango Elekezi imejikita katika maendeleo ya watu *(people-centred development)*. Mpango Elekezi unazingatia njia mtambuka za uzalishaji, ikihusisha uwiano wa ushirikiano katika uwekezaji kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fursa, Shabaha na Afua za Mpango Elekezi 2050. Mpango Elekezi 2050 umetambua kuwa nchi yetu ina fursa nyingi zinazotokana na jiografia na uwepo wa rasilimali za asili ambazo tukizitumia ipasavyo zitachangia sana katika kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050. Rasilimali hizi ni pamoja na:

(i) Uwepo wa uoto wa asili;

(ii) Uwepo wa ardhi kubwa yenye rutuba iliyosambaa nchi nzima na inayofaa kwa kila aina ya kilimo na kuzalisha mali ghafi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na biashara;

(iii) Uwepo wa madini ya aina mbalimbali yanayoweza kutumika kuharakisha ajenda ya kukuza sekta ya uzalishaji viwandani;

(iv) Uwepo wa wingi wa raslimali za maji, ikiwemo bahari, maziwa na mito inayoweza kutumika kwa ajili ya kilimo cha

umwagiliaji, uvuvi, nishati, usafirishaji na matumizi ya nyumbani;

(v) Jiografia nzuri ya nchi yetu inayotoa fursa ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na mashariki ya mbali;

(vi) Nguvukazi ya vijana, ambapo zaidi ya 70% ya nguvu kazi nchini ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 39. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliseme vizuri hili kwamba tumebarikiwa, tunao vijana wengi ambao nguvukazi yao tukiielekeza vizuri kupitia elimu bora, tuna nafasi nzuri sana ya kuitumia kwa ajili ya maendeleo. Huko duniani kwingine nchi zinakumbwa na uhaba wa wafanyakazi, hiyo ndiyo changamoto kubwa, sisi tunayo nguvukazi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa niwasilishe Mpango wa Nne baada ya kuwasilisha Mpango Elekezi 2050. Sasa ninayo heshima ya kuwasilisha Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 hadi 2030/2031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; katika kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026, Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ikiwa ni mpango wa mwisho katika utekelezaji wa Dira 2025. Muda wa utekelezaji wa mpango huu utakamilika rasmi tarehe 30 Juni, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya awali *(mid-term evaluation)* ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Matokeo ya tathmini hii yanaonesha kuwa mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kukua kwa Pato halisi la Taifa kutoka asilimia 4.9 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 5.5 mwaka 2024 na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025;

(ii) Kudhibiti mfumuko wa bei kuwa chini ya asilimia tano (5)

(iii) Kuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza kuagiza bidhaa kutoka nje kwa muda wa miezi minne au zaidi;

(iv) Kupanuka na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na usafirishaji;

(v) Kuongezeka kwa uzalishaji nishati ya umeme kutoka *megawatt* 1,606 mwaka 2020/2021 hadi kufikia *megawatt* 4,031 mwaka 2024/2025;

(vi) Kuongezeka kwa kiwango cha utoshelevu wa chakula kufikia 128% mwaka 2024/2025 kutoka 124% mwaka 2020/2021; na

(vii) Kupanuka kwa huduma za jamii ikiwemo afya, elimu, maji safi na kinga ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao ninauwasilisha hapa ni mpango wa kwanza katika kuanza kutekeleza Dira 2050 na mpango wa nne tangu nchi yetu iliporejea katika utaratibu wa kuandaa mipango ya muda wa kati ya miaka mitano mwaka 2010/2011. Mpango huu unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa tatu, pamoja na kutumia fursa mpya katika kuleta mageuzi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya mpango huu yalikuwa shirikishi na yalizingatia misingi na ushahidi wa kisayansi katika kutambua na kuainisha vipaumbele vya maendeleo ambavyo

tumevibainisha. Katika muktadha huu, ninataka kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashinda Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri wao walioutoa wakati wa vikao vingi vya Kamati ambako tulikutana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imesheshesheni wajumbe wenye weledi, umahiri na uzoefu mkubwa katika masuala ya uchumi, fedha na maendeleo na imetushauri vizuri na kutupatia maoni ya msingi katika kukamilisha mpango wetu. Ninapenda kukuhakishia kuwa maoni na ushauri wa Kamati hii vimezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya mpango huu ambao ninauwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhima na Malengo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano2026/2027 – 2030/2031; dhima ya Mpango huu ni mageuzi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi jumuishi na uzalishaji wa ajira. Ninaomba nirudie hiyo. Dhima ni mageuzi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na uzalishaji wa ajira. Hii inamaanisha kwamba mafanikio yetu yatapimwa si tu kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi kitarakimu, tutakuwa tunayapima mafanikio yetu kwa kuzingatia ni kiasi gani ukuaji huu unazalisha ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia dhima ya mpango huu, mambo kumi yafuatayo yatapewa kipaumbele na msukumo wa kipekee:

(i) Kuchochea uzalishaji wa ajira kwa vijana; kwa kuzingatia kama nilivyosema kuwa asilimia kubwa ya nguvu kazi yetu ni vijana walio katika umri wa miaka 15 – 39; ili kuweza kuvuna kikamilifu nguvu ya ujana wao *(demographic dividend)* katika kilimo, uzalishaji na huduma;

(ii) Kuhakikisha kuwa kunakuwa na ukuaji wa uchumi ulio tulivu, jumuishi na endelevu;

(iii) Kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu katika nchi;

(iv) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuimarisha uwezo wa Serikali kuhudumia wananchi;

(v) Kukuza na kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu na maendeleo ya jamii;

(vi) Kukuza uwezo wa Tanzania katika kufikia masoko ya kikanda na kimataifa kwa kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara, reli, anga na maji;

(vii) Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari na matumizi ya teknolojia za kisasa kama vile akili mnemba;

(viii) Kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(ix) Kuendelea kulinda na kuimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa; na

(x) Kuweka msukumo wa kipekee katika maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango umebaini na kuainisha vichochea vitano vya mageuzi *(drivers of transformation)* kama ifuatavyo:-

(i) Nishati; tunalenga kupanua upatikanaji wa nishati yenye bei nafuu, ya kuaminika na endelevu ili kuchochea viwanda na mageuzi ya uchumi;

(ii) Lojistiki Jumuishi; uwekezaji katika miundombinu ya usafirishaji na muunganiko wa kikanda ili kuimarisha ushindani wa biashara;

(iii) Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; kukuza utafiti, uvumbuzi na matumizi ya teknolojia mpya kwa kuongeza uzalishaji na mseto wa sekta;

(iv) Mageuzi ya Kidijitali; kuendeleza miundombinu ya *TEHAMA,* huduma za umma mtandao na mifumo ya data kwa utawala bora na uboreshaji wa uchumi; na

(v) Mazingira ya Biashara na Uendelezaji wa Uwekezaji; kuboresha mifumo ya kisheria na kukuza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuvutia uwekezaji na kuchochea ujasiriamali, hususani miongoni mwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha utekelezaji wenye mafanikio, Mpango umebainisha maeneo manne katika kuimarisha misingi ya utawala bora, amani, usalama na utulivu:-

(i) Kwa ujumla wake, shabaha kuu katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031 ni kukuza Pato halisi la Taifa kwa asilimia 10.5, ifikapo mwaka 2031;

(ii) Kuongeza pato la Taifa bila kuzingatia mfumko wa bei kufikia wastani wa Dola za Kimarekani bilioni 118.1 ifikapo mwaka 2031; na

(iii) Kukuza pato la mtu mmoja mmoja kufikia dola 1638 ifikapo mwaka 2031*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* za kielelezo *(flagship programs),* ili kuharakisha mageuzi makubwa ya kiuchumi, kuimarisha ushindani na kuzalisha ajira kwa wingi, mpango wa nne umebaini na kuainisha programu za kielelezo saba (7) na miradi shikizi 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako litakumbuka kwamba mpango uliopita ambao unamalizika muda wake mwezi Juni mwaka huu ulikuwa na kitu kinaitwa miradi ya kielelezo 17. Safari hii

tumebadilisha tunakuja kitu kinaitwa *program* za kielelezo ambazo ndani yake kunakuwa na miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hizi za kielelezo zimechaguliwa kwa kuzingatia uwezo na nafasi yake katika kuongeza; kasi ya uzalishaji viwandani, kupanua na kuboresha huduma, kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, na uwezo na nafasi yake katika kutengeneza ajira kwa wingi. Aidha, programu zitatekelezwa katika maeneo na mikoa mbalimbali nchini ili kuhakikisha kunakuwa na uwiano wa maendeleo katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba basi nitaje programu hizi kama ifuatavyo:

(i) Mji wa Ikolojia ya Bahari na Usafirishaji wa Kimataifa – Bagamoyo *(Bagamoyo Eco-Maritime City*. Programu hii itakuwa na miradi shikizi nane) na Waheshimiwa Wabunge kwenye vitabu vyenu mtaviona;

(ii) Kituo Changamani cha Chuma cha Liganga na Mchuchuma *(Liganga– Mchuchuma Integrated Iron and Steel Complex)*. Ndani yake kutakuwa na miradi shikizi sita;

(iii) Programu ya Gesi Asilia ya Kimiminika – Lindi *(Lindi Liquefied Natural Gas Programme-LNG)*. Ndani yake kutakuwa na miradi shikizi mitatu;

(iv) Kitovu cha Ubunifu wa Teknojia na Madini Muhimu ya Kimkakati cha Dodoma *(Dodoma Critical Minerals and Technology Innovation Hub)*. Ndani yake kutakuwa na miradi shikizi nane);

(v) Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Kilimo *(National Irrigation and Agro-Industrial Transformation Programme)*. Ndani yake kutakuwa na miradi shikizi minne;

(vi) Kitovu Mahiri cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu *(Great Lakes Smart Industrial and Blue Economy Mega Hub)*. Itakuwa na miradi shikizi saba); na

(vii) Programu Shirikishi ya Uendelezaji Miji Tanzania 2050 *(Tanzania Urban Growth Nexus – TUGNe 2050)*. Ndani yake itakuwa na miradi shinikizi tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jumla programu za kielelezo saba, miradi shikizi *(anchor projects*) zitakuwa 45 na zote zimesambaa nchi nzima katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia matokeo tarajiwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mpango huu una jumla ya malengo 79, shabaha 215 na afua *(interventions*) 737 na zote Waheshimiwa Wabunge tumeziweka kwenye vitabu, zinaonekana na zinaonyesha mpaka sekta gani inahusika. Nitazipitia chache kwa kila eneo kwa sababu zipo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani, pamoja na hatua zingine, Mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuanzisha Mfuko wa Akiba wa Taifa *(National Sovereign Wealth Fund)* ambao chanzo chake kitatokana na sehemu ya mapato itokanayo na maliasili za Taifa kama vile mafuta, gesi, dhahabu na madini mengine. Lengo la Mfuko huu ni kwamba hizi ni rasilimali ambazo zinakwisha. Kuna siku ambayo madini yatakwisha, gesi itakwisha, dhahabu zitakwisha. Tunaweka Mfuko huu kwa lengo la kuweka akiba ili vizazi vijavyo pia vije vifaidike na rasilimali hizi za Taifa. Wakija wakisikia tuliwahi kuwa na dhahabu waambiwe dhahabu ile akiba yake ni hii hapa ili nao waweze kufaidi;

(ii) Kuongeza makusanyo ya kodi kufikia uwiano wa 18% ya pato la Taifa *(tax to GDP ratio)*. Hii pia ni shabaha kubwa. Kwa sasa hatujafikia 13%, tunataka ifikapo mwaka 2031 tusipungue 18% ya makusanyo ya kodi ili kujenga uwezo wa Serikali kuhudumia wananchi wake;

(iii) Kujenga uwezo wa wakandarasi wa ndani ili kuongeza kiwango cha ushiriki wao katika miradi ya ujenzi. Utaona kwamba, moja ya eneo kuubwa katika mpango huu wa miaka mitano litakuwa ni eneo la *construction*. Fedha nyingi sana ya Serikali na sekta biafsi itakwenda kwenye ujenzi. Ili tuweze kuchangamsha uchumi na kufaidika na fedha hii ni lazima tujenge uwezo wa wakandarasi wa ndani ili kazi za ujenzi waweze kuzifanya wao, vinginevyo fedha nyingi itakwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa watu na kuchochea maendeleo ya jamii, pamoja na hatua zingine, Mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo jumuishi wa kujifunza unaoendana moja kwa moja na mahitaji ya nchi, ukiwekeza katika maendeleo ya walimu na kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa zana za kidijitali na miundombinu ya kisasa. Kwa hiyo mkazo utawekwa sana kwenye maendeleo ya walimu; kwa sababu hakuna elimu bila walimu, elimu ni walimu;

(ii) Kuoanisha upya mifumo ya elimu na mafunzo na mahitaji mahsusi ya uchumi wa kisasa wa viwanda, hususani kwa kufanya mageuzi ya kimkakati ya *TVET (*vyuo vyetu vya ufundi*)*, kuoanisha mitaala na viwango vya kimataifa na kujumuisha ujuzi wa kidijitali katika kila ngazi ili kuhakikisha uhalisia na ushindani wa kimataifa wa vijana wanaohitimu katika vyuo vyetu;

(iii) Kukuza mfumo hai wa mazingira kwa ajili ya kampuni changa *(startups)* na *SMEs*, sambamba na kuvutia kimkakati uwekezaji mkubwa unaozalisha ajira nyingi katika maeneo maalum ya kiuchumi na sekta muhimu;

(iv) Kulenga kuwa kituo kinara cha utalii wa tiba, ambacho kitaboresha ubora wa maisha ya Watanzania wote, lakini pia kitaweka sekta ya afya nchini kama injini muhimu ya maendeleo ya Taifa na utambuzi wa kimataifa;

(v) Wastani wa umri wa kuishi kuongezeka kutoka miaka 68.3 mwaka 2024 hadi kufikia miaka 70.4 mwaka 2031, kikiwa ni kigezo kikuu cha ubora wa maisha kwa watu wetu;

(vi) Uagizaji wa bidhaa na vifaa tiba kutoka nje kupungua kwa angalau asilimia 20 ifikapo mwaka 2031. Kwa sasa nchi yetu inaagiza vifaa tiba na madawa kutoka nje kwa zaidi ya asilimia 80. Tunataka hali hiyo ipungue;

(vii) Kupunguza vifo vya wanawake wakati wa kujifungua kutoka 104 kati ya vizazi hai 100,000 mwaka 2024 hadi kufikia 85 ifikapo mwaka 2031;

(viii) Kiwango cha wananchi waliounganishwa katika mtandao wa maji safi ya kunywa kufikia 60% ifikapo mwaka 2031. Sasa nilieleze hili; kwa sasa upatikanaji wa maji vijijini unakwenda takriban 80%. Hatua inayofuata tunataka angalau 60% ya wananchi wetu wapate maji pale alipo nyumbani kwake kwa njia ya kuunganishwa na mtandao;

(ix) 30% ya vijiji kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi na 40% ya ardhi yote vijijini kuwa imesajiliwa, kupimwa na kupangwa ipasavyo ifikapo mwaka 2031; na

(x) Kuanza utaratibu wa kufanya sensa ya watu na makazi kwa kutumia d*ashboard* za wakati uliopo (*real-time dashboards*) na hivyo kupata idadi ya watu na makazi kwa wakati

husika badala ya kusubiri kila baada ya miaka 10. Kwa sasa tunafanya sensa kila baada ya miaka 10; maana yake sensa nyingine itakuwa mwaka 2032. Kwa kuzingatia hatua kubwa za kiteknolojia hatuna sababu. Tunakuja na mpango wa kupata sensa kwa wakati ambao tunahitaji kama ni kila mwaka inapatikana bila kusubiri miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchochea mageuzi makubwa na ya haraka ya kiuchumi, pamoja na mambo mengine, Mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo: -

(i) Kuimarisha upatikanaji wa umeme, kama nilivyosema;

(ii) Kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kurahisisha urekebu *(regulatory procedures)*. Katika kufikia hatua hii, pamoja na mambo mengine, Serikali itaweka utaratibu wa kutenganisha malengo ya kimapato *(revenue motive)* na malengo ya kirekebu *(regulatory mandates)* ili kuhakikisha kuwa tozo zinalenga kuwezesha utendaji wa taasisi husika badala ya kulenga kuzalisha faida. Tunataka taasisi zetu ambazo zinarekebu biashara zikusanye tozo kwa lengo la kufanikisha utendaji na si kuzalisha faida ili kupunguza gharama ya kufanya biashara hapa nchini. Hili ni eneo ambalo ni muhimu sana;

(iii) Kuendelea kuimarisha sekta ya kilimo ili kubadilika kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kuwa kilimo cha kibiashara, kinachotumia teknolojia na kinacholenga kuongeza mauzo ya nje;

(iv) Kuhakikisha umiliki salama wa ardhi kupitia mifumo ya kisasa ya kisheria na upangaji unaoongozwa na jamii;

(v) Kuifanya sekta ndogo ya ushirika kuwa ya kitaalam, kuijengea msingi wa imani na umahiri wa kibiashara unaowezesha biashara za pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu katika nchi kama msingi mama wa kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050; dira imeweka kwamba utawala bora, demokrasia, usalama amani na utulivu ndiyo msingi mkuu wa kutekeleza malengo haya. Ikiyumba hiyo malengo yetu hatuwezi kuyatimiza. Katika kuimaisha hiyo pamoja na mambo mengine, mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuziwezesha serikali za mitaa kama injini kuu ya maendeleo kwa kuzijengea uwezo wa ndani na kuweka mifumo thabiti. Kwa ukubwa wa nchi yetu hakuna namna ya kuleta maendeleo katika nchi hii kutokea Dodoma ama Dar es Salaam. Maendeleo makubwa yatapatikana kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako wananchi wapo; kwa hiyo ni lazima tuwekeze nguvu nyingi sana kwenye eneo hilo;

(ii) Kuhuisha mchakato wa mabadiliko ya katiba;

(iii) Kuanzisha utaratibu wa kuajiri na kuteua watendaji Wakuu na Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma kwa njia ya ushindani na upimaji unaozingatia matokeo. Ninaomba nisisitize hili; kwamba Wakuu wa Mashirika ya Umma na Wajumbe wa Bodi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameidhinisha na kuelekeza kwamba sasa waanze kupatikana kwa njia ya ushindani ili kila Mtanzania awe na fursa ya kuweza ku-*apply*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze juu ya ugharamiaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Gharama za utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano zinakadiriwa kuwa shilingi trilioni 477. Mpango uliopita wa miaka mitano gharama yake ilikuwa shilingi trilioni 144. Tunaongeza mara nne, trilioni 477.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kiasi cha fedha kitakachohitajika kuwekezwa katika sekta za kimageuzi na zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo: usafiri fungamanishi, nishati na uchimbaji, viwanda na biashara, kilimo, TEHAMA, mazingira na uhimilivu wa tabianchi, huduma za kijamii na maendeleo ya watu, utawala na utumishi wa umma, pamoja na utafiti na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vikuu vya rasilimali za kugharamia Mpango huu ni viwili: sekta binafsi na sekta ya umma kwa uwiano wa 70 kwa 30, ikimaanisha kwamba sekta binafsi inatarajiwa kuchangia 70% ya kupata hizi fedha shilingi trilioni 477 na sekta ya umma 30%. Hii inamaanisha kwamba lazima katika nchi hii ili mipango hii itekelezeke tuheshimu, tuilinde na tuitambue na tuijenge sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ndiyo itakuwa mhimili wa kutekeleza mipango hii ambayo tumeiwasilisha hapa. Tunatarajia kwamba kwa upande wa Serikali Kuu kupitia mipango ya kodi na mapato yasiyo ya kikodi itachangia shilingi trilioni 115 sawa na 22%. Mashirika ya Umma yatachangia shilingi trilioni 38.22 sawa na asilimia nane na sekta binafsi itachangia shilingi trilioni 324.49 sawa na 70%. Ninaomba nirudie, sekta binafsi ndiyo itakuwa *engine* ya kutekeleza mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwasilisha sehemu ya tatu ambayo ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 ambayo ni mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne ambao nimeueleza, lakini pia ni wa kwanza kwenye kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebaini maeneo matano ya kimkakati katika mpango huu wa mwaka 2026/2027:-

(i) Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora;

(ii) kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya kidijiti, nishati, na usafirishaji fungamanishi;

(iv) Kuimarisha sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji thamani na ukuaji jumuishi; na

(v) Kuimarisha uhifadhi wa mazingira na uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa Hali ya Uchumi atauwasilisha baadaye Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika wasilisho lake. Ninaomba sehemu hiyo niiruke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze sehemu ya mwisho misingi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026. Ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/2027 utajengwa katika misingi ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji kustawi;

(ii) Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;

(iii) Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati na usafiri na usafirishaji, sambamba na matarajio ya Dira 2050;

(iv) Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia;

(v) Utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala chini ya falsafa ya *4Rs;*

(vi) Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji kupitia mashirikiano ya sekta binafsi na sekta ya umma *(PPP);*

(vii) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Mpango huu wa Nne wa Maendeleo wa Taifa umeakisi kikamilifu na umezingatia maudhui ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Aidha, mpango huu umezingatia kikamilifu maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa kupitia hotuba yake ya kufungua Bunge la Kumi na Tatu na hotuba nyingine ambazo amekwishazitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka kwamba tumejiwekea malengo na matarajio makubwa katika Dira ya 2050 na mipango ambayo nimeiwasilisha leo. Kazi kubwa tuliyonayo sasa ni kutafsiri na kugeuza maono yaliyomo katika mipango hii kuwa vitendo. Pengine hii ndiyo kazi kubwa zaidi kuliko kupanga, kutekeleza ndiyo kazi inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati akizindua rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo, Dira ya 2050 tarehe 17 Julai mwaka jana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alieleza uzito na ukubwa wa malengo na matarajio tuliojiwekea katika Dira 2050 akisisitiza kuwa tunahitaji kujipanga kikamilifu katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kubadili mtazamo katika utendaji na kwamba ili kufikia malengo na matarajio tuliyojiwekea tunahitaji kufanya kazi kwa

namna isiyo ya kawaida *(business unusual)*. Tuache kufanya kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo itakayopitishwa na Bunge lako Tukufu. Tumeandaa mfumo wa ufuatiliaji na upimaji unaozingatia kupima matokeo na uwajibikaji *(Results-based Monitoring, Evaluation, Learning and Accountability Framework)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mpya wa ufuatiliaji na upimaji umejengwa katika nguzo tatu, ambazo ni: kuainisha vipaumbele bayana na kwa uwazi kwa kila sekta *(prioritisation),* nidhamu ya utekelezaji *(discipline of implementation);* na uwajibikaji *(accountability)*. Katika kutekeleza mfumo huu, hatua tano zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kila sekta inayotekeleza programu na miradi ya maendeleo itapaswa kuweka malengo na viashiria vya utekelezaji vinayopimika, pamoja na mikakati mbalimbali itakayofanyika kufikia malengo hayo;

(ii) Taarifa ya utekelezaji itawasilishwa kwa Tume ya Taifa ya Mipango kila mwezi;

(iii) Mawaziri watawasilisha taarifa za utekelezaji kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kila baada ya miezi mitatu;

(iv) Tume ya Taifa ya Mipango itatoa taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa umma kila mwaka kupitia tukio la wazi chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu; na

(v) Kwa kuzingatia Kifungu cha 7 cha Sheria ya Tume ya Mipango, 2023, Tume itakuwa na mamlaka ya kuitisha vikao vya viongozi wa juu wanaosimamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa lengo la kuratibu

uchambuzi wa changamoto za utekelezaji na kusukuma utekelezaji wa suluhu zilizokubalika ili kuondoa vikwazo vya utekelezaji, kuboresha uratibu na kupata taarifa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hapa, tunapozungumzia Tume ya Taifa ya Mipango, Mwenyekiti wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha hotuba hii, ninapenda kuwashukuru watumishi wenzangu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri kwamba kijana huyu kutoka Manyoni aliyeteuliwa juzi amekuwa nguzo muhimu sana ya kunisaidia katika utendaji wangu. Pia, Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu mahiri kabisa, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambaye anaunganisha vizuri sana taasisi kubwa tatu: Ofisi ya Msajili wa Hazina, Tume ya Taifa ya Mipango pamoja na *TISEZA*. Taasisi zote hizi ni kubwa sana; bila kuwa na Katibu Mkuu imara inakuwa ni changamoto. Tunamshukuru sana Dkt. Tausi Kida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, ambaye anaongoza michakato yote hii ya kuandaa nyaraka hizi, kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipa katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru wataalam wote wa Tume ya Taifa ya Mipango, wakiongozwa na Dkt. Mursali Milanzi, Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango anayesimamia Mipango ya Kitaifa na Bi. Angela Shayo, Mkurugenzi wa Mipango ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasoma mambo haya lakini hawa ndiyo waandaaji wa *document* zote hizi kubwa ambazo zinakuja hapa na tunataka kuwashukuru sana kwa maandalizi mazuri ya nyaraka nimeziwasilisha leo hapa Bungeni. Kwa kweli tunawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na watumishi wote wa Tume ya Taifa ya Mipango kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba Kamati yako ipokee, ijadili na kushauri kuhusu:-

(i) Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027–2050/2051;

(ii) Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027– 2030/2031; na

(iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Siyo kutoa hoja; ni kuwasilisha. Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Arudie tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**2 FEBRUARI, 2026**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO ELEKEZI WA MAENDELEO WA MUDA MREFU 2026/27–2050/51, MPANGO WA NNE WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2026/27–2030/31 NA MAPENDEKEZOYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Dodoma, Jumatatu, 2 Februari 2026**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kifungu cha 6(2)(b) cha Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango (Sura 127) na Kanuni ya 113 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea, kujadili na kushauri kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27–2050/51, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31, na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27.

**SHUKRANI NA PONGEZI**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kutoa shukrani na pongezi. Kwanza, ninamshukuru Mungu kwa kutujalia neema ya uhai, afya njema, amani na utulivu, na kutupa fursa ya kukutana katika Bunge hili la 13 na Mkutano huu wa Pili. Pili, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hivyo kupata tena heshima na imani ya Watanzania ya kuweza kuliongoza taifa letu kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyopata kushika nafasi hiyo ya pili kwa ukubwa nchini. Nne, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tano, ninampongeza Mheshimiwa Dkt.

Mwigulu Lameck Nchemba (Mbunge wa Iramba Magharibi mkoani Singida), kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua tena kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji. Ninamuahidi bidii na weledi katika kazi na utiifu kwake binafsi, kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Chama Cha Mapinduzi na kwa watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, ninawapongeza waheshimiwa mawaziri wenzangu na naibu mawaziri kwa heshima na imani kubwa waliopata ya kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, ninakupongeza sana kwa jina lako kupendekezwa na Kamati Kuu ya CCM na hatimaye kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongera sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, ninampongeza pia Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza wenyeviti wote wa Bunge na wenyeviti wa kamati mbalimbali za kudumu za Bunge waliochaguliwa kutuongoza katika Bunge hili. Tuna imani kubwa kuwa mtaliongoza Bunge hili la Kumi na Tatu kwa busara, haki, na weledi mkubwa ili kuliwezesha kuendelea kuwa mhimili imara wa demokrasia, uwajibikaji na utawala wa sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi na kupewa dhamana kubwa ya kuwawakilisha watanzania katika Bunge lao na kutupatia fursa ya kutunga sheria na kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, ninayo heshima kubwa na ya kipekee kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ubungo Jijini Dar es

Salaam kwa kunipa heshima ya kuwawakilisha tena hapa Bungeni. Aidha, ninakishukuru sana Chama Cha Mapinduzi kwa kunipa heshima ya kugombea tena katika Jimbo la Ubungo. Ninawaahidi wananchi wa Ubungo na Chama Cha Mapinduzi utumishi wenye bidii, weledi, heshima na utiifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na mbili, naomba nihitimishe shukrani na pongezi kwa kuwashukuru walimu wote walionifundisha na kunilea kuanzia elimu ya msingi hadi chuo kikuu. Kwa leo wamewakilishwa na Mwalimu Said Swalehe Magema, mwalimu mstaafu, aliyenifundisha Shule ya Msingi Mgela iliyopo Kata ya Mtoa Wilaya ya Iramba. Mwalimu huyu alinifundisha Darasa la Kwanza na baadaye somo la Kiingereza Darasa la Tatu mwaka 1983 (miaka 43 iliyopita). Aidha, Mwalimu Magema ndiye aliyeniletea habari za mie kuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari mwezi Desemba 1987 nyumbani. Mwalimu Magema kwa niaba ya wenzako wote walionifundishia na kunilea ahsante sana!

**DIRA 2050**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa takribani miaka miwili, kati ya Aprili 2023 na Julai 2025, Tanzania iliingia katika mchakato wa kuandika dira mpya ya Taifa ya Maendeleo. Hatua hii ilifuatia kukamilika kwa kipindi cha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000 – 2025, na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kuandaa dira mpya. Mchakato wa kuandika dira mpya ulikamilika Julai 2025, na dira mpya ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 17 Julai 2025. Dira hii itatekelezwa katika kipindi cha miaka 25 (2026/27 -2050/51) na inajulikana rasmi kama Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu au mwelekeo wa Dira 2050 ni kuwa na Taifa jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Malengo mahususi manne katika Dira 2050 ni:-

(i) Uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mesto, himilivu, jumuishi na shindani;

(ii) Maisha bora na ustawi kwa wote;

(iii) Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabia nchi; na

(iv) Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2050, Serikali imeandaa nyenzo tatu muhimu kama ifuatavyo:-

(i) Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (Long-Term Perspective Plan – LTPP) 2026/27–2050/51, ambao ni nyenzo ya kimkakati itakayoongoza mipango yetu kwa kipindi cha miaka 25;

(ii) Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (Fourth Five Year Development Plan – FYDP4) 2026/27 2030/31, ambao unatafsiri kwa mapana Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu katika kipindi cha muda wa miaka mitano ya kwanza; na

(iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka (Annual Development Plan – ADP) 2026/27 ambao unatafsiri maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika kipindi cha muda mfupi cha mwaka mmoja.

## MPANGO ELEKEZI WA MAENDELEO WA MUDA MREFU (LONG-TERM PERSPECTIVE PLAN – LTPP) 2026/27–2050/51

### Muktadha

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina historia ndefu ya kuandaa mipango ya maendeleo. Mpango elekezi wa maendeleo wa muda mrefu wa kwanza uliandaliwa mwaka 1964, ukiwa ni wa kipindi cha miaka 16 (1964 – 1980). Mpango huu ulipangwa kutekelezwa kupitia mipango ya muda wa kati mitatu: I: 1964-1969; II: 1969 – 1974; na III: 1975 – 1980. Hata hivyo, mipango hii haikutekelezwa kikamilifu kutokana na changamoto za kiuchumi zilizoikumba dunia na nchi yetu, ikiwemo ukame na hali mbaya ya hewa, kuharibika kwa soko la mafuta duniani, na vita kati ya Tanzania na Uganda ya 1978/79. Kutokana na changamoto hizi, utekelezwaji wa mpango elekezi ulisitishwa rasmi mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1981 Serikali iliandaa mpango elekezi wa maendeleo wa muda mrefu wa pili wa miaka 20 (1981 – 2000). Mpango huu ulipangwa kutekelezwa kupitia mipango ya muda wa kati minne. Hata hivyo, mpango huu nao haukutekelezwa kikamilifu kutokana na majanga ya kiuchumi yaliyoendelea kuikumba dunia katika miaka ya 1970 na 1980, hali iliyolazimisha nchi yetu kujielekeza kutekeleza mipango ya muda mfupi na ya dharura. Katika kipindi hiki, mipango ya muda mfupi na ya dharura iliyotekelezwa ni pamoja na Programu ya Kitaifa ya Kujihami Kiuchumi (National Economic Survival Programme – NESP) iliyotekelezwa mwaka 1981 – 1982; Programu za Kurekebisha Uchumi (Structural Adjustment Programmes-SAPS) zilizotekelezwa mwaka 1983 - 1985; na Programu za Kufufua Uchumi (Economic Recovery Programme – ERPs) zilizotekelezwa 1986 – 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya hapo juu, Tanzania haikuwahi kutekeleza kikamilifu mpango wa maendeleo wa muda mrefu hadi mwaka 2000 ilipozindua dira ya kwanza ya Taifa ya maendeleo (Dira 2025). Hata hivyo, Dira hii haikuanza kutekelezwa mapema kutokana na kutokuandaliwa mpango elekezi wa muda mrefu wa maendeleo ambao ulipaswa kutafsiri maono na matarajio

yaliyokuwemo katika dira hiyo. Hali hii ilitokana na mashariti ya taasisi za kifedha duniani (IMF na Benki ya Dunia) ya kuitaka Tanzania kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa kupunguza umaskini (MKUKUTA), ikiwa ni sehemu ya kukidhi masharti ya kukidhi vigezo yaliyowekwa kwa nchi maskini kusamehewa madeni chini ya mpango maalum wa nchi maskini zenye madeni makubwa (Heavily Indebted Poor Counties -HIPC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025 na kubaini kuwa dira hiyo ilikuwa haijaanza kutekelezwa kikamilifu kama ilivyotarajiwa kutokana na kukosekana kwa mpango elekezi wa kuongoza utekelezaji wake. Kufuatia tathmini hiyo, Serikali iliandaa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa kwanza (first Long-Term Perspective Plan – LTPP) wa miaka 15 (2011/12 –2025/26), ulioandaliwa kwa ajili ya kuongoza utekelezaji Dira 2025 kwa miaka iliyokuwa imebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, hii ni mara kwanza kwa nchi yetu kuandaa dira na mpango elekezi kwa wakati mmoja. Hii inamaanisha kuwa hatuna sababu ya kuchelewa kuanza kutekeleza Dira 2050. Tunamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi na maelekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza kikamilifu LTPP ya kwanza, Serikali iliandaa mipango mitatu ya miaka mitano (Five Year Development Plans – FYDPs) kama ifuatavyo:

(i) FYDP I: 2011/12 – 2015/16: Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi (Unleashing Tanzani’s Latent Growth Potential);

(ii) FYDP II: 2016/17 – 2020/21: Kukuza Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu (Nurturing Industrialisation for Economic Transformation and Human Development); na

(iii) FYDP III: 2021/22 – 2025/26: Kujenga Uchumi Shindani na wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu (Realising

Competitiveness and Industrialisation for Human Development).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini iliyofanywa ilionesha mafanikio makubwa yalipatikana katokana na utekelezaji wa LTPP 2025. Mafanikio haya ni pamoja na kukua kwa pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 6.2 kwa miaka 20 mfufulizo kati ya mwaka 2002 na 2024; kudhibitiwa kwa mfumo wa bei na kuwa ndani ya wigo wa asilimia 3 – 5; kuongezeka kwa wastani wa pato la mtu mmoja kutoka Dola za Marekani 453 mwaka 2000 hadi kufikia Dola 1,277 mwaka 2024; kupungua kwa kiwango cha umaskini kutoka wastani wa asilimia 36 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 26 mwaka 2022; kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 750 kwa kila vizai hai 100,000 mwaka 2000 hadi 104 mwaka 2022; na kuimarika kwa mifumo ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hali ya ubora wa maisha iliimarika zaidi katika kipindi cha utekelezaji wa LTPP 2025 kunakothibitishwa na kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kwa mtanzania kutoka miaka 51 mwaka 2000 hadi kufikia wastani wa miaka 66 mwaka 2022. Aidha, Tanzania ilifikia hadhi ya uchumi wa pato la kati la chini lower middle-income country mwaka 2020 kwa kufikia wastani wa pato la mtu mmoja la dola za Marekani 1,271.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025 na LTPP yake ilibainisha changamoto kadhaa zilizosababisha kutokufikiwa kikamilifu kwa malengo yaliyowekwa. Changamoto hizi ni pamoja na tija ndogo ya uzalishaji katika kilimo; kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani; kasi ndogo ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; na upungufu na udhaifu wa raslimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira 2050 inalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuweka msingi wa kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Dira/LTPP 2025, pamoja na kuibua fursa mpya zitakazoisukuma mbele zaidi nchi yetu katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kuelekea mwaka 2050.

## Mwelekeo wa Jumla wa Mpango Elekezi 2050

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Elekezi umeainisha malengo mahsusi na afua kwa kuzingatia shabaha na vipaumbele vilivyobainishwa katika Dira 2050. Kwa kuzingatia kasi kubwa ya ongezeko la watu nchini na athari zake katika upatikanaji wa ardhi, huduma za jamii na miundombinu, na kwa kuzingatia haja ya kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kukuza uwekezaji nchini, Mpango Elekezi umeweka mkazo maalum katika mambo sita yafuatayo:

(i) Upangaji miji endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira;

(ii) Ushirikishwaji mpana katika kupanga mipango ya maendeleo;

(iii) Kupanua na kuongeza ubora wa huduma za jamii;

(iv) Kuongeza tija katika kilimo, uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma kwa kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia (ikiwemo matumizi ya dijitali), ubunifu na uongezaji thamani mazao mbalimbali;

(v) Kuweka mazingira rafiki na yanayotabirika ya uwekezaji na kufanya biashara ili kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi; na

(vi) Kufanya mageuzi katika mfumo wa utawala na mabadiliko ya utamaduni na mitazamo.

## Falsafa ya Maendeleo

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Mpango Elekezi (LTPP 2050) ni Dira 2050 inayolenga kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi kwa wote, lenye haki na linalojitegemea. Katika kujenga Taifa lenye ustawi kwa wote, Dira 2050 inalenga kukuza pato la Taifa na pato la mtu mmoja moja kwa kuzingatia usawa wa fursa kwa wote. Katika kujenga Taifa

linalojitegemea, Dira 2050 inaelekeza kutumia raslimali za Taifa kimkakati na kuwa wabunifu katika kuvunja mnyororo wa utegemezi huku tukizingatia na kutumia fursa za utengamano wa kikanda na jumuiya ya kimataifa, bila kujitenga na dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga Taifa jumuishi, Dira 2050 inaelekeza kuhakikisha fursa sawa kwa wote na kwa makundi yote bila kujali hali yao. Aidha, katika kujenga Taifa lenye haki Dira 2050 inaelekeza kuzingatia utawala wa sheria, usawa mbele ya sheria na uwajibikaji katika muktadha wa demokrasia. Kwa msingi huo, falsafa ya Mpango Elekezi (LTPP 2050) imejikita katika maendeleo ya watu (people-centred development). Mpango Elekezi unazingatia njia mtambuka za uzalishaji, ikihusisha uwiano wa kiushirikiano katika uwekezaji kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

**Fursa, Shabaha na Afua za Mpango Elekezi 2050**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Elekezi 2050 umetambua kuwa nchi yetu ina fursa nyingi zinazotokana na jiografia na uwepo wa raslimali za asili ambazo tukizitumia kikamilifu zitachangia sana katika kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050. Raslimali hizi ni pamoja na:

(i) Uwepo wa uoto wa asili;

(ii) Uwepo wa ardhi kubwa yenye rotuba iliyosambaa nchi nzima na inayofaa kwa kila aina ya kilimo na kuzalisha mali ghafi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda;

(iii) Uwepo wa madini ya aina mbalimbali yanayoweza kutumika kuharakisha ajenda ya kukuza sekta ya uzalishaji viwandani;

(iv) Uwepo wa wingi wa raslimali za maji, ikiwemo bahari, maziwa na mito inayoweza kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, nishati, usafirishaji na matumizi ya nyumbani; na

(v) Jiografia nzuri ya nchi inayotoa fursa ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika ya Kati, na mashariki ya mbali.

(vi) Nguvu kazi ya vijana ambapo zaidi ya asilimia 70 ya nguvu kazi nchini ni vijana (wenye umri kati ya miaka 15 – 39).

## MPANGO WA NNE WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2026/27 –2030/31

### Utangulizi

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2020/21, Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2020/21 – 2025/26, ikiwa ni mpango wa mwisho katika utekelezaji wa Dira 2025. Muda wa utekelezaji wa mpango huu utakamilika tarehe 30 Juni 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya awali (mid-term evaluation) ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Matokeo ya tathmini hii yanaonesha kuwa mafanikio makubwa yalipatikana katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

- Kukua kwa Pato Halisi la Taifa kutoka asilimia 4.9 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 5.5 mwaka 2024 na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025;

- Kudhibiti mfumuko wa bei kuwa chini ya asilimia 5 katika kipindi chote cha utekelezaji wa mpango huu;

- Kuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza kuagiza bidhaa kutoka nje kwa muda wa miezi minne au zaidi;

- Kupanuka na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na usafirishaji;

- Kuongezeka kwa uzalishaji nishati ya umeme kutoka MW 1,606 mwaka 2020/21 hadi kufikia MW 4,031 mwaka 2024/25 na hivyo kuimarika kwa upatikanaji wa huduma ya umeme nchini;

- Kuongezeka kwa kiwango cha utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 128 mwaka 2024/25 kutoka asilimia 124 mwaka 2020/21; na

- Kupanuka kwa huduma za jamii ikiwemo afya, elimu, maji safi na salama na kinga ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo, zipo changamoto mbalimbali zilizojitokeza ikiwemo: tija ndogo katika uzalishaji, kiwango kidogo cha uongezaji thamani ya bidhaa zinazolishwa nchini, ukuaji wa uchumi usiojumuishi; ushiriki mdogo katika biashara za kikanda; kasi ndogo ya uondoaji wa umasikini; na ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika uwekezaji wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (Fourth Five Year Development Plan – FYDP 4) 2026/27 – 2030/31 ni mpango wa kwanza katika kuanza kutekeleza Dira 2050 na mpango wa nne tangu nchi yetu iliporejea katika utaratibu wa kuandaa mipango ya muda wa kati ya miaka mitano mwaka 2010/2011. Mpango huu unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu, pamoja na kutumia fursa mpya katika kuleta mageuzi katika maendeleo ya uchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandalizi ya Mpango huu yalikuwa shirikishi na yalizingatia misingi na ushahidi wa kisayansi katika kutambua na kuainisha vipaumbele vya maendeleo. Katika muktadha huu, ninaishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashinda Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa vikao vya kamati. Kamati hii ambayo imesheheni wajumbe wenye weledi, umahiri na uzoefu

mkubwa katika masuala ya uchumi, fedha na maendeleo imetushauri vizuri na kutupatia maoni ya msingi. Ninapenda kukuhakikishia kuwa maoni na ushauri wa Kamati hii makini umezingatiwa kikamilifu.

**Dhima na Malengo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhima ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 ni Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji wa Uchumi Jumuishi na Uzalishaji wa Ajira. Dhima hii inaelekeza kuweka msukumo wa kipekee katika kutekeleza mageuzi makubwa yatakayobadilisha mifumo, mitazamo na mwenendo katika utendaji ili kuchochea tija katika uzalishaji, kuongeza uwezo wa nchi katika kushindana kikanda na kimataifa, na kuchochea muunganiko wa sekta mbalimbali. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji wa bidhaa, viwanda na biashara katika ukanda wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia dhima ya Mpango huu, mambo kumi yafuatayo yatapewa kipaumbele na msukumo:

(i) Kuchochea uzalishaji wa ajira kwa vijana: kwa kuzingatia kuwa zaidi ya asilimia 60 ya nguvu kazi nchini ni vijana, kipaumbele kitaweka katika kuzalisha ajira ili kuweza kuvuna kikamilifu nguvu ya ujana (demographic dividend) katika kilimo, uzalishaji na huduma;

(ii) Kuhakikisha kuwa kunakuwa na ukuaji wa uchumi tulivu, jumuishi na endelevu;

(iii) Kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu katika nchi;

(iv) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuimarisha uwezo wa serikali kuhudumia wananchi;

(v) Kukuza na kuimarisha maendeleo ya raslimali watu na maendeleo ya jamii;

(vi) Kukuza uwezo wa Tanzania katika kufikia masoko ya kikanda na kimataifa kwa kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara, reli, anga na maji;

(vii) Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari na matumizi ya teknolojia za kisasa kama vile akili mnemba;

(viii) Kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(ix) Kuendelea kulinda na kuimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa; na

(x) Kuweka msukumo katika maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani (nguzo ya kwanza ya Dira 2050), Mpango umelenga kudumisha uthabiti wa uchumi mkuu na uendelevu wa kifedha, huku ikiimarisha uhimilivu na mseto wa sekta ya nje. Nguzo hii inasisitiza kupanua sekta ya uzalishaji viwandani, maendeleo ya sekta binafsi, uunganishaji wa masoko, uongezaji thamani wa mazao na bidhaa, mseto wa mauzo ya nje, ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji, na mazingira ya biashara yanayotabirika ili kuimarisha uwezo wa nchi katika kushindana kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii (Nguzo ya Pili ya Dira 2050), Mpango umeweka mkazo katika maendeleo ya rasilimali watu kama kiini cha maendeleo ya taifa, kwa lengo la kujenga jamii yenye elimu, ujuzi na uwezo wa kubadilika. Mkazo unawekwa katika kunufaika na faida ya idadi kubwa ya vijana kupitia uwekezaji katika elimu bora na ulinganifu wa soko la ajira, mifumo madhubuti ya hifadhi ya jamii, pamoja na huduma bora za afya, makazi, usalama wa chakula na lishe, maji na usafi wa mazingira ili kuhakikisha maendeleo jumuishi. Aidha,

maendeleo jumuishi ya vijijini, mageuzi ya vyama vya ushirika, na upanuzi wa tabaka la kati ni muhimu katika kuimarisha mshikamano wa kijamii na uhimilivu wa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utunzaji wa mazingira na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (Nguzo ya Tatu ya Dira 2050), Mpango umelenga kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali, kukabiliana na athari za tabianchi, na kujenga mifumo imara ya mijini na vijijini inayolinda maisha na riziki za wananchi dhidi ya hatari za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umebaini na kuianisha vichochea vitano vya mageuzi (drivers of transformation) kama ifuatavyo:

(i) Nishati: Kupanua upatikanaji wa nishati kwa bei nafuu, ya kuaminika na endelevu ili kuchochea viwanda na mageuzi ya uchumi;

(ii) Lojistiki Jumuishi: Uwekezaji katika miundombinu ya usafirishaji na muunganiko wa kikanda ili kuimarisha ushindani wa biashara;

(iii) Sayansi, Teknolojia na Ubunifu: Kukuza utafiti, uvumbuzi na matumizi ya teknolojia mpya kwa kuongeza uzalishaji na mseto wa sekta;

(iv) Mageuzi ya Kidijitali: Kuendeleza miundombinu ya TEHAMA, huduma za umma mtandao na mifumo ya data kwa utawala bora na uboreshaji wa uchumi; na

(v) Mazingira ya Biashara na Uendelezaji wa Uwekezaji: Kuboresha mifumo ya kisheria na kukuza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuvutia uwekezaji na kuchochea ujasiriamali, hususan kwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha utekelezaji wenye mafanikio, Mpango umebainisha maeneo manne katika kuimarisha misingi ya utawala bora, amani, usalama na utulivu:

(i) Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu: Kuimarisha taasisi na utawala wa kisheria kwa maendeleo ya muda mrefu;

(ii) Utawala Bora wa Mamlaka za Serikali za Mitaa: Kuzingatia ugatuzi na ujenzi wa uwezo katika ngazi za chini ili kuboresha utoaji wa huduma na ushiriki wa wananchi;

(iii) Utawala wa Kidijitali na Takwimu Mahiri: Kuimarisha mifumo ya kidijitali na uwezo wa data kwa upangaji na maamuzi yanayotegemea ushahidi; na

(iv) Mabadiliko ya Mtazamo na Mageuzi ya Utumishi wa Umma: Kukuza utamaduni wa ubunifu, nidhamu ya utekelezaji na kuhudumia wananchi ili kufanikisha mageuzi ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake, shabaha kuu katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 ni kukuza pato halisi la taifa kwa asilimia 10.5, kuongeza pato la taifa (bila kuazingatia mfumko wa bei) kufikia wastani wa dola za kimarekani bilioni 118.1 na pato la mtu mmoja kufikia dola 1,638 ifikapo mwaka 2031.

## Programu za Kielelezo

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuharakisha mageuzi makubwa ya kiuchumi, kuimarisha ushindani na kuzalisha ajira kwa wingi, Mpango wa Nne umebaini na kuainisha Programu za Kielelezo Saba (7) na miradi shikizi (anchor projects) 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu za kielelezo (flagship projects) zimechaguliwa kwa kuzingatia uwezo na nafasi yake katika kuongeza kasi ya uzalishaji viwandani, kupanua na kuboresha huduma,

kuongeza mauzo ya nje, na uwezo na nafasi yake katika kutengeneza ajira kwa wingi. Aidha, programu zitatekelezwa katika maeneo na mikoa mbalimbali ili kuhakikisha kunakuwa na uwiano wa maendeleo katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu za Kielelezo na idadi ya miradi shikizi kwa kila programu ni kama ifuatavyo:

(i) Mji wa Ikolojia ya Bahari na Usafirishaji wa Kimataifa - Bagamoyo (Bagamoyo Eco-Maritime City-miradi shikizi nane);

(ii) Kituo Changamani cha Chuma cha Liganga na Mchuchuma (Liganga–Mchuchuma Integrated Iron and Steel Complex-miradi shikizi sita);

(iii) Programu ya Gesi Asilia ya Kimiminika – Lindi (Lindi Liquefied Natural Gas Programme-LNG-miradi shikizi mitatu);

(iv) Kitovu cha Ubunifu wa Teknojia na Madini Muhimu ya Kimkakati cha (Dodoma Critical Minerals and Technology Innovation Hub – miradi shikizi nane);

(v) Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Kilimo (National Irrigation and Agro-Industrial Transformation Programme-miradi shikizi minne);

(vi) Kitovu Mahiri cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu (Great Lakes Smart Industrial and Blue Economy Mega Hub-miradi shikizi 7); na

(vii) Programu Shirikishi ya Uendelezaji Miji Tanzania 2050 (Tanzania Urban Growth Nexus – TUGNe 2050-miradi shinikizi tisa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia matokeo tarajiwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 –

2030/31, jumla ya malengo 79, shabaha 215 na afua 737 zitatekelezwa katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya shabaha na afua hizi zinaainishwa hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani, pamoja na hatua zingine, Mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuanzisha mfuko wa akiba wa Taifa (National Sovereign Wealth Fund) ambao chanzo chake kitatokana na sehemu ya mapato itokanayo na maliasili za Taifa kama mafuta, gesi, dhahabu na madini mengine;

(ii) Kuongeza makusanyo ya kodi kufikia uwiano wa asilimia 18 ya pato la Taifa (tax to GDP ratio); na

(iii) Kujenga uwezo wa wakandarasi wa ndani ili kuongeza kiwango cha ushiriki wao katika miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa watu na kuchochea maendeleo ya jamii, pamoja na hatua zingine, Mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo jumuishi wa kujifunza unaoendana moja kwa moja na mahitaji ya nchi, kuwekeza katika maendeleo ya walimu, na kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa zana za kidijitali na miundombinu ya kisasa;

(ii) Kuoanisha upya mifumo ya elimu na mafunzo na mahitaji mahsusi ya uchumi wa kisasa wa viwanda, hususan kwa kufanya mageuzi ya kimkakati ya TVET, kuoanisha mitaala na viwango vya kimataifa na kujumuisha ujuzi wa kidijitali katika kila ngazi ili kuhakikisha uhalisia na ushindani;

(iii) Kukuza mfumo hai wa mazingira kwa ajili ya kampuni changa na MSMEs, sambamba na kuvutia kimkakati

uwekezaji mkubwa unaozalisha ajira nyingi katika maeneo maalum ya kiuchumi na sekta muhimu;

(iv) Kulenga kuwa kituo kinara cha utalii wa tiba, ambacho kitaboresha ubora wa maisha ya Watanzania wote na kitaweka sekta ya afya kama injini muhimu ya maendeleo ya taifa na utambuzi wa kimataifa;

(v) Wastani wa umri wa kuishi kuongezeka kutoka miaka 68.3 mwaka 2024 hadi kufikia miaka 70.4 mwaka 2031;

(vi) Uagizaji wa bidhaa na vifaa tiba kutoka nje kupungua kwa angalau asilimia 20 ifikapo mwaka 2031;

(vii) Kupunguza vifo vya wanawake wakati wa kujifungua kutoka 104 kati ya vizazi hai mwaka 2024 hadi kufikia 85 ifikapo mwaka 2031;

(viii) Kiwango cha wananchi waliounganishwa katika mtandao wa maji safi ya kunywa kufikia asilimia 60 ifikapo mwaka 2031;

(ix) Asilimia 30 ya vijiji kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi na asilimia 40 ya ardhi yote vijijini kuwa imesajiliwa, kupimwa na kupangwa ipasavyo ifikapo mwaka 2031; na

(x) Kuanza utaratibu wa kufanya sensa ya watu na makazi kwa kutumia dashboard za wakati uliopo (real-time dashboards) na hivyo kupata idadi ya watu na makazi kwa wakati husika badala ya kusubiri kila baada ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchochea mageuzi makubwa na ya haraka ya kiuchumi, pamoja na mambo mengine, Mpango umeelekeza kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha upatikanaji wa uhakika na bei nafuu wa umeme kwa kuongeza uzalishaji kufikia megawati 15,000 ifikapo mwaka 2031;

(ii) Kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kurahisha urekebi. Katika kufikia hili, pamoja na mambo mengine, serikali itaweka utaratibu wa kutenganisha malengo ya kimapato (revenue motive) na malengo ya kirekebu (regulatory mandates) ili kuhakikisha kuwa tozo zinalenga kuwezesha utendaji wa taasisi husika badala ya kulenga kuzalisha faida;

(iii) Kuendelea kuimarisha sekta ya kilimo ili kubadilika kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kuwa kilimo cha kibiashara, kinachotumia teknolojia na kinacholenga kuongeza mauzo ya nje;

(iv) Kuhakikisha umiliki salama wa ardhi kupitia mifumo ya kisasa ya kisheria na upangaji unaoongozwa na jamii, kuwekeza katika miundombinu ya kilimo inayozingatia tabianchi, na kutoa ruzuku kwa pembejeo muhimu za kisasa, kama sehemu ya mikakati ya kuharakisha maendeleo vijini;

(v) Kuifanya sekta ndogo ya ushirika kuwa ya kitaalamu, kuijengea msingi wa imani na umahiri wa kibiashara unaowezesha biashara za pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu katika nchi kama msingi mama wa kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050, pamoja na masuala mengine, mpango umeweka mkazo katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuziwezesha serikali za mitaa kama injini kuu ya maendeleo kwa kujenga uwezo wa ndani na kuweka mifumo thabiti ya mrejesho wa wananchi na ukaguzi wa kijamii;

(ii) Kuhuisha mchakato wa mabadiliko ya katiba;

(iii) Kuanzisha utaratibu wa kuajiri na kuteua watendaji wakuu na wajumbe wa bodi wa mashirika ya umma kwa njia ya

ushindani na upimaji unaozingatia matokeo (transparent and merit-based recruitment and appointment system);

(iv) Kujumuisha falsafa ya 4Rs katika mifumo ya utawala wa kitaifa na utumishi wa umma.

**Ugharamiaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31**

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano zinakadiriwa kuwa TZS trilioni 477. Hiki ni kiasi cha fedha kitakachohitajika kuwekezwa katika sekta za kimageuzi na vichocheo vya ukuaji wa uchumi, ikiwemo usafiri fungamanishi; nishati na uchimbaji; viwanda na biashara; kilimo; TEHAMA; mazingira na uhimilivu wa tabianchi; huduma za kijamii na maendeleo ya watu; utawala na utumishi wa umma; pamoja na utafiti na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vikuu vya rasilimali za kugharamia Mpango huu ni sekta binafsi na sekta ya umma kwa uwiano wa 70:30, ambapo sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza takribani TZS trilioni 324.49 (70%), taasisi za serikali (MDAs na LGAs) zitachangia TZS trilioni 115.04 (22%), na Mashirika ya Umma (PSCs) yatawekeza TZS trilioni 38.22 (8%).

**MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/2027**

**Maeneo ya Kipaumbele**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ni ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 - 2030/31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kimkakati yanayopendekezwa kupewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni:

(i) Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora;

(ii) Kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya kidijitali, nishati, na usafirishaji fungamanishi;

(iv) Kuimarisha sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji thamani na ukuaji jumuishi; na

(v) Kuimarisha uhifadhi wa mazingira na uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mwenendo wa Hali ya Uchumi**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Uchumi wa Taifa inaonesha kuwa Pato Halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2025 lilikua kwa wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na: uwekezaji wa Serikali katika miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuimarika kwa huduma za fedha na bima; pamoja na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.1 Juni 2025 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,971.5 Juni 2025, kiasi kilichotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa miezi 4.8. Thamani ya shilingi ya Tanzania

dhidi ya dola ya Marekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024/25, ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2023/24 ukionyesha kuimariaka kwa shilingi ya Tanzania ukilinganisha na dola ya kimarekani. Vilevile, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 15.9 mwaka 2024/25 na mikopo chechefu ilipungua hadi asilimia 3.3 kutoka asilimia 4.1 mwaka 2023/24 ikiashiria kuendelea kuimarika kwa ubora wa rasilimali za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha na malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2026/27 ni kama ifuatavyo:

(i) Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.9 katika kipindi cha muda wa kati;

(ii) Mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na wastani wa asilimia 17.1 katika kipindi cha muda wa kati;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27;

(v) Kuhakikisha misamaha ya kodi haizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa;

(vi) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(vii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

**Misingi ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/27 utajengwa katika misingi ifuatayo:

(i) Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji kustawi;

(ii) Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;

(iii) Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati na usafiri na usafirishaji, sambamba na matarajio ya Dira 2050 ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;

(iv) Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;

(v) Utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala chini ya falsafa ya 4Rs, unaolenga kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji;

(vi) Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji kupitia mashirikiano ya sekta binafsi (PPP) na ushirikiano wa kikanda (EAC na SADC);

(vii) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari zake.

## HITIMISHO

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka kwamba tumejiwekea malengo na matarajio makubwa katika Dira 2050 na mipango niliyowasilisha leo. Kazi kubwa tuliyo nayo sasa ni kutafsiri maono yaliyomo katika Dira 2050 na mipango ya maendeleo kuwa vitendo. Pengine hii ni kazi kubwa zaidi kuliko kupanga!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati akizindua rasmi Dira 2050 tarehe 17 Julai 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alieleza uzito na ukubwa wa malengo na matarajio tuliojiwekea katika Dira 2050 akisisitiza kuwa tunahitaji kujipanga kikamilifu katika utekelezaji wake. Aidha, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kubadili mtazamo katika utendaji, na kwamba ili kufikia malengo na matarajio tuliyojiwekea tunahitaji kufanya kazi kwa namna isiyo ya kawaida (business unusual). Tuache kufanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo itakayopitishwa na Bunge lako tukufu. Tumeandaa mfumo wa ufuatiliaji na upimaji unaozingatia kupima matokeo na uwajibikaji (Results-based Monitoring, Evaluation, Learning and Accountability Framework).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mpya wa ufuatiliaji na upimaji umejengwa katika nguzo tatu, ambazo ni: kuainisha vipaumbele bayana na kwa uwazi kwa kila sekta (prioritisation); nidhamu ya utekelezaji (discipline of implementation); na uwajibikaji (accountability). Katika kutekeleza mfumo huu, hatua zifuatazo zitatekelezwa:

(i) Kila sekta inayotekeleza programu na miradi ya maendeleo itapaswa kuweka malengo na viashiria vya utekelezaji vinayopimika, pamoja na mikakati mbalimbali itakayofanyika kufikia malengo hayo;

(ii) Taarifa ya utekelezaji itawasilishwa kwa Tume ya Taifa ya Mipango kila mwezi;

(iii) Mawaziri watawasilisha taarifa za utekelezaji kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kila baada ya miezi mitatu;

(iv) Tume ya Taifa ya Mipango itatoa taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa umma kila mwaka kupitia tukio la wazi; na

(v) Kwa kuzingatia Kifungu cha 7 cha Sheria ya Tume ya Mipango, 2023, Tume itakuwa na mamlaka ya kuitisha vikao vya viongozi wa juu wanaosimamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa lengo la kuratibu uchambuzi wa changamoto za utekelezaji na kusukuma utekelezaji wa suluhu zilizokubalika ili kuondoa vikwazo vya utekelezaji, kuboresha uratibu na kupata taarifa kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha hotuba hii, napenda kuwashukuru watumishi wenzangu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Nawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya (Mbunge wa Manyoni Mashariki), Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, pamoja na Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, kwa ushirikiano tulio nao katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Aidha, ninawashukuru wataalam wote wa Tume ya Taifa ya Mipango, wakiongozwa na Dkt. Mursali Milanzi, Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango (Mipango ya Kitaifa) na Bi Angela Shayo, Mkurugenzi (Mipango ya Kitaifa) kwa maandalizi mazuri ya nyaraka nilizowasilisha leo katika Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba Kamati yako ipokee, ijadili na kushauri kuhusu:

(i) Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27–2050/51;

(ii) Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31; na

(iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb.),
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**
Dodoma, Jumatatu, 02 Februari 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkubo, kwa taarifa hiyo.

Sasa ninamkaribisha Waziri wa Fedha Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar ili aweze kuwasilisha taarifa kutoka Wizara yake, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba kutumia fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana siku hii ya leo ili kuwasilisha na kujadili mapendekezo ya mwongozo ya bajeti ya mipango na bajeti ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati mwaka 2026/2027 hadi 2028/2029.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha pili. Hii inadhihirisha umahiri wa uongozi wake na moyo wa dhati wa kuwatumikia Watanzania ili kuwaletea maendeleo kwa kuboresha uchumi, miundombinu na huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa busara, hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar katika miaka mitano hii inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naye ninampongeza kwa uongozi wake makini ndani ya Serikali na hapa Bungeni pamoja na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala na Naibu Spika Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Sina shaka kuwa mtaendelea kutekeleza kwa umahiri majukumu ya kuliongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge mlioaminiwa na kuchaguliwa kuongoza vikao vya Bunge na kwa namna ya pekee ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na kuchaguliwa au kuteuliwa kuhudumu katika nafasi za Ubunge kwenye Bunge hili la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni imani yangu kuwa sote tutaungana na Mheshimiwa Rais katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitumie fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na ambaye pia amewahi kuhudumu kama Waziri katika Wizara mbalimbali pamoja na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia wafanyakazi. Mwenyezi

Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina. Sisi sote ni waja wa Mungu na kwake tutarejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kwanza kuwa Mbunge na baadaye msaidizi wake kama Waziri wa Fedha. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa nitaibeba dhamana hii kwa uadilifu, uwezo wangu wote na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mimi binafsi kwa kushirikiana na Naibu Mawaziri waliopo Wizarani kwangu pamoja na uongozi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake tupo tayari kutimiza wajibu wetu wa kushirikiana kwa karibu na Bunge wakati wote kwa lengo la kuimarisha zaidi usimamizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawasilisha mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti wa Serikali katika kipindi cha muda wa kati 2026/2027 hadi 2028/2029 mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kuzingatia matakwa ya kisheria kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 21.1 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni ya 116(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025. Lengo kuu la kuwasilisha mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuchambua, kutoa maoni na kushauri ili mapendekezo haya yaakisi ipasavyo matarajio ya wananchi na vipaumbele vya kuzingatiwa katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali kuwa Bunge lako litatoa mchango muhimu utakaoboresha mapendekezo haya na hatimaye kuyaridhia ili kuwa nyenzo rasmi katika maandalizi ya mipango na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti katika kipindi cha muda wa kati kwa mujibu wa sheria kama nilivyosema Sura 439 kama nyenzo mahususi ya kutoa mwelekeo wa kisera na kiutendaji katika kusimamia mipango

na uchumi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Mapendekezo ya mwongozo huu ni ya kwanza kuandaliwa chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2020-2050 na Mpango wa kKanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano chini ya Dira hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha mwongozo umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2025 pamoja na makubaliano ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kutoa mwelekeo wa sera za kibajeti zinazotabirika na kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanaakisi mikakati ambayo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya CCM imeendelea kutekeleza ili kuimarisha uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuzalisha fursa za ajira hasa kwa vijana, kuimarisha utoshelevu wa chakula nchini, kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii, kuimarisha miundombinu wezeshi kwa wajasiriamali na wawekezaji, kuongeza kasi ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, kuweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji hususan viwanda, kuendelea kuimarisha utawala bora na wa sheria na kudumisha amani, usalama, umoja na utulivu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa maandalizi wa mpango na baajeti wa Serikali katika kipindi cha muda wa kati unajumuisha taarifa juu ya mwenendo wa mwelekeo wa hali ya uchumi, vipaumbele vya mpango na bajeti, usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti wa mwaka 2024/2025 na miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/2026 na maelekezo mahususi ya kuzingatiwa wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti katika kipindi cha muda wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi. Pato halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 lilikuwa kwa wastani wa 5.8% ikilinganishwa na ukuaji wa 5.2% katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia yaani mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za madini, fedha na bima, kilimo na

ujenzi. Hata hivyo, lengo la ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025 linakadiriwa kufikia 5.9%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ukuaji wa pato halisi la Taifa unakadiriwa kuendelea kuongezeka kufikia 6.3% mwaka 2026 na wastani wa 6.9% katika kipindi cha muda wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2025 ulifikia wastani wa asilimia tatu nukta nne ikilinganishwa na wastani wa asilimia tatu nukta moja katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa ugavi wa bidhaa na mazao ya vyakula katika soko la ndani kufuatia ongezeko la mauzo ya nafaka kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kiwango hicho cha mfumuko wa bei kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia tatu hadi tano, lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutozidi asilimia nane na lengo la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la kati ya asilimia tatu hadi saba. Kwa kuzingatia mwelekeo wa shughuli za kiuchumi na kijamii, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la maeneo hayo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa migogoro ya kisiasa na mivutano ya kibiashara duniani, *geopolitics na tariff wars.* Katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2025, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi iliendelea kupungua na kufikia Dola za Marekani milioni 433.1 ikilinganishwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 632.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan utalii na bidhaa zisizo asilia sambamba na kasi ndogo ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/2026, thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za

nchi washirika wakuu wa kibiashara iliendelea kuimarika, ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,444.81 mwezi Novemba, 2025, ikilinganishwa na shilingi 2,659.03 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani ya shilingi kwa asilimia nane nukta moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huo ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Aidha, mabadiliko ya Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania kinachozuia matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani, yaliyochangia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2025, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 18.1, ikilinganishwa na asilimia 15.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mikopo chechefu ilipungua na kufikia asilimia tatu nukta moja mwezi Novemba, 2025, ikilinganishwa na asilimia tatu nukta sita katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia 2024, hali inayoashiria kuendelea kuimarika kwa ubora wa rasilimali za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Novemba, 2025, Deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 109.01 ikilinganishwa na shilingi trilioni 100.35 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia nane nukta sita. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo mipya na iliyosainiwa miaka ya nyuma kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba, 2025 inaonesha kuwa Deni la Serikali litaendelea kuwa himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika Kiambatisho Na. 1A cha Mpendekezo ya Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti, mwaka 2024/2025, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 50,291.4. Hadi Juni 30, 2025, Serikali ilikusanya na kutoa ridhaa ya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2, sawa na 99.1% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 34,845.9, misaada na mikopo nafuu shilingi bilioni 5,075.1 na mikopo ya ndani na nje ya kibiashara shilingi bilioni 9,900.3. Aidha, kati ya ridhaa ya matumizi iliyotolewa, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 34,418.4 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 15,402.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 ni pamoja na yafuatayo: -

(i) Kuvuka lengo la makusanyo ya mapato ya ndani kwa ufanisi wa 100.7% ambapo ufanisi wa *TRA* ulikuwa 102.3% na Mamlaka za Serikali za Mitaa 105.9%;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kielelezo na kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli ya SGR na miradi ya kuzalisha na kusambaza umeme;

(iii) Kulipa mishahara ya watumishi kwa wakati;

(iv) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha unaendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja;

(v) Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025;

(vi) Kuendelea kulipa malimbikizo ya madai; na

(vii) Kuendelea kuwekeza katika huduma za jamii ikiwemo maji, afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025/2026, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 56,490.3. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2025, mapato yalifikia shilingi bilioni 15,901.6, sawa na 98.2% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 16,693.9. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 13,105.5; mapato mengine yalikuwa shilingi bilioni 2,429.1 na misaada ilifikia shilingi bilioni 367.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ridhaa ya matumizi iliyotolewa isiyojumuisha malipo ya mtaji wa deni ilikuwa shilingi bilioni 20,831.1, sawa na 98.9% ya lengo la shilingi bilioni 21,068.6. Aidha, Serikali iligharamia nakisi kwa mikopo ya nje na ndani ya shilingi bilioni 6,979.4, sawa na 99.4% ya lengo la kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kiasi hicho, malipo ya mtaji yalikuwa shilingi bilioni 876.0 kwa mikopo ya ndani na shilingi bilioni 1,230.4 kwa mikopo ya nje. Hivyo, mikopo halisi kwa ajili ya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 4,873.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa awali uliofanywa unaonesha kuwa utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026 na muda wa kati unaweza kuathiriwa na mabadiliko ya sera za Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 27 Novemba, 2025, Bunge la Umoja wa Ulaya liliazimia kuahirisha utoaji wa fedha za msaada kwa mikataba mipya ambayo Serikali ilitarajia kuingia yenye thamani ya takribani *Euro* milioni 156, sawa na shilingi bilioni 445.75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mikataba inayoendelea, Serikali inaweza kukosa misaada ya kibajeti kutoka Umoja wa Ulaya yenye thamani ya takribani *Euro* milioni 39.20, sawa na shilingi bilioni 113.8 kwa mwaka 2025/2026 na shilingi bilioni 27.2 kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la kusitisha misaada pia limetolewa na nchi ya Sweden ambapo imesitisha kutoa *Crona (SEK)* za Sweden 119,552,997, sawa na shilingi bilioni 31 kwa ajili ya programu ya Elimu ya *Education for R* kwa mwaka 2025/2026 baada ya kulazimika kuongeza misaada zaidi kwa nchi ya Ukraine ambayo imeathiriwa na mgogoro wa kivita kati yake na Urusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mikakati ya Serikali ya kukabiliana na mabadiliko haya ni kuendelea kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuwianisha mapato na matumizi, pamoja na kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya msingi ikiwemo mishahara, deni la Serikali na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti katika kipindi cha muda wa kati. Misingi na shabaha za viashiria vya uchumi, misingi iliyotumika katika kuandaa malengo ya uchumi jumla ni pamoja na hii ifuatayo: -

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(iii) Uwepo wa uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani, kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi na maoteo yaliyofanyika, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa katika kipindi cha muda wa kati ni pamoja na haya yafuatayo: -

(i) Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia tano nukta tisa mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia sita nukta tatu mwaka 2026 na wastani wa asilimia sita nukta tisa katika muda wa kati;

(ii) Mfumuko wa bei kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya tatu mpaka tano;

(iii) Mapato ya ndani kufikia 17.1% ya pato la Taifa mwaka 2026/2027 na wastani wa 17.2%;

(iv) Mapato ya kodi kufikia 13.7% ya pato la Taifa mwaka 2026/2027 na wastani wa 13.7%;

(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia tatu ya pato la Taifa; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaanza kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031 ikiwemo kuwa na uchumi imara, jumuishi na shindani, kujenga uwezo wa rasilimali watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha msingi wa uendelevu wa Taifa na programu za kielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maeneo mahsusi ya kipaumbele katika matumizi ni kugharamia miradi ya kielelezo na kimkakati inayoendelea, deni la Serikali, mishahara ya watumishi, malimbikizo ya madai na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha muda wa kati, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 204,087.7, sawa na

wastani wa shilingi bilioni 68,029.2 kwa mwaka. Aidha, kwa mwaka 2026/2027, bajeti ya Serikali inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 61,934.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha muda wa kati, mapato ikijumuisha misaada yanakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 52,480.8, sawa na ukuaji wa wastani wa 12.1%. Kwa mwaka 2026/2027, mapato yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 46,691.3, ambapo mapato ya kodi ni shilingi bilioni 36,889.3, mapato mengine ni shilingi bilioni 9,238.8 ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya shilingi bilioni 1,966.2 na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 563.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo limezingatia misingi ya uchumi ya jumla na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa na Serikali ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika malipo na ukusanyaji wa mapato, kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi, urasimishaji wa sekta isiyo rasmi na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yatakayowezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha muda wa kati, matumizi bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali yanakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 59,250.1, sawa na ukuaji wa asilimia tisa nukta saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2026/2027, matumizi bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 54,098.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 48,775.0 mwaka 2025/2026, sawa na ongezeko la 10.9%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yanajumuisha stahiki za watumishi na michango ya pensheni shilingi bilioni 9,685.7; malipo ya riba shilingi bilioni 7,257.9; ununuzi wa mali zisizo za kifedha shilingi bilioni 3,030.4; na ruzuku kwa baadhi ya taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 22,909.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa usimamizi wa matumizi unalenga kutekeleza kwa ufanisi programu na miradi inayoendelea yenye matokeo ya haraka na kujenga msingi imara wa mageuzi ya kiuchumi, kufungamanisha utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo ili kuongeza tija ya rasilimali za umma na kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ili kuhakikisha uwajibikaji na thamani halisi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali wa Mwaka 2025/2026 – 2027/2028, Serikali inatarajia kukopa wastani wa shilingi bilioni 15,548.5 kwa mwaka katika kipindi cha muda wa kati kutoka vyanzo vya ndani na nje. Aidha, kwa mwaka 2026/2027, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,242.9 ambapo shilingi bilioni 7,407.3 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 7,835.6 kwa ajili ya malipo ya mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu vipaumbele na makadirio ya bajeti ya Serikali katika muda wa kati yameainishwa katika sura ya pili ya mwongozo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maelekezo mahsusi ya mwongozo katika kipindi cha muda wa kati. Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Kipindi cha Muda wa Kati umeainisha maelekezo mahususi ambayo Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti. Miongoni mwa maelekezo hayo ni pamoja na yafuatayo: -

(i) Maafisa Masuuli wanaosimamia mifuko yenye vyanzo maalum kutenga asilimia tano ya mapato ya mifuko husika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za msingi za mfuko kwenye miundombinu ya maeneo maalum ya kiuchumi ili kuvutia uwekezaji na kuongeza fursa za ajira;

(ii) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja asilimia tano kati ya 15%

inayopendekezwa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi. Mtakumbuka kwamba hapa kulikuwa na 10% ambayo ilitengwa kwa madhumuni haya, lakini pendekezo ni kuongeza asilimia tano katika mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya kuimarisha miundombinu katika halmashauri zetu; *(Makofi)*

(iii) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuandaa na kutekeleza mpango wa dharura wa kutokomeza ugonjwa wa Malaria ifikapo Desemba, 2030 na kuendelea kuratibu utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote;

(iv) Maafisa Masuuli kuzingatia mkakati wa kulinda wawekezaji wa ndani kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika zabuni, masharti ya mikataba na malipo ya hati za madai;

(v) Maafisa Masuuli kuandaa mikakati ya kuzalisha, kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa kupitia ushirikishaji katika utekelezaji wa dhana ya wazawa na kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu ili kuwezesha uibuaji wa fursa za ajira;

(vi) Taasisi na mashirika ya umma hususan yanayojiendesha kibiashara yaweke mikakati ya kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu ifikapo mwaka 2029; na

(vii) Miradi ambayo utekelezaji wake utakuwa haujakamilika kuelekea mwishoni mwa mwaka itengewe bajeti mwaka unaofuata kwa kuwa Serikali haitaruhusu mafungu kuvuka na ridhaa ya matumizi mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu maelekezo ya mwongozo yanapatikana katika sura ya nne ya mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kuridhiwa kwa mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati kutawezesha kukamilika kwa maandalizi ya Bajeti za Mafungu kwa wakati; kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarika kwa utawala bora wa utawala wa sheria na kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika uandaaji, utekelezaji pamoja na ufuatiliaji wa tathmini ya Mpango na Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati yaani 2026/2027 – 2028/2029 sambamba na Sheria ya Bajeti, Sura 439 na kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ninatumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ally Omar King, Mbunge wa Jang'ombe, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri wao wa kina wakati wa vikao vya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa katika kuboresha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati ninayowasilisha katika Bunge hili leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Mbunge wa Jimbo la Kavuu, na Mheshimiwa *Eng*. Mshamu Ali Munde, Mbunge wa Jimbo la Liwale, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mwalimu, Mtafiti, Mhadhiri, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, wasaidizi wake wote na watendaji wote kwa

ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ikiwemo maandalizi ya mapendekezo ya mwongozo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru sana Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, washirika wa maendeleo na wadau wengine kwa maoni na michango yao katika kukamilisha mapendekezo ya mwongozo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninawashukuru Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa ushirikiano ambao tunaendelea kupata katika Wizara zao katika utendaji wa Serikali na utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa Kamati ya Bunge lako Tukufu ipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati 2026/2027 - 2028/2029. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAELEKEZO YA WAZIRI WA FEDHA, MHE. BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI (2026/27 – 2028/29) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana siku ya leo ili kuwasilisha na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29). Kwa dhati kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge

wenzangu, kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Hii inajidhihirisha kutokana na uongozi wake mahiri na moyo wa dhati wa kuwatumikia watanzania ili kuwaletea maendeleo kwa kuboresha miundombinu na huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Aidha, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa busara, hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu.

2. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kipekee ninampongeza **Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu,** Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza kwa uongozi wake hodari ndani ya Serikali na hapa Bungeni pamoja na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za Serikali.

3. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** napenda pia kukupongeza wewe binafsi **Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu,** Mbunge wa Jimbo la Ilala, na **Naibu Spika Mheshimiwa Daniel Baran Sillo,** Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Ni imani yangu mtaendelea kutekeleza kikamilifu majukumu ya kuliongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi. Aidha, nawapongeza wenyeviti wa Bunge walioaminiwa na kuchaguliwa kuongoza vikao vya Bunge. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na kuchaguliwa au kuteuliwa kuhudumu katika nafasi za ubunge kwenye Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni imani yangu sote tutamsaidia Mheshimiwa Rais katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa letu.

4. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, napenda nitumie fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na ambaye pia amewahi kuhudumu

katika wizara mbalimbali pamoja na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (Wafanyakazi). Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi Amini. Innalillahi Wainnailayhi Raajiun!

5. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa moyo wa dhati nimshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Fedha. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na watanzania wote kuwa, nitaibeba dhamana hii kwa uadilifu, weledi na uwezo wangu wote. Aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mimi binafsi, kwa kushirikiana na Manaibu Waziri wangu, pamoja na uongozi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake, tupo tayari kushirikiana kwa karibu na Bunge wakati wote kwa lengo la kuimarisha zaidi usimamizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

6. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** nawasilisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29) mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa kuzingatia matakwa ya kisheria kama yalivyoainishwa katika Kifungu cha 21(1) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, pamoja na Kanuni ya 116(3)(i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zilizochapishwa mwezi Agosti 2025. Lengo kuu la kuwasilisha mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuchambua, kutoa maoni na kushauri ili mapendekezo haya yaakisi ipasavyo matarajio ya wananchi na vipaumbele vya maendeleo ya Taifa. Ni matarajio ya Serikali kuwa Bunge lako litatoa mchango muhimu utakaoboresha mapendekezo haya na hatimaye kuyaridhia ili kuwa nyenzo rasmi katika maandalizi ya mipango na bajeti ya Serikali.

7. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Serikali imeandaa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29) kwa mujibu wa Kifungu cha 21(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kama nyenzo mahsusi ya kutoa mwelekeo wa kisera na kiutendaji katika kusimamia mipango na uchumi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Mapendekezo ya Mwongozo huu ni ya kwanza kuandaliwa chini ya Dira ya Taifa ya

Maendeleo 2050 na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31. Aidha, Mwongozo umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 pamoja na makubaliano ya kikanda na kimataifa, kwa lengo la kutoa mwelekeo wa sera za kibajeti zinazotabirika na kuaminika.

8. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mapendekezo haya yanaakisi mikakati ambayo Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya CCM, imeendelea kutekeleza ili kuimarisha uchumi na kuboresha maisha ya watanzania. Mikakati hiyo ni pamoja na: kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; kuzalisha fursa za ajira hasa kwa vijana; kuimarisha utoshelevu wa chakula nchini; kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii; kuimarisha miundombinu wezeshi kwa wajasiriamali na wawekezaji; kuongeza kasi ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; kuweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji na viwanda; kuendelea kuimarisha utawala bora na wa sheria; na kudumisha amani, usalama, umoja na utulivu nchini.

9. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Muda wa Kati unajumuisha mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; vipaumbele vya mpango na bajeti; usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti; mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25 na miezi mitano ya kwanza kwa mwaka 2025/26; na maelekezo mahsusi ya kuzingatiwa wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti katika kipindi cha muda wa kati.

## 2.0 MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI

10. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Pato halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2025 lilikua kwa wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za madini, fedha na bima, kilimo na ujenzi. Hata hivyo, uchambuzi wa awali uliofanywa kuhusiana na athari za matukio ya wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 inaonesha uwezekano wa kupungua kwa kasi ya ukuaji wa

uchumi, hususan katika robo ya nne ya mwaka 2025. Hivyo, lengo la ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025 linakadiriwa kufikia asilimia 5.9. Aidha, ukuaji wa Pato halisi la Taifa unakadiriwa kuendelea kuongezeka kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 na wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha muda wa kati.

11. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* mfumuko wa bei katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025 ulifikia wastani wa asilimia 3.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa ugavi wa bidhaa na mazao ya vyakula katika soko la ndani kufuatia ongezeko la mauzo ya nafaka kwenda nchi jirani. Hata hivyo, kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 3.0 hadi 5.0, lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutozidi asilimia 8.0 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0. Kwa kuzingatia mwelekeo wa shughuli za kiuchumi na kijamii, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo.

12. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa migogoro ya kisiasa na mivutano ya kibiashara duniani (geopolitics). Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi iliendelea kupungua na kufikia dola za Marekani milioni 433.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 632.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan utalii na bidhaa zisizo asilia sambamba na kasi ndogo ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi.

13. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26, thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara iliendelea kuwa imara, ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,444.81 mwezi Novemba 2025, ikilinganishwa na shilingi 2,659.03 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani ya shilingi kwa asilimia 8.1. Mwenendo huo ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na

shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Aidha, mabadiliko ya Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania kinachozuia matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani, yalichangia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini.

14. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Januari na Novemba 2025, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 18.1, ikilinganishwa na asilimia 15.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi. Vilevile, mikopo chechefu ilipungua na kufikia asilimia 3.1 mwezi Novemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, hali inayoashiria kuendelea kuimarika kwa ubora wa rasilimali za benki.

15. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, hadi Novemba 2025, Deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 109.01 ikilinganishwa na shilingi trilioni 100.35 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo mipya na iliyosainiwa miaka ya nyuma kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. Aidha, tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba 2025 inaonesha kuwa deni la Serikali litaendelea kuwa himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

16. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1A cha Mpendekezo ya Mwongozo**.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

17. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mwaka 2024/25, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 50,291.4. Hadi Juni 30, 2025, Serikali ilikusanya na kutoa ridhaa ya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2, sawa na asilimia 99.1 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 34,845.9, misaada na mikopo nafuu shilingi bilioni 5,075.1, na mikopo ya ndani na nje ya kibiashara shilingi

bilioni 9,900.3. Aidha, kati ya ridhaa ya matumizi iliyotolewa, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 34,418.4 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 15,402.7.

18. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na: kuvuka lengo la makusanyo ya mapato ya ndani kwa ufanisi wa asilimia 100.7 ambapo ufanisi wa TRA ulikuwa asilimia 102.3 na Mamlaka za Serikali za Mitaa asilimia 105.9; kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kielelezo na kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli ya SGR na miradi ya kuzalisha na kusambaza umeme; kulipa mishahara ya watumishi kwa wakati; kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha unaendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja; kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025; kuendelea kulipa malimbikizo ya madai; na kuendelea kuwekeza katika huduma za jamii ikiwemo maji, afya na elimu.

19. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mwaka 2025/26, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 56,490.3. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, mapato yalifikia shilingi bilioni 15,901.6, sawa na asilimia 98.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 16,693.9. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 13,105.5; mapato mengine yalikuwa shilingi bilioni 2,429.1; na misaada ilifikia shilingi bilioni 367.0. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa (isiyojumuisha malipo ya mtaji wa deni) ilikuwa shilingi bilioni 20,831.1, sawa na asilimia 98.9 ya lengo la shilingi bilioni 21,068.6. Aidha, Serikali iligharamia nakisi kwa mikopo ya nje na ndani ya shilingi bilioni 6,979.4, sawa na asilimia 99.4 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, malipo ya mtaji yalikuwa shilingi bilioni 876.0 kwa mikopo ya ndani na shilingi bilioni 1,230.4 kwa mikopo ya nje. Hivyo, mikopo halisi kwa ajili ya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 4,873.0.

20. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** uchambuzi wa awali uliofanywa unaonesha kuwa utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 na muda wa kati unaweza kuathiriwa na mabadiliko ya sera za Washirika wa Maendeleo. Mnamo tarehe 27 Novemba 2025, Bunge la Umoja wa Ulaya liliazimia kuahirisha utoaji wa fedha za

msaada kwa mikataba mipya ambayo Serikali ilitarajia kuingia yenye thamani ya takribani EUR milioni 156, sawa na shilingi bilioni 445.75. Kwa mikataba inayoendelea, Serikali inaweza kukosa misaada ya kibajeti kutoka Umoja wa Ulaya yenye thamani ya takribani EUR milioni 39.20, sawa na shilingi bilioni 113.8 kwa mwaka 2025/26 na shilingi bilioni 27.2 kwa mwaka 2026/27.

21. ***Mweshimiwa Mwenyekiti,*** nchi nyingine iliyotoa tamko la kusitisha misaada ni Sweden ambapo imesitisha kutoa SEK 119,552,997, sawa na shilingi bilioni 31 kwa ajili ya programu ya elimu ya EpforR kwa mwaka 2025/26 baada ya kulazimika kuongeza misaada zaidi kwa nchi ya Ukraine iliyoathiriwa na mgogoro wa kivita kati yake na Urusi. Miongoni mwa mikakati ya Serikali ya kukabiliana na mabadiliko haya ni kuendelea kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuwianisha mapato na matumizi, pamoja na kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya msingi ikiwemo mishahara, deni la Serikali na huduma za jamii.

## 4.0 MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI

### 4.1 Misingi na Shabaha za Viashiria vya Uchumi Jumla

22. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, misingi iliyotumika katika kuandaa malengo ya uchumi jumla ni pamoja na:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;
(ii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
(iii) Uwepo wa uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;
(iv) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula; na
(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani, kikanda na kimataifa.

23. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kutokana na uchambuzi na maoteo yaliyofanyika, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa katika kipindi cha muda wa kati ni pamoja na:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.3 mwaka 2026 na wastani wa asilimia 6.9 katika muda wa kati;
(ii) Mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0;
(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na wastani wa asilimia 17.2;
(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na wastani wa asilimia 13.7;
(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na
(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 4.2 Maeneo ya Vipaumbele

24. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaanza kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 ikiwemo uchumi imara, jumuishi na shindani; kujenga uwezo wa rasilimali watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; kuimarisha msingi wa uendelevu wa Taifa; na programu za kielelezo. Aidha, maeneo mahsusi ya kipaumbele katika matumizi ni kugharamia miradi ya kielelezo na kimkakati inayoendelea; deni la Serikali; mishahara ya watumishi; malimbikizo ya madai; na huduma za jamii.

### 4.3 Mapendekezo ya Mfumo wa Mapato na Matumizi ya Serikali

25. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* katika kipindi cha muda wa kati (2026/27 – 2028/29), Serikali inatarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 204,087.7, sawa na wastani wa shilingi bilioni 68,029.2 kwa mwaka. Aidha, kwa mwaka 2026/27, bajeti ya Serikali inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 61,934.2.

26. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* katika kipindi cha muda wa kati, mapato ikijumuisha misaada yanakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 52,480.8, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 12.1. Kwa mwaka 2026/27, mapato yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 46,691.3, ambapo mapato ya kodi ni shilingi bilioni 36,889.3, mapato mengine ni shilingi bilioni 9,238.8 (ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya shilingi bilioni 1,966.2) na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 563.1. Ongezeko hilo limezingatia misingi ya uchumi jumla na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa na Serikali ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika malipo na ukusanyaji wa mapato, kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi, urasimishaji wa sekta isiyo rasmi na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yatakayowezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

27. ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* katika kipindi cha muda wa kati, matumizi (bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali) yanakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 59,250.1, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 9.7. Kwa mwaka 2026/27, matumizi bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 54,098.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 48,775.0 mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Matumizi yanajumuisha stahiki za watumishi na michango ya pensheni shilingi bilioni 9,685.7; malipo ya riba shilingi bilioni 7,257.9; ununuzi wa mali zisizo za kifedha shilingi bilioni 3,030.4; na ruzuku kwa baadhi ya taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 22,909.2. Mikakati ya usimamizi wa matumizi inalenga kutekeleza kwa ufanisi programu na miradi inayoendelea yenye matokeo ya haraka na kujenga msingi imara wa mageuzi ya kiuchumi, kufungamanisha utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo ili kuongeza tija ya rasilimali za umma, na kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ili kuhakikisha uwajibikaji na thamani halisi ya fedha.

28. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali (2025/26 – 2027/28), Serikali inatarajia kukopa wastani wa shilingi bilioni 15,548.5 kwa mwaka katika

kipindi cha muda wa kati kutoka vyanzo vya ndani na nje. Aidha, kwa mwaka 2026/27, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,242.9 ambapo shilingi bilioni 7,407.3 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 7,835.6 kwa ajili ya malipo ya mtaji.

29. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, maelezo ya kina kuhusu vipaumbele na makadirio ya bajeti ya Serikali katika muda wa kati yameainishwa katika **Sura ya Pili ya Mwongozo**.

### 4.4 Maelekezo Mahsusi ya Mwongozo Katika Kipindi cha Muda wa Kati

30. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 - 2028/29) umeainisha maelekezo mahsusi ambayo Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti. Miongoni mwa maelekezo hayo ni:

(i) Maafisa Masuuli wanaosimamia mifuko yenye vyanzo maalumu kutenga asilimia tano (5) ya mapato ya mifuko husika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za msingi za Mfuko kwenye miundombinu ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZs & EPZs) ili kuvutia uwekezaji na kuongeza fursa za ajira;

(ii) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja asilimia tano (5) kati ya asilimia 15 inayopendekezwa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;

(iii) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kuandaa na kutekeleza mpango wa dharura wa kutokomeza ugonjwa wa malaria ifikapo Desemba 2030 na kuendelea kuratibu utekelezaji wa bima ya afya kwa wote;

(iv) Maafisa Masuuli kuzingatia mkakati wa kulinda wawekezaji wa ndani kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika zabuni, masharti ya mikataba na malipo ya hati za madai;

(v) Maafisa Masuuli kuandaa mikakati ya kuzalisha, kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa kupitia ushirikishaji katika utekelezaji wa dhana ya wazawa na kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu ili kuwezesha uibuaji wa fursa za ajira;

(vi) Taasisi na mashirika ya umma hususan yanayojiendesha kibiashara yaweke mikakati ya kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu ifikapo Juni 2029; na

(vii) Miradi ambayo utekelezaji wake utakuwa haujakamilika kuelekea mwishoni mwa mwaka zitengewe bajeti mwaka unaofuata kwa kuwa Serikali haitaruhusu mafungu kuvuka na ridhaa ya matumizi mwisho wa mwaka.

31. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, maelezo ya kina kuhusu maelekezo ya Mwongozo yanapatikana katika **Sura ya Nne ya Mwongozo**.

## 5.0 Hitimisho

32. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kuridhiwa kwa mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati kutawezesha kukamilika kwa maandalizi ya Bajeti za Mafungu kwa wakati; kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarika kwa utawala bora na utawala wa sheria; na kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika uandaaji, utekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya Mpango na Bajeti.

Hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo

yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29) sambamba na Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake.

33. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki - Mbunge wa Maswa Magharibi, pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ally Omar King - Mbunge wa Jang'ombe, kwa maoni na ushauri wao mzuri wakati wa vikao vya Kamati. Maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa katika kuboresha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29) ninayowasilisha katika Bunge hili leo.

34. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ninatoa shukrani zangu pia kwa Manaibu Waziri wa Fedha, **Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula** – Mbunge wa Jimbo la Kavuu, na **Mheshimiwa Eng. Mshamu Ali Munde** – Mbunge wa Jimbo la Liwale, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na **Katibu Mkuu**, **Dkt. Natu El-maamry Mwamba** kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ikiwemo maandalizi ya mapendekezo ya Mwongozo. Aidha, ninawashukuru sana Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine kwa maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mwongozo huu.

35. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 - 2028/29).

36. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, naomba kuwasilisha.

Balozi Khamis Mussa Omar (Mb)
**WAZIRI WA FEDHA**
02 Februari, 2026

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar. Waziri wetu wa Fedha kwa taarifa hiyo.

Sasa ninamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki kwa ajili ya maoni na mapendekezo ya Kamati.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaotaka kuusoma, ni muhtasari wa Tarifa ya Kamati. Hivyo naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka 25 (2026/2027 - 2050/2051); Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2026/2027 - 2030/2031); Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja (2026/2027); pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Muda wa Kati (2026/2027 - 2028/2029).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge lina majukumu ya kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vifungu vya 8(1)(b), 9(1)(a), 21(1)(2) na (5) vya Sheria ya Bajeti Sura ya 439 vinabainisha majukumu ya Bunge pamoja na Kamati ya Bajeti katika kuchambua na kuidhinisha Mpango na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 116(4) na Kanuni ya (6)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Maoni na Mapendekezo ya

Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka 25; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja; pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Muda wa Kati (2026/2027- 2028/2029).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nane kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati ambayo mnayo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo Mwaka 2050; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 yenye dhima ya kujenga Taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea, ni ya pili kuandaliwa baada ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo iliandaliwa mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira imeweka misingi mitano ili tuweze kufikia malengo. Misingi hiyo ni demokrasia, haki na uhuru, utu, amani na umoja, utajiri wa rasilimali asilia pamoja na utamaduni na maadili ya Taifa. Uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini nguzo kuu inayoshikilia misingi yote hiyo ni amani na umoja. Bila amani na umoja hakuna litakalowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza Watanzania na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kulinda na kudumisha amani ya Taifa letu chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai ya Kamati kwa Watanzania wote ili tuweze kufikia malengo yetu ni kuendelea kulinda amani ya Taifa letu kwa wivu mkubwa kwa sababu endapo ikipotea hakuna aliye salama na malengo ya dira hii yatakuwa ni ndoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malengo ya dira; dira imekusudia kufikia malengo manne na shabaha 17. Malengo hayo ni:-

(i) Uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani;

(ii) Maisha bora na ustawi kwa wote;

(iii) Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi; na

(iv) Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijiti katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wa malengo na shabaha zote za dira, kulibainika kuwepo na wasiwasi kuhusu utekelezaji wake. Wasiwasi huo ni sawa na ule uliobanishwa kwenye aya ya 2.2.4. *Ineffective Implementation Syndrome* ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, na hapa nanukuu: "*Tanzanians have developed a propensity to prepare and pronounce plans and programmes which are not accompanied by effective implementation, monitoring and evaluation mechanisms. As a result, implementation has been weak.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inamaanisha Watanzania wamekuwa na hulka ya kuandaa mipango na programu ambayo mara nyingi imekuwa haina mpangilio mzuri wa utekelezaji, uratibu na taratibu za tathmini. Matokeo yake utekelezaji wa mipango na programu hizo umekuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai ya Kamati kwa Serikali, ni lazima tuwe na mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini ili tuweze kufikia malengo na shabaha tulizojiwekea. La sivyo, changamoto iliyojitokeza itaendelea kuathiri utekelezaji wa mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Miaka 25, (2026/2027 - 2050/2051) wenye dhima ya "Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi,

Haki na Linalojitegemea" ndiyo nyenzo kuu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Mpango wa aina hii ni wa pili nchini kuandaliwa, wa kwanza ulikuwa kati ya Mwaka 2011/2012 - 2025/2026 uliokuwa na dhima ya "Mpango kazi wa Kuifikisha nchi kwenye Kipato cha Kati."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misingi ya kufikia malengo; Mpango umeainisha misingi mikuu mitatu ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya dira 2050. Misingi hiyo ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati, lakini michache kwa kuitaja, kuna moja kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umekusudia kuboresha utawala bora, demokrasia, usalama, na utulivu. Baadhi ya masuala yatayotekelezwa ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuajiri Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri *(DEDs)* kwa kuzingatia sifa na uwezo kupitia mchakato wa wazi na wenye ushindani na watatambulika kama Wakurugenzi Wakuu wa maendeleo ya ndani ili kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, watatakiwa kuingia mikataba ya ufanisi ili kusimamia utendaji kazi wao. Lengo la mapendekezo haya ni kuimarisha utendaji kazi wa Serikali za Mitaa na kuzipa nguvu ya kiutendaji pamoja na kuimarisha uwezo wa kukusanya mapato ili zijitegemee. Vilevile, Mpango umekusudia kuboresha miundombinu ya usalama kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa mapendekezo hayo, hata hivyo ina maoni na ushauri ufuatao: -

(i) Mikataba ya utendaji kazi isiishie kwa Wakurugenzi wa Halmashauri peke yao, bali itumike hata kwa Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji; na

(ii) Serikali ihakikishe kwamba utaratibu wa ugawaji rasilimali fedha kutoka Serikali Kuu unakuwa linganifu kwa kuangalia

uwezo wa halmashauri kujitegemea na uwekezaji unaoweza kuchochea ukuaji wa sekta katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni kuimarisha mageuzi ya kifikra na kimtazamo. Ili kufanikisha Mpango huu, ni lazima kubadili fikra na mtazamo wa wananchi kwamba ni Serikali pekee inawajibika kutoa huduma zote za kijamii na badala yake kuona jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ya utoaji huduma. Kamati imechambua mikakati iliyobainishwa na Serikali, na ina ushauri ufuatao: -

(i) Serikali ibadili mtazamo wake wa kimsingi kutoka kuwa mtoa huduma wa kila shughuli na kuwa mratibu wa sera na mlinzi wa kanuni na mwezeshaji wa mazingira ya biashara na uvumbuzi;

(ii) Kubadili utamaduni wa Utumishi wa Umma kutenda kazi kwa mazoea na badala yake kuzingatia matokeo na tija;

(iii) Kuandaa raia wanaowajibika kwa Taifa lao kwa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo, ulipaji kodi, maadili ya kazi pamoja na uzalishaji;

(iv) Wananchi kubadili fikra ya namna wanavyojadili matatizo yanayolikabili Taifa, kutoka kuilaumu Serikali na badala yake kutafuta suluhu ya matatizo hayo; na

(v) Kuunganisha sera na mabadiliko ya fikra zinazolenga kujenga kizazi chenye maadili, uwajibikaji, nidhamu na chenye uwezo wa kutambua fursa na kuzitumia kwa ajili ya maendeleo kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 36(2), ninaongeza muda wa nusu saa ili Mwenyekiti aweze kukamilisha Taarifa yake. *(Makofi)*

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maeneo ya Kielelezo katika Programu, Mapendekezo ya Mpango Elekezi umeainisha programu 14 kama zinavyoonekana kwenye Taarifa za Kamati za kielelezo zenye uwezo wa kuchochea na kuharakisha mageuzi ya kiuchumi, kufungua fursa za uwekezaji na kuchochea ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maeneo hayo yanatoa mwongozo wa uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano hadi mwaka 2050, kwa kuhakikisha kunakuwa na mwendelezo wa programu na miradi mikubwa ambayo bado haijakamilika kutoka Mpango Elekezi wa Mwaka 2025, hususan katika sekta za nishati, usafirishaji na uchukuzi, pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mapendekezo hayo, kwani kukamilika kwa miradi hii kutaleta manufaa na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Elekezi wa Muda Mrefu utagharimu Dola za Marekani bilioni 3,582 na kati ya kiasi hicho sekta binafsi inatarajiwa kuchangia 70% na sekta ya umma kuchangia 30%. Kati ya 70% ya mchango wa sekta binafsi, 13% itachangiwa na sekta za ndani na 57% itatokana na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje *(FDIs)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa 30% ya mchango wa sekta ya umma, 22% zitatokana na mapato ya kodi, yasiyo ya kodi na mikopo na asilimia nane zitachangiwa na mashirika. Vilevile, Serikali imepanga kutenga uwiano wa 60:40 wa bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Jedwali Namba moja

linaonesha mchanganuo wa mahitaji ya fedha kwa kila Mpango wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa vyanzo vya ugharamiaji wa Mpango na ina ushauri ufuatao: -

(i) Serikali kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Hatua hii iende sambamba na kuipatia Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kiasi cha shilingi bilioni 480 kwa ajili ya ujenzi, uboreshaji na ukamilishaji wa mifumo;

(ii) Mpango umeelekeza Mashirika na Taasisi za Serikali kuchangia asilimia nane katika utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, Mashirika haya yamekuwa na ufanisi mdogo kwenye ukusanyaji wa mapato ukizingatia kuwa Serikali imewekeza takribani shilingi trilioni 86.3. Ni dhahiri mashirika haya yanahitaji kuongeza ufanisi ili kufikia lengo;

(iii) Sekta binafsi katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ilitarajiwa kuchangia shilingi trilioni 40.61 sawa na 35% ya gharama za Mpango. Hata hivyo, hadi Kamati inakamilisha Taarifa hii haikuwa imepokea taarifa ya mchango wa sekta binafsi katika kugharamia mpango huo kwa kipindi cha miaka minne na nusu iliyopita. Hivyo Kamati ilishindwa kupima ni kwa kiasi gani malengo ya 70% yataweza kufikiwa. Hivyo kuna haja ya Serikali kuanzisha utaratibu wa kutambua na kutunza takwimu za uwekezaji wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo; na

(iv) Kushirikisha mapema sekta binafsi katika kupanga na kusanifu miradi na kufanya maamuzi ya haraka na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji na tathmini ni nguzo muhimu katika kuhakikisha mpango unatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kutoa taarifa sahihi za utekelezaji wa

mpango, kubaini changamoto mapema, kuhakikisha uwajibikaji pamoja na matumizi bora ya rasilimali fedha. Hata hivyo, hakuna mwongozo wa kisheria unaoongoza suala zima la ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Serikali iweze kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya Serikali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza masuala yafuatayo: -

(a) Kutunga Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini itakayosimamia masuala yote ya ufuatiliaji na tathmini na hivyo kuleta ufanisi na uwajibikaji; na

(b) Serikali ifanye tathmini ya umuhimu wa kuwa na mamlaka moja itakayosimamia jukumu la ufuatiliaji na tathmini ya mipango na shughuli za Serikali ili kuongeza ufanisi wa jukumu hilo. Hivi sasa, Tume ya Mipango inafanya ufuatiliaji na tathmini ya Mipango ya Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu ikifanya tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mapendekezo ya Serikali katika mpango wa muda mrefu ni kutenganisha mashirika katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusisha mashirika ya Serikali yanayotoa huduma na hayajiendeshi kwa misingi ya kibiashara; na kundi la pili ni mashirika yanayojiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, inapendekezwa mashirika yanayojiendesha kibiashara yabaki chini ya uongozi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na yanayotoa huduma yasimamiwe na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huo pamoja na kwamba una nia njema ya usimamizi, Kamati inaishauri Serikali kuuangalia upya kwa sababu hata mashirika yanayotoa huduma lazima yawe na msimamizi atakayeweka vigezo vya utoaji huduma kwa ufanisi na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara zina majukumu ya kusimamia utendaji wa kisera na siyo utendaji wa kila siku wa mashirika. Hivyo, kurejesha majukumu ya usimamizi kwenye wizara kutazorotesha utendaji kazi wa mashirika hayo. Aidha, Kamati inadhani ni wakati mwafaka wa Serikali kurejesha Bungeni Muswada wa Sheria ya kuunda upya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027–2030/2031) ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Mwaka 2050 na wa nne tangu uanzishwe utaratibu wa kutekeleza Mipango ya miaka mitano. Aidha, Mpango huu una lengo la kuweka msingi imara wa utekelezaji wa sera za kiuchumi, kijamii na miundombinu itakayoharakisha maendeleo endelevu ya Taifa na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango unalenga kufikia pato la Taifa *(nominal GDP)* la Dola za Marekani bilioni 118.052, ukuaji wa pato la Taifa halisi *(real GDP)* wa 10.5% pamoja na pato la Taifa kwa kila mtu la Dola za Marekani 1,638 ifikapo mwaka 2031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo mahsusi yanayoweka msingi wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano. Kamati imefanya uchambuzi wa malengo mahsusi ya mapendekezo ya mpango na inaishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kutekeleza kikamilifu Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na uwekezaji nchini (MKUMBI) ili kuondoa vikwazo vya biashara na kuendeleza mazingira ya uwekezaji yanayowezesha sekta binafsi kushindana kikanda na Kimataifa;

(ii) Kuwekeza katika miundombinu wezeshi ya usafiri na usafirishaji mfano bandari, reli, viwanja vya ndege, barabara ili kuharakisha shughuli za ugavi;

(iii) Kuendeleza elimu na ujuzi ili kukuza uwezo wa rasilimali watu, kuboresha miundombinu ya msingi ya huduma za jamii, kusimamia kikamilifu sera na sheria za utunzaji mazingira pamoja na kuimarisha mifumo na kusimamia taasisi za utoaji haki;

(iv) Kuanzisha na kuendeleza vyuo vya kitaaluma vitakavyotoa wataalamu wenye ujuzi mahsusi kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati ili kujenga nguvu kazi yenye weledi na uwezo wa kuchangia kikamilifu katika sekta za uzalishaji na huduma; na

(v) Kutumia teknolojia ya kisasa katika uzalishaji wa bidhaa ambazo Tanzania ina nguvu ya kiushindani, kupata ithibati ya bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na kuimarisha masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa viashiria vya utulivu wa uhimilivu wa uchumi jumla na inapendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, mfumuko wa bei unabaki katika kiwango kisichozidi asilimia tano. Endapo mfumuko wa bei utazidi lengo lililowekwa, utaathiri viashiria vingine vya uchumi ikiwemo kupanda kwa riba za mikopo ambazo zitaathiri ukuaji wa sekta binafsi, kushusha thamani ya shilingi, pamoja na kuongezeka kwa gharama za kukopa katika soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Usimamizi Bora wa Deni la Taifa, Serikali ihakikishe katika wakati wote wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano inakopa kwa kuzingatia Masharti ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134. Aidha, mikopo yote inayokopwa na Serikali ielekezwe kwenye miradi na shughuli zenye uwezo wa kuzalisha mapato yatakayosaidia kurejesha mikopo hiyo na siyo vinginevyo. Jedwali namba nne linaonesha viashiria vya kuimarisha Sera za Kibajeti na Kifedha zinazotabirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba deni letu ni himilivu, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, ili kufikia malengo ya viashiria hivyo, ni lazima Serikali ihakikishe inaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa kodi na kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidigitali katika ukusanyaji. Hatua hii iende sambamba na kudhibiti matumizi ya Serikali yasiyo na tija, kuwekeza kwenye miradi yenye manufaa kiuchumi pamoja na kuboresha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano Serikali imekusudia kufanya mageuzi katika sekta mbalimbali ambazo ndiyo nguzo za mabadiliko ya nchi kuelekea uchumi imara wenye ushindani na unaongozwa na mauzo nje ya nchi. Mageuzi ya kisekta yanakusudia kubadilisha sera, sheria, miundo ya uendeshaji, matumizi ya teknolojia mpya, kuboresha mbinu za utoaji huduma pamoja na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imechambua mikakati ya mageuzi yanayotarajiwa kufanyika katika sekta husika kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo na ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuboresha sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maghala na mabwawa ya umwagiliaji, upatikanaji wa mbegu, mbolea ya ruzuku na pembejeo za kisasa, kuongezeka kwa bajeti ya sekta ya kilimo kufikia shilingi trilioni 1.24 na uanzishwaji wa Benki ya Ushirika Tanzania. Hata hivyo, ili kufikia malengo yanayotarajiwa, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kudhibiti upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kwa kuwa na maghala, vihenge na vyumba vya baridi vya kutosha ambavyo vitakodishwa kwa wananchi, ili wavitumie kuhifadhi mazao yao na hivyo kupunguza upotevu;

(ii) Benki Kuu kuendelea kulegeza masharti ya utoaji wa mkopo wa dirisha maalum wa shilingi trilioni moja kwa benki za

biashara zinazotoa mikopo ya kilimo baada ya kujiridhisha kwamba, mikopo hiyo inaelekezwa kwenye kilimo cha uzalishaji badala ya biashara ya mazao ya kilimo;

(iii) Kuwekeza zaidi katika upatikanaji wa mbegu bora, miradi ya umwagiliaji, zana za kilimo pamoja na uhifadhi;

(iv) Kuendelea na jitihada za kuhimilisha mifugo pamoja na kuanzisha, kufufua na kuendeleza viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo; na

(v) Kutekeleza na kukamilisha miradi ya kilimo kwa wakati, ili kupunguza gharama na kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa shabaha zinazotarajiwa kufikiwa na Sekta ya Viwanda na Uzalishaji ifikapo mwaka 2030/2031 na ina ushauri na maoni yafuatayo: -

(i) Kuunganisha mamlaka zote za udhibiti na kuanzisha mamlaka moja, ili kupunguza wingi wa mamlaka za udhibiti pamoja na kuwa na mfumo mmoja wa malipo *(single payment system)* utakaotumiwa na wafanyabiashara kulipa ada, tozo, leseni na faini zote za mamlaka za udhibiti kwa wakati mmoja;

(ii) Kuhamasisha viwanda vilivyopo kutumia teknolojia ya kisasa, hatua hii iende sambamba na upatikanaji wa nishati ya uhakika na nafuu, ili kupunguza gharama za uzalishaji;

(iii) Kuweka vivutio kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa ambazo zinachochea uanzishwaji wa viwanda vingine; na

(iv) Serikali kuhakikisha inatenga walau asilimia moja nukta tano ya bajeti kila mwaka, kwa ajili ya utafiti na maendeleo ikilinganishwa na bajeti inayotengwa hivisasa ya chini ya asilimia sifuri nukta tano. Hatua hii itasaidia kuongeza ubunifu na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua umuhimu wa sekta ya utalii kwenye uchumi ambapo mwaka 2024 ilichangia 27% kwenye pato la Taifa na kuiletea nchi fedha za kigeni zilizoongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 3.37 mwaka 2023 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024. Ufanisi huu umetokana na kuongezeka kwa idadi toka watalii milioni 1.8 mwaka 2023 hadi watalii milioni 2.14 Mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa shabaha za sekta ya utalii zinazotarajiwa kufikiwa na inashauri kuimarisha miundombinu ya utaalii, kuhamasisha utalii wa picha, michezo, matibabu, mikutano, fukwe za bahari, utamaduni, urithi wa kihistoria pamoja na kuendelea kuboresha jumuiya za hifadhi za wanyamapori. Hatua hii itasaidia kuongeza shughuli za utalii na kuboresha sekta za huduma za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi ifikapo Mwaka 2030/31 mapato yanayotokana na biashara ya hewa ukaa yanatarajiwa kuwa Dola za Marekani bilioni tatu na ushiriki wa jamii katika miradi ya biashara ya hewa ukaa kuongeza kufikia kati ya 10% hadi 15% ikilinganishwa na asilimia tano ya mwaka 2024. Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kujenga mfumo wa kisasa wa kidigitali wa upimaji, utoaji ripoti na uthibitishaji *(Measurement, Reporting and Verification - MRV)* utakaotumika kubainisha thamani ya misitu katika biashara ya kaboni; na

(ii) Kuhakikisha biashara ya hewa ukaa inakuwa shirikishi kwa wananchi, ili wawe walinzi wa mazingira kwa kuwa, wao ndio wanufaika wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugharamiaji wa Mpango, katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Miaka Mitano, uwekezaji unaohitajika unakadiriwa kuwa shilingi trilioni 477.8 sawa na dola za Marekani bilioni 183. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 324.5 sawa na

70% zinatarajiwa kuchangiwa na sekta binafsi na shilingi bilioni 153.26 sawa na 30% zinatarajiwa kuchangiwa na sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ugharamiaji wa Mpango unaonesha nia ya dhati ya Serikali kutoa kipaumbele kwa sekta binafsi, kama injini ya ukuaji wa uchumi. Aidha, ili kuhakikisha Serikali inafikia malengo yaliyokusudiwa ya kugharamia Mpango wa Nne wa Miaka Mitano, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na kuendelea kutoa upendeleo kwa wawekezaji wa ndani katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Nne wa Miaka Mitano, Serikali imekusudia kutekeleza programu za kielelezo kama zinavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati, ili kuweka msingi wa mageuzi ya muda mrefu yatakayochochea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, moja ya changamoto iliyoathiri utekelezaji wa mpango wa muda mrefu uliopita ni miradi kutokukamilika kwa wakati na hivyo kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaanza na utekelezaji wa miradi michache itakayochochea utekelezaji wa miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye dhima ya Mageuzi, kwa ajili ya ukuaji jumuishi wa uchumi na uzalishaji ajira unaotekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mpango yanabainisha maeneo ya kimkakati ambayo yametokana na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa Shabaha za Mpango wa Mwaka 2026/2027, kama zinavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati kwa kulinganisha na malengo. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo; Kuongeza Uwiano wa Mapato ya Ndani na Mapato ya Kodi kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Serikali inakusudia kuongeza uwiano wa mapato ya kodi kwa pato la Taifa hadi kufikia 13.7% kutoka 13.3% ya mwaka 2025/2026. Hata hivyo, uwiano huu upo chini ya wastani wa kodi kwa pato la Taifa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa baadhi ya sababu zinazofanya uwiano kuwa chini ya wastani na kubaini yafuatayo:-

(i) Uwepo wa changamoto za kiutawala katika kusimamia mfumo mzima wa kodi;

(ii) Uwepo wa sekta isiyo rasmi ambayo ni takribani 54% ya uchumi; na

(iii) Uwepo wa misamaha ya kodi isiyo na tija. Mfano, katika mwaka 2024/25 misamaha ya kodi kwa pato la Taifa ilikuwa asilimia mbili nukta tano. Aidha, jumla ya shilingi trilioni 5.5 sawa na 15% zilisamehewa kutoka kwenye mapato ya kodi ya shilingi trilioni 35.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, inashughulikia changamoto hizo, ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya kodi sambamba na kutumia sheria zilizopo, ili kuleta uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2026/2027 yamechaguliwa kwa kuzingatia vigezo vinavyolenga kujenga msingi wa utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendelo wa Miaka Mitano kuelekea Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/2027 umejikita katika kuendeleza utekelezaji wa afua za maendeleo ambazo hazikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa mpango elekezi wa maendeleo wa muda mrefu. Hatua hii ni muhimu kwa kuwa, inahakikisha utekelezaji na ukamilishaji wa miradi iliyokuwa imeanza na kutumia rasilimali fedha kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi inayopendekezwa ya utekelezaji wa mpango inaonesha mfumo mpana na wa kimkakati, hata hivyo ufanisi wake utategemea namna Serikali itakavyoshughulikia changamoto zilizopo na kutumia fursa na uwezo wa kimuundo uliopo kwa ufanisi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kufungamanisha vipaumbele vinavyofanana, ili kutumia rasilimali fedha kwa ufanisi;

(ii) Kuimarisha uwezo wa taasisi katika usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya miradi, ili kuhakikisha miradi inatekelezwa na kuleta manufaa yaliyokusudiwa; na

(iii) Kuweka mikakati thabiti ya ufadhili, hususan kwenye miradi ya mazingira na miundombinu, ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi trilioni 84.9. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 19.3 ni kutoka kwenye bajeti ya Serikali, shilingi trilioni 5.5 ni kutoka katika mashirikia ya umma yanayojiendesha kibiashara na shilingi trilioni 60.1 ni kutoka sekta binafsi. Mgawanyo huo unaonesha kwamba, ugharamiaji wa mpango umegawanyika kwa uwiano wa 70:30 kati ya sekta binafsi na umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Miaka Mitano uliopita (2021/2022 - 2025/2026) sekta binafsi ilitarajiwa kuchangia jumla ya shilingi trilioni 40.61 sawa na 35.38% ya mahitaji yote ya fedha ya shilingi trilioni 114.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali katika kuhakikisha sekta binafsi inachangia shilingi trilioni 60 kwa mwaka mmoja linaweza lisifikiwe kutokana na mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kutokuwa rafiki. Hivyo, ni lazima kuhakikisha suala la uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji linakuwa kipaumbele cha kwanza, ili tuweze kufikia lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungua soko la mitaji maana yake ni kuondoa vizuizi vinavyoathiri uhuru wa kuingia na kutoka kwa mitaji, ili kuvutia wawekezaji wa ndani na wa Kimataifa. Ili kufungua masoko ya mitaji masuala yafuatayo ni lazima yazingatiwe: Kwanza ni utulivu wa uchumi jumla, utayari na uimara wa Taasisi za usimamizi, vihatarishi vya kufungua soko la mtaji na madhara yanayoweza kujitokeza, kufanya mabadiliko ya soko la fedha, taratibu na kwa mpangilio pamoja na kupima manufaa na athari za kufungua soko la mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya athari za kufungua soko la mitaji ni kuruhusu sehemu ya uchumi kumilikiwa na wageni na uchumi kuathirika kirahisi inapotokea misukosuko katika masoko ya dunia. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ya faida na hasara za kufungua soko la mitaji kabla ya kutekeleza mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati kwenye Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali Katika Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29). Kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi, Kamati ilifanya uchambuzi wa baadhi ya viashiria vya uchumi na kubaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Novemba, 2025 deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 109.012 sawa na ongezeko la nane nukta sita tatu ikilinganishwa na shilingi trilioni 100.35 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na ukopaji, kwa ajili ya kugharamia miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, maji, pamoja na kupokelewa kwa

mikopo mipya. Jedwali namba sita linaonesha deni la Serikali ni himilivu katika muda wa kati kwa viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, deni letu ni himilivu, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kwamba, tunaongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje, ili kuepuka kufikia ukomo wa 15%;

(ii) Kuweka ukomo wa uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani, ili kuhakikisha katika kipindi chote malipo ya mikopo iliyoiva haizidi 30% ya mapato ya Serikali yanayotokana na kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha muda wa kati, Serikali imekusudia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 204.09 sawa na shilingi trilioni 61.93, shilingi trilioni 69.16 na shilingi trilioni 72.99 kwa mwaka 2026/2027, 2027/2028 na 2028/2029 mtawalia. Mgawanyo wa mapato na matumizi ni kama unavyoonekana katika jedwali namba saba na namba nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu mfumo wa bajeti katika muda wa kati na inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

1. Mapato ya kodi yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi trilioni 32.30 mwaka 2025/2026 hadi shilingi trilioni 36.89 mwaka 2026/2027 sawa na ongezeko la 14.2%. Hata hivyo, uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa *(tax to GDP ratio)* unatarajiwa kufikia 13.7% mwaka 2026, kiwango ambacho ni kidogo kuliko kiwango cha wastani cha nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara cha 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati. Kamati ilifanya uchambuzi wa maelekezo ya mwongozo kwa Maafisa Masuuli katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko iliyolindwa *(Ring Fenced Funds)*. Maafisa Masuuli wanaosimamia mifuko yenye vyanzo maalumu kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Taifa wa Maji, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Mfuko wa Maendeleo ya Utalii wanaelekezwa kutenga asilimia tano ya mapato ya mifuko husika, kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kuendeleza miundombinu kwenye Maeneo Maalumu ya Kiuchumi *(SEZs & EPZs),* ili kuvutia uwekezaji na kuongeza fursa za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuachana na pendekezo hili hivi sasa kwa kuwa, mapato ya mifuko hiyo hayakidhi mahitaji ya msingi ya mifuko tajwa. Endapo maelekezo haya yatatekelezwa, ni wazi kwamba, kuna baadhi ya miradi inayotekelezwa na mifuko hiyo hivi sasa itaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga asilimia tano ya mapato ghafi ya Halmashauri, kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali. Mwongozo umetoa maelekezo ya kimkakati kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja asilimia tano kati ya 15% ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali, ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira kwa wanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, maelekezo hayo yaliyobainishwa katika Mapendekezo ya Mwongozo yalikuwa na mkanganyiko. Mkanganyiko huu ulikuwa katika maeneo yafuatayo: -

(i) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, inatambua mgawanyo wa 10% ya mapato ghafi, kwa ajili ya mikopo kwa uwiano wa wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne na watu wenye ulemavu asilimia mbili na siyo 15% iliyopo kwenye Mwongozo;

(ii) Kamati ilitaka kufahamu kama mapendekezo hayo yatalazimu marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290; na

(iii) Asilimia tano inayotakiwa kutengwa kwa baadhi ya Halmashauri zenye uwezo mdogo ni kiasi kidogo cha fedha ambacho hakitoshi kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia majadiliano baina ya Kamati na Serikali, Serikali ilifafanua kwamba maelekezo ya mwongozo yalilenga Halmashauri zenye uwezo tu ndizo zitatakiwa kutenga asilimia tano ya mapato ghafi na siyo kama inavyosomeka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilijulishwa kuwa hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa uchambuzi wa Halmashauri ambazo zitapaswa kufuata maelekezo hayo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kufuta na kuandika upya sehemu hiyo ili kuondoa mkanganyiko katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ili maelekezo hayo yaweze kutekelezwa kikamilifu, ni vema Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ifanyiwe maboresho kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maoni mahsusi yaliyotolewa na Kamati katika kila eneo, Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika upangaji, upimaji, na umilikishaji wa ardhi pamoja na makazi ya bei nafuu, kuna msemo wa Kiswahili unasema "Ardhi Ndiyo Mama wa Mali." Msemo huu unamaanisha ardhi ndiyo msingi mkuu wa maendeleo. Shughuli za kiuchumi kama vile uzalishaji mali, ujenzi wa miundombinu ya msingi, kilimo, madini, utalii, TEHAMA na biashara, zote zinafanyika ardhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na umuhimu wa sekta ya ardhi nchini, bado Serikali haijaipa rasilimali hii umuhimu

unaostahili. Sekta hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ucheleweshaji wa upatikanaji wa Hatimiliki, migogoro ya ardhi, kipande kimoja cha ardhi kugawiwa kwa watu zaidi ya mmoja, wawekezaji kutopata ardhi iliyopimwa na ina Hatimiliki, wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi pamoja na ardhi ya vijiji kutopimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kuwa kipindi cha miaka mitano ijayo ili Wizara ya Ardhi iweze kupanga, kupima na kukamilisha ardhi, zinahitajika jumla ya shilingi trilioni 2.9 sawa na wastani wa shilingi bilioni 591.7 kila mwaka. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, katika mwaka wa fedha 2026/2027 inatengwa siyo chini ya shilingi bilioni 250 kwa kuanzia, ili mipango ya Serikali iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itasaida pia kufikia lengo la mpango la kuwa na miji iliyopangwa na inayovutia. Bila kutenga kiasi hicho cha fedha, ni wazi kwamba karibia malengo yote ya mpango wa maendeleo yanayohusu miundombinu, mazingira, kilimo, utalii, madini na kuvutia wawekezaji itakuwa vigumu kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kutunga sheria inayosimamia utekelezaji wa mpango. Ibara ya 63 (3), (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, pamoja na mambo mengine Ibara hii inalitaka Bunge kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango. Lengo la sheria hiyo ni kuweka masharti yatakayowezesha Bunge kuhakikisha Serikali inatekeleza shughuli zilizopangwa na kuidhinishwa katika mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hakuna sheria moja inayoongoza usimamizi na utekelezaji wa mipango, isipokuwa masharti yametawanyika katika sheria mbalimbali. Kwa kuwa Bunge hivi sasa linatoa mapendekezo yake kuhusu Mpango Elekezi wa muda mrefu wa miaka 25, ni vema Serikali ikawasilisha mapema iwezekenavyo sheria ya kutekeleza mpango ambayo itawalazimu viongozi wajao kuhakikisha kwamba haianzishwi miradi mipya ambayo haipo kwenye mipango. Mfano, nchi zenye sheria hizo ni pamoja na Mongolia na China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina za viongozi, ahadi za viongozi wa Kitaifa na utekelezaji wa mpango. Kumekuwa na changamoto ya utekelezaji wa ahadi za viongozi zinazohusu miradi ya maendeleo kwa wananchi, wanazozitoa pindi wanapokuwa ziara katika maeneo mbalimbali. Hivi sasa ahadi za viongozi hukusanywa kwa mfumo wa *Dashboard* ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na baadaye hupelekwa katika fungu husika ili zipangiwe bajeti katika mwaka unaofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu haupo kisheria wala kikanuni. Hatua hii ndiyo imekuwa chanzo cha ahadi za viongozi wakuu wa Kitaifa kutotekelezwa kikamilifu. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wakati tunasubiri Sheria ya Utekelezaji wa Mipango itakayozingatia ahadi za viongozi, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2026/2027 utoe maelekezo kwa Maafisa Masuuli kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi za viongozi wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uandaaji wa takwimu. Kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya utofauti wa takwimu zinazowasilishwa na taasisi za Serikali kuhusu jambo linalofanana. Pamoja na kwamba Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa nguvu ya kisheria kukusanya na kuchakata takwimu, bado kuna changamoto ya baadhi ya taasisi za Serikali kutowasilisha Takwimu za Kiutawala *(Administrative Data)* kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutoa maelekezo kupitia mwongozo wa maandalizi ya bajeti ya muda wa kati, yatakayowataka Maafisa Masuuli kuhakikisha wanatenga bajeti ya kuandaa na kuwasilisha takwimu sahihi na kuwasilisha kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya kielelezo. Kamati inatambua Serikali imehama kutoka kupanga mipango kwa kuangalia miradi na kwenda kwenye kupanga mipango kwa kuangalia programu. Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Miaka 25, Mpango wa

Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, imeainisha programu na afua mbalimbali zitakazotekelezwa katika kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2026/2027 umebainisha afua mbalimbali zitakazotekelezwa bila kuainisha miradi itakayotekelezwa chini ya afua hizo. Hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali kuainisha ni miradi ipi itakayotekelezwa kwa kila programu na afua kwa mwaka 2026/2027 ili Bunge liweze kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wake kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kutoa dhamana kwa benki za maendeleo ziweze kukopa katika vyanzo vya nje. Benki za maendeleo duniani huwa zina jukumu la kutoa mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, kwa kuwa mikopo yake ni ya muda mrefu, benki hizi zinakabiliwa na vihatarishi zaidi ya benki za biashara ambazo zinatoa mikopo ya muda mfupi na kwa riba ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina benki mbili za maendeleo. Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* na Benki ya Uwekezaji Tanzania *(TIB)* ambazo zinamilikiwa na Serikali kwa 100%. Hivi sasa, benki hizi zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mtaji. Aidha, mtaji wa benki za maendeleo nchini hivi sasa ni asilimia sifuri nukta moja nne ya pato la Taifa, na mpango wa miaka mitano umeweka lengo la kufikia walau asilimia moja nukta mbili tano ifikapo mwaka 2030/2031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali haijaweza kuziwezesha kimtaji benki hizi hasa benki ya *TIB*, Kamati inaishauri Serikali kutumia Kifungu cha 13A cha Sheria ya Mikopo, Dhamana, na Misaada, Sura 134 ili kutoa dhamana kwa benki za uwekezaji kukopa kwenye vyanzo nafuu nje ya nchi. Hatua hii itasaidia kukuza mtaji na kuchagiza utekelezaji wa mipango ya maendeleo kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, endapo benki hizi zitapewa dhamana, ni lazima Serikali iwe na usimamizi wa karibu ili kuhakikisha

mtaji uliopatikana unakuwa endelevu na mikopo inayotolewa inatolewa kwa kuzingatia vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya tabianchi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nenda kwenye hitimisho.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu wa kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango, kwani hatua hii ilitekeleza kwa vitendo azma yake ya kuimarisha utekelezaji wa mpango na kuimarisha uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ilienda sambamba na uanzishwaji wa vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ili kuimarisha na kuongeza ufanisi. Pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Mipango, bado utekelezaji wa miradi unakabiliwa na changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hitimisho kuweka *summary* ya Mawaziri wawili, ni ngumu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo kushika wadhifa huo. Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninakupongeza pamoja na Wenyeviti wenzako wawili ambao mmechaguliwa hivi karibuni kuwa Wenyeviti wa Bunge. Ninawatakia nyote kila lililo jema katika utekelezaji wa majukumu yenu mapya. Ninawahakikishia kwamba

miongozo yenu mnayoipatia Kamati ya Bajeti itakuwa nyenzo kuu katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge, na Waziri wa Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Mbunge, na Waziri wa Fedha; pamoja na Naibu Mawaziri wa Fedha; Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, Mbunge; Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Mbunge; pamoja na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mbunge, na Waziri wa Mipango na Uwekezaji; kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili mipango na mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; pamoja na Dkt. Fred Msemwa, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninawashukuru Naibu Makatibu Wakuu Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Makamishna, Wakuu wa Taasisi, na wataalam wote kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Kamati kipindi chote cha uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upendo wa dhati, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa kunisaida wakati wote wa shughuli za Kamati. Ninatumia fursa hii pia kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri wao katika kuchambua mipango na miongozo iliyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati. Ninaomba niwatambue Wajumbe hao kama majina yao yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ila siyo kwa umuhimu, ninamshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO ELEKEZI WA MAENDELEO WA MIAKA ISHIRINI NA TANO (2026/27-2050/51), MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (2026/27 - 2030/31), MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA MMOJA (2026/27) PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MUDA WA KATI (2026/27- 2028/29) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0. **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge lina majukumu ya kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Aidha, Vifungu vya 8(1)(b), 9(1)(a), 21(1)(2) na (5) vya Sheria ya Bajeti Sura ya 439 vinabainisha majukumu ya Bunge pamoja na Kamati ya Bajeti katika kuchambua na kuidhinisha Mpango na Bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 116(4),(6)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 naomba kuwasilisha Taarifa ya maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka Ishirini na

Tano (2026/27-2050/51), Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31), Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka mmoja (2026/27) pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Muda wa Kati (2026/27- 2028/29).

### 1.1. Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Nane. Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, Sehemu ya Tatu ni Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Miaka Ishirini na Tano, Sehemu ya Nne ni Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sehemu ya Tano ni Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja, Sehemu ya Sita ni Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa muda wa kati, Sehemu ya Saba ni Maoni ya ujumla na Sehemu ya Nane ni Hitimisho.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0. DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 yenye dhima ya kujenga ***Taifa Jumuishi lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea*** ni ya Pili kuandaliwa baada ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo iliandaliwa mwaka 1995. Kabla ya hapo Taifa halikuwa na Dira na badala yake lilikuwa likitekeleza mageuzi ya kichumi yaliyotokana na mabadiliko yaliyopendekezwa na Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa kile kinachojulikana kama "*Structural Adjustment Program*". Utekelezaji wa maagizo hayo kimsingi ulikuwa unaliondoa Taifa katika msukosuko wa uchumi na sio kutoa Dira thabiti ya wapi watanzania walitaka kulifikisha Taifa lao.

### 2.1. Misingi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Dira imeweka misingi mitano ili tuweze kufikia malengo. Misingi hiyo ni Demokrasia, Haki na Uhuru, Utu, Amani na Umoja, Utajiri wa Rasilimali asilia pamoja na Utamaduni na Maadili ya Taifa. Uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini nguzo kuu inayoshikilia misingi yote hiyo ni Amani na Umoja. Bila amani na umoja hakuna litakalowezekana. Kamati inawapongeza watanzania na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kulinda na kudumisha amani ya Taifa letu chini ya Uongozi wa ***Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu***. Rai ya Kamati kwa watanzania wote ili tuweze kufikia malengo yetu ni kuendelea kulinda amani ya Taifa letu kwa wivu mkubwa kwa sababu endapo ikipotea hakuna alie salama na malengo ya Dira hii yatakuwa ni ndoto.

### 2.2. Malengo ya Dira

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Dira imekusudia kufikia Malengo 4 na Shabaha 17. Malengo hayo ni:-

i. Uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani;

ii. Maisha bora na ustawi kwa wote;

iii. Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi; na

iv. Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi wa Malengo na Shabaha zote za Dira, ilibainika kuwepo na wasiwasi kuhusu utekelezaji wake. Wasiwasi huo ni sawa na ule uliobanishwa kwenye Aya ya **2.2.4. *Ineffective Implementation Syndrome*** ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Nanukuu

***"Tanzanians have developed a propensity to prepare and pronounce plans and programmes, and ambitions which are not accompanied by effective implementation, monitoring and evaluation mechanisms. As a result, implementation has been weak…."*** Mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hii inamaanisha *watanzania wamekuwa na hulka ya kuandaa mipango na programu ambayo* mara nyingi imekuwa haina mpangilio mzuri wa utekelezaji, uratibu na taratibu za tathmini. *Matokeo yake utekelezaji wa mipango na programu hizo umekuwa hafifu*. Rai ya Kamati kwa Serikali ni lazima tuwe na mifumo thabiti ya ufuatiliaji na Tathmini ili tuweze kufikia malengo na shabaha tulizojiwekea la sivyo changamoto iliyojitokeza itaendelea kuathiri utekelezaji wa Mipango.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0. UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA MPANGO ELEKEZI WA MAENDELEO WA MUDA MREFU WA MIAKA 25

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Mwaka 2026/27-2050/51 wenye Dhima ya ***"Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea***" ndio nyenzo kuu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Mpango wa aina hii ni wa Pili nchini kuandaliwa, wa kwanza ulikuwa kati ya Mwaka 2011/12 - 2025/26 uliokuwa na dhima ya ***"Mpango kazi wa Kuifikisha nchi kwenye Kipato cha Kati"***. Mpango wa Muda Mrefu wa 2050, unaweka malengo na viashiria vitakavyotumika katika kupima utekelezaji na mafanikio ili kufikia Taifa lenye uchumi wa kipato cha kati cha juu (Upper Middle Income Country). Aidha, utekelezaji wa Mpango huu utagawanywa katika utekelezaji wa mipango ya miaka mitano na ya mwaka mmoja mmoja.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imechambua malengo 4, Shabaha 2 na Mikakati 7 ya utekelezaji, lengo likiwa ni kujiridhisha na uhalisia wake katika utekelezaji na kutoa ushauri wa nini kifanyike ili kufikia

malengo ya Dira 2050. Uchambuzi huu unatoa muhtasari wa maeneo muhimu ambayo yatachochea ukuaji wa sekta nyingine.

### 3.1. Misingi ya Kufikia Malengo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango umeainisha misingi mikuu mitatu ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya Dira 2050. Misingi hiyo ni:-

#### 3.1.1 Kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango umekusudia kuboresha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu. Baadhi ya masuala yatayotekelezwa ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuajiri Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri (DEDs) kwa kuzingatia sifa na uwezo kupitia mchakato wa wazi na wenye ushindani na watatambulika kama Wakurugenzi Wakuu (CEOs) wa maendeleo ya ndani ili kuongeza uwajibikaji. Vilevile, watatakiwa kuingia mikataba ya ufanisi ili kusimamia utendaji kazi wao. Lengo la mapendekezo haya ni kuimarisha utendaji kazi wa Serikali za Mitaa na kuzipa nguvu ya kiutendaji pamoja na kuimarisha uwezo wa kukusanya mapato ili zijitegemee. Vilevile, Mpango umekusudia kuboresha miundombinu ya usalama kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa mapendekezo hayo, hata hivyo ina maoni na ushauri ufuatao:-

i. Mikataba ya utendaji kazi isiishie kwa Wakurugenzi wa Halmashauri peke yao bali itumike hata kwa wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji;

ii. Kutumia teknolojia katika utoaji wa huduma, kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara, kudhibiti upotevu wa mapato na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha; na

iii. Serikali kuhakikisha kwamba utaratibu wa ugawaji rasilimali fedha kutoka Serikali kuu unakuwa linganifu kwa kuangalia uwezo wa Halmashauri kujitegemea na uwekezaji unaoweza kuchochea ukuaji wa sekta katika Halmashauri husika.

### 3.1.2 Kuimarisha Usimamizi wa Kidijitali na Matumizi ya Takwimu na Taarifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali imekusudia ifikapo mwaka 2035 huduma zote za Serikali zitolewe kwa njia ya kidigiti. Vilevile, ifikapo mwaka 2040 watu wote waweze kupata vitambulisho vya kidigiti na huduma za kidigiti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

i. kujenga miundombinu ya msingi ya kidijitali ikiwa ni pamoja na kusambaza mkongo wa Taifa wa mawasiliano ili kuhakikisha mtandao wa intaneti unapatikana maeneo yote nchini. Hatua hii itafikiwa endapo sekta binafsi itashirikishwa katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa kwa njia ya ubia (PPP);

ii. kuhakikisha kwamba elimu ya umuhimu wa matumizi ya mtandao wa kidigiti inatolewa kwa wananchi sambamba na kuhamasisha matumizi yake;

iii. kutumia mifumo ya kisasa ya TEHAMA inayotumia takwimu na taarifa mbalimbali kama vile, akili unde (AI) na mifumo ya taarifa za kijiografia (GIS) ili kuboresha upangaji, ufuatiliaji na tathmini ya sera na miradi ya maendeleo;

iv. Serikali ifanye mapitio ya mara kwa mara ya Sera, Sheria,na Kanuni zinazohusu masuala ya TEHAMA ili kuhakikisha kuna kuwa na mazingira wezeshi ya ubunifu, uwekezaji na matumizi salama ya teknolojia; na

v. kuhakikisha shughuli zote za Serikali zinafanyika kidigitali ili kupunguza msongamano wa wananchi kwenye ofisi za Serikali pamoja na kupunguza muda wa kutoa maamuzi.

### 3.1.2.1. Matumizi ya Akili Unde (Artificial Intelligence - AI)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali imelenga kutumia akili unde kwenye malengo na shabaha mbalimbali. Akili unde ni teknolojia ambayo inatumia takwimu na taarifa mbalimbali zilizopo ili kutoa taarifa. Aidha, ili akili unde ilete matokeo sahihi, inategemea uwepo wa takwimu sahihi, hivyo Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. kuhakikisha kuwa Taasisi za Serikali zinakuwa na mfumo wa kukusanya takwimu na kuandaa taarifa sahihi ili kuondoa mkanganyiko wa takwimu;

ii. kuwa na takwimu sahihi na zinazoaminika; iii. takwimu ziwe zinapatikana kwa urahisi na kwa wakati; na iv. kuhakikisha kuwa takwimu zinahuishwa kila wakati ili kuepuka matumizi ya takwimu zilizopitwa na wakati.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, hatua hizi zitafanikisha malengo ya Serikali ya kuuza takwimu kama sehemu ya kuongeza mapato *(data monetization)*. Pamoja na umuhimu wa matumizi ya akili unde, ni lazima Serikali ijiandae kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya teknolojia hiyo, ikiwa ni pamoja na kupoteza ajira katika baadhi ya shughuli.

### 3.1.3 Kuimarisha Mageuzi ya kifikra na kimtazamo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kufanikisha Mpango huu ni lazima kubadili fikra na mtazamo wa wananchi kwamba ni Serikali pekee inawajibika kutoa huduma zote za kijamii na badala yake kuona jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ya utoaji huduma. Kamati imechambua mikakati iliyobainishwa na Serikali, na inaushauri ufuatao:-

i. Serikali ibadili mtazamo wake wa kimsingi kutoka kuwa mtoa huduma wa kila shughuli na kuwa mratibu wa sera, mlinzi wa kanuni na mwezeshaji wa mazingira ya biashara na uvumbuzi;
ii. kubadili utamaduni wa Utumishi wa Umma kutenda kazi kwa mazoea na badala yake kuzingatia matokeo na tija;

iii. kuandaa raia wanaowajibika kwa Taifa lao kwa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo, ulipaji kodi, maadili ya kazi pamoja na uzalishaji;

iv. wananchi kubadili fikra ya namna wanavyojadili matatizo yanayolikabili Taifa, kutoka kuilaumu Serikali na badala yake kutafuta suluhu ya matatizo yanayotukabili kwa pamoja kama Taifa; na

v. kuunganisha sera na mabadiliko ya fikra zinazolenga kujenga kizazi chenye maadili, uwajibikaji, nidhamu na chenye uwezo wa kutambua fursa na kuzitumia kwa ajili ya maendeleo kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo.

**3.2. Masuala ya msingi yanayohitajika katika ukuaji na mabadiliko**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango elekezi umeweka miongozo inayotakiwa kufuatwa ili kuleta mabadiliko katika ukuaji wa uchumi. Miongozo hii ni muhimu katika kuwezesha mtiririko wa mitaji, kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na kukuza maendeleo ya kiteknolojia pamoja na mageuzi ya kiuchumi ambayo ni:-

i. upatikanaji wa fedha na mitaji;
ii. maendeleo ya miundombinu;
iii. maendeleo ya ujuzi na ujasiriamali;
iv. ufanisi wa udhibiti na urasimishaji;
v. utawala bora; na
vi. mabadiliko ya fikra na mageuzi ya kiutamaduni.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa masuala hayo na inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. Serikali kuimarisha Taasisi za Fedha za Maendeleo (DFIs) kwa kufanya tathmini na maboresho ya kina kwa kuziongezea mitaji na kuzielekeza kufadhili miradi ya kimkakati yenye matokeo makubwa kiuchumi;

ii. kukuza Biashara ndogo na za Kati (SMEs) kwa kutoa mikopo nafuu na ruzuku kwa wajasiriamali katika sekta za uzalishaji na kuchochea ubunifu kwa biashara zinazoibukia;

iii. Serikali kuendeleza miundombinu ya Msingi na ya kimkakati kwa kuanza na barabara, viwanja vya ndege, bandari, reli, mtandao *(internet)* ya uhakika ili kujenga msingi imara wa kufikia malengo;

iv. kuongeza kasi ya kurasimisha biashara kwa kutumia mifumo sambamba na kutenga na kuendeleza maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya wafanyabiashara;

v. kupunguza na kuunganisha Mamlaka za Udhibiti zenye majukumu yanayoshabihiana ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; na

vi. kuendelea kudhibiti vitendo vya rushwa na ubadhilifu kwenye mali za umma na binafsi. Hivi sasa takwimu zinaonyesha kuwa Fahirisi ya rushwa kwenye mali za umma *(Corruption Perceptions Index – CPI) Tanzania* ni (41/100). Hii inamaanisha kwa kila matukio **100** ya rushwa Serikali inaweza kuzuia matukio **41** tu. Hivyo, ili kufikia malengo ni lazima kudhibiti kikamilifu vitendo vya rushwa, ubadhilifu na ufujaji wa mali za umma.

### 3.3. Uhimilivu wa Sera za uchumi jumla na za kibajeti

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Muda Mrefu umeweka shabaha za uchumi jumla na za kibajeti zitakazosaidia kufikia malengo ya Dira 2050. Shabaha hizo ni kama ifuatavyo:-

#### 3.3.1 Uhimilivu wa Uchumi Jumla

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchumi wa Tanzania kwa takribani miongo miwili umekuwa ukikua kwa wastani wa **asilimia 6.2** na kufikia Pato la Taifa halisi la **shilingi trilioni 156.6** mwaka 2024 kutoka **shilingi trilioni 141.87** mwaka 2022 na pato la mtu mmoja kufikia **shilingi milioni 2.85** mwaka 2024 kutoka **shilingi milioni 2.84** mwaka 2022**.** Ukuaji huo ulichangiwa na sekta za kilimo, ujenzi, uchimbaji wa madini, usafiri na uzalishaji. Mpango elekezi umeweka shabaha na mikakati itakayowezesha kufikia malengo yaliyowekwa kama ifuatavyo:-

i. mfumuko wa bei wa wastani kati ya **asilimia 3** hadi **5**;
ii. viwango imara vya ubadilishaji wa fedha;
iii. kuimarisha uwezo wa nchi kukabiliana na misukosuko ya uchumi kutoka nje; na
iv. Pato la Taifa (GDP) kufikia **Dola za Marekani trilioni moja** na Pato la Mtu mmoja kufikia **Dola za Marekani 7000** ifikapo mwaka 2050.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa shabaha hizo na ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

i. kuendelea kusimamia Sera za fedha ili kudhibiti mfumuko wa bei;

ii. kuendelea kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ili kuondokana na kutegemea kilimo cha msimu ili kuwa na chakula cha kutosha na cha uhakika nchini pamoja na ziada kwa kwa ajili ya malighafi viwandani na mauzo nje ya nchi;

iii. kuwekeza kwenye vyanzo vya nishati mbalimbali vinavyopatikana nchini kama vile gesi asilia, jua, upepo na jotoardhi ili kutimiza azma ya uwepo wa nishati mseto na kupunguza utegemezi wa uagizaji wa mafuta ya dizeli, petroli, na gesi kutoka nje;

iv. kuboresha mifumo ya taarifa za masoko ili kupunguzauwezekano wa kuhodhi bidhaa kwa lengo la kupandisha bei;

v. kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kwa wingi (import substitution industries)

ili kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni ya kununua bidhaa hizo mfano sukari ya viwandani, mbolea, pamba na mafuta ya kula;

vi. kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kupanua masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini; na

vii. Serikali kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kutumia jiografia ya kimkakati ya Taifa kama kitovu cha usafirishaji na biashara kwa nchi tunazopakana nazo.

### 3.3.2 Uhimilivu wa Sera za Kibajeti

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango elekezi yamelenga kuweka mfumo endelevu wa sera ya fedha za umma kwa kuongeza makusanyo ya kodi kufikia **asilimia 25** ya Pato la Taifa, kupunguza uwiano wa deni kwa Pato la Taifa hadi kufikia **asilimia 40**, kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi, kupunguza nakisi ya bajeti kuwa kati ya **asilimia 1** hadi **3** ya Pato la Taifa na kutenga **asilimia 50** ya bajeti kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa malengo hayo na kushauri yafuatayo:-

i. kuimarisha mifumo ya usimamizi wa kodi na kuendelea kujenga utamaduni wa watanzania kulipa kodi kwa hiari kwa ajili ya maendeleo ya Taifa;

ii. kupunguza misamaha ya kodi kutoka **asilimia 2.5** ya sasa hadi **asilimia 1** ya Pato la Taifa ili kuongeza mapato ya Serikali; na

iii. kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili fedha hizo zielekezwe kwenye kutekeleza shughuli za maendeleo zitakazochochea ukuaji wa uchumi.

### 3.4. Maeneo ya Kielelezo katika Programu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mapendekezo ya Mpango Elekezi umeainisha programu 14 za kielelezo zenye uwezo wa kuchochea na kuharakisha mageuzi ya kiuchumi, kufungua fursa za uwekezaji na kuchochea ubunifu. Aidha, maeneo hayo yanatoa mwongozo wa uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano (FYDPs) hadi mwaka 2050, kwa kuhakikisha kunakuwa na muendelezo wa programu na miradi mikubwa ambayo bado haijakamilika kutoka Mpango Elekezi wa mwaka 2025, hususan katika sekta za nishati, usafirishaji na uchukuzi, pamoja na kilimo. Programu hizo ni kama zifuatazo:-

i. Tanzania inayokua kiviwanda;
ii. Kufungamanisha Sekta ya Madini na Viwanda;
iii. Tanzania inayoongoza katika ugunduzi;
iv. Tanzania inayo himili Mabadiliko ya Tabianchi;
v. Taifa lililounganishwa na miundombinu bora;
vi. Nishati ya Kisasa;
vii. Maendeleo yanayozingatia watu;
viii. Mageuzi ya Utawala bora;
ix. Miji ya Kisasa;
x. Tanzania inayovutia Biashara na Uwekezaji
xi. Tanzania inayokua katika Sekta ya Utamaduni na Utalii;
xii. Mageuzi katika sekta ya kilimo;
xiii. Tanzania yenye nguvu ya ubunifu na uvumbuzi; na
xiv. Mageuzi ya dijitali, TEHAMA na mifumo ya fedha.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa programu hizi na inaishauri Serikali kutoa kipaumbele mahsusi katika kukamilisha miradi ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Miradi hiyo ni kama vile Liganga na Mchuchuma, Magadi Soda Engaruka, Ruhudji na Rumakali, na miradi ya uchimbaji wa gesi na mafuta katika maeneo ya Pwani. Kukamilika kwa miradi hii kutaleta manufaa na kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, ni muhimu kuweka kipaumbele cha kipekee katika kukamilisha miradi ya ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kutokana na umuhimu kwa nchi na nchi jirani.

### 3.5. Ugharamiaji wa Mpango

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango Elekezi wa Muda Mrefu utagharimu **dola za Marekani bilioni 3,582** na kati ya kiasi hicho sekta binafsi inatarajiwa kuchangia **asilimia 70** na Sekta ya Umma kuchangia **asilimia 30.** Kati ya **asilimia 70** ya mchango wa sekta binafsi, **asilimia 13** itachangiwa na sekta za ndani na **asilimia 57** itatokana na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDIs). Aidha, kwa upande wa **asilimia 30** ya mchango wa sekta ya umma, **asilimia 22** zitatokana na mapato ya kodi, yasiyo ya kodi na mikopo na **asilimia 8** zitachangiwa na mashirika ya Umma. Vilevile, Serikali imepanga kutenga uwiano wa **60:40** wa bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Jedwali Na. 1 linaonyesha mchanganuo wa mahitaji ya fedha kwa kila Mpango wa miaka mitano.

**Jedwali Na 1: Mahitaji ya Fedha kwa Ajili ya Kugharamia Mpango (Dola Bilioni)**

| Mpango Wa Maendeleo Wa Miaka Mitano | Mchango wa Sekta ya Umma | | Sekta Binafsi Asilimia (70%) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | Mchango wa Serikali (22%) | Mchango wa Mashirika (8%) | | |
| IV | 43 | 12 | 128 | 183 |
| V | 67 | 20 | 203 | 290 |
| VI | 118 | 45 | 379 | 542 |
| VII | 201 | 96 | 692 | 989 |
| VIII | 317 | 157 | 1,106 | 1,580 |
| **JUMLA** | **746** | **330** | **2,508** | **3,584** |

**Chanzo**: *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Muda mrefu*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ilifanya uchambuzi wa vyanzo vya ugharamiaji wa Mpango na kubaini kwamba vimegawanyika katika makundi makuu mawili. Moja ni vyanzo vinavyotokana na Serikali na pili ni Sekta Binafsi na ina maoni na ushauri ufuatao:-

**a) Mapato ya Serikali**

i. Serikali kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Hatua hii iende sambamba na kuipatia Mamlaka ya Mapato Tanzania kiasi cha **shilingi bilioni 480** kwa ajili ya ujenzi, uboreshaji na ukamilishaji wa mifumo;

ii. Mamlaka, Wakala na Taasisi za umma kuhakikisha wakati wote zinatumia mifumo kukusanya na kuhasibu mapato yote ya Serikali na iweke katazo la kukusanya mapato ya Serikali kwa fedha taslimu;

iii. Mpango umeelekeza Mashirika na Taasisi za Serikali kuchangia asilimia 8 katika utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, Mashirika haya yamekuwa na ufanisi mdogo kwenye ukusanyaji wa mapato ukizingatia kuwa Serikali imewekeza takribani shillingi trilioni 86.3. Aidha, kwa takribani miaka 10 mchango wa Mashirika katika mapato ya Serikali unaotokana na gawio, mchango wa asilimia 15 na asilimia 70 ya mapato ya ziada ni wastani wa shilingi trilioni 1. Hivyo, kwa matarajio ya Dira 2050, ni dhahiri Mashirika haya yanahitaji kuongeza ufanisi; na

iv. Kuimarisha matumizi ya masoko ya mitaji ya ndani na ya nje kupitia utoaji wa hati fungani maalum kama vile hati fungani za miundombinu, kijani na za tabianchi.

**b) Mchango wa Sekta Binafsi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sekta Binafsi inatarajiwa kuchangia **asilimia 70** ya gharama za Mpango. Hatua, hii inaonyesha nia ya Serikali kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuifanya Sekta Binafsi kuwa injini ya ukuaji wa uchumi. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba sekta binafsi katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ilitarajiwa kuchangia **shilingi trilioni 40.61** sawa na **asilimia 35** ya gharama za Mpango. Hata hivyo, hadi Kamati inakamilisha Taarifa hii haikuwa imepokea taarifa ya mchango wa sekta binafsi katika

kugharamia mpango huo kwa kipindi cha miaka minne na nusu, hivyo Kamati ilishindwa kupima ni kwa kiasi gani malengo ya **asilimia 70** yatafikiwa. Aidha, ili Serikali iweze kufikia malengo hayo, Kamati inashauri itekeleze masuala yafuatayo:-

i. kuanzisha utaratibu wa kutambua na kutunza takwimu za uwekezaji wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo;
ii. kutangaza miradi ambayo Serikali itataka itekelezwe na Sekta binafsi;
iii. kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji;
iv. kushirikisha mapema sekta binafsi katika kupanga nakusanifu miradi;
v. kufanya maamuzi ya haraka na kwa wakati; vi. watumishi wa umma kuboresha utoaji wa huduma kutoka udhibiti kwenda kwenye mtazamo wa kuwezesha; na
vi. kuwa na Sera za kodi zinazotabirika pamoja na kuweka utaratibu wa haraka wa kutatua migogoro ya masuala ya kodi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** endapo masuala hayo hayatafanyiwa kazi ni dhahiri kuwa lengo la sekta binafsi kuchangia **asilimia 70** halitofikiwa na hivyo itaathiri utekelezaji wa mpango.

### 3.6. Utekelezaji na Usimamizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango elekezi wa muda mrefu wa mwaka 2050 utasimamiwa na Tume ya Taifa ya Mipango kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Bajeti Sura 439 na Sheria ya Tume ya Mipango Sura 127. Aidha, katika usimamizi huo, Tume itashirikiana na Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi mbalimbali za Serikali, sekta binafsi, sekretarieti za mikoa pamoja na Serikali za Mitaa. Hivyo, ili kuhakikisha kuwa Mpango huu unatekelezwa na kusimamiwa kikamilifu, Kamati inashauri yafuatayo:-

### 3.6.1 Kuimarisha Ufuatiliaji na Tathmini

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ufuatiliaji na tathmini ni nguzo muhimu katika kuhakikisha mpango unatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kutoa taarifa sahihi za utekelezaji wa mpango, kubaini changamoto mapema, kuhakikisha uwajibikaji pamoja na matumizi bora ya rasilimali fedha. Hata hivyo, hakuna mwongozo wa kisheria unaoongoza suala zima la tathmini na ufuatiliaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ili Serikali iweze kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya Serikali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza masuala yafuatayo:-

a) kutunga Sheria ya ufuatiliaji na tathmini itakayosimamia masuala yote ya ufuatiliaji na tathmini na hivyo kuleta ufanisi na uwajibikaji. Aidha Kamati inasisitiza kuweka sharti la kuwasilisha taarifa ya ufuatiliaji na tathmini Bungeni kupitia Kamati ya Bajeti ili kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa wa miradi ya umma; na

b) Serikali ifanye tathmini ya umuhimu wa kuwa na Mamlaka moja itakayosimamia jukumu la ufuatiliaji na tathmini ya mipango na shughuli za Serikali ili kuongeza ufanisi wa jukumu hilo. Hivi sasa, Tume ya Mipango inafanya ufuatiliaji na tathmini ya Mipango ya Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu ikifanya tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali. Mwingiliano wa majukumu wa namna hii husababisha mkanganyiko, kupunguza ufanisi, uwajibikaji hafifu na hivyo kuathiri matokeo.

### 3.6.2 Usimamizi wa Mashirika ya Umma

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** moja ya mapendekezo ya Serikali katika mpango wa muda mrefu ni kutenganisha Mashirika katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusisha mashirika ya Serikali yanayotoa huduma na hayajiendeshi kwa misingi ya kibiashara na kundi la pili ni mashirika yanayojiendesha kibiashara. Aidha, inapendekezwa Mashirika yanayojiendesha kibiashara yabaki chini ya uongozi wa Ofisi

ya Msajili wa Hazina na yanayotoa huduma yasimamiwe na Wizara husika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uamuzi huo pamoja na kwamba una nia njema ya usimamizi, Kamati inaishauri Serikali kuuangalia upya kwa sababu hata Mashirika yanayotoa huduma lazima yawe na msimamizi atakayeweka vigezo vya utoaji huduma kwa ufanisi na kusimamia utekelezaji wake. Wizara zina majukumu ya kusimamia utendaji wa kisera na sio utendaji wa kila siku wa Mashirika. Hivyo kurejesha majukumu ya usimamizi kwenye Wizara kutazorotesha utendaji kazi wa Mashirika hayo. Aidha ni wakati muafaka kwa Serikali kurejesha Bungeni Muswada wa Sheria ya kuunda upya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo sambamba na uimarishaji wa usimamizi wa mashirika ya umma kwa ujumla.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0. UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (2026/27 - 2030/31)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27–2030/31) ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mapendekezo ya Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa mwaka 2050 na wa nne tangu uanzishwe utaratibu wa kutekeleza Mipango ya miaka mitano. Aidha, Mpango huu una lengo la kuweka msingi imara wa utekelezaji wa sera za kiuchumi, kijamii na miundombinu itakayoharakisha maendeleo endelevu ya taifa na ustawi wa jamii. Mpango unalenga kufikia Pato la Taifa *(nominal GDP)* la **Dola za Marekani bilioni 118.052**, ukuaji wa Pato la Taifa halisi *(real GDP)* wa **asilimia 10.5** pamoja na Pato la Taifa kwa kila mtu la **Dola za Marekani 1,638** ifikapo mwaka 2031. Kufikia malengo hayo kutategemea uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, ongezeko la upatikanaji wa nishati ya uhakika na ya gharama nafuu, mifumo thabiti ya usafirishaji na usambazaji, kukuza ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali pamoja na kujenga utumishi wa

umma wenye ujuzi, maadili, nidhamu, uwajibikaji na uzalendo kwa Taifa.

### 4.1. Malengo Mahsusi yanayoweka Msingi wa Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Misingi iliyowekwa ili kufanikisha matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka mitano ni pamoja na:-

i. kuendelea na mageuzi ya kimuundo ili kuimarisha uchumi jumla na kufungua fursa za ukuaji jumuishi unaoongozwa na sekta binafsi;

ii. kuongeza ushindani wa kimataifa kwa kuwa kitovu cha kikanda na kimataifa cha usafiri na masoko kwa kuboresha miundombinu ya ugavi na usafirishaji na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara;

iii. kudumisha ajira jumuishi na ustawi wa muda mrefu kwa kujenga uwezo wa rasilimali watu, kuboresha huduma na mifumo ya hifadhi ya jamii, ustahimilivu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kukuza utawala bora na kuzingatia misingi ya utawala wa sheria; na

iv. kuongeza ushindani wa kimataifa kwa kuchochea mageuzi ya sekta za uzalishaji ili kuongeza ajira zenye staha, kuimarisha thamani ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa malengo mahsusi ya mapendekezo ya mpango na inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. kutekeleza kikamilifu Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na uwekezaji nchini (MKUMBI) ili kuondoa vikwazo vya biashara na kuendeleza mazingira ya uwekezaji yanayowezesha sekta binafsi kushindana kikanda na kimataifa;

ii. kuwekeza katika miundombinu wezeshi ya usafiri na usafirishaji mfano bandari, reli, viwanja vya ndege na barabara ili kurahisisha shughuli za ugavi;

iii. kuendeleza elimu na ujuzi ili kukuza uwezo wa rasilimali watu, kuboresha miundombinu ya msingi ya huduma za jamii, kusimamia kikamilifu sera na sheria za utunzaji mazingira pamoja na kuimarisha mifumo na kusimamia taasisi za utoaji haki;

iv. kuanzisha na kuendeleza vyuo vya kitaaluma vitakavyotoa wataalamu wenye ujuzi mahsusi kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati ili kujenga nguvu kazi yenye weledi na uwezo wa kuchangia kikamilifu katika sekta za uzalishaji na huduma; na

v. kutumia teknolojia ya kisasa katika uzalishaji wa bidhaa ambazo Tanzania ina nguvu ya kiushindani, kupata ithibati ya bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na kuimarisha masoko ya ndani na nje.

**4.1.1. Matokeo ya Utekelezaji wa Mpango katika kipindi cha miaka Mitano**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yamebainisha matokeo matano yenye vipengele 18 kama yanavyonekana kwenye jedwali na. 2 yanayotarajiwa kufikiwa mwaka 2030/31. Matokeo hayo ni:-

*i. Uchumi Imara na Shindani*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufikia 2030/31 uchumi unatarajiwa kukua kwa **asilimia 10.5** na pato la taifa la mtu mmoja kufikia **Dola za Kimarekani 1,638**.

*ii. Kutokomeza umaskini uliokithiri*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali ina mpango wa kupunguza kiwango cha umaskini uliokithiri kutoka **asilimia 8** mwaka 2017/18 hadi **asilimia 5**

mwaka 2030/31. Hatua hii itasababisha kupungua kwa *Gini Coefficient* kutoka **0.38** hadi **0.34.** Kipimo cha *Gini Coefficient* kinaashiria mgawanyo wa mapato. Hivyo, kadri *Gini Coefficient* inavyopungua ndivyo utofauti kati ya kipato cha juu na cha chini unavyopungua.

*iii.* *Afya na Maisha Bora*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango yamekusudia kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka **33** kwa vizazi hai **1,000** mwaka 2022 hadi vifo **27** na vifo vya akina mama kutoka **104** kwa vizazi hai **100,000** hadi **85** ifikapo mwaka 2030/31. Kamati inampongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kutekeleza afua mbalimbali kwenye sekta ya afya zilizopelekea kupunguza vifo vya Watoto wachanga na kina Mama wajawazito kwa.

*iv.* *Elimu Bora na Jumuishi*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango yamekusudia kufikia lengo la uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa **40:1** mwaka 2030/31 kutoka **105:1** mwaka 2024. Kuongeza uandikishaji wa sekondari (O level) kutoka **asilimia 51.7** hadi **asilimia 79.1.**

*v.* *Jamii ya Kidijitali*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango yamelenga kufikia zaidi ya **asilimia 70** ya wananchi wanaotumia intaneti yenye kasi (*broadband)* na **asilimia 95** ya huduma za Serikali kupatikana mtandaoni.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa malengo mahsusi na inaushauri ufuatao kwenye baadhi ya vipengele:-

i. kwa kuwa uchumi wa nchi kwa muda mrefu umekuwa ukichochewa na shughuli za Serikali, hivyo ili Serikali ifikie lengo la

kuwa na uchumi imara na shindani lazima itengeneze mazingira wezeshi ili sekta binafsi iwe injini ya ukuaji wa uchumi;

ii. Serikali ihakikishe sekta zinazotoa ajira kwa watanzania walio wengi zinakuwa kwa kasi. Sekta hizo ni kilimo cha mazao, uvuvi, mifugo, na utalii;

iii. Serikali kuendelea kuboresha sekta ya afya kwa kuendelea kujenga zahanati na vituo vya afya katika ngazi zote kwa kuzingatia mahitaji pamoja na kuendelea kuajiri wahudumu wa afya;

iv. Serikali kuendelea kuboresha sekta ya elimu kwa kuongeza miundombinu ya kujifunza na kujifunzia pamoja na kuajiri walimu wa kutosha na wenye ujuzi. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa mitaala mipya ya elimu ya msingi na ufundi inatekelezwa kikamilifu; na

v. Serikali kuhakikisha inaweka miundombinu itakayohamasisha jamii kuwa ya kidigitali.

**Jedwali Na. 2: Malengo Mahsusi ya Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano ifikapo 2030/31**

| SHABAHA KUU | KIASHIRIA (INDICATOR) | HALI YA MSINGI (BASELINE) | LENGO (2030/31) |
|---|---|---|---|
| Uchumi Imara na Shindani | Pato la Taifa (GDP – USD Bilioni) | 81.537 (2024) | 118.052 |
| | Pato la Kila Mtu (USD) | 1,343.91 (2024) | 1,638 |
| | Ukuaji wa Pato Halisi (%) | 5.5% (2024) | 10.5% |
| Kutokomeza Umaskini Uliokithiri | Kiwango cha Umaskini Uliokithiri (%) | 8% (2017/18) | 5% |
| | Kiwango cha Umaskini wa Kawaida (%) | 26.4% (2017/18) | 22% |
| | Kiwango cha Usawa wa Mapato (Gini coeffient) | 0.38 | 0.34 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kuwa Kapu la Chakula Barani Afrika | Kiwango cha Kujitosheleza kwa Chakula (%) | 128% | 130% |
| | Nafasi ya Upatikanaji wa Chakula Barani Afrika | Nafasi ya 5 | Nafasi ya 3 |
| Afya na Maisha Bora | Vifo vya Watoto Wachanga kwa vizazi hai 1,000 | 33 (2022) | 27 |
| | Vifo vya Watoto chini ya Miaka 5 | 43 (2022) | 34 |
| | Vifo vya Akina Mama kwa vizazi hai 100,000 | 104 (2022) | 85 |
| Elimu Bora na Jumuishi | Uwiano wa Walimu Wenye Sifa kwa Wanafunzi | 105:1 (2024) | 40:1 |
| | Uwiano wa Uandikishaji Shule ya Msingi (%) | 98.2% (2023) | 100% |
| | Uwiano wa Uandikishaji Sekondari ya Chini (%) | 51.7% (2024) | 79.1% |
| Ulinzi wa Jamii na Huduma za Afya | Utoaji wa Bima ya Afya (%) | 67.8% (2023/24) | 100% |
| | Utoaji wa Hifadhi ya Jamii (%) | 10.1% (2023/24) | 18.1% |
| Maji Safi na Nishati | Upatikanaji wa Maji Safi Vijijini (%) | 79.6% | 87.9% |
| | Upatikanaji wa Maji Safi Mijini (%) | 90.0% | 97.2% |
| | Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme (MW) | 4032 MW ) (2025 | 15,000 MW |
| Usawa wa Kijinsia | Fahirisi ya Usawa wa Kijinsia (Global Gender Gap Index GGGI) | 0.734 (2024) | 0.77 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Nafasi ya Tanzania Kimataifa kwa Fahirisi ya Usawa wa Kijinsia (GGGI) | Nafasi ya 55 (2024) | Nafasi ya 40 |
| Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi | Nafasi katika Fahirisi ya Utunzaji Mazingira *(Environmental Performance Index Africa)* | Nafasi ya 19 (2022) | Top 15 |
| | Nafasi katika fahirisi ya kukabiliana na mbadiliko ya tabia (Climate Adaptation Index Afrika | Nafasi ya 18 (2022) | Top 15 |
| Jamii ya Kidijitali | Matumizi ya Intaneti ya Broadband (%) | 40% (2025) | >70% |
| | Kiwango cha Uelewa wa Kidijitali (%) | 30% (2024) | >60% |
| | Huduma za Msingi za Serikali zinazopatikana Mtandaoni (%) | 45% (2025) | 95% |

**Chanzo:** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa miaka 5 (2026/27-2030/31)*

## 4.2. Uthabiti wa Uchumi Jumla na Fedha za Umma

### 4.2.1. Utulivu wa Uchumi Jumla

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** jedwali lifuatalo linaonesha viashiria vya utulivu na uhimilivu wa uchumi jumla na malengo yanayotarajiwa ifikapo 2030/31.

**Jedwali Na. 3: Viashiria vya Utulivu vya Uchumi Jumla na Malengo**

| KIASHIRIA CHA MATOKEO | KIWANGO CHA MSINGI (MWAKA) | LENGO (2030/31) |
|---|---|---|
| Pato la Taifa (GDP) kwa Dola za Marekani Bilioni | 81,537 (2024) | 118.052 |
| | | |
| Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa (GDP) (%) | 5.5% (2024) | 10.5% |
| Pato la Taifa kwa Kila Mtanzania (GDP per capita) (USD) | 1,343.91 (2024) | 1,638 |
| Uwiano wa Deni la Umma kwa pato la Taifa (GDP) ukilinganishwa na viwango vya kupima uhimilivu wa deni (DSA) | 48.9% (2025) | <55% |
| Mfumuko wa Bei | 3.1% (2024) | 3–5% |
| Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi (kwa mwaka) | 15.9% (2024) | 22.4% |
| Mikopo ya Ndani kwa Sekta Binafsi kwa pato la Taifa (GDP) | 16.3% (2025) | 25% |
| Kiwango cha Mfumuko wa Bei Jumla | 3.1% (2024) | 3–5% |
| Kiwango cha Mfumuko wa Bei wa Msingi | 3.4% (2024) | 3–5% |
| Mikopo chechefu | 3.3% (2024) | <5% |
| Ujumuishaji wa Huduma za Kifedha (watu wazima) | 72.76% (2023) | 90% |
| Watu wazima wenye akaunti za miamala | 72% (2023) | 85% |
| Watu wazima wanaotumia malipo ya kidijitali | 13% (2023) | 40% |

| KIASHIRIA CHA MATOKEO | KIWANGO CHA MSINGI (MWAKA) | LENGO (2030/31) |
|---|---|---|
| Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa (GDP) | 14.9% (2024/25) | 20.0% |
| Uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa (GDP) | 13.3% (2024/25) | 18.0% |
| Uwiano wa mapato yasiyo ya kodi kwa Pato la Taifa (GDP) | 2.7% (2024/25) | 5.0% |
| Uwiano wa deni la Serikali kwa Pato la Taifa ukilinganisha na viwango vya kupima uhimilivu wa deni (DSA) | 47.0% (2024/25) | <50.0% |
| Thamani ya deni la sasa (PV) ya deni la | 40.3 (2024/25) | 19.6 |
| Taifa kwa Pato la Taifa (GDP) | | |
| Thamani ya sasa (PV) ya huduma ya deni la Taifa kwa mapato ya ndani | 44.3 (2023/24) | 15 |
| Thamani ya sasa (PV) ya deni la nje kwa mauzo ya nje | 123.8 (2024/25) | 100.3 |
| Nakisi ya bajeti (%) kwa Pato la Taifa (GDP) | -3.1% (2024) | -2.8% |
| Matumizi ya maendeleo (% ya bajeti yote) | 31% (2024/25) | 35%–40% |
| Uwiano wa malipo ya riba kwa mapato yote ya mwaka | 11% (2023) | ≤8% |
| Mahitaji ya fedha ya jumla kwa Pato la Taifa (GDP) (%) | 35% (2024) | 35% |
| Wastani wa kuiva kwa deni (miaka) | Miaka 9 (2023) | Miaka 12 |
| Gawio halisi linalotolewa na Mashirika ya Umma kwa Pato la Taifa (%) | <0.2% (2023) | 0.5–1% |
| Kiasi cha dhamana kwa Pato la Taifa (%) | 2.8% (2023) | ≤3% |

**Chanzo:** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa miaka 5 (2026/27-2030/31)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa viashiria hivyo na inapendekeza yafuatayo:-

*i. Mfumuko wa Bei*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali ihakikishe katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Miaka mitano mfumuko wa bei unabaki katika kiwango kisichozidi **asilimia 5.** Endapo mfumuko wa bei utazidi lengo lililowekwa utaathiri viashiria vingine vya uchumi vikiwemo kupanda kwa riba za mikopo ambazo zitaathiri ukuaji wa sekta binafsi, kushusha thamani ya shilingi pamoja na kuongezeka kwa gharama za kukopa katika soko la ndani.

*ii. Fedha jumuishi kwa Uchumi Imara*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kuendeleza jitihada za wananchi kujiunga na mfumo wa fedha jumuishi, Serikali inapaswa kuwekeza na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi kwenye miundombinu ya msingi inayowezesha fedha jumuishi *(financial inclusion)* sambamba na kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kupunguza gharama za miamala.

*iii. Usimamizi bora wa deni la taifa*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali ihakikishe katika wakati wote wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka mitano inakopa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134. Aidha, mikopo yote inayokopwa na Serikali ielekezwe kwenye miradi na shughuli zenye uwezo wa kuzalisha mapato yatakayosaidia kurejesha mikopo hiyo na si vinginevyo. Jedwali na. 4 linaonyesha viashiria vya kuimarisha Sera za kibajeti na kifedha zinazotabirika.

**Jedwali Na. 4: Viashiria vya kuimarisha Sera za Kibajeti na Kifedha Zinazotabirika**

| KIASHIRIA CHA MATOKEO | KIWANGO CHA MSINGI (MWAKA) | LENGO (2030/31) |
|---|---|---|
| Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa (GDP) | 14.9% (2024/25) | 20.0% |
| Uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa (GDP) | 13.3% (2024/25) | 18.0% |
| Uwiano wa mapato yasiyo ya kodi kwa Pato la Taifa (GDP) | 2.7% (2024/25) | 5.0% |

| | | |
|---|---|---|
| Uwiano wa deni la Serikali kwa Pato la Taifa ukilinganisha na viwango vya kupima uhimilivu wa deni (DSA) | 47.0% (2024/25) | <50.0% |
| Thamani ya deni la sasa (PV) ya deni la | 40.3 (2024/25) | 19.6 |
| Taifa kwa Pato la Taifa (GDP) | | |
| Thamani ya sasa (PV) ya huduma ya deni la Taifa kwa mapato ya ndani | 44.3 (2023/24) | 15 |
| Thamani ya sasa (PV) ya deni la nje kwa mauzo ya nje | 123.8 (2024/25) | 100.3 |
| Nakisi ya bajeti (%) kwa Pato la Taifa (GDP) | -3.1% (2024) | -2.8% |
| Matumizi ya maendeleo (% ya bajeti yote) | 31% (2024/25) | 35%–40% |
| Uwiano wa malipo ya riba kwa mapato yote ya mwaka | 11% (2023) | ≤8% |
| Mahitaji ya fedha ya jumla kwa Pato la Taifa (GDP) (%) | 35% (2024) | 35% |
| Wastani wa kuiva kwa deni (miaka) | Miaka 9 (2023) | Miaka 12 |
| Gawio halisi linalotolewa na Mashirika ya Umma kwa Pato la Taifa (%) | <0.2% (2023) | 0.5–1% |
| Kiasi cha dhamana kwa Pato la Taifa (%) | 2.8% (2023) | ≤3% |

**Chanzo:** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa miaka 5 (2026/27-2030/31)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** jedwali hapo juu limebainisha malengo yanayotarajiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2030/31. Aidha, uchambuzi wa Kamati kuhusu viashiria vilivyopo kwenye jedwali hilo umebaini kwamba ili kufikia malengo ya viashiria hivyo ni lazima Serikali ihakikishe inaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa kodi na kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidijitali katika ukusanyaji. Hatua hii iende sambamba na kudhibiti matumizi ya Serikali yasiyo na tija, kuwekeza kwenye miradi yenye manufaa kiuchumi pamoja na kuboresha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

### 4.3. Kuimarisha Misingi Imara na Endelevu ya Taifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kuhakikisha utekelezaji wa Mpango unafanikiwa na kuleta matokeo yaliyokusudiwa, Serikali imeweka misingi minne. Misingi hiyo ni:-

i. kuimarisha na kuendeleza Utawala bora, Demokrasia, ulinzi na usalama;

ii. kujenga Serikali za Mitaa zilizo imara na zenye ufanisi;

iii. kuimarisha Serikali mtandao na matumizi ya takwimu; na

iv. kuhimiza mabadiliko ya kifikra ili kuendana na mageuzi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imechambua kwa kina misingi hiyo na ina maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa Serikali:-

i. kuendelea kuhakikisha kwamba Serikali za mitaa zinakuwa ndio kitovu cha maendeleo katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Mitaa, Vijiji na vitongoji kwa kuhakikisha kuna rasilimali fedha na watu wa kutosha wenye ujuzi na ufanisi; na

ii. takwimu ndio msingi wa kufanya maamuzi sahihi na yenye tija, hivyo Serikali ihakikishe katika wakati wote inatumia takwimu sahihi zilizothibitishwa katika kufanya maamuzi. Hatua hii iende sambamba na kutenga bajeti ya kutosha kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (National Bureau of Statistics - NBS) ili kutekeleza jukumu lake la msingi na la kisheria la kuandaa na kutunza takwimu kwa matumizi mbalimbali.

### 4.4. Sekta za Mageuzi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa miaka mitano (2026/27 - 2030/31) Serikali imekusudia kufanya mageuzi katika sekta mbalimbali ambazo ndio nguzo za mabadiliko ya nchi kuelekea uchumi imara wenye ushindani

na unaongozwa na mauzo nje ya nchi. Mageuzi ya kisekta yanakusudia kubadilisha Sera, Sheria, miundo ya uendeshaji, matumizi ya teknolojia mpya, kuboresha mbinu za utoaji huduma pamoja na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imechambua mikakati ya mageuzi yanayotarajiwa kufanyika katika sekta husika kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo na ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

### 4.4.1. Kilimo

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Sekta ya kilimo ni kati ya sekta muhimu ambayo mchango wake katika Pato la Taifa umefikia **asilimia 26.3** mwaka 2024 na kufanya sekta hiyo kuwa miongoni mwa sekta zilizochangia ukuaji wa uchumi kwa **asilimia 15.3.** Manufaa mengine ya sekta hiyo ni uhakika wa utoshelevu wa chakula hadi kufikia **asilimia 128** mwaka 2023/24 pamoja na kuajiri zaidi ya **asilimia 54.2** ya watanzania. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa sekta hii, ukuaji wake ni **asilimia 4.1** mwaka 2024 ikiwa ni chini ya lengo lilowekwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo la **asilimia 5.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano, yameainisha shabaha 8 zinazotarajiwa kufikiwa kwenye sekta ya Kilimo ifikapo mwaka 2030/31. Jedwalli Na. 4 linaonyesha shabaha ambazo zinatarajiwa kufikiwa na Serikali katika Sekta ya Kilimo ifikapo 2031.

**Jedwali Na. 4. Shabaha za Sekta ya Kilimo**

| Shabaha | 2024 | 2030/31 |
|---|---|---|
| Mchango wa kilimo katika Pato la Taifa (%) | 26.3 | 25.6 |
| Ukuaji wa Sekta ya Kilimo (%) | 4.1 | 10 |
| Mchango wa ajira za Sekta ya Kilimo kwa ajira zote zinazopatikana nchini (%) | 54.2 | 50 |
| Thamani ya Mauzo ya Bidhaa za Kilimo | 3.54 | 5 |

| | | |
|---|---|---|
| Nje ($ bilioni) | | |
| Upotevu wa mazao ya kilimo (%) | 35 | 10 |
| Mikopo kwa Sekta ya Kilimo (%) | 14.9 | 20 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa Miaka Mitano*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuboresha sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maghala na mabwawa ya umwagiliaji, upatikanaji wa mbegu, mbolea ya ruzuku na pembejeo za kisasa, kuongezeka kwa bajeti ya sekta ya kilimo kufikia **shilingi trilioni 1.24** na uanzishwaji wa Benki ya Ushirika Tanzania. Hata hivyo, ili kufikia malengo yanayotarajiwa Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. kudhibiti upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kwa kuwa na maghala, vihenge na vyumba vya baridi vya kutosha ambavyo vitakodishwa kwa wanachi ili wavitumie kuhifadhi mazao yao na hivyo kupunguza upotevu;

ii. Kuweka kipaumbele mahsusi katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati ya biashara kama vile korosho, kahawa,chai, pamba na tumbaku yanayouzwa nje ya nchi ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni;

iii. Benki Kuu kuendelea kulegeza masharti ya utoaji wa mkopo wa dirisha maalum wa **shilingi trilioni 1** kwa benki za iashara zinazotoa mikopo ya kilimo baada ya kujiridhisha kwamba mikopo hiyo inaelekezwa kwenye kilimo cha uzalishaji badala ya biashara ya mazao ya kilimo;

iv. Kuhakikisha mapato ya mfuko wa maendeleo ya kilimo yanaelekezwa katika uwekezaji unaongeza uzalishaji na tija wa sekta;

v. kuwekeza zaidi katika upatikanaji wa mbegu bora, miradi ya umwagiliaji, zana za kilimo pamoja na uhifadhi;

vi. kuendelea na jitihada za kuhimilisha mifugo pamoja na kuanzisha, kufufua na kuendeleza viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo;

vii. kutekeleza na kukamilisha miradi ya kilimo kwa wakati ili kupunguza gharama na kuleta tija iliyokusudiwa;

viii. kuhamasisha ushiriki wa sekta ya binafsi ili kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo; na

ix. Kutumia vyama vya ushirika ili kuchochea mapinduzi ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo hasa katika maeneo ya vijijini. Hatua hii itasaidia kuzalisha ajira maeneo ya vijijini na hivyo kuzuia wimbi la vijana kuhamia maeneo ya mjini.

### 4.4.2. Sekta ya viwanda na uzalishaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, sekta ya viwanda inajumuisha uzalishaji, ujenzi, madini na nishati ambapo kwa pamoja sekta hizo kwa kipindi cha miaka 25 zimekua kwa **asilimia 5.5** na mchango wa sekta hizo kwenye Pato la Taifa kufikia **asilimia 30.4**. Aidha, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano, yameainisha shabaha 8 zinazotarajiwa kufikiwa kwenye sekta hii ifikapo mwaka 2030/31. Kamati imefanya uchambuzi wa shabaha zote, hata hivyo imejielekeza katika baadhi ya Shabaha kama zinavyoonekana kwenye jedwali na. 5.

**Jedwali Na. 5. Shabaha za Sekta ya Viwanda na Uzalishaji**

| Shabaha | 2024 (%) | 2030/31(%) |
|---|---|---|
| Mchango wa ujumla wa Sekta wa viwanda na uzalishaji katika Pato la Taifa (%) | 30.4 | 36.5 |
| Ukuaji wa Sekta ya Viwanda (%) | 5.5 | 8.0 |
| Mchango wa ajira za Sekta ya viwanda kwa ajira zote zinazopatikana nchini (%) | 9 | 15 |

| | | |
|---|---|---|
| Mchango wa ajira za Sekta ya uzalishaji kwa ajira zote zinazopatikana nchini (%) | 6 | 10 |
| Mchango wa Bidhaa zinazozalishwa viwandani kwa bidhaa zote zinazouzwa nje (%) | 22 | 30 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa Miaka Mitano*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa shabaha zinazotarajiwa kufikiwa na sekta hii ifikapo mwaka 2030/31 na ina ushauri na maoni yafuatayo:-

i. kuunganisha mamlaka zote za udhibiti na kuanzisha Mamlaka moja ili kupunguza wingi wa Mamlaka za udhibiti pamoja na kuwa na mfumo mmoja wa malipo (single payment system) utakaotumiwa na wafanyabiashara kulipa ada, tozo, leseni na faini zote za Mamlaka za Udhibiti kwa wakati mmoja;

ii. kuongeza thamani za malighafi na mazao ya kilimo na uvuvi kabla ya kuuza nje;

iii. kuhamasisha viwanda vilivyopo kutumia teknolojia ya kisasa, hatua hii iende sambamba na upatikanaji wa nishati ya uhakika na nafuu ili kupunguza gharama za uzalishaji;

iv. kuweka vivutio kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa ambazo zinachochea uanzishwaji wa viwanda vingine;

v. Serikali kuhakikisha inatenga walau **asilimia 1.5** ya bajeti kila mwaka kwa ajili ya utafiti na maendeleo (R&D) ikilinganishwa na bajeti inayotengwa hivi sasa ya chini ya **asilimia 0.5**. Hatua hii itasaidia kuongeza ubunifu na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali katika soko.

*4.4.3. Sekta ya utalii*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, sekta ya utalii inachangia **asilimia 27** ya Pato la Taifa mwaka 2024. Ufanisi huu umetokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka watalii **milioni 1.8** mwaka 2023 hadi kufikia **milioni 2.14** mwaka 2024. Aidha, mapato yaliongezeka kutoka **dola za Marekani bilioni 3.37** mwaka 2023 hadi kufikia **dola za Marekani bilioni 3.9** mwaka 2024. Sekta hii inahitaji kufikia shabaha zifuatazo ifikapo mwaka 2030/31:-

i. Mapato ya kigeni yatokanayo na sekta ya utalii kufikia **Dola za Marekani bilioni 4.81** ikilinganishwa na **Dola za Marekani bilioni 3.9** ya mwaka 2024; ii. Mchango wa mapato ya Utalii katika mapato ya nje kufikia **asilimia 35** ikilinganishwa na **asilimia 27** ya mwaka 2024; na iii. Mchango wa huduma za malazi katika Pato la Taifa kufikia **asilimia 1.4** ikilinganishwa na **asilimia 1.1** ya mwaka 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa shabaha hizo na inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

i. kuendelea kuboresha na kuimarisha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege vidogo (Airstrips) kwenye maeneo yenye vivutio vya utalii;

ii. kuendeleza mikakati mbalimbali ya kukuza na kuhamasisha shughuli za utalii kama vile utalii wa picha, michezo, matibabu, mikutano, fukwe za bahari, utamaduni, urithi wa kihistoria pamoja na kuendelea kuboresha jumuiya za hifadhi za wanyamapori. Hatua hii itasaidia kuongeza shughuli za utalii;

iii. kuboresha mitaala ya vyuo vya utalii hususan katika eneo la ukarimu ili iweze kutoa huduma kwa kiwango cha juu na matumizi ya lugha za kimataifa;

iv. kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji kwenye ujenzi wa hoteli kwa sababu moja ya changamoto inayoikabili sekta hii ni ukosefu wa vitanda;

v. ushiriki wa watanzania katika mnyororo wa thamani wa shughuli zautalii; na

vi. kuimarisha kampeni za utalii za kidigitali katika masoko yetu ya kimkakati.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inatambua jitihada mbalimbali ambazo Serikali imeendelea kufanya ili kuboresha sekta ya utalii ikiwemo filamu ya *The Royal Tour* ambayo imeleta mafanikio makubwa.

### *4.4.4. Uchumi wa Buluu*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uchumi wa buluu unahusisha matumizi ya rasilimali zipatikanazo majini ili kukuza uchumi na uboreshaji wa maisha huku mfumo wa ikolojia ya bahari ukihifadhiwa. Uchumi wa buluu unahusisha uvuvi, ufugaji wa samaki (aquaculture), usafirishaji, bandari, utalii, nishati za pwani na bioteknolojia ya baharini. Tanzania ina eneo la **kilometa za mraba 61,500** za maji safi, **kilometa za mraba 64,000** za maji ya bahari, eneo la Uchumi Maalum (Exclusive Economic Zone) la **kilometa za mraba 223,000** na pwani ya **kilometa za mraba 1,424** na hivyo kuifanya nchi kuwa na fursa za kutosha za rasilimali za maji barani Afrika. Pamoja na uwepo wa fursa hizo bado hazijaweza kutumika kikamilifu ili kuchangia uchumi na maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchumi wa buluu unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile miundombinu duni, uvuvi usio endelevu, uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira ya baharini unaohatarisha bioanuwai pamoja na uharibifu unaotokana na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, mifumo dhaifu ya utafiti na ubunifu pamoja na ukosefu wa viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya baharini kwa pamoja vinasababisha kutotumia kikamilifu fursa zilizoko kwenye bahari na maziwa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuboresha sekta hii kwa kuandaa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024, kujenga bandari ya uvuvi ya Kilwa Masoko, kutoa mikopo nafuu ya boti na kujenga vizimba ili kuhakikisha inafikia malengo ya kuchangia **asilimia 3.5** ya Pato la Taifa ikilinganishwa na **asilimia 1.7** ya mwaka 2024. Aidha, afua hizi zitaongeza mapato yatokanayo na utalii wa baharini kufikia **shilingi trilioni 2** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 800** ya mwaka 2024. Kamati inaishauri Serikali kutanzua changamoto zinazosababisha kutotumia fursa za uchumi wa buluu na kuhakikisha inatekeleza kikamilifu mipango na mikakati ikiwemo kukamilisha ijenzi wa bandari ya uvuvi ya kilwa masoko na uvuvi na ununuzi wa meli za wa uvuvi bahari Kuu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ifikapo mwaka 2030/31.

## 4.5. Uwezo wa kustahimili mabadiliko ya tabianchi

### 4.5.1. Biashara ya Hewa Ukaa

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na kwamba Tanzania ina misitu yenye ukubwa unaokadiriwa kufikia hekta **milioni 48.1** sawa na **asilimia 55** ya eneo lote la ardhi la nchi. Tanzania bado haijaweza kunufaika kikamilifu na biashara ya kaboni. Mfano wa nchi zilizonufaika na biashara ya kaboni ni Brazili kupitia msitu wa Amazon, Indonesia kupitia miradi ya kupunguza uharibifu wa misitu ya Peatland na Kenya kupitia miradi ya carbon offset zimekuwa wanufaika wakubwa wa biashara ya hewa ukaa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kukuza biashara hii ushiriki wa nchi katika masoko ya kimataifa ya hewa ukaa bado ni mdogo ambapo umekuwa ukiingiza takribani **Dola za Marekani bilioni 1** kwa mwaka ikilinganishwa na soko la Kimataifa la **Dola za Marekani bilioni 20** kwa mwaka. Mchango mdogo umetokana na changamoto kama vile kutokamilika kwa usajili na uthibitisho wa misitu, uelewa mdogo wa wananchi kuhusiana na biashara ya hewa ukaa, matumizi hafifu ya nishati mbadala na ukataji wa miti unaoendelea.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hadi ifikapo mwaka 2030/31 mapato yanayotokana na biashara ya hewa ukaa yanatarajiwa kuwa **Dola za Marekani bilioni 3** na ushiriki wa jamii katika miradi ya biashara ya hewa ukaa kuongeza kufikia kati ya **asilimia 10** hadi **15** ikilinganishwa na **asilimia 5** ya mwaka 2024, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. kujenga mfumo wa kisasa wa kidigitali wa upimaji, utoaji ripoti na uthibitishaji *(Measurement, Reporting and Verification MRV)* utakaotumika kubainisha thamani ya misitu katika biashara ya kaboni;

ii. kuhakikisha biashara ya hewa ukaa inakuwa shirikishi kwa wananchi ili wawe walinzi wa mazingira kwa kuwa wao ndio wanufaika wakuu; na

iii. kutoa elimu na mafunzo kwa wataalamu wa misitu ili kuongeza ujuzi na utaalamu utakaowezesha kufikia malengo ya Serikali ya kunufaika na biashara ya hewa ukaa.

### 4.6. Ugharamiaji wa Mpango

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Miaka Mitano jumla ya uwekezaji unaohitajika unakadiriwa kufikia **Shilingi bilioni 477,746.46** sawa na **Dola za Marekani bilioni 183**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 324,487.46** sawa na **asilimia 70** zinatarajiwa kuchangiwa na sekta binafsi na **Shilingi bilioni 153,259.30** sawa na **asilimia 30** zinatarajiwa kuchangiwa na sekta ya Umma. Kati ya kiasi kitakachochangiwa na sekta ya Umma **shilingi trilioni 115.04** zitachangiwa kupitia taasisi za Serikali na **shilingi trilioni 38.22** zitafadhiliwa na Mashirika ya Umma kupitia faida zilizopatikana pamoja na ongezeko la mitaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mfumo wa ugharamiaji wa Mpango unaonyesha nia ya dhati ya Serikali kutoa kipaumbele kwa sekta binafsi kama injini ya ukuaji wa uchumi. Uwekezaji wa sekta binafsi unatarajiwa kutokana na uwekezaji binafsi wa ndani *(Domestic Private*

*InvestmentDPI),* Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje *(Foreign Direct Investment – FDI)*, ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), masoko ya mitaji ya ndani pamoja na vyanzo vya ugharamiaji vinavyotokana na mazingira (*climate-financing instruments)*.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kuhakikisha Serikali inafikia malengo yaliyokusudiwa ya kugharamia Mpango wa Nne wa Miaka Mitano, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuendelea kutoa upendeleo kwa wawekezaji wa ndani katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

### 4.7. Miradi ya kielelezo

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mpango wa Nne wa Miaka Mitano Serikali imekusudia kutekeleza programu za kielelezo ili kuweka msingi wa mageuzi ya muda mrefu yatakayochochea maendeleo. Kati ya programu hizo, **asilimia 20** ya afua zilizoainishwa zinakadiriwa kugharimu kati ya **asilimia 40** hadi **50** ya gharama zote za mpango na kuwezesha kufikia takribani **asilimia 80** ya matokeo ya kiuchumi na kijamii yanayotarajiwa ifikapo 2030/31. Programu hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Mji wa ikolojia na Bahari Bagamoyo;
ii. Mradi wa Mchuchuma na Liganga;
iii. Mradi wa gesi asilia (LNG) wa Lindi;
iv. Kituo cha ubunifu wa teknolojia na madini muhimu cha Dodoma;
v. Mpango wa Taifa wa umwagiliaji na viwanda vya mazao ya kilimo;
vi. Kitovu mahiri cha viwanda na uchumi wa buluu cha maziwa makuu; na
vii. Muunganiko wa ukuaji wa miji Tanzania.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchaguzi wa programu hizi umezingatia masuala mbalimbali kama vile:-

i. ulinganifu wa vipaumbele vya Dira ya Taifa ya 2050, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2026/27-2050/51) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III);

ii. matokeo ya kiuchumi na kijamii katika upatikanaji wa ajira, kuongeza mnyororo wa thamani na ukuaji jumuishi wenye tija;

iii. utayari wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa upembuzi yakinifu na upatikanaji wa vibali stahiki;

iv. kuimarisha ushirikiano wa sekta mbalimbali;

v. uwezo wa kuvutia mitaji ya sekta binafsi hususan uwekezaji wa ndani na wa moja kwa moja kutoka nje pamoja na mitaji ya watanzania waishio nje ya nchi;

vi. uwezo wa kuongeza ushindani wa kimataifa kupitia mauzo ya nje, matumizi ya teknolojia ya kisasa na ubunifu wa viwanda; na

vii. uwiano wa ukuaji wa miji na ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, moja ya changamoto iliyoathiri utekelezaji wa Mpango wa muda mrefu uliopita ni miradi kutokukamilika kwa wakati na hivyo kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaanza na utekelezaji wa miradi michache itakayochochea utekelezaji wa miradi mingine.

### 4.8. Utekelezaji, usimamizi na uwajibikaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mpango wa Maendeleo wa Kwanza na wa Pili wa Miaka mitano Majukumu ya utekelezaji, usimamizi na uwajibikaji wa Mpango yalikasimiwa kwa wadau mbalimbali kama vile Wizara, Idara, Wakala, Mashirika, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, asasi za kiraia na Washirika wa Maendeleo. Aidha, katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano utekelezaji, usimamizi na uwajibikaji uliboreshwa kufuatia kurejeshwa kwa Tume ya Taifa ya Mipango *(National Planning Commission -NPC)* kupitia Sheria ya Tume ya Mipango Sura 127

ambayo ilikasimiwa majukumu ya uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango. Kamati inampongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuona umuhimu wa kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango kwani hatua hii ilitekeleza kwa vitendo azma yake ya kuimarisha utekelezaji wa mpango na kuimarisha uwajibikaji. Hatua hii ilienda sambamba na uanzishwaji wa vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ili kuimarisha na kuongeza ufanisi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na uanzishwaji wa Tume ya Mipango bado utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. ugharamiaji wa miradi kwa kiasi kikubwa kutegemea rasilimali fedha kutoka Serikalini;

ii. Serikali kutawanya rasilimali fedha finyu zilizopo kwenye miradi mingi, matokeo yake miradi kutokamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa; na

iii. vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini kutokuwa na Bajeti ya kutosha na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaitaka Tume ya Mipango kutumia kifungu cha 26 cha Sheria ya Tume ya Mipango Sura 127 kuhakikisha kwamba maafisa masuuli wanatekeleza jukumu la ufuatiliaji na tathmini kama inavyotakiwa kisheria. Aidha, kifungu hicho kiboreshwe ili kuweka hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa kwa maafisa masuuli na wakuu wa vitengo watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0. UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ni wa kwanza katika utekelezaji wa

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV: 2026/27–2030/31) wenye dhima ya *"Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira"* unaotekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango yanabainisha maeneo ya kimkakati ambayo yametokana na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo hayo ni:-

i. uchumi imara, jumuishi na shindani;
ii. kuimarisha tija na kuleta mageuzi ya kiuchumi kwenye sekta za kimkakati;
iii. uwezo wa watu na maendeleo ya jamii;
iv. uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;
v. kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo;
vi. kuimarisha misingi endelevu ya taifa; na
vii. ujumuishaji wa mabadiliko na kuwekeza kwenye maeneo yanayoleta mageuzi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Shabaha za Mpango wa Mwaka 2026/27 kwa kulinganisha na malengo. Shabaha hizo ni:-

### 5.1. Shabaha za Mpango wa Mwaka 2026/27

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka 2026/27 Serikali imekusudia kutekeleza Malengo na shabaha zifuatazo:-

i. kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia **asilimia 6.3** mwaka 2026 ikilinganishwa na matarajio ya ukuaji wa **asilimia 5.9** kwa mwaka 2025;

ii. kudhibiti mfumuko wa bei ili ubaki katika wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati kwa lengo la kulinda uwezo wa wananchi kumudu mahitaji muhimu;

iii. kuongeza mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2026/27, kutoka matarajio ya asilimia 16.8 mwaka 2025/26;

iv. kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2026/27, kutoka matarajio ya asilimia 13.3 mwaka 2025/26;

v. kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2026;

vi. kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

vii. kuongeza uzalishaji wa ajira kufikia 1,700,000 mwaka 2026 kutoka ajira 981,000 zilizozalishwa mwaka 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ilifanya uchambuzi wa baadhi ya shabaha kwa kulinganisha na malengo ya Dira 2050. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 5.1.1. Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2026/27

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha miaka mitatu (20232025) kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi nchini kimekuwa ni uwekezaji wa Serikali. Aidha, mwaka 2026 uchumi unatarajiwa kukua kwa **asilimia 6.3**, ukuaji huo utachagizwa na uwekezaji wa Serikali katika sekta za mageuzi. Pamoja na kwamba si vibaya ukuaji wa uchumi kuchochewa na uwekezaji wa Serikali, kihatarishi kilichopo ni endapo itatokea mdororo wa kiuchumi itakuwa ni vigumu kuurejesha uchumi katika hali ya kawaida kwa sababu njia inayotumika mara nyingi kuurudisha katika hali ya kawaida ni kupitia uwekezaji wa Serikali ambapo kwa wakati huo itakuwa imeshindikana.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na kihatarishi hicho, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi ya kuvutia sekta binafsi kuchangia **Shilingi trilioni 60** katika utekelezaji wa

mpango wa maendeleo ili kuchochea ukuaji wa uchumi kama inavyotarajiwa.

### 5.1.2. Kuongeza uwiano wa Mapato ya Ndani na Mapato ya Kodi kwa Pato la Taifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka 2026/27 Serikali inakusudia kuongeza uwiano wa mapato ya kodi kwa pato la Taifa hadi kufikia **asilimia 13.7** kutoka **asilimia 13.3** ya mwaka 2025/26. Hata hivyo, uwiano huu upo chini ya wastani wa kodi kwa pato la Taifa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara wa **asilimia 15**. Kamati imefanya uchambuzi wa baadhi ya sababu zinazofanya uwiano kuwa chini ya wastani na kubaini yafuatayo:-

i. uwepo wa changamoto za kiutawala katika kusimamia mfumo mzima wa kodi;

ii. baadhi ya maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kushiriki kwenye vitendo visivyokuwa na uadilifu;

iii. uwepo wa sekta isiyo rasmi ambayo ni takribani **asilimia 54** ya uchumi; na

iv. uwepo wa misamaha ya kodi isiyo na tija, mfano katika mwaka 2024/25 misamaha ya kodi kwa pato la taifa ilikuwa **asilimia 2.5**. Aidha, jumla ya **Shilingi trilioni 5.5** sawa na **asilimia 15** zilisamehewa kutoka kwenye mapato ya kodi ya shilingi **trilioni 35.6**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba inashughulikia changamoto hizo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya kodi sambamba na kutumia sheria zilizopo ili kuleta uwajibikaji.

## 5.2. Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 yamejielekeza katika maeneo matano (5) mahsusi ambayo ni:

i. kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora;
ii. kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko;
iii. kuimarisha miundombinu ya kidijitali, nishati na usafirishaji fungamanishi;
iv. kuimarisha Sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji thamani na ukuaji jumuishi; na
v. uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2026/27 yamechaguliwa kwa kuzingatia vigezo vinavyolenga kujenga msingi wa utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendelo wa Miaka Mitano (Five Year Development Plan-FYDP IV) kuelekea Dira 2050. Vigezo hivyo ni pamoja na uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimfumo kwa kuondoa urasimu na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, utayari wa kuanza utekelezaji wa miradi iliyokwama au iliyotayari kutekelezwa, kuchochea ukuaji wa sekta nyingine kupitia sekta zinazokua kwa kasi na kuzalisha ajira kwa wingi hususan kwa vijana.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** vigezo hivyo pia vinatoa kipaumbele kwa sekta zenye uwezo wa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kuongeza ushindani kimataifa kwa kuongeza thamani ya huduma na bidhaa, kuchangia fedha za kigeni, mapato ya Serikali, miradi inayohimiza uhifadhi wa mazingira pamoja na kuongeza uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 umejikita katika kuendeleza utekelezaji wa afua za maendeleo ambazo hazikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa mpango elekezi wa maendeleo wa muda mrefu (2011/12 – 2025/26). Hatua hii ni muhimu kwa sababu zifuatazo:-

i. inahakikisha utekelezaji wa miradi na programu ambazo zilikuwa hazijatekelezwa zinatekelezwa ili kuleta manufaa na tija iliyokusidiwa;

ii. inahakikisha rasilimali zilizotumika hazipotei kwa kutotekeleza miradi kikamilifu ili ilete manufaa yaliyokusudiwa; na

iii. inalenga kukamilisha afua zilizobaki ziwe msingi wa kufanya mageuzi ya kimfumo na kimuundo ili kuongeza tija na ushindani.

### 5.3. Misingi ya kufikia Malengo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/27 utajengwa katika misingi ifuatayo:-

i. kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji;

ii. kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;

iii. kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati, bandari, barabara na reli ili kuchochea biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda waAfrika Mashariki na Kati;

iv. kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;

v. utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala chini ya falsafa ya 4Rs, unaolenga kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji;

vi. kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji kwa kushirikiana na sekta binafsi na ushirikiano wa kikanda (EAC na SADC); na

vii. kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari zake.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** misingi inayopendekezwa ya utekelezaji wa Mpango inaonesha mfumo mpana na wa kimkakati, hata hivyo ufanisi wake utategemea namna Serikali itakavyoshughulikia changamoto zilizopo na kutumia fursa na uwezo wa kimuundo uliopo kwa ufanisi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i. kufungamanisha vipaumbele vinavyofanana ili kutumia rasilimali fedha kwa ufanisi;
ii. kuimarisha uwezo wa taasisi katika usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa na kuleta manufaa yaliyokusudiwa;
iii. kuweka mikakati thabiti ya ufadhili, hususan kwenye miradi ya mazingira na miundombinu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
iv. kupanua huduma za kidijitali na miundombinu vijijini ili kuhakikisha kunakuwa na ustawi wa jamii; na
v. kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi.

## 5.4. Ugharamiaji wa Mpango

### 5.4.1. Uwiano wa Ugharamiaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 unatarajiwa kugharimu jumla ya **shilingi trilioni 84.9.**

Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 19.3** ni kutoka kwenye bajeti ya Serikali, **Shilingi trilioni 5.5** ni kutoka katika Mashirikia ya umma yanayojiendesha kibiashara na **Shilingi trilioni 60.1** ni kutoka sekta binafsi. Mgawanyo huo unaonyesha kwamba ugharamiaji wa Mpango umegawanyika kwa uwiano wa **70:30** kati ya sekta binafsi na Umma.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika Mpango wa miaka mitano uliopita (2021/22 - 2025/26) sekta binafsi ilitarajiwa kuchangia jumla ya **Shilingi trilioni 40.61** sawa na **asilimia 35.38** ya mahitaji yote ya fedha ya **Shilingi trilioni 114.8.** Lengo la Serikali katika kuhakikisha sekta binafsi inachangia **Shilingi trilioni 60** kwa mwaka mmoja linaweza lisifikiwe kutokana na mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kutokuwa rafiki. Hivyo, ni lazima kuhakikisha suala la uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji linakuwa kipaumbele cha kwanza ili tuweze kufikia lengo.

**5.4.2. Vyanzo Vya Mapato**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/27, Serikali pamoja na kutegemea vyanzo vilivyozoeleka ambavyo ni mapato ya ndani, mikopo na mitaji, imepanga kutumia vyanzo vingine kama vile hatifungani za makampuni (corporate bonds) na hatifungani za watanzania wanaoishi nje ya nchi pamoja na kufungua masoko ya mitaji ifikapo 2027.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufungua soko la mitaji maana yake ni kuondoa vizuizi vinavyoathiri uhuru wa kuingia na kutoka kwa mitaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na wa kimataifa. Ili kufungua masoko ya mitaji masuala yafuatayo ni lazima yazingatiwe. Kwanza ni utulivu wa uchumi jumla; utayari na uimara wa Taasisi za usimamizi; vihatarishi vya kufungua soko la mtaji na madhara yanayoweza kujitokeza; kufanya mabadiliko ya soko la fedha taratibu na kwa mpangilio pamoja na kupima manufaa na athari za kufungua soko la mitaji. Baadhi ya athari za kufungua soko la mitaji ni kuruhusu sehemu ya uchumi kumilikiwa na wageni na uchumi kuathirika kirahisi inapotokea

misukosuko katika masoko ya dunia. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ya faida na hasara za kufungua soko la mitaji kabla ya kutekeleza mapendekezo hayo.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0. UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KATIKA MUDA WA KATI (2026/27 – 2028/29)

### 6.1. Mwenendo wa Hali ya Uchumi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ilifanya uchambuzi wa baadhi ya viashiria vya uchumi na kubaini masuala yafuatayo:-

#### 6.1.1. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hadi kufikia mwezi Novemba, 2025 deni la Serikali lilikuwa **Shilingi trilioni 109.012** sawa na ongezeko la **asilimia 8.63** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 100.35** katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji pamoja na kupokelewa kwa mikopo mipya. Jedwali na. 6 linaonyesha deni la Serikali ni himilivu katika muda wa kati kwa viwango vya Kimataifa.

**Jedwali Na.6. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (2023/24-2025/26)**

| Viashiria vya Uhimilivu | Ukomo | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|
| Deni la Nje | | | | |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Pato la Taifa | 40 | 23.6 | 24.1 | 24 |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | 180 | 127.5 | 123.8 | 124.5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nchi | 15 | 11.7 | 13.9 | 12.8 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | 18 | 14.5 | 17.2 | 15.5 |
| Deni la Serikali (Ndani na Nje) | | | | |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa | 55 | 41.1 | 40.3 | 39.5 |
| pato la Taifa | | | | |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa Mapato | N/A | 267.6 | 251.1 | 241.3 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | N/A | 35.4 | 50.9 | 40.8 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Tathmini ya Utelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na kwamba deni letu ni himilivu, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatao:-

i. kuhakikisha kwamba tunaongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ili kuepuka kufikia ukomo wa **asilimia 15**; na

ii. kuweka ukomo wa uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani ili kuhakikisha katika kipindi chote malipo ya mikopo iliyoiva haizidi **asilimia 30** ya mapato ya Serikali yanayotokana na kodi;

### 6.2. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti Katika Kipindi cha Nusu Mwaka 2025/26

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/26 katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2025 na katika uchambuzi wake ilibaini masuala yafuatayo:-

### 6.2.1. Mwenendo wa Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2025, Serikali ilikusanya jumla ya **shilingi trilioni 22.88** kutoka vyanzo vya ndani na nje sawa na **asilimia 40.5** ya lengo la mwaka la kukusanya **shilingi trilioni 56.49.** Mapato ya kodi yalikuwa **shilingi trilioni 13.1** sawa na **asilimia 38.4** ya lengo la mwaka la **shilingi trilioni 34.1**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi hicho, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya **shilingi trilioni 22.94** sawa na **asilimia 40.5** ya matumizi yote kwa mwaka 2025/26 ya **shilingi trilioni 56.5.** Matumizi yaliyozidi ya **shilingi bilioni 60** yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu (*overdraft*) ambao unaruhusiwa chini ya Vifungu vya 34 na 35 vya Sheria ya Benki Kuu Sura ya 197.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia mwenendo huo wa ukusanyaji wa mapato, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mifumo pamoja na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari ili kufikia lengo la utekelezaji wa Bajeti.

### 6.3. Usimamizi wa Vihatarishi

### 6.3.1. Madeni Sanjari

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** moja ya kihatarishi kilichobainishwa na Serikali ni uwezekano wa uwepo wa madeni sanjari ambayo yatalazimika kulipwa na Serikali endapo Shirika ama kampuni ya Umma iliyopewa dhamana na Serikali itashindwa kulipa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuyaacha mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yajiendeshe yenyewe ili kuongeza ufanisi na kupunguza mzigo wa Serikali kwa kuyapa ruzuku na hivyo kuongeza mchango wa mashirika hayo kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, hatua hii iende sambamba na kuimarisha mifumo ya usimamizi ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba ya utendaji kazi na kuimarisha uwajibikaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mapendekezo ya Serikali ya kuyaachia mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yanatoa fursa kwa mashirika hayo kuwa na uwezo wa kutumia masoko ya mitaji ili kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma kama Dira ya 2050 inavyoelekeza.

### 6.3.2. Mabadiliko ya Sera za Nchi Wahisani

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuimarisha Diplomasia ya Uchumi na kuhamasisha wahisani kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18 - 2029/30, pamoja na Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2021. Hata hivyo, kumekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya masharti ya misaada na wakati mwingine yanakinzana na vipaumbele vya kitaifa. Kamati inaitaka Serikali kufanya mapitio ya Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/182029/30 ili kuhakikisha unaenda sambamba na utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka ishirini na tano pamoja na mwenendo wa mabadiliko ya siasa za dunia.

### 6.3.3. Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mabadiliko ya Tabianchi na majanga ya asili yanaendelea kuwa kihatarishi kikubwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kwani husababisha uharibifu wa miundombinu, kupungua kwa uzalishaji katika sekta muhimu kama vile nishati pamoja na kuibua mahitaji ya dharura yanayolazimu kubadilisha vipaumbele vya matumizi ya fedha. Aidha, Kamati inampogeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mfuko wa dharura katika kipindi chote unakuwa na fedha za kutosha ili kukabiliana na majanga na hivyo kutoathiri Bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, uendeshaji wa mfuko huo uzingatie matakwa ya vifungu vya 38 hadi 40 vya Sheria ya Bajeti Sura 439.

## 6.4. Mfumo wa Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha muda wa kati, Serikali imekusudia kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 204.09** sawa na **shilingi trilioni 61.93, shilingi trilioni 69.16 na shilingi trilioni 72.99** kwa mwaka 2026/27, 2027//28 na 2028/29 mtawalia. Mgawanyo wa mapato na matumizi ni kama unavyoonekana katika **jedwali Na. 7** na **8**.

**Jedwali Na. 7: Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27 hadi 2028/29**

| | 2025/26 | 2026/27 | | | 2027/28 | 2028/29 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | BAJETI INAYOPENDEKEZWA | TOFAUTI | UKUAJI/ ONGEZEKO | MAOTEO | MAOTEO |
| **A: Mapato** | **41,536,016** | **46,691,299** | **5,155,283** | **12.4** | **52,360,781** | **58,390,269** |
| Mapato ya kodi | 32,306,123 | 36,889,320 | **4,583,197** | **14.2** | 41,393,268 | 46,260,777 |
| Misaada/ Michango | 1,069,884 | 563,139 | **-506,745** | **-47.4** | 516,459 | 486,219 |
| Mapato mengine | 8,160,009 | 9,238,839 | **1,078,830** | **13.2** | 10,451,054 | 11,643,273 |
| Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680,507 | 1,966,193 | **285,686** | **17.0** | 2,300,446 | 2,691,522 |
| D1 - Mikopo ya ndani | **6,278,186** | **6,257,744** | **-20,442** | **-0.3** | **7,681,816** | **6,723,935** |
| E1 - Mikopo ya nje | **8,676,050** | **8,985,150** | **309,100** | **3.6** | **9,118,969** | **7,877,782** |
| **Jumla ya Bajeti (A + D1 + E1)** | **56,490,252** | **61,934,193** | **5,443,941** | **9.6** | **69,161,566** | **72,991,986** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Maandalizi ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29)*

**Jedwali Na. 8: Makadirio ya matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2026/27 hadi 2028/29**

| | 2025/26 | 2026/27 | | | 2027/28 | 2028/29 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **BAJETI ILIYOIDHINISHWA** | **BAJETI INAYOPENDEKEZWA** | **TOFAUTI** | **ONGEZEKO** | **MAOTEO** | **MAOTEO** |
| **Matumizi** | **45,994,829** | **51,068,233** | **5,073,404** | **11.0** | **56,087,146** | **60,965,872** |
| Mishahara na stahiki za watumishi | 7,711,867 | 9,685,742 | **1,973,875** | **25.6** | 11,530,985 | 13,293,402 |
| Gharama za bidhaa na huduma | 7,812,245 | 8,202,857 | **390,612** | **5.0** | 8,613,000 | 9,043,650 |
| Malipo ya riba | 6,493,715 | 7,257,876 | **764,161** | **11.8** | 8,019,853 | 8,208,854 |
| Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji | 1,936,023 | 1,923,246 | **-12,777** | **-0.7** | 1,888,215 | 1,854,057 |
| Ruzuku na michango | 21,107,935 | 23,018,817 | **1,910,882** | **9.1** | 25,006,413 | 27,485,795 |
| Mafao na misaada ya kijamii | 752,516 | 790,141 | **37,625** | **5.0** | 829,649 | 871,131 |
| Gharama nyingine | 180,528 | 189,554 | **9,026** | **5.0** | 199,032 | 208,984 |
| **Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | **2,780,160** | **3,030,375** | **250,215** | **9.0** | **3,203,774** | **3,394,826** |
| **Malipo ya mikopo ya ndani** | **3,325,557** | **3,285,395** | **-40,162** | **-1.2** | **4,024,778** | **3,649,007** |
| **Malipo ya mikopo ya nje** | **4,389,707** | **4,550,190** | **160,483** | **3.7** | **5,845,868** | **4,982,281** |
| **Jumla ya Bajeti** | **56,490,252** | **61,934,193** | **5,443,941** | **9.6** | **69,161,566** | **72,991,986** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Maandalizi ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu mfumo wa bajeti katika muda wa kati na inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

### *6.4.1. Mapato ya Kodi*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mapato ya kodi yanatarajiwa kuongezeka kutoka **shilingi trilioni 32.30** mwaka 2025/26 hadi **shilingi trilioni 36.89**

mwaka 2026/27 sawa na ongezeko la **asilimia 14.2.** Hata hivyo uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa (*tax to GDP ratio*) unatarajiwa kufikia **asilimia 13.7** mwaka 2026, kiwango ambacho ni kidogo kuliko kiwango cha wastani cha Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara cha **asilimia 15**. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. Wizara ya Fedha kufanyia kazi changamoto zinazohusu sera za kodi zinazowasilishwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kwa lengo la kuboresha mifumo ya kodi na ukusanyaji wa mapato;

ii. kuanzisha somo la kodi katika ngazi zote za elimu sambamba na kuendelea kutumia klabu za kodi ili kujenga tabia ya ulipaji kodi kwa hiari;

iii. kuhakikisha Bodi ya Rufani za Kodi (Tax Revenue Appeals Board-TRAB) na Mahakama ya Rufaa za Kodi (Tax Revenue Appeals Tribunal-TRAT) zinafanya kazi kwa ufanisi ili kupunguza mlundikano wa mashauri; na

iv. kufanya tathmini ya misamaha yote ya kodi na kuiondoa isiyo na tija ili kuongeza mapato ya kodi yatakayoweza kutumika katika miradi ya maendeleo.

### *6.4.2. Sekta ya Elimu*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, bajeti ya sekta ya elimu inatarajiwa kuongezeka kutoka **shilingi trilioni 7.39** mwaka 2025/26 hadi **Shilingi trilioni 8.19** mwaka 2026/27 sawa na ongezeko la **asilimia 10.8**. Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonyesha dhamira ya kuwekeza zaidi katika sekta ya elimu kwa kutambua elimu kama nguzo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi mfano kutoa mikopo kwa elimu ya vyuo vya kati pamoja na kuanzisha na kutekeleza mtaala mpya wa elimu ya msingi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ongezeko hilo litatumika katika kutekeleza mtaala mpya wa elimu. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi kwenye

kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa kwa kuajiri walimu wa kutosha sambamba na kuboresha miundombinu ya kujifunza na kujifunzia.

### *6.4.3. Sekta ya Kilimo*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, bajeti ya sekta ya Kilimo inatarajiwa kuongezeka kutoka **shilingi trilioni 1.92** mwaka 2025/26 hadi **Shilingi trilioni 2.13** mwaka 2026/27 sawa na ongezeko la **asilimia 10.8.** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba ongezeko hilo litatumika kugharamia shughuli zifuatazo:-

i. kuimarisha utafiti wa kilimo ;
ii. kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji;
iii. kuimarisha huduma za ugani;
iv. ujenzi wa masoko na maghala ya uhifadhi wa chakula kufikia uwezo wa kuhifadhi tani milioni moja;
v. kufungua masoko mapya nje ya nchi kwa kufanya tathmini ya athari za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia;
vi. kuendelea kuwekeza katika mashamba makubwa na kuhamasisha vijana na wanawake kushiriki katika kilimo biashara; na
vii. kuwekeza katika viwanda vya ndani kuzalisha mbolea ili kuongeza matumizi na upatikanaji wa mbolea nchini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inataka Serikali kuhakikisha pindi bajeti itakapopitishwa fedha hizo zitolewe kama ilivyopangwa ili kutekeleza miradi na miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa.

### 6.4.4. Madeni ya Wakandarasi, Wazabuni na Watoa Huduma

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Serikali haikutambua ulipaji wa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma kama kihatarishi kinachoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti. Madeni hayo yanaathiri utekelezaji wa miradi kwa sababu fedha zinazotengwa mwaka husika hutumika kulipa madeni ya mwaka uliopita na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya mwaka huo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba katika kipindi cha miaka mitano (2019/20 - 2023/24) Wizara ya Fedha ilipokea madeni yenye thamani ya **Shilingi trilioni 6.87.** Kati ya kiasi hicho, madeni yaliyohakikiwa na kukidhi vigezo ni **Shilingi trilioni 3.70** na kiasi cha **Shilingi trilioni 3.16** hakikukidhi vigezo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kutowasilishwa kwa nyaraka za madeni au kuwasilisha nyaraka zikiwa na upungufu, nyaraka zisizo sahihi, baadhi ya madeni kuwa yameshalipwa na baadhi ya madeni kukosa kibali cha Afisa Masuuli, kukosekana kwa uthibitisho wa kupokelewa kwa huduma au bidhaa iliyosababisha uwepo wa deni husika, baadhi ya madeni kujirudia na uwepo wa makosa ya ukokotoaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Serikali yake inatenga kati ya **shilingi bilioni 700** hadi **trilioni 1** kila mwaka kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni, watoa huduma na wakandarasi. Hata hivyo,

Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. kuhakikisha kuwa Maafisa Masuuli wanazingatia maagizo ya Waraka namba 1 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa bajeti uliokuwa na maagizo ya namna ya kutolimbikiza madeni;

ii. Wizara ya Fedha kubainisha wazi utaratibu wa uhakiki na ulipaji wa madeni ya wakandarasi ili kuondoa malalamiko ya upendeleo katika kuhakiki na kulipa;

iii. Maafisa wa Serikali waliofanya matumizi bila kibali cha afisa masuuli wachukuliwe hatua za kinidhamu;

iv. kwa kuwa Serikali inatenga kati ya **Shilingi bilioni 700** hadi **trilioni 1** kila mwaka kulipa madeni, na kwa kuwa nchi bado inaweza kukopesheka, Kamati inaishauri Serikali kukopa kupitia hati fungani ya muda mrefu ili kulipa madeni na kiasi kinachotengwa kila mwaka cha kulipa madeni kitumike kulipa riba na mtaji wa hati fungani hiyo; na

v. Kwa kuwa baadhi ya madeni yanakosa viambatisho licha ya huduma kutolewa ni vyema kigezo cha uthibitisho wa huduma kutolewa kikatumika kama ushahidi ili kutowanyima haki wazabuni, watoa huduma na wakandarasi waliotekeleza shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaamini kwamba ushauri huu ukitekelezwa tutaondokana na changamoto ya malimbikizo ya madeni yanayoathiri utekelezaji wa Bajeti.

### *6.4.5. Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ilifanya uchambuzi wa maelekezo ya mwongozo kwa maafisa masuuli katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2026/27:-

#### 6.4.5.1. Mifumo ya Uwasilishaji wa Mpango wa Bajeti

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mifumo inayotumika kwa ajili ya kuandaa Bajeti ni *Central Budget Management System* (CBMS) kwa Serikali kuu na PlanRep kwa Serikali za Mitaa. Hivi sasa Mifumo hii haijaunganishwa na haibadilishani Taarifa na hivyo kulazimu baadhi ya nyaraka za maandalizi na utekelezaji wa Bajeti kufanywa nje ya mfumo kwa kutumia nyaraka ngumu. Kamati iliishauri Serikali kuwa na mfumo mmoja wa kibajeti kwa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za mitaa. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha maandalizi ya Bajeti ya Mwaka 2027/28 yanafanyika katika mfumo uliounganishwa ili kuondoa changamoto ya maandalizi ya bajeti kutumia nakala ngumu.

#### 6.4.5.2. Mifuko iliyolindwa *(Ring Fenced Funds)*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Maafisa Masuuli wanaosimamia mifuko yenye vyanzo maalumu kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Taifa wa Maji, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Mfuko wa Maendeleo ya Utalii wanaelekezwa kutenga **asilimia tano (5)** ya mapato ya mifuko husika kwa ajili ya utekelezaji

wa shughuli za kuendeleza miundombinu kwenye Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZs & EPZs) ili kuvutia uwekezaji na kuongeza fursa za ajira. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuachana na pendekezo hili hivi sasa kwa kuwa Mapato ya mifuko hiyo hayakidhi mahitaji ya msingi ya mifuko tajwa. Endapo maelekezo haya yatatekelezwa ni wazi kwamba kuna baadhi ya miradi inayotekelezwa na mifuko hiyo hivi sasa itaathirika.

**6.4.5.3. Kutenga Asilimia 5 ya Mapato Ghafi ya Halmashauri kwa ajili ya Uwekezaji kwenye Miradi ya Kuboresha Mazingira ya Biashara na Ujasiriamali**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mwongozo umetoa maelekezo ya kimkakati kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja **asilimia tano (5)** kati ya **asilimia 15** ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira kwa wanufaika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba maelekezo hayo yaliyobainishwa katika Mapendekezo ya Mwongozo yalikuwa na mkanganyiko. Mkangayiko huu ulikuwa katika maeneo yafuatayo;-

i. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 inatambua mgawanyo wa **asilimia 10** ya mapato ghafi kwa ajili ya mikopo kwa uwiano wa wanawake **asilimia 4,** vijana **asilimia 4** na watu wenye ulemavu **asilimia 2**, na si **asilimia 15** iliyopo kwenye Mwongozo;

ii. Kamati ilitaka kufahamu kama mapendekezo hayo yatalazimu marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali zaMitaa Sura 290; na

iii. **Asilimia 5** inayotakiwa kutengwa kwa baadhi ya Halmashauri zenye uwezo mdogo ni kiasi kidogo cha fedha ambacho hakitoshi kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia majadiliano baina ya Kamati na Serikali ilikubalika kwamba Maelekezo ya Mwongozo yalilenga Halmashauri zenye uwezo tu ndio zitatakiwa kutenga **asilimia 5** ya mapato ghafi na sio kama inavyosomeka hivi sasa. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa uchambuzi wa Halmashauri ambazo zitapaswa kufuata maelekezo hayo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kufuta na kuandika upya sehemu hiyo ili kuondoa mkanganyiko katika utekelezaji. Vilevile, ili maelekezo hayo yaweze kutekelezwa kikamilifu ni vyema Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 ifanyiwe maboresho kupitia Muswada wa Sheri ya Fedha ya mwaka 2026. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia *Self Microfinance* ambayo ni Taasisi ya serikali katika utoaji wa mikopo ya **asilimia 10** ili kuondokana na gharama ambayo inaweza kujitokeza kwa kutumia Taasisi za fedha kama benki za biashara.

### *6.4.5.4. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali imeweka mikakati ya kuibua, kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa kupitia ushirikishaji katika kuwawezesha watanzania (Local Content) kwa kusaidia upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu ili itumike katika fursa zilizopo za kiuchumi kwa lengo la kutoa ajira hasa kwa vijana.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (National Economic Empowernment Council -NEEC) halina nguvu ya kisheria ya kuratibu shughuli zote za uwezeshaji zilizotawanyika katika maeneo mbalimbali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. kutunga Sheria Mpya ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo italipa Baraza mamlaka ya kusimamia mikakati yote ya uwezeshaji Wananchi kiuchumi nchini; na

ii. Sheria hiyo ijumuishe afua zote zenye lengo la kuwawezesha watanzania kiuchumi zilizotawanyika katika Sheria, mipango na mikakati mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha rasilimali fedha

zilizotawanyika zinaunganishwa na hivyo kuleta matokeo yanayotarajiwa, yanayopimika pamoja na kuleta ustawi kwa walengwa.

## SEHEMU YA SABA

## 7.0. MAONI YA UJUMLA

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na maoni mahsusi yaliyotolewa na Kamati katika kila eneo, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo:-

### 7.1. Upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi pamoja na makazi ya bei nafuu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kuna msemo wa kiswahili unasema ***"Ardhi ndio Mama wa Mali"*** msemo huu unamaanisha ardhi ndio msingi mkuu wa maendeleo. Shughuli za kiuchumi kama vile uzalishaji mali, ujenzi wa miundombinu ya msingi, kilimo, madini, utalii, tehama na biashara zote zinafanyika ardhini. Hata, hivyo pamoja na umuhimu wa sekta ya ardhi nchini bado Serikali haijaipa rasilimali hii umuhimu unaostahili. Sekta hii imekuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile: ucheleweshaji wa upatikanaji wa hati miliki, migogoro ya ardhi, kipande kimoja cha ardhi kugawiwa kwa watu zaidi ya mmoja, wawekezaji kutopata ardhi iliyopimwa na ina hati miliki, wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi pamoja na ardhi ya vijiji kutopimwa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ili Wizara ya Ardhi iweze kupanga, kupima na kumilikisha ardhi zinahitajika jumla ya **Shilingi trilioni 2.958** sawa na wastani wa **shilingi bilioni 591.7** kila mwaka. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha 2026/27 inatengwa si chini ya **shilingi bilioni 250** kwa kuanzia ili mipango ya Serikali katika sekta hii iweze kutekelezeka. Hatua hii itasaidia pia kufikia lengo la mpango la kuwa na miji iliyopangwa na inayovutia. Bila kutenga kiasi hicho cha fedha ni wazi kwamba karibia malengo yote ya mpango ya maendeleo yanayohusu miundombinu,

mazingira, kilimo, utalii, madini na kuvutia wawekezaji itakuwa vigumu kufikiwa.

### 7.2. Kutunga Sheria itakayosimamia Utekelezaji wa Mpango

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na mambo mengine ibara hii inalitaka Bunge kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango. Lengo la Sheria hiyo ni kuweka masharti yatakayowezesha Bunge kuhakikisha Serikali inatekeleza shughuli zilizopangwa na kuidhinishwa katika mpango. Hivi sasa hakuna sheria moja inayoongoza usimamizi na utekelezaji wa mipango isipokuwa masharti yametawanyika katika sheria mbalimbali. Kwa kuwa, Bunge hivi sasa linatoa mapendekezo yake kuhusu Mpango elekezi wa muda mrefu wa Miaka 25 ni vyema Serikali ikawasilisha mapema iwezekanavyo Sheria ya kutekeleza mpango ambayo itawalazimu viongozi wajao kuhakikisha kwamba haianzishwi miradi mipya ambayo haipo kwenye Mipango. Mfano wa nchi zenye sheria hizo ni pamoja na Mongolia na China.

### 7.3. Ahadi za Viongozi wa Kitaifa na Utekelezaji wa Mpango

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kumekuwa na changamoto ya utekelezaji wa ahadi za viongozi zinazohusu miradi ya maendeleo kwa wananchi wanazozitoa pindi wanapofanya ziara katika maeneo mbalimbali. Hivi sasa ahadi za viongozi hukusanywa kwa mfumo wa *Dash Board* ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na baadae hupelekwa katika fungu husika ili zipangiwe Bajeti katika mwaka unaofuata. Utaratibu huu haupo kisheria wala kikanuni. Hatua hii ndio imekuwa chanzo cha ahadi za viongozi wakuu wa kitaifa kutotekelezwa kikamilifu. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wakati tunasubiri sheria ya utekelezaji wa mipango itakayozingatia ahadi za viongozi, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2026/27 kutoa maelekezo kwa Maafisa masuuli kutenga Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi za viongozi wa kitaifa.

### 7.4. Kuwa na Vipaumbele Vichache

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, moja ya changamoto iliyoathiri utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano ni wingi wa vipaumbele. Changamoto hiyo ilisababisha uanzishwaji wa miradi ambayo haikukamilika kwa wakati na mingine kutotekelezwa. Aidha, kutokana na wingi wa vipaumbele na kufuatia kwa ufinyu wa rasilimali fedha, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwanza kwa miradi ambayo ina matokeo makubwa ya kiuchumi na itakayochochea utekelezaji wa miradi mingine.

### 7.5. Uandaaji wa Takwimu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya utofauti wa takwimu zinazowasilishwa na Taasisi za Serikali kuhusu jambo linalofanana. Pamoja na kwamba Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imepewa nguvu ya kisheria ya kukusanya na kuchakata takwimu, bado kuna changamoto ya baadhi ya Taasisi za Serikali kutowasilisha Takwimu za kiutawala (administrative data) kwa wakati. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutoa maelekezo kupitia mwongozo wa maandalizi ya Bajeti ya Muda wa Kati yatakayowataka maafisa masuuli kuhakikisha wanatenga bajeti ya kuanda na kuwasilisha takwimu sahihi na kuwasilisha kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

### 7.6. Utoroshaji wa Mapato kwa njia Haramu (Illicit Financial Flows - IFFs)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa mujibu wa ripoti za *Trade Misinvoicing in Developing Countries* (2021) inayoandaliwa na *Global Financial Integrity* inaonyesha kwamba Tanzania inapoteza takribani **Dola za Marekani bilioni 1.83** katika sekta ya madini na gesi. Upotevu huo unatokana na uhamishaji wa mapato kwa njia haramu kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile umiliki usio wazi *(beneficial ownership)*, bei ya uhamisho *(transfer pricing)* na kutumia bei zisizo za soko *(mis-invoicing)* kwa lengo la kuhamisha mapato nje ya nchi. Ili kuzuia uhamishaji haramu wa mapato, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. kuimarisha matumizi ya mifumo na teknolojia ya kidigitali ili kufuatilia na kudhibiti udanganyifu wenye lengo la kuhamisha mapato;

ii. kuimarisha usimamizi wa mikataba ya utozaji wa kodi mara mbili *(Double Taxation Agreement)* ili kudhibiti mianya inayoweza kutumika kutorosha mapato;

iii. kuimarisha sheria za kodi za ndani kwa kuondoa mianya inayoweza kutumika kutorosha au kuhamisha mapato; na

iv. kuimarisha ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Tume ya Madini (TCM) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), ili kukabiliana na vitendo vya ukwepaji kodi vinavyofanywa na makampuni katika sekta hizo.

**7.7. Miradi ya Kielelezo**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kamati inatambua Serikali imehama kutoka kupanga mipango kwa kuangalia miradi na kwenda kwenye kupanga Mipango kwa kuangalia programu**.** Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa miaka 25 na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano imeainisha programu na afua mbalimbali zitakazotekelezwa katika kipindi husika. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2026/27 umebainisha afua mbalimbali zitakazotelezwa bila kuanisha miradi itakayotekelezwa chini ya afua hizo. Hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali kuainisha ni miradi ipi itakayotekelezwa kwa kila programu na afua kwa mwaka 2026/27 ili Bunge liweze kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wake.

**7.8. Vihatarishi vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kihatarishi ni jambo linaloweza kujitokeza na endapo litajitokeza litasababisha madhara. Kamati imechambua vihatarishi vya kiutawala ambavyo ni ukosefu wa nidhamu katika

utekelezaji wa miradi; mifumo dhaifu ya ufuatiliaji, udhibiti na uwajibikaji; uhaba wa rasilimali watu wenye ujuzi na ustadi unaohitajika na mapungufu katika utawala bora.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa tafsiri ya vihatarishi, vihatarishi vilivyoorodheshwa chini ya kihatarishi cha utawala havikidhi vigezo vya kuwa vihatarishi bali ni changamoto ambazo zipo na zinaendelea kuathiri utekelezaji wa shughuli za Serikali. Hivyo, Kamati inashauri kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo badala ya kuendelea kuzitambua kama kihatarishi.

**7.9. Serikali kutoa Dhamana kwa Benki za Maendeleo ili ziweze Kukopa Katika Vyanzo vya Nje**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Benki za Maendeleo Duniani huwa zina jukumu la kutoa mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, kwa kuwa mikopo yake ni ya muda mrefu zinakabiliwa na vihatarishi zaidi ya Benki za biashara zinazotoa mikopo ya muda mfupi na kwa riba ya juu. Tanzania ina Benki mbili za maendeleo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ambazo zinamilikiwa na Serikali kwa **asilimia 100**. Hivi sasa Benki hizi zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mtaji. Aidha, Mtaji wa Benki za Maendeleo nchini hivi sasa ni **asilimia 0.14** ya pato la Taifa na Mpango wa miaka mitano umeweka lengo la kufikia walau **asilimia 1.25** ifikapo mwaka 2030/31.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa kuwa Serikali haijaweza kuziwezesha kimtaji Benki hizi hasa Benki ya TIB, Kamati inaishauri Serikali kutumia Kifungu cha 13A cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali Sura 134 ili kutoa dhamana kwa Benki za uwekezaji kukopa kwenye vyanzo nafuu nje ya nchi. Hatua hii itasaidia kukuza mtaji na kuchagiza utekelezaji wa mipango ya maendeleo kupitia Sekta Binafsi. Hata hivyo, endapo Benki hizi zitapewa dhamana ni lazima Serikali iwe na usimamizi wa karibu ili kuhakikisha mtaji uliopatikana unakuwa endelevu na mikopo inatolewa kwa kuzingatia vigezo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha benki za TADB na TIB pamoja na kampuni ya Taifa ya fedha za

maendeleo (TDFL) ili kuwa na benki moja kubwa ya maendeleo itakayotoa mikopo kwa sekta mbalimbali nchini.

### 7.10. Utaratibu wa utoaji wa misamaha ya kodi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa mujibu wa Kifungu cha 130(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kikisomwa pamoja na Kifungu cha 61 cha Sheria ya Bajeti vinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutoa msamaha wa kodi ya ushuru wa bidhaa kwa mtu yeyote anapoona inafaa kwa maslahi ya umma. Pamoja na nia njema ya vifungu hivi, ni vyema vikafanyiwa maboresho ili kuweka sharti litakalomlazimu Waziri wa mwenye dhamana na masuala ya Fedha kufanya mashauriano na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato ili kubaini kama misamaha yote inayopendekezwa kutolewa ina manufaa kwa umma. Marekebisho hayo yana nia ya kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija pamoja na kuongeza wigo wa mapato kwa Serikali.

### 7.11. Ufuatiliaji na Tathmini

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kutekeleza Mpango elekezi kutakuwa na mapitio mawili, moja ni mapitio ya muda wa kati ya miaka 10 ili kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Mpango na mapitio ya mwisho (miaka 25) ambayo yanalenga kuweka msingi wa maandalizi ya Mpango utakaofuata. Hata hivyo, Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Serikali una changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. hadi hivi sasa hakuna Sera wala Sheria inayosimamia masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini na badala yake unatumika Mwongozo;

ii. utengaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathminiumeendelea kuwa mdogo;

iii. utofauti kati ya utolewaji wa fedha na utekelezaji wa miradi;

iv. baadhi ya miradi inayotekelezwa kutokuwepo kwenye Mpango;

v. Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali kutoshirikiana wakati wa kufanya Ufuatiliaji na Tathmini;

vi. Tume ya Mipango hivi sasa kutokuwa na nguvu ya kuwawajibisha maafisa masuuli au wakuu wa Taasisi wanaoshindwa kufanya ufuatiliaji na tathmini na kutoa Taarifa; na

vii. Muingiliano wa Majukumu ya Tathmini na Ufuatiliaji baina ya Viongozi na Wataalamu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i. Tume ya Mipango kuhakikisha maandiko yote ya miradi yanabainisha namna Ufutialiaji na Tathmini utakavyofanyika kabla ya kuidhinishwa;

ii. kuhakikisha wakati wote hatua stahiki na za haraka zinachukuliwa dhidi ya mapungufu yanayobainishwa wakati wa Ufanyaji waTathmini na Ufuatiliaji;

iii. kushirikisha jamii katika kupanga, kusimamia na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

iv. kufungamanisha mfumo wa bajeti na ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha fedha zinazotolewa zinaendana na hatua ya utekelezaji.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo kushika wadhifa huo. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Daniel Baran Sillo, (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia nyote kila lililo jema katika utekelezaji wa majukumu yenu mapya. Niwahakikishie kwamba miongozo yenu mnayoipatia Kamati ya Bajeti itakuwa nyenzo kuu katika utekelezaji wa majukumu yetu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu Waziri wa Fedha Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb) na Mhe. Laurent Deogratius Luswetula (Mb) pamoja na Dkt. Pius Chaya Naibu Waziri Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili Mipango na Mwongozo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pia niwashukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Dkt. Fred Msemwa, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango. Vilevile, niwashukuru Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi**.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa upendo wa dhati napenda kumshukuru Mhe. Ali Hassan King, (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kunisaidia wakati wote wa shughuli za Kamati. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri wao katika kuchambua Mipango na Mwongozo iliyowasilishwa. Aidha, niwashukuru wajumbe wote wa Kamati kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati. Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Stella Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Enock Zadock Koola, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Bal.Dkt. Pindi Azara Chana, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mwisho ila si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.**

Mashimba Mashauri Ndaki (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
02 Februari, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa taarifa hiyo ya Kamati.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linarudia.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuwashukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa taarifa yetu ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru Kamati ya Bajeti kupitia Mwenyekiti wao Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki kwa taarifa nzuri ambayo ninaamini Waheshimiwa Wabunge mmezipata na zipo kwenye vishikwambi vyetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana kuchangia katika taarifa hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Wale ambao hawatapata fursa ya kuchangia moja kwa moja mnaweza kuchangia kwa mujibu wa Kanuni yetu kupitia vishikwambi. Kama mtapata changamoto katika kuchangia, basi mnaweza kuwaomba watu wa *IT* ili waweze kuwawekea sawa na wote mpate fursa ya kuchangia mpango wa Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaanza uchangiaji kwa Wabunge jioni, nitawataja Wabunge watano watakaoanza jioni. Ataanza Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninawatakia mchana mwema, ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni. *(Makofi)*

*(Saa 7.31 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Mipango

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027;**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/2027 – 2028/2029.**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo imetangazwa asubuhi, tunaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuwa mzungumzaji wa kwanza kwenye hoja iliyopo Mezani. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima wa kuwa mahali hapa. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kikubwa na kuwa Rais na hatimaye kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi hiki cha 2025/2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niwapongeze pia Mawaziri, waliowasilisha hoja zilizopo mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa kuanzia na Mheshimiwa Prof. Alexander Mkumbo, ambaye ni Waziri katika Ofisi ya Rais akisimamia eneo la Mipango na Uwekezaji; na Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, ambaye ni Waziri wa Fedha kwa mawasilisho yao ambayo wameyatoa mbele ya Bunge letu Tukufu na sisi sasa tunao wajibu wa kutoa mapendekezo yetu, namna bora ambavyo mipango hii takribani yote mitatu itakwenda kuongeza tija katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa wakati anafungua Bunge hili, alieleza bayana kwamba anatamani itakapofika mwaka 2030 nchi yetu iwe katika kipato cha juu cha kati. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba zipo sekta ambazo zimetajwa katika mpango ni lazima tuzipe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaziona sekta mbili ambazo ningependa nitoe mchango wangu. Sekta ya kwanza ni sekta ya kilimo, ambayo kwa sasa inachangia zaidi ya takribani 26% katika pato la Taifa. Sekta nyingine ni sekta ya madini ambayo sasa imefikia wastani wa 10.1% kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini haya mapendekezo tunayoyatoa yakienda kufanyiwa kazi baada ya kipindi kifupi kufika hiyo 2030 tunaweza tukafikia hicho kiwango cha kati cha juu cha uchumi kama ambavyo ninakwenda kueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza kwenye kilimo bado nina imani kwamba 65% ya Watanzania wamejiajiri katika kilimo; na

hawa ni wale ambao shughuli yao akiamka asubuhi, akishinda mchana, akilala jioni anawaza kilimo. Ukiacha zile kama 15% hivi za wengine ambao wanajishughulisha na kilimo na shughuli nyingine kufikia 80% au 65% ndio wanabeba jukumu la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, katika viwanda malighafi zinazotokana na mazao mbalimbali ni zaidi ya 65% kwenye uzalishaji wa viwanda. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, sisi tukitaka tuwe na uchumi mkubwa na uchumi shirikishi, ni lazima tuingize fedha nyingi katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka kusema bado hatujakuwa na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba pamoja na miradi ya umwagiliaji ambayo inaendelea kujengwa kote nchini, lakini bado tupo nyuma sana. Kwa hiyo, ni vyema tukapiga hatua za haraka ili tuweze kufikia haya malengo ambayo ninayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, tunazo takribani hekta milioni 44 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini ninavyozungumza sasa tunazo hekta 500 na mpango wetu ni kwamba ikifika 2030 tufike hekta 1,200; kwa hiyo, utaona bado tupo nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi zaidi ya 146 ya umwagiliaji ambayo inatekelezwa kote nchini. Miradi 428 imefanyiwa usanifu. Ningependa kuona kwamba hapa juhudi kubwa inaongezwa ili miradi hii ikikamilika wananchi wengi wawe wamejiajiri katika sekta ya kilimo. Tayari tuna *geographical advantage* kwamba sisi tunauza zaidi katika Ukanda wa *SADC* na ukanda wa Afrika Mashariki mpaka Afrika ya Kati. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo tulitumie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji amesema tuna tija ndogo kwenye kilimo. Kwa hiyo, ni lazima tuongeze chachu ya kuongeza tija katika kilimo. Mapinduzi ya viwanda yaliyotokea katika karne ya 19 kwenye Bara la Ulaya yalitokana kwanza na mapinduzi ya kilimo. Ni lazima tuanze na mapinduzi katika kilimo. Tija itaongezeka, pia malighafi zitapatikana

na kwenda kuchechemua kasi, ambayo amesema; kasi ndogo ya ukuaji wa viwanda, itakwenda kuwa kasi kubwa tu endapo tutakuwa na malighafi za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tija tunazopaswa kuongeza ni pamoja na kuokoa mazao yanayoharibika kabla ya kwenda kwenye masoko, na kuongeza miundombinu wezeshi katika maeneo ya mashambani ili mazao yaweze kutoka mashambani na kwenda katika maeneo ya viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yetu inapaswa kuwa jumuishi, himilivu na shindani. Ninapenda kusema, dhima na malengo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa umeweka vipaumbele, lakini kwa masikitiko makubwa Profesa ameweka kipaumbele namba 10 kuweka msukumo katika maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hii ndiyo ingekuwa kipaumbele namba moja. Tutakapoweka msukumo wa maendeleo vijijini, maana yake kule ndiko uzalishaji ulipo na ndiko ajira za Watanzania wengi zitapatikana, na hili tatizo la ukosefu wa ajira pia tunaweza tukapata majawabu yake kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kutoa mchango ni kwenye sekta ya madini. Sekta hii ya madini pamoja na kwamba tuna madini mengi, lakini bado Taifa letu hatujaweza kujitambulisha vizuri kwamba sisi tumejikita katika eneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika madini, tunayo madini ya kipekee kabisa ya *Tanzanite*, ambayo dunia nzima yapo Tanzania peke yake, lakini hayajatutangaza vyema na kuona kwamba sisi ni watu wa namna gani? Bado tuna *reserve* kubwa sana ya dhahabu, ambapo inasadikika kuwa tuna zaidi ya tani 1,600 za dhahabu. Tunayo madini ya aina mbalimbali mengi. Shida kubwa ipo kwenye *data*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini yetu tunayo, lakini hatuna *data* za uhakika. Niombe sana kwenye mpango huu tuhakikishe kwamba tunaiwezesha *GST* ili iweze kufanya utafiti wa kijiolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi yenye miamba ambayo yanasadikika kuwa na madini ni 16% peke yake ambayo yameshafanyiwa utafiti. Zaidi ya 84% hayajafanyiwa utafiti. Kwa hiyo, inawezekana hata hapa ndani ya Bunge kuna madini, hatujui. Kwa hiyo, ni vyema tukaongeza nguvu katika eneo hili la utafiti wa kijiolojia ili tuwe na *data* za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana ya kuwa na *data*? Tunapokuwa na *data* tunajijengea uwezo hata wa kujenga ushawishi wakati tunaingia mikataba. Sasa hivi sehemu kubwa ya mikataba yetu inategemea zaidi aidha wachimbaji wadogo au wachimbaji wakubwa ambao wamekuja na wamefanya utafiti wenyewe. Tutakapokuwa na *data* za kwetu wenyewe ni rahisi hata wawekezaji kutoka nje wakija tunazitumia *data* kama sehemu mojawapo ya kuanza kufanya *proper bargaining*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunashindwa kufanya *bargaining* ya kueleweka kwa sababu hatuna uhakika na kilichopo ardhini. Sambamba na hilo, kwenye madini huku ni vyema sana tukatengeneza dira ya madini angalau ya miaka 10 au 15; kwamba tunataka madini yetu yawe namna gani? Pia tuweke malengo, na malengo haya yawe yanapimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amesema kwenye hotuba yake, kwamba angetamani kuona kwamba siku madini haya yatakapokwisha, basi vizazi vitakavyokuja baadaye tuwaonyeshe kwamba tuliwahi kuwa na madini na rasilimali hizi hapa ama tuwaonyeshe miradi ya kielelezo ambayo imetokana na rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu tukatengeneza dira ya madini ya kati ya miaka 15 mpaka 25 yenye malengo yanayopimika ambayo yanaelekeza tunataka nini? Tunaweka vigezo.

Ni vigezo gani tutavifikia hapo na sekta zipi tunazipanga kuziinua kupitia pato linalotokana na madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Amour Seif Abdalla. Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge, ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie mpango uliopo mbele yetu leo. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazoendelea kufanya kwa Taifa letu. Pia niwapongeze Mawaziri wa wizara zetu mbili ambao wameleta mpango hapa ili tuweze kushauri na kujadili kwa kina juu ya mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme mambo kama matatu au mawili hivi. Tumeona kwenye mpango uliowasilishwa kwetu hapa asubuhi, pato la mwananchi mmoja mmoja kwa mwaka katika mwaka 2024/2025 ni dola za Kimarekani 1,277; lakini pia *GDP* yetu kwa 2024/2025 inasadikika kuwa Dola za Kimarekani bilioni 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika mpango ambao umeelezwa hapa, mpango wa nne ambao utaisha mwaka 2030/2031 inasadikika yaweza kuwa pato la mwananchi mmoja mmoja kufika dola za Kimarekani 1,638 na *GDP* kufikia dola za Kimarekani bilioni 118.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma Dira ya Taifa ambayo itakwenda mpaka 2050/2051 *GDP* inasadikika kuwa dola za Kimarekani trilioni moja na pato la mwananchi mmoja mmoja ifikapo 2050/2051 iwe dola za Kimarekani 7,000. Leo tuna 1,277; tunafikaje 2030/2031 dola za Kimarekani za pato la mwananchi mmoja mmoja kuwa 1,638 na 2050/2051 pato la mwananchi mmoja mmoja dola za Kimarekani 7,000? Tunafikaje hapa? Ni lazima kuanzia leo tuanze kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji. Tunazo sekta za uzalishaji mfano, sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima leo tukubaliane hapa kwamba kilimo ni biashara na mkulima ni mwekezaji. Ni lazima tuwachukulie wakulima kama wawekezaji kwenye nchi yetu ili tuweze kupandisha pato la mwananchi mmoja mmoja. Tunajua wazi kuwa Watanzania takribani 80% ni wakulima; lakini kati ya hao wakulima 80%, 65% ni wakulima ambao hawana ofisi. Yaani anatoka nyumbani anaenda kulima; akitoka kulima anarudi nyumbani kwake, ndiyo amemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ni lazima tumwezeshe huyu mwananchi wa kipato cha chini cha leo ambacho ni dola za Kimarekani 1,277 kwa mwaka afikie dola za Kimarekani 1,638 mwaka 2030 au dola za Kimarekani 7,000 mwaka 2050/2051. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tukiwekeza katika kilimo cha umwagiliaji tutatoboa. Mwananchi mmoja mmoja tukiwekeza katika kilimo cha umwagiliaji, kwa sababu ni lazima tukubaliane sote, sisi wakati tunalima kule enzi za zamani mbolea wala haikuwa kipaumbele; pembejeo siyo kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini mwananchi akilima yakiwepo maji enzi hizo, mwananchi atapata. Kwa hiyo, ni kitu ambacho hakipingani. Ili tulime, cha kwanza, tunategemea maji. Sasa maji tunayapataje? Ni lazima tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanatamani kuvuna hata mara mbili kwa mwaka, lakini watavunaje mara mbili kwa mwaka kama wanategemea mvua? Haitawezekana. Ili wavune mara mbili kwa mwaka au mara tatu ni lazima tuwe na kilimo cha umwagiliaji. Tutengeneze mabwawa kwenye maeneo yetu, ikiwepo Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo *potential* kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Ukienda kule kata za Lutubiga, Shigala, na Lamadi utakuta maeneo mazuri kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, ni lazima tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji. Tukiwekeza mahali hapa, kwanza tutakuwa tumemsaidia mwananchi katika

kipato chake, mwananchi mmoja mmoja kutoka hizi dola za Kimarekani 1,277 kufika huko tunapotaka leo kwenye dola 1,638. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi akiwa na uhakika na maji atalima na atapata kipato, na tutapandisha kipato katika mazao ambayo tutakuwa tumetarajia. Nchi kama nchi, leo tumeona tumeambiwa hapa na Mheshimiwa Shangazi, kilimo kinachangia takribani 26%. Tukiwekeza katika eneo hili, ifikapo 2030 tunaweza kuwa tumefika kwenye 40% hata 50% kwa sababu sehemu mojawapo tuliyo na uhakika na ajira ni eneo la kilimo pamoja na eneo la viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni tukawekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji ili wananchi wetu waweze kunufaika na kilimo ambacho leo wanataabika na upatikanaji wa maji kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tunatambua wazi kwamba ili tumsaidie mwananchi huyu ni lazima pia makato yanayojitokeza kwenye kilimo tuyapunguze. Wakati mwingine mwananchi analima kwa tabu, wakati mwingine hatuendi kumsaidia wakati wa kulima, lakini wakati wa kuvuna anapokwenda kuuza tunakuwa na makato mengi, ambapo hatumsaidii mwananchi anayetegemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa sasa ifike sehemu Mheshimiwa Waziri, hasa Waziri wa Kilimo aliangalie sana hili, ili tumsaidie mwananchi tumpunguzie makato ambayo hayana tija. Nitoe mfano mmoja, sisi Mkoa wa Simiyu ni wakulima wa pamba. Ukilima pamba unapata pembejeo. Unapewa pembejeo kwa mkopo ambapo utakuja ulipe wakati wa kuuza pamba yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na hilo. Mimi sina tatizo, lakini wananchi hawa wanakatwa shilingi 300 kwa kilo ya pamba unapoenda kuuza kugharamia pembejeo bila kufuata ni kiasi gani mwananchi huyu alichukua pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani mwananchi alipe kulingana na kile alichokopa na kulingana na kile alichopewa. Kama mwananchi amepewa pembejeo; tuchukulie pembejeo kilo 100 akazalisha pamba kilo 10,000 na mwingine hapa amepewa pembejeo kilo 100 akazalisha pamba kilo 1,000 kuna tofauti kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wamechukua pembejeo kilo 100, lakini uzalishaji huu unatofautiana kulingana na vile ambavyo wewe umetunza eneo lako na ulivyotunza kilimo chako, lakini mwisho wa siku katika kurudisha ule mkopo unalipa kulingana na vile alivyozalisha shilingi 300/= kwa kilo bila kujali ni kiasi gani ulikopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningetamani mtu aliyekopa kilo 100 akatwe kulingana na kilo 100 alizokopa na wala siyo kukata *lumpsum* ambapo tunawanyonya wananchi wadogo wadogo ambao wanategemea kilimo, na leo tunataka wafike kwenye pato la mwananchi kwa mwaka 2030/2031, 1,638 *US Dollars.* Hawatafika kama tutakuwa tunawalimbikizia makato makubwa kiasi hiki ambayo wao yatawakatisha tamaa kwenye suala zima la kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani kuishauri Serikali iliangalie hili. Kwenye ushuru huko kuna kitu kinaitwa *Pay As You Earn.* Sasa ninatamani na huku kwenye zao la pamba na lenyewe kuwepo na kitu kinaitwa *Pay As You Use,* yaani ulichotumia ndicho ambacho urudishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tuna haja ya kuliangalia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimeona kwenye Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti, Waziri wa Fedha amesema hapa kwamba wale Maafisa Masuuli wanaosimamia mifuko maalumu, waweze kutenga asilimia tano kwa ajili ya kupeleka kwenye uzalishaji wa kiuchumi kwenye maeneo mengine. Mimi la kwenye uchumi huko sina tatizo, tatizo langu ni kutenga asilimia tano kwenye mifuko mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tu hapa kwamba tunayo mifuko ya maji, tuna mfuko wa barabara, tuna mfuko wa *TRC*, tuna Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; yakikatwa asilimia tano, tunadidimiza sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Watanzania walio wengi bado wana shida ya maji, leo Watanzania walio wengi bado wana shida ya barabara. Tumeweka vyanzo kwa ajili ya ku-*boost* barabara, kwa ajili ya ku-*boost* maji, kwa ajili ya ku-*boost* maendeleo ya mawasiliano kwa wote...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tena tunakuja na mpango tukate asilimia tano ili tupeleke kwingine wakati huku bado hatujamaliza. Hili siungi mkono, ninaunga mkono maelezo ya Kamati kwamba tuachane na hii habari, hizi fedha ambazo tumetenga kwa ajili ya mifuko, tuiache kama ilivyo, tupeleke kwa wananchi. twende tukatekeleze miradi ya maji, miradi ya barabara na miradi mingine. Wakandarasi bado hawajalipwa, leo tunataka tukate tena! Haiwezekani. Mimi kwa hili siungi mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge, Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, ajiandae.

Mheshimiwa Patrick Mwalunenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel, ajiandae.

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu wa 2050, 2026 - 2031, na 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi alioupata. Kwa kuwa hii ni mara ya kwanza kusimama hapa, niseme wazi kwamba, katika Uchaguzi Mkuu, hizi kura alizitafuta yeye mwenyewe baada ya kutekeleza miradi mikubwa ambayo iliachwa na mtangulizi wake. Mfano, mradi wa umeme, mradi wa *SGR* na Kigongo - Busisi, barabara na miradi mingi ya maji aliitekeleza katika kipindi chake. Kwa hiyo, ushindi alioupata alistahili. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupewa dhamana na kuaminiwa kuwa Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nimpongeze Mheshimiwa Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Naibu Spika kwa kutuongoza vyema. Vilevile, niwapongeze Wabunge wenzangu wote waliochaguliwa katika kipindi hiki 2025/2030 kuja kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Prof. Kitila kwa wasilisho zuri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwenye Wizara hiyo. Pia, nimpongeze Waziri wa Fedha kwa wasilisho lake, Naibu Waziri na Watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliposikiliza huu mpango wa nchi, ukiufuatilia, na pia Waziri wa Fedha alivyowasilisha, kiukweli unaona kuna mwanga mkubwa sana kwa Watanzania na unaona ni Serikali imedhamiria kutatua changamoto za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina maoni, na hasa ninajikita kwenye sekta za uzalishaji. Wameongea wenzangu; ameongea Mheshimiwa Shangazi na mwenzangu aliyepita hapa na mimi nitapita mlemle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 75% au 80% ya watu wetu, wako kwenye kilimo, lakini tumekubaliana na mpango wa Wizara ya Kilimo kwamba 2030 kilimo kichangie 10% ya *GDP* ya nchi yetu. Hatuwezi kufika huko kama hatuna *commitment*. Mashaka yangu makubwa yapo kwenye utekelezaji wa mpango wenyewe, na Waziri wa Mipango ameongea kwamba kuandika mpango kwenye karatasi ni jambo moja, lakini kutekeleza mpango wenyewe ni jambo lingine. Hapo ndio kwenye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa la rasilimali watu. Nilidhani mpango huu pamoja na mambo yote mazuri yaliyoongelewa, lakini tungejikita pia kuangalia mpango huu unaendaje sambamba na kutengeneza rasilimali watu? Hilo ndilo tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapanga hivi, lakini watu wanaotekeleza huko chini *especially* kwenye halmashauri zetu unakuta wanakuwa na matatizo makubwa sana, na huwa mara nyingi wanakuwa kama miungu watu na hawana zile fikra za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuangalia huu mpango kwa 100% ni kama biashara, na nina-*declare interest,* mimi ni mfanyabiashara. Mfanyabiashara kwanza anaulinda mtaji, anapunguza matumizi, lakini pia mfanyabiashara anataka kuona matokeo, na biashara yake ikue, na ukiuangalia huu mpango, malengo yake ni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitajikita zaidi kwenye kilimo. Sekta ya Kilimo ndiyo imeajiri watu wengi sana kwenye nchi yetu na ndiyo inaweza ikaleta jawabu la matatizo ya ajira kwenye nchi yetu kama tukijipanga sawasawa. Kwa nini, ninasema hivyo? Tunayo sisi mazao ya kimkakati. Tunalo zao la pamba, tunalo zao la korosho, tunayo kahawa, tunayo chai, tunayo kokoa na pia tunayo mazao ambayo yanaitwa *cereals* (alizeti, ufuta na mazao mengine) na yote haya yameundiwa bodi zake za zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia namna zile bodi zinavyofanya kazi, utaona kabisa kwamba mpango unasema hivi lakini ile dhamira ya dhati haipo, kwa sababu zile bodi zinasuasua, hazijatengewa bajeti ya kutosha ili ziweze kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unaona Bodi ya Pamba kwa miaka mitano mfululizo wanahangaika ili waweze kufikia angalau tani 500,000 za uzalishaji. Pamba hiyo ukiangalia watu wa huko kanda ya ziwa ni zaidi ya watu 15,000,000 wanategemea zao lile, lakini uzalishaji kila siku unasuasua. Kwa sababu gani? Bodi ya Pamba maana yake na sekta zima haina mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa takwimu, mimi siyo mtaalamu wa takwimu, lakini watu wa fedha watatusaidia, *percentage* ya dola zinazokwenda nje kwa ajili ya kuagiza nguo ni fedha nyingi sana zinakwenda China na Uturuki, lakini sisi tunalima pamba hapa. Ili kiwanda cha pamba kiweze kuanzishwa hapa, na kuzalisha kuanzia nyuzi mpaka nguo, angalau tuweze kuzalisha tani 1,000,000; lakini leo hii hatujawahi kufikisha tani 1,000,000 hata tani 500,000 hatujafikisha. Sasa utaona ni jinsi gani tunavyopishana. Mpango unasema hivi, lakini na kwenye utekelezaji ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maoni yangu hapo, mpango na Wizara ya Fedha tuziwezeshe hizi bodi za mazao kwa kuzipa mitaji. Ninafurahi na ninaipongeza pia Kamati. *Commitment* yao kwamba lazima hawa Wakurugenzi wa Taasisi na Wakurugenzi wa Halmashauri wawe wanashindanishwa ili waweze kupatikana; maana yake ni nini? Kama ni Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba au Bodi ya Pareto au Bodi ya Chai ameshindanishwa kibiashara na amepewa mtaji. Maana yake lazima atazalisha kwa faida, na mwisho wa siku tutapata viwanda vya kuzalisha nguo hapa kuanzia nyuzi mpaka nguo, *final product*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kimoja cha nguo kikitengenezwa kinaweza kulisha watu wasiopungua 3,000. Sasa tukiwa na viwanda 10, maana yake uzalishaji utakuwa mkubwa lakini na watu wetu watapata ajira za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa makusudi kupitia Wizara ya Kilimo waliwekeza kupeleka pembejeo kwenye zao la korosho na tija imeonekana. Uzalishaji umetoka tani 200,000, 150,000 ikawa inasuasua mpaka tani 500,000 na pesa zilizoenda kwa wakulima ni zaidi ya shilingi trilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile pesa imekwenda kwa wakulima na nyingine Serikali imepata kodi. Sasa tukiwekeza kwa makusudi kwenye sekta ya kilimo nina uhakika tutajibu matatizo mengi. Kwanza, tutajibu tatizo la bima ya afya kwa sababu haya mazao yote yapo kwenye mfumo wa ushirika. Tunaweza tukaamua hawa wakulima wote ambao wapo kwenye sekta ya korosho wakatiwe bima za afya kupitia zao lao na inawezekana kabisa kwa sababu wana mapato ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama wakulima wa zao la kahawa kule kwetu Mbeya na Songwe na wenyewe pia hivyo hivyo. Serikali ikiwezesha mitaji kule, maana yake watakatiwa bima na watapata mazao, lakini hata kujengewa nyumba za bei rahisi kwa sababu tayari wana mazao ya uhakika na uhakika wa kuvuna. Kwa hiyo, ninaiona sekta ya kilimo kwamba ndiyo *solution* ya matatizo kwenye nchi yetu na tunaweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tu iweke *commitment* hapa kwamba uwekezaji wote unaoenda kuzalisha basi, *central bank,* kwa maana ya Wizara ya Fedha iwe inatoa *guarantee* kwenye haya hizi sekta. Kwa mfano, hizi bodi za mazao siyo lazima wawape fedha *cash*. Wanatoa *guarantee* kwamba huu ni mradi unaoenda kuzalisha ajira za watu labda 10,000. Kwa hiyo, Serikali itoe *guarantee* pale ili hawa watu wanaoenda kukopa kwenye *commercial bank* wakope kwa *ratio* ambayo iko chini ya 10%, na nina uhakika tija kubwa sana itapatikana kwenye mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuwe na mpango wa makusudi wa kutafuta masoko nje ya nchi. Tunao mabalozi wetu sisi kila mahali na wenyewe watusaidie au tutengeneze chombo maalum

kinachoshirikiana na mabalozi wetu kwenye kutafuta masoko kwa sababu kuna masoko mengi sana nje ambayo hatujayafikia ili tuweze kuleta *foreign currency* (fedha za kigeni) ambazo mimi nina uhakika kama tukishirikiana vizuri na mabalozi wetu na tukaunda chombo maalum kwa ajili ya kutafuta masoko tija itakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano. Mimi nilipata *order* ya kupeleka machungwa Shanghai. Nilipopeleka *sample* ya machungwa yetu yaliyoko Tanga na Mbeya kule yakaonekana hayana vigezo. Kwa hiyo, mimi ninayatoa machungwa *South Africa* ninayapeleka Shanghai na China, wakati kumbe tungetengeneza mpango mzuri hapa kupitia Wizara ya Kilimo, wale watu wanaolima machungwa Mbeya na Tanga kule kwa wenzetu, yaka-*meet* zile *standard,* ni dola nyingi sana zingeingia, na nchi yetu ingetengeneza mapato na ajira zingepatikana. Kwa hiyo, iko mifano hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni uagizaji wa mafuta ya kupikia na ngano. Lazima tuamue kama nchi kwamba sasa tunakomesha uagizaji wa mafuta nje ya nchi kwa kulima alizeti na michikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalunenge. Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, atafuatiwa na Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando, Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, ajiandae.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia ninaomba nianze kwanza kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uzima na kubwa kuruhusu mimi kuwa Mbunge na kuruhusu mimi kuwemo Bungeni leo hii. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wangu wa CCM na Halmashauri Kuu kupitisha jina langu, na mimi leo kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa alioupata; na ushindi huu alistahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee pia ninawashukuru wanawake wa Mkoa wa Tabora ambao walinipa kura ambazo ziliniwezesha leo kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Ahsanteni sana wanawake wote wa Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kinara mwongoza njia kwa kazi anazozifanya. Amegusa sekta zote, kila kijiji amegusa, kila mtaa amegusa, kila wilaya amegusa, kila mkoa amegusa na leo Tanzania ya leo, siyo Tanzania ya jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kuwapongeza walioshiriki wote kuandaa mpango huu. Hongereni sana. Wote mlioshiriki mpango huu ni mzuri ambao unaonesha dira ya wapi tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajielekeza kwenye ushauri, nianze na *agenda* ya nishati safi ya kupikia. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yeye ndiye kinara namba moja nchini wa nishati safi ya kupikia, ndiye kinara namba moja wa Afrika na ndiye kinara namba moja wa ulimwengu wa nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona *agenda* hii imeleta mafanikio makubwa sana. Sasa hivi idadi ya watumiaji wa nishati safi ya kupikia wameongezeka kutoka asilimia sita nukta tisa mpaka 23.2%. Kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana na ndugu zangu walioandaa mpango huu, wamegusia suala hili. Katika hili ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ruzuku ya 50% kwa mitungi 452,445 ya gesi ya kilo sita na kutoa ruzuku ya 85% kwa majiko banifu 200,000 kwa wananchi waishio vijijini na wanufaika wakubwa ni wanawake. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu, nishati safi ni uchumi, nishati safi ni afya, na nishati safi ni mazingira. Ninaomba sasa katika hili tuendelee kupanua wigo wa utoaji wa elimu ya matumizi ya nishati safi kwa wananchi kama ilivyoelekezwa katika mkakati wa nishati safi ya kupikia aliyoizindua Mheshimiwa Rais mwezi Mei, mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika hili niwashauri tuongeze wigo wa upatikanaji wa majiko ya gesi na majiko banifu yenye ruzuku. Vilevile, nizipongeze taasisi 1,136 ambazo zimeitikia wito wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa vitendo zikiwemo Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa, baadhi ya vyuo vya elimu, hospitali zetu, shule na vyuo vingine vya kati, tunazipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu katika mpango huu ningeshauri, zipo taasisi ambazo bado hazijaunga mkono juhudi hizi za Mheshimiwa Rais. *Agenda* hii Mheshimiwa Rais ameileta kwa Watanzania kwa nia njema na nzuri akiwa yeye ni mwanamazingira namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke sheria, kanuni na miongozo mbalimbali na tuisimamie. Taasisi ambazo zinalisha watu zaidi ya 100 ambazo bado hazijaanza kutumia nishati safi ya kupikia zitumie. Isiwe

sasa ni hiari, bali iwe ni lazima kwa mujibu wa sheria na taratibu ili mazingira yetu tuyatunze. Vilevile, sasa hivi kuna kaya takribani 2,000 zinatumia gesi asilia *(natural gas)* kwa ajili ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali hii inapatikana nchini kwa manufaa ya Watanzania. Ninashauri katika mpango wetu tuongeze wigo wa matumizi ya gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninashauri tunahitaji uwekezaji katika nishati safi ya kupikia. Tunahitaji nishati safi, na teknolojia ya nishati safi. Tunamlenga mwanamke kwa sababu nishati safi ni Uchumi. Mama atatumia muda mfupi kupika na muda mrefu kufanya shughuli za uzalishaji mali. Tunamtaja mwanamke kwa sababu mwanamke ndiyo anatumia muda mwingi jikoni, yeye na mtoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kama ilivyoelekezwa kwenye mkakati wa nishati safi ya kupikia, tupunguze tozo na kodi kwenye nishati safi na teknolojia ya nishati safi ya kupikia na mashine za kutengenezea majiko haya ili sasa yapatikane kwa bei nafuu na wafanyabiashara wengi wawekeze katika nishati safi ya kupikia, na vilevile tuwe na teknolojia ya *Pay As You Use*. Unalipa kulingana na matumizi yako ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kutokana na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba Taifa hili linahama kutumia nishati isiyo salama na kutumia nishati iliyo salama, tuweke mazingira mazuri ili sasa wawekezaji waje kuwekeza zaidi na zaidi katika nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaomba kushauri ni suala la watoto njiti. Takribani watoto 300,000 huzaliwa njiti ndani ya nchi yetu. Tupanue sana huduma ya watoto hawa ili wasipotee kwa sababu wakipotea ni nguvu kazi inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la *Special Economic Zone*. Haya maeneo ni muhimu sana kwa ukuaji wa Uchumi. Tupanue

wigo ili sasa hizi *Special Economic Zone* zifanye kazi. Zikifanya kazi, wanawake wa Kitanzania watafanya biashara katika maeneo yao wanapopatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kongani *(clusters)* tuzipe umuhimu na kuzipanua, kongani za kilimo, za mifugo, za viwanda. Hizi kongani zikifanya vizuri uzalishaji ukaongezeka, mwanamke huyu wa Kitanzania atafanya biashara katika maeneo hayo na atatupatia fedha ya kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni viwanda kufufuliwa. Tufufue viwanda vilivyokufa. Kwa mfano, Kiwanda cha Nyuzi Tabora kimekufa, kiwanda cha Maziwa Mkoani Tabora kimekufa. Tufufue viwanda hivi ili wanawake hawa na vijana wetu wapate ajira na uchumi ukue, wazalishe ili pato la nchi liweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhakikisha kwamba wale waliopewa viwanda wameshindwa kuviendeleza wanyang'anywe wapewe wenye uwezo ili sasa vifanye kazi, uchumi ukue na watu wapate ajira wakiwemo akinamama; watafanya biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuongeza kasi ya ujenzi wa viwanda. Tujenge viwanda ili sasa maeneo ya kufanya biashara yawepo na ajira ikue ili uchumi wa wananchi wetu uweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mikopo kwa wanawake. Ninaomba tuongeze wigo wa utoaji wa elimu ya mikopo hii inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mikopo ile inapotolewa tuhakikishe mazingira ya kufanyia biashara yanakuwa mazuri, na pia tutoe elimu, biashara za kuzalisha, wazalishe biashara zenye tija; *TBS* wafanye kazi, watembelee wanawake wawape elimu ya uzalishaji mali ili akinamama hawa waweze kukua katika bidhaa wanazozalisha. Pia wanapokwenda kwenye benki, wapate mikopo ya masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaona muda wangu unakwenda, ni suala la mazingira…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na Taifa lenye kustahimili mabadiliko ya tabia ya nchi na himilivu, tutunze mazingira yatulinde na sisi tuyatunze sekta ya kilimo ikue ili sasa mwanamke afanye kazi maana mama ndiyo mkulima mkubwa nchini, kwa sababu sisi tupo wengi zaidi, takribani ya 51%. Tulime, tuzalishe, tutunze familia zetu na uchumi ukue kuanzia ndani ya familia na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa muda ulionipa, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando, atafuatiwa na Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuwa mwakilishi wa wanawake wa Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee sana niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa kunichagua kwa kura zao ili niweze kuwawakilisha katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo Oktoba 29. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nipo hapa leo niseme mawili matatu ambayo Rais wetu ametufanyia. Kama inavyosemwa mara zote, moyo usio na shukrani hukausha mema. Sisi wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, Mheshimiwa Rais ametufanyia mengi sana ndani ya miaka minne iliyopita toka aingie madarakani ametupa zahanati, vituo vya afya, kwenye sekta ya elimu, maji na hapa nitapenda niseme vichache tu ambavyo wajue kwamba Mheshimiwa Rais anafanya kazi sio tukisema tunasema hewani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametupatia Halmashauri ya Mbinga Vijijini, hospitali ya wanawake yenye thamani ya shilingi bilioni 2.9; zahanati 17 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.7; vituo vya afya vitano vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.7; vituo vya afya kule Wilaya ya Tunduru; Kituo cha Malumba kinaendelea na kazi, Kituo cha Afya cha Kata ya Mbaa Wilaya ya Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya maji ametupatia vitu vingi. Kwa kuwa mimi ni kiungo mchezeshaji namba sita nitataja wilaya zote ambazo amefanya vitu hivi kwa macho. Mheshimiwa Rais alitupa shilingi milioni 900 Hospitali ya Wilaya ya Mbinga ambayo kwa kweli ile hospitali ni kongwe alitupa tufanye ukarabati wa hospitali ile. Tuliweza kufanikisha kutengeneza *OPD*, *emergency* nzuri sana ipo pale, tulitengeneza *theatre*, tukatengeneza na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo alitoa fedha hospitali ya Wilaya ya Tunduru, shilingi milioni 900, tulitengeneza *OPD* nzuri sana, tukatengeneza *theatre*. Siku zote wanasema ukisema ahsante maana yake unaomba tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri haya, bado niwakumbushe kwenye bajeti ambayo itakuja tunahitaji au tunaomba mtujengee wodi za akinamama *(maternity ward)* kwa kuwa hospitali

hizi ni kongwe na zinapokea wamama wengi sana. Kwa mwezi wanajifungua wanawake takribani 400 - 500 kwa Tunduru, lakini pia wanajifungua akinamama 700 - 1,000 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye suala la maji. Ninamaanisha kwamba tunaposema uzalishaji na mpango wa ukuwaji wa uchumi kwa jamii, tunaangalia zaidi afya ya watu hawa. Jamii ikikosa afya, ikikosa huduma za jamii maana yake uchumi huu hautakua. Ndiyo maana nimempa hongera nyingi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukumbuka kuwa uchumi unaendana na afya ya jamii na mazingira mazuri. Tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais bado anajua unapotakiwa kuwa na uchumi mwanamke anatakiwa asikae bombani au asitafute maji masaa manne hadi matano ameendelea kutupatia maji Wilaya ya Mbinga shilingi bilioni 4.6. Pia amekwenda kutupatia mradi mkubwa wa maji Halmashauri ya Tunduru shilingi bilioni 3.4, tunasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa sasa ningeomba nijielekeze kwenye ushauri wa mpango na sera wa mwaka 2027/2028. Kwanza ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri mwenye dhamana walipotuambia kuhusu suala la wanaopata kazi wasihame kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninapenda kuishauri Serikali, niseme kuwa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema kuwa inatakiwa watu wasihame, tunaomba iwekwe sheria ili kuilinda kauli za viongozi walizosema zitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano watu wakienda kuripoti kwenye vituo vyao, unakuta kuna wakati wanakuja na barua moja kwa moja wanasema wasainiwe ili wahame. Tunaomba, kuwalinda Wakurugenzi na watu wenye mamlaka husika basi waweke sheria ambayo ita-*cement* hii kauli ya kuwa watu wasihame ili watu wetu waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nishauri jambo lingine kwenye suala la elimu. Tunasema hawa watu wanaopelekwa kwenye vijiji mbalimbali, wanaokwenda kufanya kazi, ajira za vijijini, ningependa kushauri tuwape *motivation*, kwani kijijini kuna mazingira fulani ambayo sisi wote tunayafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetamani sana waajiriwa hawa wanaokwenda vijijini wapewe motisha. Kwa mfano, tuna ile Mei Mosi ambayo inasema, mtu Mei Mosi ndiyo anatambulika. Asitambulike Mei Mosi peke yake, kuwe na utaratibu, idara husika kama ni walimu, kama ni afya, waishi kule wakiwa wanajua wanajaliwa na wanapendwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu akifanya vizuri, labda tunasema anunuliwe bati, labda atakayefanya vizuri atanunuliwa hiki, itamfanya yule mtu aone kuwa inawezekana kubaki pale. Kama Mheshimiwa Rais alivyoanzisha kuanza kuwatengenezea nyumba zaidi ya 70 kwenye maeneo yao, na sisi kama watendaji na wataalam na Serikali, tuwape *motivation* hawa watu badala ya kuona tu kuwa wanakosea wapi? Kwa nini wanataka kuhama? Tuwatengenezee mazingira ya wao kupenda kukaa kwenye maeneo yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikifika hapo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando. Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima ajiandae.

Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Mpango. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kura nyingi alizozipata na

kupewa dhamana ya Watanzania. Pia ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili; Waziri anayeshughulikia mpango Mheshimiwa Profesa Kitila na Waziri wa Fedha kwa kuleta mpango ambao ni mzuri endapo utatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nijikite zaidi kwenye eneo ambalo Watanzania wengi wanategemea hasa kwenye suala zima la kilimo. Watanzania wengi wanategemea sekta ya kilimo ambayo ndiyo inaendesha maisha yao. Kwenye mpango tumeona mipango mizuri ya Serikali, lakini tunakazia kwenye eneo la utekelezaji. Ili wananchi waweze kuendelea, ni vyema Serikali sasa ikajikita kwenda kusimamia miradi ya kilimo hasa cha umwagiliaji. Eneo hili ni muhimu ili wananchi waweze kuwa na uhakika wa uzalishaji kuliko ilivyo kwa sasa wanalima kilimo cha kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mipango mizuri iliyofanywa na Serikali hasa kwenye ruzuku ya pembejeo, wamejitahidi sana, Serikali wamepeleka mbolea na pembejeo nyingi, lakini bado wakulima wetu wanalima kilimo cha kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa mwaka 2025 ulioishia mwaka 2025, Serikali ilikuja na mkakati wa kilimo cha umwagiliaji, lakini bahati mbaya sana karibu miradi yote ya umwagiliaji ni mibovu na haijafanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba kwenye eneo la usimamizi waende wakasimamie ili kilimo kiweze kuwainua Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi wanalima kilimo cha kujikimu. Sasa tunataka watoke kwenye kilimo hicho cha kujikimu waende kwenye uzalishaji ambao utakuwa na tija sambamba na kuwapa vifaa vya uzalishaji ambavyo vitawawezesha Watanzania kuzalisha na nchi iweze kupata ziada ya kuuza mazao sehemu ya nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kilimo kinaenda sambamba na viwanda; ili mkulima aweze kunufaika tunahitaji sasa tupate viwanda ambavyo vitawasaidia Watanzania kuweza kuweka thamani ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna eneo la uvuvi, na tuna eneo la ufugaji. Tanzania ni nchi ambayo bado uvuvi ni eneo dogo sana linalotoa mchango kwenye pato la Taifa. Eneo hili tunapaswa kuwasaidia wananchi. Nchi zilizoendelea sasa hivi wanapata fedha nyingi sana kwenye uvuvi, ni kwa sababu wamewekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uwekezaji mkubwa, kwani nchi yetu ina eneo la bahari kuanzia eneo la Mtwara mpaka Tanga, lakini bado hakuna kitu ambacho kinaweza kuwawezesha hawa wafugaji, wavuvi ambao wanafanya shughuli za uvuvi kwenye maeneo haya. Tuwape fedha, tuwawezeshe vitendea kazi ili waweze kuwa na uzalishaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa kisasa unahitaji vifaa, uvuvi wa kisasa unahitaji vizimba ambavyo vimetumika katika maeneo mengi ambayo wanazalisha. Tunaomba kwenye maeneo haya yafanyiwe kazi. Pia tuangalie eneo la mifugo. Kwenye mifugo kama hakuna uwekezaji hasa wa kutenga maeneo ya malisho na maeneo ambayo watanyweshwa mifugo wapate huduma, hatuwezi kupata mifugo mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina nafasi ya kupata masoko ya nje, kama tutakuwa tumewekeza kwenye eneo hili. Ninaomba tuwekeze kwenye maeneo haya. Kwenye eneo la madini, nchi yetu ina madeni mengi, lakini tupo nyuma sana kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti tunaoutegemea kwa sasa ni wa wachimbaji wadogo wadogo. Kwa bahati mbaya hawa wachimbaji wadogo wadogo wakivumbua madini, wanakuja kufukuzwa na watu wanaoitwa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana tuwekeze kwenye utafiti. Utafiti ndiyo utakaotufanya sisi tutoke kwenye hatua tuliyopo kwa sasa. Leo tunazungumzia machimbo ya almasi, toka madini haya ya almasi yalivyogunduliwa pale Mwadui, miaka yote, miaka nenda rudi hiyo almasi ni ya hapo hapo Mwadui. Ni kwa sababu hakuna utafiti uliofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba maeneo ya madini tuwekeze zaidi utafiti, kwani nchi itanufaika kwa sababu tuna madini ya aina mbalimbali kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mazingira, nchi yetu ina misitu mingi ambayo imemilikiwa na Serikali, lakini bado hatujanufaika kwenye maeneo haya ya uhifadhi wa mazingira. Nchi nyingine zinanufaika kwa kiwango kikubwa. Kuna sera ya utunzaji wa mazingira pamoja na uhifadhi unaopata na hewa ya ukaa *(Carbon)*. Niombe sana, Serikali kwenye maeneo haya iweze kuangalia kwa jicho pana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wananufaika sana, wanapata fedha nyingi. Ninawaomba wenzetu ambao wapo kwenye suala la usimamizi, waweze kutafuta masoko tuweze kuuza kwa wanunuzi ambao ndio wanaonunua kuliko ilivyo sasa tunawapa *middleman* ambao wapo katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaishauri Serikali hata maeneo ambayo misitu inamilikiwa na Serikali kwa maana ya *(National Park)* na wao waweze kunufaika kuliko ilivyo kwa sasa wanufaikaji ni misitu ambayo iko chini ya Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye eneo la miundombinu. Pamoja na yote mazuri tutakayoyafanya, kama hatujakuwa na uwekezaji mzuri kwenye maeneo yale ambayo yanaweza yakakuza uchumi, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenye eneo la mpango mmezungumzia ukuzaji wa uchumi hasa kwenye eneo la Liganga na Mchuchuma. Sasa ili uweze kuchimba hayo machimbo ya makaa ya mawe na chuma ni lazima ujenge reli ya kutoka Mtwara kwenda Liganga ifike kwenye eneo la Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga bandari karibu kila eneo na tunaipongeza sana Serikali. Bandari ya Mtwara ni nzuri; Bandari ya Dar es Salaam imekuwa na mapato mazuri; Bandari ya Tanga kumechangamka, lakini zipo bandari zilizopo kwenye maziwa makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Karema tumejenga bandari kubwa ambayo bado haijafanya kazi. Kwenye Mpango, lazima twende sambamba na uwekezaji nje ya nchi ya *DRC Congo* ili tuweze kupata rasilimali zitakazoifanya bandari ile iweze kufanya kazi, sambamba na kujenga barabara ya kutoka Karema kuja eneo la Kabungu ili iwe kiunganishi kwa ajili ya kuifanya Bandari ya Dar es Salaam iweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana wa kunipa nafasi. Nami ninataka kuungana na wenzangu waliosema ni vyema mifuko yote iliyowekwa kisheria tusiingize kwenda kupunguza, itatufanya tusipate hiyo miradi ya maendeleo. Mfuko wa Reli, Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maji vinategemea sana upatikanaji wa hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso. Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, atafuatiwa na Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, na Mheshimiwa Asha Juma Feruz ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika mipango na bajeti ambayo Serikali imetuletea siku ya leo. Kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia, basi ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, uhai na kutujalia afya tele sisi wote tulio hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fursa ya kuwepo maeneo haya kwa sababu tulipitia michakato mingi kwenye kura za maoni huko na hatimaye tukaingia kwenye uchaguzi mkuu na tukaweza kufika hapa eneo lako hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niwapongeze sana Spika, wewe Naibu Spika, na Wenyeviti wote kwa kuchaguliwa. Zaidi ya yote

niwapongeze wananchi wa Jimbo la Ikungi Mashariki kwa kunipatia ushindi mkubwa, kuipatia hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi ushindi mkubwa, tukiongoza kwa kura nyingi sana za kishindo na Mheshimiwa Rais akiwa ameongoza sana katika Jimbo la Ikungi Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia Mpango elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu; Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa miaka mitano; Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka 2026/2027; na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti katika muda wa kati (2026/2027 hadi 2028/2029).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwa namna mawasilisho yaliyowekwa Mezani, ni mawasilisho mazuri ambayo yanavutia na kila mtu akiyasikiliza anapata hamu ya kuona utekelezaji wake unafanyika haraka. Kila mtu anashawishika kuona kwamba, kama kweli hii mipango ambayo iko Mezani itatekelezwa kwa asilimia zote, basi Tanzania itaenda kuwa nchi yenye uchumi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia mipango inasema, pato la Taifa *(GDP)* inaweza kufikia dola za Marekani trilioni moja, lakini pato la mtu mmoja mmoja linategemewa kufikia dola za Marekani 7,000 ifikapo 2050. Sekta binafsi inatakiwa kuchangia 70% ya gharama ya Mpango. Kwa mantiki hiyo, unaona ni namna gani haya mawasilisho yalivyo mazuri na kama yataenda ipasavyo, basi tutafikia hiyo dira ambayo tunaitazamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna angalizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia hotuba yake aliyoitoa mwezi Novemba ambapo alisema, ninaomba ninukuu: "Watendaji msipobadilika kuendana na matarajio ya wananchi tutawabadilikia." Kwa maana gani? Hii mipango tayari ni kifungo. Hii mipango tayari inatuweka katika mazingira ya uwajibikaji. Inaitaka Serikali iwajibike kwa kadiri ya namna tulivyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Mheshimiwa Rais amesema, kama watendaji hawatabadilika kuanzia Mawaziri mpaka

viongozi wa ngazi za kata na vijiji, kama hawatabadilika na hawataendana na kauli za Mheshimiwa Rais, ina maana hii mipango huenda isifanikiwe. Hata hivyo, tunategemea kwa namna Waziri wa Fedha alivyowasilisha na Waziri wa Mipango alivyowasilisha tunategemea haya mambo yataenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite nianze moja kwa moja kwenye sekta ya elimu. Tunafahamu kabisa ya kwamba katika maendeleo yoyote lazima uwezo wa watu uweze kujengwa. Watu wanatakiwa wajengwe kupitia elimu. Sasa je, elimu yetu kwa wakati huu ikoje? Tunaweza kuona kwamba mwaka 2007 tulikuja na Sera ya Elimu kila Kata, lakini hatujaendelea mbele zaidi ya hapo na tuna mpango wa maendeleo mpaka mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninashauri, sasa twende mbele zaidi, tuwe na mawazo ya kujenga shule za sekondari kila kijiji, tuwe na mawazo ya kujenga shule za msingi kila kitongoji, ili hawa watu wapate elimu. Kwa sababu tukiangalia tu, tukibakiza hizi shule zetu za kata ambazo sasa hivi zinafanya vizuri; na ninamshukuru Mkuu wangu wa Shule Bwana Mtoi amefaulisha shule yetu ya Siuyu imefanya vizuri kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tutaishia kwenye kata, ina maana kuna watu wengi tutawaacha na tukumbuke kwenye elimu kuna watu wakimaliza Darasa la Saba tunawaacha pembeni. Kuna watu wakimaliza shule ya sekondari tunawaacha pembeni, na wengine wakimaliza *Form Six* tunawaacha pembeni, wale ambao hawabahatiki kuendelea. Sasa Mpango huu unatakiwa uje na mawazo ya kuhakikisha kwamba hakuna mtu hata mmoja anayeachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu aingizwe kwenye Mpango. Yule anayeachwa darasa la nne, yule anayeachwa darasa la tano, yule anayeachwa *form four,* anayeachwa *form six,* anayeachwa chuo kikuu wote waingie kwenye Mpango, wahusishwe kama vile mpango unavyosema mpango jumuishi na ushirikishwaji… *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea na mpango wa kujenga shule za sekondari kwenye kila kata Tanzania nzima, maeneo yote ambayo kata hizo hazina shule za sekondari. Siyo hivyo tu, nchi hii ina vijiji 12,261, lakini tunazo shule za msingi zaidi ya 15,000 hiyo ni kumaanisha kwa uwiano ni karibia kila kijiji kina shule ya msingi na tunaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa, tunajenga shule ya msingi kila palipo na shule ya sekondari. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka shilingi trilioni 1.3 kupitia Mradi wa *SEQUIP* kwa shule za sekondari na ameweka zaidi ya shilingi trilioni 1.13 kupitia Mradi wa *BOOST* kwa shule za msingi. Kwa hiyo, mpango anaouelezea ndiyo tunaoendelea kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Thomas Taarifa unaipokea?

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, ninapokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *speed* iwe kali ili maneno ya Mheshimiwa Rais ya kwamba watendaji wasipobadilika, basi watabadilishwa. Kwa hiyo, ni jambo zuri alilozungumza, lakini mimi

nitilie mkazo kwamba kila kijiji ijengwe shule ya sekondari kwa sababu sasa hivi wanafunzi ni wengi. Hizo shule za msingi sasa hivi zielekezwe kwenye vitongoji, ndiyo hoja yangu ilikuwepo hapo, kwa sababu, sasa hivi wanafunzi ni wengi na shule sasa hivi zimeelemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia sasa hivi shule ambazo tuko nazo hata madawati hayatoshi kwa sababu wanafunzi ni wengi sana. Pia, hata madarasa na yenyewe hayatoshi. Kwa hiyo, kama Serikali itaelekeza elimu kwa kila kitongoji, shule za msingi zikajengwa na kila sekondari ikaenda kila Kijiji, tutakuwa tumesaidia sana kwenye suala la elimu na watu wetu watakuwa wamepata maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni katika sekta ya ujenzi. Ninaomba nichangie hapo. Tunaona katika bajeti zetu za kila mwaka, sekta ya forodha huwa inachangia sehemu kubwa sana. Sasa ili sekta iendelee kuchangia vizuri na iweze kuleta pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado ninatilia mkazo yale ambayo yapo kwenye Mpango, kwamba zile bandari kavu, kwa mfano, Kwala ambayo tumeainisha, lakini kuna maeneo mengi hapa nchini Tanzania, hata mkoani Singida. Kuna shida gani kujenga bandari kavu Mkoa wa Singida? Kujenga bandari kavu karibu kila maeneo itasaidia kuondoa *congestion* pale Dar es Salaam. Zile bandari ambazo tunazijenga ya Bagamoyo, Tanga, na Mtwara, lakini bado hazipumui kwa sababu hatujatoa matoleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ushauri wangu ni kwamba tujitahidi kadiri tuwezavyo tujenge bandari kavu maeneo mbalimbali, ili kuachia zile sehemu ambazo zinapokea mizigo ili papumue na mizigo mingine ipokelewe katikati mwa nchi hata hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni katika sekta ya kilimo na ufugaji. Mipango yote imetajwa vizuri, lakini kwenye sekta ya kilimo na ufugaji haijataja vizuri, na sijaona kipengele ambacho kimetiliwa mkazo kwenye ufugaji. Ukumbuke watu wetu hawa ni wakulima na wafugaji kwa asilimia kubwa na tumeona hapa kilimo ni *almost* 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndivyo ilivyo, mimi nilikuwa ninafikiria masuala ya mifugo yawekwe katika namna ambayo hawa watu wanaweza wakafuga kisasa. Kwa mfano, tuna shida kubwa sana ya majosho kwenye maeneo yetu. Tuna shida kubwa sana ya mabwawa, ikifika miezi ya kiangazi hasa mikoa yetu, unakuta mifugo inaanza kufa kwa sababu ya kukosa malisho na kukosa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sekta hii ni muhimu kweli kweli. Ukitaja sekta ya kilimo, inaenda sambamba na sekta ya ufugaji, kwa sababu watu wetu ndio wakulima na wafugaji. Sasa nilikuwa ninaomba tuhakikishe ya kwamba pamoja na kwamba tuna dira nzuri, tuhakikishe ya kwamba hii sekta tunaipanua kuhakikisha kwamba watu wetu hawa wanajengewa mabwawa karibu na maeneo yao, wanasaidiwa katika masuala ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinii lingine la kumalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Juma Feruz, Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa ajiandae.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii uliyonipatia. Nianze kwa kumshukukru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Nchi kwa kunipatia nafasi hii, lakini hata kwa kukubali niwe sehemu ya hili Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, na pia ninampongeza kwa kura nyingi alizopata. Ninamshukuru kwa sababu ya kuidhinisha kuteua jina langu, na baada ya hapo kuingia kwenye mchakato na Mungu akanisaidia nikashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali Hassan Mwinyi; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ninampongeza hata Spika pamoja na Naibu Spika kwa kupata ridhaa ya kuwa sehemu ya uongozi wa Bunge hili. Ninawapongeza pia Mawaziri mbalimbali hususan ni Mawaziri ambao wamewasilisha Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa. Vilevile, ninawapongeza Wabunge kwa ujumla kwa kuaminiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kueleza yale ambayo nimejifunza baada ya kusoma huu Mpango. Wakati ninausoma nimeona kwa sehemu kubwa umejibu haja za wananchi wetu. Umejibu mategemeo na matarajio ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia jinsi ambavyo Mpango wa Maendeleo umeandaliwa, ni vipaumbele gani ambavyo vimezingatiwa? Nikiangalia vipaumbele ambavyo vimezingatiwa kwenye mpango huu wa maendeleo na malengo ambayo yamewekwa, ninaona moja, Mpango umeeleza kwamba lengo ni kuimarisha uchumi imara; pia, kuimarisha uchumi jumuishi na kuongeza ushindani katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaangalia hivi vipaumbele vimeandaliwa kwa kuzingatia nini, napo Mpango ukawa umejibu kwamba vipaumbele vimeandaliwa kwa kuzingatia namna ambavyo tumetekeleza ule Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano. Pia, umeandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya uchumi na mabadiliko ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita zaidi kwenye sekta ya kilimo na kwenye sekta ya mifugo. Mpango wetu umeeleza namna ambavyo utatekelezwa na ukawa umeeleza pia *risk* ambazo zinaweza zikajitokeza na namna ambavyo zinaweza kuwa *mitigated*. Umeeleza sehemu ya tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana waandaaji pamoja na Tume ya Mipango kwa sababu wameweka hata ile Tume

ya Mipango ambayo imehusika kuandaa hii kuwa sehemu ya tathmini. Ingeweza tu kuandaa, halafu ikakaa pembeni, lakini kwa kuwa inakuwa ni sehemu ya kufanya tathmini ya kile ambacho tutaenda kutekeleza, inatupa matumaini kwamba tutaenda kukiishi kile ambacho tumekiandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ile ya *risk* imenifurahisha zaidi kwa sababu kupanga ni kitu kimoja, lakini ikiwa hautabaini *risk* ambazo zinaweza kujitokeza njiani unaweza kuwa na mipango mingi na isitekelezeke. Ndiyo maana wengi tunaanzisha vitu, lakini havifiki mwisho. Kwa hiyo, mpango umejibu kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya Kilimo ambayo ndiyo najikita, kwa sababu mimi wananchi wangu ni wakulima, lakini wananchi ambao wameniamini ni wafugaji. Mpango wa Maendeleo umeeleza kwa kuzingatia ile *reference* ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo, umeeleza mafanikio ambayo tumeyapata kupitia huo mpango. Zipo changamoto ambazo nimeziona kwenye huu Mpango, kwa mfano, Mpango kwenye kilimo umeeleza kwamba, tutaenda kuboresha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukifanya *reference* ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa ile miaka mitano, ukiangalia tumepiga hatua kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka hekta 695,000 mpaka hekta 983,000 kwa maana kwamba, kuna ongezeko la hekta 288,000. Sasa ukiangalia hizi zimeongezeka kwa muda gani? Utaona ule ukuaji hauendani na malengo yetu. Ikiwa tulikuwa tumejiwekea tufikie angalau hekta 1,200,000, maana yake tumepiga hatua kama kwa 24% tu. Ukiangalia kwa muda uliobaki kukamilika kwa utekelezaji huu utaona *speed* yetu haiendani na kile ambacho tumejipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaangalia hili ongezeko la hizi hekta, ninaona pia, halijaenda kwa usawa. Kwa mfano, jimboni kwangu mimi hakuna bwawa hata moja la umwagiliaji wala hakuna

kisima hata kimoja kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Maeneo ambayo wengine tunatoka ni maeneo ambayo ni nusu jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri tunapoenda kwenye Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ni vizuri yawe yanazingatiwa maeneo kwa kufuata vipaumbele. Yale maeneo ambayo yana hali ya jangwa zaidi yapewe vipaumbele ukilinganisha na maeneo ambayo siyo ya jangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango umeeleza kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula. Ukiangalia tumeongeza tani 5,655,000 ambapo hii *rate* na lengo ambalo tulikuwa tumejiwekea, ni *speed* nzuri, lakini haijaonesha hapa *benchmark*. Ukiangalia tumetoka tani 17,148,000 mpaka tani 22,000, maana yake ni ongezeko la tani 5,000,000, lakini mpango hauoneshi kuwa tulikuwa tumejipangia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa ninapata wasiwasi inapofika wakati wa kufanya tathmini, tutafanya tathmini kwa rejea ipi ikiwa hatukuweka lengo? Kwa hiyo, yapo madhaifu ambayo nimeyaona. Nikawa ninashauri, ni vizuri sasa kila sehemu tuweke *benchmark*, tuweke lengo la kulifikia, ili unapokuja wakati wa kufanya tathmini, inakuwa ni rahisi kurejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwenye sehemu ya kilimo imeeleza mazao ya biashara jinsi ambavyo yameongezeka. Sasa mimi ninataka niongelee zao la pamba kwa sababu, kwetu pamba ndiyo dhahabu, kwetu pamba ndiyo Tanzanite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo zao la pamba lilikuwa kwenye kilimo cha mkataba na kilimo cha mkataba kilikuwa kinalazimisha mnunuzi mmoja. Kimeleta madhara makubwa kwa wananchi wetu kwa sababu, mnunuzi mmoja inafika hatua anazidiwa na wakulima, analazimika kuwakopa na wakati mwingine wanalazimika kutoa rushwa, ili walipwe haki yao. Kwa hiyo, kilimo cha mkataba kwenye zao la pamba hakijafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa kwa sehemu kubwa tume-*address* ulimaji wa tija, lakini hatujaangalia kwenye upande wa bei. Hata kama Soko la Dunia likiwa limeshuka, kama tuna wanunuzi wengi maana yake ni panakuwa na ushindani wa bei. Kwa hiyo, ninashauri tunapoenda kwenye Mpango wa Nne, ni vizuri zao la pamba, ikiwa tutaendelea na kilimo cha mkataba, basi tuangalie namna ya kuwa na wanunuzi wengi, ili kuwa na ushindani kwenye bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa mifugo, tumefanya vizuri, lakini ili tuongeze tija, ni lazima tuhakikishe tunajenga majosho kila sehemu. Ni lazima pia, tuongeze malisho.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, muda wako...

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma Feruz, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa. Mheshimiwa Rashid Habib Ali ajiandae.

**MHE. ASHA J. FERUZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo Mezani ya Mpango wa Serikali. Nachukue nafasi hii kwanza kabisa ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuchangia, nawashukuru sana wapigakura wangu, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa UWT Taifa, kwa kunipa ridhaa kwa kura nyingi niweze kusimama hapa kuwa mwakilishi ninayewakilisha kundi la Vyuo na Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nakishukuru sana chama changu pendwa, Chama Cha Mapinduzi, kwa kuniteua kuwa mwakilishi katika nafasi hiyo ndani ya Bunge lako Tukufu. Ninachukua nafasi hii pia, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata katika Uchaguzi Mkuu tulioufanya Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nachukua nafasi hii pia, kuwapongeza Mawaziri wote tukiamini kwamba, sisi ni timu moja. Wao wako mbele kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza malengo na mahitaji ya wananchi wanayoyatarajia katika Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najielekeza katika mchango wangu. Kama alivyowasilisha Waziri wa Mipango asubuhi, amesema kuwa, mpango huu umeandaliwa kutokana na Hotuba ya Rais, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na matamko ya viongozi ambayo ndiyo kiu ya wananchi ambao ndiyo tunawawakilisha humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mpango huu mimi najielekeza katika maeneo matatu; eneo la kwanza ni ajira kwa vijana. Katika sensa tuliyoifanya, nguvu kazi ya Taifa ni watu 25,000,000 lakini katika watu 25,000,000 milioni 14,000,000 ni vijana, sawa na 55.6%. Nini mchango wangu sasa ninaotaka kuusema? Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 21, Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake ambayo imeundwa kimejielekeza kutengeneza ajira 8,500,000. Sasa Serikali kwa mpango huu mzuri waliotuletea ninaomba kutoa ushauri kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwasaidia vijana katika maeneo yetu tunaowawakilisha hapa waweze kupata ajira rasmi na zisizo rasmi, tuisadie Wizara ya Ajira. Pamoja na Wizara ya Vijana kuweza kupata taasisi chache ambazo zitakuwa na kazi ya kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa vijana, ili vijana hawa watakapotoka kwenye hizo taasisi ama vyuo tupate *positive impact* kwa muda mfupi kwenye jamii zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naishauri Serikali kutoa mafunzo mahsusi, ikiwemo ujuzi wa fani adimu *(real skills)* kwa vijana, ili kupata fursa za ajira ndani na nje ya nchi. Nchi yetu ina miradi mingi ya kimkakati, nikitoa mfano Mradi wa Bomba la Mafuta, zipo kazi tunasema kwa Kiswahili chepesi, mafundi mchundo. Hawa ni watu wanaohitajika sana. Hatuna sababu ya kwenda kuchukua watu hawa nje, ili waje wafanye kazi zile hali ya kuwa sisi tuna vijana wengi

ambao bado hawajapata ajira. Kwa hiyo, tutumie ombwe hilo kuweza kuwapa vijana wetu ajira za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichangie kuendeleza kuzisaidia sekta binafsi, kuwawekea mazingira bora na mazuri ya kukuza mitaji yao, ili waweze kutoa ajira kwa vijana wetu. Kuwa na utaratibu maalumu wa *knowledge transformation* kutoka kwa wafanyakazi wa kigeni kwenda kwa wafanyakazi wa ndani, wazawa. Hii itatusaidia kupunguza kuajiri watu kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na mkakati wa kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo vidogo vijijini na kukuza ongezeko la thamani katika sekta za kimkakati ikiwemo uvuvi, misitu, kilimo na mifugo. Kufuatia hayo niliyoyachangia kwenye eneo la vijana tutakuwa tunajielekeza katika kuongeza ajira kwa vijana wetu, ajira rasmi na zisizo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni eneo la ubunifu na utafiti. Ninapenda kuipongeza Wizara ya Elimu, kupitia Chuo cha *UDOM,* kuwa washindi wa shindano la vyuo 29 nchini katika masuala ya *cyber*. Hapa chuo chetu cha *UDOM* kimetuonesha umahiri mkubwa na kimetuvisha nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nawaombe Serikali tutengeneze misingi au mpango wa kudumu kuelekea bajeti inayokuja kuimarisha ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidigitali katika huduma za kijamii, Serikali iwekeze zaidi katika kuwaendeleza na kuwaongoza wataalamu wa *Artifical Intelligence*, kwa maana dunia ndiko inakojielekeza. Hii itasaidia kukidhi mahitaji ya matumizi ya *AI* na pia, kuendana na hali ya kiuchumi kupitia ushindani wa sekta mbalimbali zinazotumia teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawapongeza Serikali kwa kuanza kutumia teknolojia hii kwenye baadhi ya taasisi za umma, kwa mfano, Mfumo wa *E-File*. Tumeanza hivyo, tunavyoendelea tutaendelea kupunguza ajira za watu. Kwa hiyo, sisi hatuna budi kuweza kujikita katika eneo fulani la *Artificial Intelligence*. Kama tunajikita kwenye

*maintenance,* tujikite hapo, tusibebe yote kwa wakati mmoja, tuangalie *focus* yetu sisi, kama Taifa, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho ni katika eneo la elimu. Nawapongeza sana Wizara ya Elimu, tumeanza vizuri. Wiki iliyopita nimeona Mheshimiwa Rais akifungua mpango wa KKK wa kuhamasisha suala la Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa watoto wetu na amesisitiza mtoto asifike darasa la tatu hajui kusoma na kuandika, lakini sasa katika bajeti nimeona inaelekea shilingi trilioni 8.19 kwa 2026/2027. Ninataka kusema nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa najielekeza zaidi katika ongezeko la mikopo ya elimu ya juu. Ni kweli, udahili umeongezeka, 2020/2021 udahili ulikuwa 295,919; 2024/2025 udahili ukawa 361,257; bajeti ya mikopo ilikuwa shilingi bilioni 570 na sasa 2025/2026 shilingi bilioni 916.7; udahili wa 2024/2025 ulikuwa 248,331. Udahili huu umeweza kuwanufaisha wanafunzi 248,331. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza kuona hawa wanufaika wa mikopo ni wale ambao wanaendelea, kwa maana ya *first year*, *second year*, *third year*, *fourth year* na *fifth year,* kwa zile kozi zinazokwenda mpaka miaka mitano na wale wapya. Kwa hiyo, tunaweza kuona kwamba, bado uhitaji wa mikopo ya elimu ya juu ni mkubwa, fedha haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie Wizara ya Elimu na Bodi ya Mikopo kuweza kuongeza bajeti. Pili, tuweke mikakati thabiti ni namna gani tutakiongezea hiki chombo, bodi ya mikopo, kupata fedha. Kwa nini tusi-*engage private sector* ili hii fedha iongezeke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahitaji ni wengi, watoto wa maskini wengi wamekosa mikopo na waliomaliza chuo wengi hawajaweza kurudisha. Kutegemea *source* moja ambayo ni ruzuku ya Serikali, kuuchunga huu mfuko wa bodi ya mikopo, ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaongezee bajeti ili mipango iweze kufikia malengo ambayo tunahitaji. Sasa wanafunzi

wetu wafundishwe ujuzi pamoja na vitu ambavyo vitawasaidia kwenda kujiajiri moja kwa moja. Wakishaajiriwa au kujiajiri moja kwa moja wataweza kurudisha fedha hizi na wengine wakanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja iliyowekwa Mezani. Mwenyezi Mungu atusaidie wote tufanye kazi vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana. Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Habib Ali. Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija ajiandae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rashid Habib Ali.

**MHE. RASHID HABIB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi hii niweze kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwanza, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na leo kuweza kuwa hapa katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninakishukuru chama changu, *ACT-Wazalendo*, chama ambacho kimenilea kisiasa na hatimaye kikaniamini kunipa dhamana ya kupeperusha bendera yake katika Uchaguzi wa Mwaka 2025 kwa nafasi ya Ubunge wa Jimbo la Mtambwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, pia ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Mtambwe kwa kunichagua kwa kura nyingi za kishindo na hatimaye leo nikawa mmoja miongoni mwa Wajumbe wa Bunge hili la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ijumaa ya tarehe 19 Disemba, 2025, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, wakati akiwa kwenye semina inayohusu muungano na wahariri wa vyombo vya habari Zanzibar, alinukuliwa, na mimi ninaomba ninukuu

sehemu ya hotuba yake. Alisema kwamba, “Wizara hii haihitaji kuzungumzia tena kuhusu kero za muungano badala yake inahitaji kuzungumzia fursa zinazotokana na muungano huo”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ya Mheshimiwa Waziri bado tunayaweka kwenye mabano. Tukiangalia Mpango wetu wa Mwaka 2026/2027 na Mwaka 2028/2029, moja ya nyenzo iliyotumika hapa ni Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Mwaka huu wa Fedha wa 2026/2027. Maelekezo ya mwongozo huu ni moja kati ya mambo ambayo yamezungumzwa. Wamesema kwamba, zitengwe fedha kwa ajili ya miradi ambayo inahusu mambo ya muungano na utekelezaji wake uonyeshwe wazi kwa pande zote mbili za muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msikitiko makubwa, pamoja na maelezo ya mwongozo huu, lakini haioneshi dhamira ya utekelezwaji wa mambo haya kwamba, yatachambuliwa na pande zote mbili za muungano, zitaoneshwa maslahi yake kwa uwazi, kwa sababu, tukiangalia bajeti ya mwaka 2024/2025 miradi yote ya kimkakati ambayo imetekelezwa, imetekelezwa kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar anatajwa kama jina tu bila kuonesha bajeti na mkakati mahsusi, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Zanzibar. Badala yake Wizara hii inajificha kwenye vikao vya pamoja ikisema kwamba, inaenda kujadili masuala ya muungano kama kichaka cha kuinyamazisha Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajadili Mpango huu ambao ni dira yetu itakayotuongoza mpaka mwaka 2050, ni lazima twende tukakirekebishe kipengele hiki na hatimaye…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango anaochangia Mheshimiwa Mbunge, ninaomba afahamu na kutambua juhudi kubwa inayofanywa na Serikali kwenye kudumisha Muungano wetu. Muungano wetu huu ni tunu ambayo wote kwa pamoja tunapaswa kuilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa mashaka, lakini pia ninaomba Kiti chako kiendelee kujielekeza kutufundisha jinsi ya kutumia lugha nzuri ili tusiendelee kutumia lugha ambayo ni ya kuudhi kwa kusema pengine Serikali inatumia kama kichaka, ambayo inakuwa siyo lugha nzuri ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid taarifa unaipokea?

**MHE. RASHID HABIB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge atulie, sisi tunajenga nchi na hatuwezi kujenga nchi kwa kichaka cha kufichaficha, tutajenga nchi kwa kuweka kila kitu wazi, ambapo pande hizi mbili za Muungano kila mmoja atapata maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia sekta ya anga, miradi pekee ambayo wamesema inaenda kutekelezwa katika mpango huu ni kupanua viwanja vya ndege. Huwezi ukaichukua Zanzibar ukaiweka na Songwe, huwezi ukaichukua Zanzibar ukaiweka na Mwanza, lazima kuwe na *specific chapter* ambayo inazungumzia masuala ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi pekee ambayo inatekelezwa Zanzibar ni miradi ambayo ina hadhi ya kuetekelezwa kwa fedha za

maendeleo ya Mfuko wa Mbunge lakini miradi ya kimkakati huikuti ikitekelezwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba mpango huu ndiyo dira yetu na utakaodumisha Muungano wetu ni haki na siyo vinginevyo. Hivyo basi, Kamati ikakae iende ikafanye tena uchakachuzi ili ituletee rasimu ambayo iko vizuri ioneshe maslahi ya pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, atafuatiwa na Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima ajiandae.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na vikao vyake vyote kuniwezesha kuniteua mimi kuwa Mbunge katika Jimbo la Ulyankulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ulyankulu wote wa Chama cha Mapinduzi na wananchi wote kwa kuniamini, naweka ahadi yao kwamba nitawawakilisha vema kwa muda wangu wote, nikiwa ndani ya Bunge na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea mpango mzuri wa Serikali, mpango wa utekelezaji wa miradi kwa wananchi wetu. Mchango wangu nataka nijikite kwenye Wizara yetu ya Kilimo, ambapo naamini ajira kubwa ya Watanzania iko kule. Pamoja na mipango mizuri iliyoelezwa na Waziri wetu hapa, ninataka niishauri Serikali kwamba

uwekezaji wetu mkubwa wa Serikali, twende tukawekeze kwenye kupima mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na mashamba ambako shughuli zote za kilimo zinafanyika kule, tutatambua kwamba eneo fulani linatumika kwa kilimo gani? Pia maeneo ya ufugaji tunaamini wananchi wetu ndio wakulima na wafugaji. Yapo maeneo mengi ambayo Baraza la Mawaziri lilifanya maamuzi ya kubadilisha matumizi, lakini tunayo migogoro mikubwa kwenye maeneo hayo ya mipaka baina ya uhifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili kuweza kuitekeleza vizuri dira hii ni vizuri kila eneo wataalam wetu, Maafisa Mipango Miji, lakini pia na watu wa Idara ya Ardhi waliopo huko kwenye maeneo yetu, kwenda kusimamia mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo hayo. Mpango huu usiposimamiwa vizuri, malengo haya tutakwenda kukwama. Nilikuwa najaribu kusisitiza sana kwenye hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mpango wa uchimbaji wa mabwawa, umewekwa vizuri na umeainishwa. Katika bajeti ambayo inapangwa, nilikuwa naweka sisitizo, maeneo haya ambayo yameainishwa kuchimbwa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji ni vizuri yakapewa kipaumbele ili kuendelea kutekelezwa. Tukitekeleza haya, nina imani kubwa kwamba tutaondokana na kilimo cha kutegemea mvua ili wananchi waweze kuzalisha kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka niliwekee uzito kuishauri Serikali ni suala la huduma za afya. Tumejenga vituo vingi vya afya na zahanati, lakini katika maeneo hayo ni vizuri kuimarisha afya za Watanzania kuendelea kuimarisha miundombinu kwenye vituo vya afya ambavyo tayari vimeshaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua vimejengwa vingine watumishi wetu kwa maana ya Madakari na Manesi hakuna hata nyumba za kuweza kuishi. Wanalazimika kuishi mbali ambapo ili kuwapata

wananchi, wanalazimika kutafuta usafiri wa kumfuata mhudumu kwenye eneo la kituo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kuishauri Serikali iweze kusimamia jambo la kuhakikisha kwamba miundombinu rafiki kwenye maeneo yetu ya vituo vya afya, zahanati na hospitali yanaimarika ili kumarisha afya za Watanzania kwa ajili ya kutengeneza Taifa lenye afya bora na kuimarisha afya za Watanzania ili waweze kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hotuba pia ya Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na ushauri wake, nami naungana nao kabisa, kwamba yako maeneo muhimu sasa yanatakiwa kuangaliwa. Ule ushauri wa Kamati uzingatiwe ili kwenda kuitekeleza vizuri hii Dira ya Taifa ya Maendeleo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unanionesha kwamba, asilimia kubwa ya Watanzania walioko kijijini ni vijana ambao ndio Taifa tunalolitegemea. Kwa hiyo, naendelea kushauri kwamba kuwe na sheria na sera nzuri za kuweza kutengeneza mazingira kuhamasisha vijana hawa wanakwenda kutimiza majukumu, utendaji wa kazi kuliko vijana wengi kubaki wakizurura wakati wa kazi. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali ili kuweza kwenda vizuri na Mpango wetu wa Dira ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, tunavyo vijiji vingine vipya ambavyo Baraza la Mawaziri lilikubali viendelee ambavyo vilikuwa ndani ya hifadhi. Eneo hilo la wananchi wetu halipitiki. Ninaiomba Serikali kupitia TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi kupeleka miundombinu ya barabara katika maeneo hayo. Kuwekwe bajeti kubwa ili barabara zifunguke ili kuwasaidia wananchi kusafirisha bidhaa wanazozalisha na kuyapata masoko bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanakosa fursa ya kupata bei kwa sababu tunakuwa na changamoto maeneo mengine, usafirishaji wa mazao yao wanaingia gharama kubwa. Kwa hiyo,

magari hayawezi kufika wanalazimika kusafirisha kwa usafiri ambao ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuiomba sana Serikali kuyatazama wakati wa bajeti maeneo haya ya vijiji vipya ili kuweza kufungua miundombinu ya barabara iweze kuimarika ili wananchi wetu waweze kukuza uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ambao tumeupokea hapa ni mpango mzuri. Kikubwa tu ni kuweka sheria na sera nzuri za kwenda kutekeleza vizuri mpango huo. Mimi natoka Jimbo la Ulyankulu, iko mipango ambayo Serikali iliekeza kwa muda mrefu, lakini unaweza kuona utekelezaji wake, pamoja na mambo mazuri ambayo yamefanyika, inahitaji *speed* ya kukimbia tu ili kuweza kuitimiza mipango ya wananchi ili waweze kupata fursa ya maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi hii ya mchango wangu nilipenda kuishauri hivyo Serikali katika maeneo hayo ya uwekezaji kwenye kilimo, kwenye mifugo, kwenye mambo ya afya kuhakikisha kwamba tunaelekeza fedha nyingi ili Watanzania waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhael kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly jiandae.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ndiye aliyetufanya na kutupa uhai mpaka kufika siku ya leo tuko hapa tumesimama tunazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nataka nisome kidogo maandiko Matakatifu. Warumi 13:1 ili kuonesha kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa nini yupo amekaa pale kwenye kile kiti, Biblia yangu inasema kwamba, "Kila mtu na atii mamlaka iliyo kuu, kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu, na ile iliyopo imeamriwa na Mungu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni chaguo la Mwenyezi Mungu, ndiyo maana amemuweka pale. Hata sisi ambao tumefika humu siku ya leo, nasi pia tumepitishwa na Mwenyezi Mungu kupitia vyama vyetu, ndiyo maana tumefika humu na tunazungumza katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Makamu wa Rais Emmanuel Nchimbi kwa kuchaguliwa kupitia Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa mgombea naye kuwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Spika wa Bunge, ninakupongeza na wewe Naibu Spika Daniel Sillo kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika katika Bunge hili kwa kura nyingi 100% nadhani zote zilipatikana. Ninampongeza pia Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa pia kuwapongeza wananchi wa Katoro walionichagua kuwa Mbunge au mwakilishi wao walionipigia kura nyingi za kutosha ili niwe Mbunge wao katika Jimbo la Katoro. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Katoro ninayeongoza wananchi wote, wawe wa upinzani wawe wa chama gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiye Mbunge wao na mimi niko tayari kufanya nao kazi kwa namna yoyote ambayo tutaongozwa na kwa sababu tuna Rais jemedari kabisa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tutawatumikia wananchi wote wa Katoro wa vyama vyote na wa itikadi zote ambazo zipo katika Jimbo la Katoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye mambo machache. Jambo la kwanza nizungumzie suala la madini. Ninaomba kupendekeza jambo moja kwa Wizara ya Madini, kama itawapendeza, tufike hatua basi turuhusu wachimbaji wetu ambao wapo wa kati na wadogo, kama inawezekana kutunza mali zao katika Benki ya *BoT* au benki ny,ingine watunze na kuweza kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa ungekuwa umetunza mali kuanzia mwezi wa Kwanza au mwezi wa 12, leo mchimbaji mdogo angeuza kwa fedha nyingi sana kwa soko ambalo lipo kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza benki zetu zitoe nafasi au fursa ya kutunza mali katika benki zetu. Kama mtu anao mtaji wa kutosha na hahitaji kuuza mali yake kwa siku hiyo, aweze kuitunza iwe akiba na akihitaji kuchukua fedha benki, apatiwe nafasi ya kuchukua fedha benki kwa dhamana ya mali aliyoiweka benki katika benki zetu ili imsaidie kufanya maendeleo na kupiga hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Wizara ya Nishati ambao hata mimi ni mnufaika wa umeme ambao sasa nitakwenda kupata kaya 4,151 zinakwenda kuwashiwa umeme. Ninawapongeza Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wake ambao wamekubali hata kwenye nyumba za matope wanakwenda kuwasha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kule Katoro kuna nyumba nyingi. Nimemwambia Naibu Waziri Salome Makamba aje atuwashie umeme kwenye zile nyumba ambazo ni za matope kwa sababu ni haki ya wananchi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwashiwa umeme katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametujengea shule nzuri nyingi na mahiri Katoro. Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Profesa Shemdoe alifika akashuhudia shule nyingi za kisasa ambazo zimejengwa Katoro kwa fedha za

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wale ambao hawajaona shule nzuri, njooni mshuhudie Katoro, kuna shule nzuri ambazo amejenga Rais ambazo ni bora na imara zinazotoa mafunzo kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu jambo moja, tunapoelekea katika mipango hii na kusaidia vijana wetu, kuna vijana ambao wako mtaani, wengine wamemaliza shule, lakini baadhi ya vijana hao hawajapata vyeti vyao, vipo chuoni mpaka leo, lakini wapo wanazurura mtaani. Wengine wameanza kujiajiri. Mmoja nimemkuta anafanya kazi ya *car wash*, lakini amemaliza chuo ni kijana mzuri na ni mwalimu, anakwambia sina cheti cha *form four* na cha chuo viko wapi? Viko chuo vimeshikiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Wizara imejipangaje kusaidia hawa vijana ili wapatiwe vyeti vyao. Wanapoomba ajira wanaambiwa mpaka uende na cheti *original*, anakitoa wapi cheti *original*? Cheti *original* kiko chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoenda na mipango hii tukumbuke kuna vijana ambao vyeti vyao hawana, lakini wanataka ajira. Ndiyo hawa ambao tunawaona kila siku huenda wanatangatanga kutafuta ajira, lakini ajira hawapatiwi kwa sababu hawana vyeti katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea tu kupongeza na kusema kwamba, tunapoendelea kujipanga na huu mpango wetu niwakumbushe Wizara ya Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, sisi Katoro tuna uvuvi mkubwa sana, tunahitaji tungepata viwanda vya kuchakata Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile viwanda vinavyochakata samaki ili kuwasaidia wananchi wetu wanapovua samaki, maana tuna samaki wengi sana. Katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imeeleza, kupata kiwanda kimoja cha samaki, mtusaidie ili wananchi wetu waweze kufanya biashara nzuri wanapokwenda kuuza bidhaa zao katika maeneo hayo ya viwanda ili waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninapenda kulizungumzia ni hili jambo ambalo ni kama tu la kupongeza sasa. Tunamshukuru Rais mambo ambayo ameyafanya; ukisikia mtu anayesema Mheshimiwa Dkt. Samia hajafanya; Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipatiwa hii nchi na mtangulizi wake Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli akiwa ameacha Daraja la Busisi kwa asilimia ndogo sana kukamilika, lakini leo sisi tunaotoka Katoro, tunaotoka Geita, tunapita pale kwa dakika tatu tu, na huyu ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyekamilisha daraja hili. Leo tunavuka kwa kishindo kikubwa tukitokea Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunakaa masaa matatu, mpaka manne, mama huyu aliachiwa daraja hili likiwa lina asilimia kama 20, leo limekamilika. Tumpongeze, tumtie moyo, tumtie shime, tumuunge mkono, tushirikiane naye ili aweze kutuongezea, aweze kutusaidia kutuvusha mpaka kufika 2030, tuweze kupata maendeleo makubwa katika sehemu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kija. Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda ajiandae.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii, kwa kuwa ni mara ya kwanza kusimama katika Bunge Tukufu, kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kuweza kutufikisha mahali hapa na mimi nikiwa mwakilishi wa kundi la Vyuo na Vyuo Vikuu, ninashukuru sana kwa kibali alichonipatia na kuweza kusimama mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kushukuru chama changu Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wajumbe wa Kamati Kuu kwa kuteua jina langu na

hatimaye leo ninasimama hapa kama Mbunge wa Viti Maalum, kundi la Vyuo na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisahau Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa UWT Taifa, ambao walinichagua na kuwa miongoni mwa Wabunge watatu wa Vyuo na Vyuo Vikuu, ninashukuru sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nichukue fursa hii pia kusema jambo katika mipango hii ambayo tangu asubuhi ikiwa ikiwasilishwa hapa, ni jambo zuri sana kama nchi kuwa na mikakati kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia miongozo hii tukiona Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na hiyo miongozo mingine. Yote haya ni mambo ambayo ni ya msingi katika Taifa ili kuwa na Taifa lenye ustawi wa wananchi, lakini ikiwa pia na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kabisa Taifa linafika katika mipango ambayo imejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Kamati ambayo imeandaa na kuratibisha mambo haya. Ni mambo ya kitaalamu sana. Kwa hiyo, tunapongeza sana juhudi za kuhakikisha kuwa tunakuwa na mikakati kama hii na mipango kama hii katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja muhimu za kuongeza katika hotuba mbalimbali ambazo zimetolewa kuhusiana na mipango hii. Kwanza ni utekelezaji kwa vitendo hadi ngazi ya chini. Tumeona kabisa ya kwamba hata Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza habari ya ushirikishwaji wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ninaliona kama ni jambo la msingi sana. Ni lazima kuwe na utekelezaji kwa vitendo hadi ngazi ya chini, ambapo tunaita *localization of vision* 2050. Hii itasaidia kutafsiriwa katika lugha nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tunaona ni mkakati ambao upo kitaalamu sana. Mimi nipongeze lakini nitoe ushauri kwamba dira hii itafsiriwe kwa lugha rahisi na kushushwa hadi mikoani katika halmashauri, hata kata na vijiji ili basi *ownership* ya wananchi iwepo, waweze kufahamu nchi inatoka wapi, na inakwenda wapi? Kwa hiyo, ninaomba, mpango huu mahususi uwe na mikakati ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusu uhusiano wa moja kwa moja kati ya Dira ya 2050 na Mipango ya Miaka Mitano na ule Mpango wa Mwaka Mmoja. Tumeona kabisa ya kwamba ni vizuri mipango yote hii ikawa inaenda pamoja, yaani kuwe na *link* kati ya mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, mpango ule wa mwaka mmoja pamoja na bajeti za kila mwaka, ni vizuri ikasomana. Nilitamani, na ninafikiri wenzangu pia waliongea habari ya kuwa na *legal framework; binding legal framework* ambayo itakuwa inalinda hii mipango mikakati ambayo tumejiwekea kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, na hiki wenzangu pia wameongea, ni habari ya mtaji wa watu *(human capital development)*. Tumeshuhudia Serikali ikiwa na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kabisa kuwa Taifa linakuwa na mtaji wa watu ambao watafanya kazi katika viwango na katika tija inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Elimu, wamekuwa wakiwekeza kwa kiwango kikubwa katika sekta hii. Tumeona kabisa upande wa vyuo na vyuo vikuu bajeti za mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu imeongezeka. Hili siyo jambo la kubeza, ni jambo la kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii niseme ni *initiative* ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kabisa wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu wanapata mikopo na kusoma vizuri. Hii ukijaribu kuioanisha na Dira ya 2050 na hii

mipango mingine utaona kabisa tunahitaji uwekezaji mkubwa katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize tu kwamba uwekezaji huu uende sambamba na afya, ujuzi na ubunifu ili tuwe na *manpower* ambayo itaweza kuhimili soko la ajira na kuweza kufanya kazi katika tija na hivyo Taifa liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee jambo lingine, kuhusu usawa wa kimaendeleo kati ya mikoa. Hili ni jambo la msingi sana. Mipango hii ikajaribu ku-*reflect* jambo hili kwa wigo mpana; usawa wa kimaendeleo kati ya mikoa *(regional equity)*. Ni kwa nini ninasema hivi? Kama tunavyojua, kuna mikoa haifanani, mikoa inatofautiana kimaendeleo na namna ambavyo jiografia zilivyo. Kwa hiyo, ninaomba mipango hii ijaribu kuliangalia hili kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikoa ambayo ipo pembezoni, kuna mikoa ambayo ipo katika visiwa. Kuwe na *special intervention;* kuwe na miradi ambayo ni maalum katika maeneo haya. Hii inaweza ikaleta ile *balance* ya maendeleo katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapongeza, na Kamati wamejaribu kulielezea kwa mapana ni kuhusu masuala ya ufuatiliaji, tathmini pamoja na uwajibikaji *(monitoring, evaluation and accountability)*. Hili ni jambo la msingi sana. Tunapokuwa na miradi, lazima jambo hili liwe kazini kuhakikisha kabisa kila kinachofanyika kinakuwa na tija katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ambalo ninaomba niongee hapa ni kuhusiana na sekta ya maendeleo ya jamii kama chombo cha utekelezaji. Tumeona kabisa ya kwamba dira inaongelea habari ya maendeleo ya watu, lakini ni nani atawajibika katika utekelezaji wa majukumu haya?

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ninaomba tu niongee hii nikiwa na lengo la kuonyesha namna ambavyo sekta ya maendeleo ya jamii ni muhimu sana katika

utekelezaji wa mpango huu, kwa sababu ni taaluma hii ambayo watu wa maendeleo ya jamii wanapaswa kuhakikisha kabisa kuwa mpango huu unawafikia wananchi kule walipo; kujua kabisa ya kwamba ni nini ambacho wamepanga? Wana vipaumbele gani? Mchango wao ni nini katika mpango huu maalum wa nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta ya maendeleo ya jamii iwe ni kiungo kati ya sera, iwe ni kiungo muhimu kati ya dira na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninaweza kuliongea hapa ni kuhusiana na masuala ya utawala bora na mabadiliko ya tabia, *(mindset change)*. Utawala bora umetajwa kama msingi katika miongozo hii. Ninaomba tu, kuwa tuongeze masuala ya maadili, uwajibikaji wa viongozi na pia tuongeze masuala ambayo viongozi wanaweza wakawa wabunifu. Kunaweza kukawa na *innovation* na mambo kama hayo. Viongozi wa namna hii watalisaidia Taifa kuhakikisha kabisa mambo haya yanasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya pekee sana ambayo nimepewa. Pia niongeze kitu kimoja, ni kuhusu ushirikishwaji wa wadau muhimu hususan wa sekta binafsi. Tumeangalia, hapa kuna sekta binafsi, vyuo vikuu, na taasisi za utafiti. Ninaomba Serikali ihakikishe kabisa inashirikisha taasisi hizi muhimu ili nao wawe na umiliki wa dira na kuongeza ubunifu katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise*, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya pekee ambayo nimepewa. Kwa kumalizia niseme tu ya kwamba, ninasisitiza kuwa Dira ya Taifa 2050 siyo hati ya sera pekee, bali ni mkataba wa kijamii kati ya Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo tunayoitekeleza leo inaweka msingi imara wa Tanzania tunayoitamani kesho. Hili ndilo tabasamu ambalo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anataka liwe katika maisha ya Watanzania siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Regina. Tutamalizia na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ambayo nimepata ya kuchangia leo kwenye Dira na Mpango wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri pamoja na Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha kwa wasilisho zuri ambalo kwa kweli lilikuwa siyo wasilisho tu, bali ni darasa tosha ambalo lilikuwa limejitosheleza kueleza namna Serikali ilivyojipanga kwenye Dira ya Maendeleo, pia kwenye Mpango wa Miaka 25 na ule Mpango wa Niaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba nijielekeze sasa kwenye mchango wangu ili kuhakikisha kwamba mipango hii pamoja na mambo mazuri ambayo yameelezwa na Serikali. Vilevile niwapongeze pia Kamati ya Bajeti kupitia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa namna walivyochambua nyaraka hizi zote tatu ambazo kwa kweli zikifanyiwa utekelezaji mzuri kama ambavyo Kamati imeelekeza, kutakuwa na tija kubwa kwenye Taifa letu na kufikia dira ya maendeleo, hasa ile ya mpango wa miaka mitano hata kabla ya miaka mitano kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie hasa kuhusu Serikali kuongeza mapato yasiyo ya kikodi. Hizi *non tax revenue* ziwe kama mbadala wa mikopo ambayo inagharimu fedha nyingi kwenye uchumi wetu. Hapa tunategemea mashirika na taasisi zetu za umma kuwa wabunifu na kuongeza mikakati katika vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mashirika na taasisi ambazo zinafanya biashara zije na mikakati mipya ya kubuni biashara

ambazo hazihitaji *stake* kubwa ya Serikali kwenye uwekezaji. Kwa mfano, kuja na mbinu mpya kwenye uwekezaji wa biashara ya *carbon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa mashirika kama *TRC* wanayo maeneo makubwa ambayo ukiangalia barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma wana eneo kubwa ambalo pia wanaweza wakajielekeza kwenye uwekezaji wa *carbon* kama ambavyo wanafanya vizuri Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, ambao kwa mwaka wanapata mapato zaidi ya shilingi bilioni 20 kwenye uwekezaji ya biashara ya *carbon*. Biashara hii haihitaji mtaji wa Serikali, inahitaji tu kubadilisha *mindset* na kufanya uwekezaji na kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye mashirika ambayo yana *assets* nyingi ambazo *non-performing assets* kwa shirika kama Shirika la Posta, shirika kama hili linazo rasilimali nyingi ambazo zipo *idle,* hazitumiki, haiziingizi, zinaweza zikafanyiwa mikakati, hasa zile *assets* kama majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanashindwa kuyatumia kama *assets* za uwekezaji, matumizi yake yanaweza yakabadilishwa au yakafanyiwa *PPP* na *private sector* yakaweza kuleta tija kubwa kwenye ukusanyaji wa mapato ambalo ndiyo changamoto kubwa kwenye miradi mikubwa na hasa kwenye mapato ya Serikali, kuliko kuacha, kama ambavyo sasa hivi hizi *non-performing assets* zinaendelea kuleta hasara kwenye mashirika haya, na hasa Shirika hili la Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuja na mikakati na mawazo chanya. Kwa mfano, leo shirika la Posta linaweza likageuka likawa *Amazon* ya Tanzania. Wafanyabiashara hasa wanaofanya kwenye hizi *digital platform,* wakatumia Shirika la Posta kwa kushirikiana na *TCRA* ikawa ni *platform* kubwa ya kufanya biashara kama ambavyo *Amazon* au na mashirika mengine ya kimtandao yanavyofanya baishara, kuliko kusubiria biashara ambazo imeendelea kufanya au

imeendelea kufanyika kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wa shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ambalo Kamati pia wamelisema, nami ninaungana nao, mashirika au taasisi zetu kupunguza mzigo wa bajeti au kutegemea ruzuku ya Serikali na kuanza kujiendesha kibishara ili kuongeza ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kuongeza ushindani, bali pia kuanza kufikiria mashirika haya, kama ambavyo makampuni binafsi yanaweza kufanya ushindani kwenye masoko; kwa sababu mashirika na taasisi za Serikali zina rasilimali ya mtaji mkubwa, zina rasilimali watu wa kutosha lakini bado yanaweza kufanyiwa *reforming* kubwa ambayo inaweza ikaleta tija ya mageuzi ya kifikra na kuanza kufikiria mashirika haya kujiendesha kibiashara kuliko kutegemea ruzuku ya Serikali. Hii itasaidia sana kupunguza utegemezi na kupunguza bajeti ya matumizi ya Serikali kwenye mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lingine ambalo tunaweza tukalifanya, na Kamati wamelisema, kutumia utalii kwenye maeneo ambayo bado hatujayagusa. Ni kweli kabisa utalii imekuwa sekta muhimu sana katika pato la Taifa. Kwa mfano, kwa mwaka 2024 waliweza kuingiza pato la Taifa *3.5 billion US Dollar,* lakini mapato haya yote yameingizwa kwenye utalii wa aina moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo *diversity* kubwa kwenye utalii kama utalii wa asili lakini pia utalii wa vivutio mbalimbali ambavyo kwa mtawanyiko wetu na namna ambavyo Tanzania ilivyo kwa wingi wa makabila na wingi wa mikoa na mgawanyiko wa rasilimali watu, tunaweza tukatumia utalii mwingine wa ekolojia na mambo mengine ukatusaidia sana kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunao utalii ambao bado haujaingizwa, ambao tukiusimamia vizuri kama Serikali tunaweza tukapata mapato makubwa. Tumezoea kuona ile *migration* ya Serengeti, lakini kule Mtwara tunayo *migration* ya nyangumi ambayo

kwa duniani inapatikana Tanzania pekee, kwenye maingilio ya Ghuba ya *Mnazi Bay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuanzia Julai mpaka mwezi wa Novemba tunapata makundi ya nyangumi maelfu kwa maelfu yanakuja kwa ajili ya kuzaliana kwenye maingilio ya Mto Ruvuma na kwenye Ghuba ya Mnazi Bay pekee, Tanzania hii. Hilo tu linaweza likaingiza fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukanda tu wa bahari na eneo dogo ambalo linaweza likafanyiwa kazi na mapato haya yakaweza upanda kama ambavyo Serengeti imekuwa ikifanya vizuri kwenye hii *migration* ya nyumbu. Pia tunao ukanda wa bahari mkubwa; na Kamati pia wameeleza vizuri kwamba tunaweza kutumia ukanda ule wa Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatolea tu mfano kwa Wilaya moja ya Mtwara ambayo ina ukanda wa bahari wa kilomita zaidi ya 101, tena ni *clean* na ina *beach* nzuri. Ukanda ule, pamoja na kuleta uchumi wa buluu tunaweza pia kuutumia kwa biashara ya *carbon* ambayo haiihitaji mtaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii tukiweza kuisimamia vizuri italeta fedha nyingi sana. Leo hii kwenye halmashauri 189, tukiweza kusema, halmashauri ambayo inaweza ikatoa *dividend* kwa Serikali ni Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ambayo inafanya vizuri kwenye biashara hii ya *carbon.* Imekuwa kinara kwa sababu viongozi walikaa wakaamua na wakasimamia na ikawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunaweza tukalifanya vizuri na kuongeza mapato ni kwenye miundombinu na viwanda. Serikali iendelee kuunganisha miundombinu ya barabara na umeme, hasa kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu, huku kukiwa na umeme wa uhakika hasa kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ambao wanatumia gharama kubwa sana kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vinapata umeme na miradi inaendelea, tunaipongeza sana, lakini wajielekeze kwenye maeneo ya kimkakati, hasa haya maeneo ya uzalishaji, kama vile maeneo ya wachimbaji wadogo au maeneo ya wavuvi ambayo yataleta mapato makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia wachimbaji wadogo wenyewe wakisema kwamba siyo tu wachimbaji wadogo, bali ni nguzo kubwa ya mapato ambayo wananchangia kwa asilimia kubwa na kufanya *stabilization* kwenye sekta hii ya uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa migodi mikubwa ya wachimbaji wadogo, lakini hawa ndio wanasaidia pia kufanya *stabilization* ya uchumi kwa sababu fedha yao inazunguka ndani ya Watanzania na manufaa yake tunayaona moja kwa moja kwenye maisha ya Watanzania ambao pia ndiyo uchumi jumuishi ambao tunausema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ambalo tunaweza tukalifanya, yapo maeneo ambayo Serikali imewekeza mtaji, tena ambayo ni *minority shareholder*. Kwa mfano, kwenye Benki ya *NMB* Serikali inapata gawio hadi kufikia shilingi bilioni 70, lakini ni maeneo ambayo wamewekeza mtaji ambao siyo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo tukiyasimamia vizuri, Serikali inaweza ikapunguza *stake* yake na bado tukapata gawio kubwa. Serikali ibadilishe *mindset,* siyo tu kwenda kwenye umiliki, na kuja na fikra mpya ya uwekezaji. Kwa sababu unapomiliki ile hali ya uwekezaji inaondoka. Kwenye maeneo ambayo Serikali imewekeza kwa asilimia kubwa hatuoni kama tunapata faida kubwa kama maeneo ambayo tumewekeza kwa asilimia kidogo na yanaleta tija kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni hii Benki ya *NMB* ambayo mwanzo ilikuwa haileti gawio kubwa, lakini sasa imekuwa kinara pia kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, tunaweza tukabadilisha

uelekeo tukaenda kwenye uelekeo huu ambao Serikali imeufanya kwenye Benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunaendelea kuishauri Serikali kuja na fikra mpya ya uwekezaji na siyo tu ya umiliki mali. Ikija na fikra ya uwekezaji, tutakuja na mikakati mipya kwenye maeneo ambayo yataleta tija kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka niungane na Kamati ya Bajeti, kwenye yale maeneo yote ambayo wamesema kwamba Serikali ije na mikakati mipya ya uwekezaji hasa kwenye maeneo ambayo yataleta tija kwa haraka, ambayo ni maeneo ya migodi, maeneo ya madini pia na maeneo ya utalii. Maeneo haya yakiwekewa nguvu na tija tunaweza tukapata rasilimali ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, ambaye kwa jioni ya leo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana mliopata nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Muda Mfupi, Muda wa Kati na Muda Mrefu pamoja na Maandalizi ya Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Ninalo tangazo moja hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa

Ofisi ya Bunge kuwa wataalamu wa afya kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wapo kwenye Kituo cha Afya cha Bunge kwa ajili ya huduma ya kumwona daktari bingwa wa mifupa, huduma ya kumwona daktari bingwa wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu, huduma ya kumwona daktari bingwa wa magonjwa ya ndani, huduma za mazoezi tiba na mtaalamu wa tibalishe.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, kutakuwa na elimu mbalimbali kama tibalishe, kwa maana ulaji unaofaa, elimu ya ukaaji na ulaji unaofaa, elimu ya mtindo bora wa maisha, elimu ya huduma bora za kibobezi za *MOI* na elimu ya mfumo wa *online appointment* huduma hii itatolewa kuanzia leo tarehe mbili hadi tarehe 6 Februari, 2026. Hivyo, wote pamoja na watumishi wa Bunge mnakaribishwa kupata huduma hizo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.22 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 3 Februari, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*